*NAKALA YA MTANDAO (ONLINE DOCUMENT)*

**BUNGE LA TANZANIA**

---

**MAJADILIANO YA BUNGE**

---

**MKUTANO WA KUMI NA NANE**

**Kikao cha Pili - Tarehe 29 Januari, 2020**

*(Bunge Lilianza Saa Tatu Asubuhi)*

**D U A**

*Naibu Spika (Mhe. Dkt. Tulia Ackson) Alisoma Dua*

**NAIBU SPIKA:** Tukae.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**HATI ZILIZOWASILISHWA MEZANI**

Hati Zifuatazo Ziliwasilishwa Mezani na:-

**MHE. FELISTER A. BURA - K.n.y MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali kuhusu shughuli za Kamati kwa mwaka 2019.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA – MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:**

Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu ya Serikali za Mitaa kuhusu Usimamizi wa Matumizi ya Fedha za Umma katika Serikali za Mitaa kwa mwaka 2019.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante.

Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO - KATIBU MEZANI:**

**MASWALI NA MAJIBU**

**NAIBU SPIKA:** Maswali tutaanza na Ofisi ya Rais TAMISEMI Mheshimiwa Cosato David Chumi Mbunge wa Mafinga Mjini sasa aulize swali lake.

Na. 12

**Ujenzi wa Barabara za Mji Mafinga**

**MHE. COSATO D. CHUMI** aliuliza:-

Barabara za Mji Mafinga hazipitiki kwa mwaka mzima na kati ya kilomita 407 kwa mujibu wa DROMAS lami ni kilometa 5.58.

Je, Serikali ipo tayari kuongezea fedha TARURA ili ijenge barabara za kupitika kwa mwaka mzima?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi, ya Rais TAMISEMI, majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Cosato David Chumi, Mbunge wa Mafinga Mjini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa DROMAS Mji wa Mafinga una Mtandao wa barabara wenye urefu wa kilometa 325.67. Aidha, urefu wa mtandao wa barabara unatarajiwa kuongezeka pindi zoezi la uhakiki wa mtandao wa barabara linaloendelea litakapokamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoa fedha kwa ajili ya matengenezo ya barabara za Mji wa Mafinga ili kuhakikisha zinapitika wakati wote na imeongeza bajeti ya matengenezo ya barabara kwa Halmashauri ya Mji wa Mafinga kutoka Shilingi milioni 876.81 mwaka kwa fedha 2017/2018 hadi Shilingi bilioni 1.036 mwaka wa fedha 2019/2020. Wakala wa Barabara za Vijijini na Mijini yaani (TARURA) unakamilisha zoezi la kuhakiki mtandao wa barabara zake na itaweka vipaumbele vya ujenzi na matengenezo ya barabara na madaraja kwa kuzingatia urefu na umuhimu wa barabara husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali itaendelea kupitia formula ya mgao wa fedha za Mfuko wa Babarara ili kuona namna bora ya kuiwezesha TARURA kwa kuiongezea fedha ili iweze kuboresha miundombinu ya barabara na madaraja katika halmashauri mbalimbali nchini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cosato David Chumi swali la nyongeza.

**MHE. COSATO D. CHUMI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuuliza swali la nyongeza na kabla ya swali la nyongeza ningependa kuwasilisha shukrani zangu kwa *TARURA* Mafinga na *TARURA* Iringa kwa jinsi ambavyo wanajituma kufanya kazi pamoja na mazingira ya uhaba wa fedha. Pia na Wakala wa Misitu Tanzania kwa maana ya shamba la Sao Hill ambao mara kwa mara tumeshirikiana nao kwa kutusaidia Greda na sisi halmashauri kujaza mafuta kusembua barabara zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nina maswali mawili ya nyongeza swali la kwanza kwa mujibu wa mgao wa fedha za mfuko wa barabara kama alivyosema Mheshimiwa Naibu Waziri mpaka hapa tulipo *TARURA* inapata asilimia 30 na *TANROADS* inapata asilimia 70 na wote wanashughulika na barabara ambazo ni za muhimu katika Taifa letu, lakini bado *TARURA* barabara zao ndiyo zinazobeba mazao zinabeba biodhaa, zinabeba mbolea.

Je, mbali ya hiyo kanuni Serikali iko tayari kutafuta namna nyingine ya kuwa chanzo maalum cha kuiwezesha *TARURA* ifanye kazi zake kwa ufanisi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mji wa Mafinga Mjini unakuwa kwa kasi na ndiyo kitovu cha uchumi wa mazao ya misitu katika Wilaya Mufindi na Mikoa ya Nyanda za Juu Kusini.

Je, Serikali iko tayari japo kuiangalia Mafinga kwa macho mawili ili kusudi miundombinu yake iweze kuboreshwa na hivyo mchango wake katika uchumi wa Taifa ukaongezeka?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwamba tumekuwa na changamoto ya mgao wa fedha na tumepokea pongezi kwa niaba ya Serikali kwa kazi nzuri ambayo inafanyika na TARURA na nchi karibu kila halmashauri. Changamoto kubwa ni ufinyu wa bajeti na upungufu wa fedha ambao upo inapelekea changamoto hizo kuendelea kuwepo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na mambo mengine kama alivyosema Mheshimiwa Mbunge jambo hili la mgao wa fedha linafanyiwa kazi kuna Kamati maalum iliundwa naifanyia kazi na Waheshimiwa Wabunge humu ndani walishatoa maoni mbalimbali kutafuta chanzo mbadala, pia kuangali formula ambayo itatumika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, pamoja na mambo mengine tutaendelea kufanya pia kazi hiyo huu mchakato tutakamilisha na ikishindikana kupata mgao wa fedha hizi au hata 50 kwa 50 basi tuangalie vyanzo vingine vya kusaidia barabara zetu ziweze kupitika. Ni kweli kwamba barabara hizi ni muhimu sana ndipo walipo wananchi wengi, huduma za kijamii nyingi tunajua zinapitika wakati wote na hasa wakati huu wa mvua.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Mbunge anataka kujua kama Serikali inampango wa kuboresha Mji wa Mafinga. Niseme tu kwamba Serikali ina mpango wa kuboresha maeneo yote ya Miji ikiwepo Mafinga Mjini pindi tukipata uwezo wa fedha wa kutosha na kuhakikishia Mheshimiwa Mbunge kwamba kazi hiyo itafanyika kwenye eneo lake ili uchumi uweze kukua na huduma iweze kupatikana kwa haraka na kwa gharama nafuu, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Grace Tendega swali la nyongeza.

**MHE. GRACE V. TENDEGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kuniona, barabara ya kutoka Iringa Mjini kwenda Wilaya ya Kilolo kilometa 133 ambayo kuna kipande cha Jimbo la Kalenga napo kuna changamoto ya barabara mvua zimenyesha barabara nyingi zinakuwa hazipitiki vizuri wananchi wanapata adha na mazao yao yanashindwa na ni ahadi ya Rais ambayo alitoa kwamba kufikia 2020 itakuwa imetengenezwa.

Ni lini sasa Serikali itahakikisha barabara hii inatengenezwa na wananchi wanapita bila matatizo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge watakubaliana na mimi kwamba kipindi hiki tumepata mvua myingi sana na uharibifu wa miundombinu umekuwa ni mkubwa sana, sisi kama Seriikali tumejipanga kuhakikisha kwamba tunakwenda kufanya urejeshaji wa miundombinu hii. Niseme tu kilometa 4217 hadi Desemba zimekuwa na hali mbaya hizi ndiyo barabara katika nchi tunaendelea na uratibu nimuombe Mheshimiwa Mbunge avute subira tumeshatambua maeneo yote yenye shida na tunahitaji fedha za ziada kwenda kufanya marejesho ya miundombinu ya barabara.

Kwa hiyo, wananchi wavute subira sisi kama Serikali kupitia Wizara ya Ujenzi kwa kushirikiana na wenzetu upande wa Serikali za Mitaa kwa maana TARURA tunafanya uratibu wa pamoja ili tuhakikishe kwamba tunaenda kufanya uridhishaji maeneo mbalimbali ya nchi maeneo ambayo yameharibiwa na mvua, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Timotheo Mzava swali la nyongeza.

**MHE. TIMOTHEO P. MNZAVA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru halmashauri ya Wilaya ya Korogwe ni miongoni mwa halmashauri ambazo zilielekezwa kuhamisha Makao yake Makuu ya halmashauri kutoka Mjini kwenda kwenye maeneo yake ya utawala, lakini kuna changamoto kubwa sana ya barabara haswa kwa wananchi wa Tarafa ya Bungu barabara ya kutoka Makuyuni Kwemshai na barabara ya Makuyuni, Zege Mpakayi.

Je, Serikali iko tayari sasa kuwa na mkakati maalum wa kusaidia uboreshaji wa miundimbinu ili wananchi hawa waweze kufika kiurahisi kwenye maeneo ya Makao ya halmashauri mpya zilizoanzishwa?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa kwanza nimpongeze kwa namna anavyohangaika na barabara za eneo lake na nimshukuru alinipa ushirikiano wa hali ya juu nilivyotembelea maeneo haya na maeneo mengine ambayo hakuyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, na niseme tu labda ni kwa kutoa kumbukumbu sahihi kwa mvua ambazo ambazo ziliathiri Mkoa wa Tanga zilikuwa ni kubwa sana kiasi kwamba urejeshaji wa maeneo ambao tumeyafanya hadi sasa tumetumia bilioni 7.8 kurejesha eneo la Tanga peke yake kwa mvua za mwezi Octoba peke yake na nikubaliane na yeye kwamba sasa tumefanya tena kwenye uratibu huu wa mvua zilizonyesha kuanzia Octoba kuja Januari kwa upande wa Tanga pia kumbukumbu kwamba kuna mahitaji makubwa ikiwepo maeneo ambayo Mheshimiwa Mbunge umeyataja.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikuhakikishie tu Mheshimiwa Mbunge kwamba tumetambua maeneo yote yenye shida hizi ikiwepo maeneo uliyoyataja na tunafanya utaratibu wa kuwa na fedha tena kama tulivyofanya Awamu ya I ya mvua za mwezi Octoba tutakwenda kufanya kazi kubwa kufanya marejesho ya maeneo haya ambayo nayataja kwa sababu nafahamu eneo la kwako pia ndiyo limekumbwa na maporomoko ya udongo wananchi wamepata athari kubwa sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunatambua hivyo na tutakuja kufanya uharaka wa kurejesha maeneo hayo uliyoyataja,ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwaombe maswali ya nyongeza yawe mafupi. Tutaendelea na Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 13

**Barabara ya MeiMosi Nanenane – Morogoro**

**MHE. DEVOTHA M. MINJA** aliuliza:-

Barabara ya Meimosi Nanenane katika Manispaa ya Morogoro imegharimu fedha nyingi sana za Serikali lakini barabara hiyo haikujengwa katika viwango vinavyofaa.

Je, kwa nini Wakandarasi waliohusika na ujenzi wa barabara hiyo wasichukuliwe hatua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante, kwa niaba ya Waziri wa Nchi, Ofisi ya Raisi TAMISEMI, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Devotha Mathew Minja, Mbunge wa Viti Maluum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, barabara ya Meimosi-Nanenane yenye urefu wa kilometa 5.1 (Meimosi (2.6 km), Meimosi 2 (1km) na Meimosi 3 (1.5 km) ilijengwa kwa kiwango cha lami nzito (*asphalt concrete*) kwa gharama ya Shilingi bilioni 11.81. Ujenzi ulianza Julai, 2015 na kukamilika mwaka 2017 chini ya usimamizi wa Mhandisi Mshauri *Ms DOCH Ltd* ambaye alikabidhi mradi kwa Mkurugenzi wa Manispaa ya Morogoro mnamo tarehe 30 Aprili, 2017.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi zote zilizoainishwa kwenye mradi huu zilifanyika kwa viwango vya ubora vilivyoelekezwa na upimaji wa ubora kwa kila hatua ulifanyika. Tangu barabara hii ilipokabidhiwa, haijaonesha udhaifu wowote na inatumika kama ilivyokusudiwa hivyo, Serikali haina sababu yoyote ya kuchukua hatua kwa Mkandarasi aliyejenga barabara hiyo, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Devotha Mathew swali lanyongeza.

**MHE. DEVOTHA M. MINJA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana yapo mambo ya ajabu sana, barabara hii ya Meimosi ni barabara ambayo imelalamikiwa kutumia fedha nyingi sana za walipa kodi na hili limekuwa *question* kwa *LAAC* walipokwenda kuitembelea barabara hii *CAG* mwenyewe ali-*question* barabara hii, Mainjinia wa *TANROADS* wali-*question* barabara hii na cha kushangaza mpaka sasa kama kweli Waziri anasema barabara haina shida

Ni kwa nini mpaka Serikali haijazindua barabara hii?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili Mheshimiwa Rais alikuja Morogoro mwaka 2018, na akamuagiza Waziri wa TAMISEMI kuunda tume ya kuchunguza barabara hii baada ya kubaini kuna ubadhirifu.

Je, ni kwa nini toka miaka hiyo miwili mpaka sasa hakuna taarifa yoyote ya barabara hii?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Mbunge ameuliza swali na ukweli kwamba majibu haya kule kuna Mkuu wa Mkoa tena makini ameleka juzi karibuni kazi imefanyika kwa sasas hayo ndiyo majibu ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili anazungumza maelekezo ambayo Mheshimiwa Rais alitoa, Mheshimiwa Rais akitoa maelekezo kwamba ufanyike uchunguzi sehemu fulani aliyetoa maelekezo uchunguzi ufanyike ndiyo unapewa taarifa. Kwa hiyo, sitarajii kwamba taarifa ya Mheshimiwa Rais tutaileta Bungeni hapa labda kama Bunge litaagiza vinginevyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba barabara hii imejengwa kwa makubaliano na mikataba iliyokuwepo ndiyo imepitiwa. Kama kuna jambo ambalo analizungumza yeye na tofauti na maelezo yetu haya tutalifanyia kazi, lakini kimsingi kwa sasa majibu ya Serikali ni hayo tumetuma wqatu wetu wameenda *site* Mheshimiwa Waziri amefanya kazi yake na haya ndiyo majibu ya Serikali kwa sasa katika eneo hili, la barabara ya Meimosi Morogoro Mjini, ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Dkt. Christine Ishengoma swali la nyongeza.

**MHE. DKT. CHRISTINE G. ISHENGOMA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana licha ya barabara ya Meimosi kuwa haina matatizo yoyote, lakini Manispaa ya Morogoro barabara za pembezoni ni mbovu kiasi hazipitiki kwa muda wa mvua. Kwa hiyo, kuna mkakati gani wa kutengeneza hizi barabara ? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Ofisi ya Rais TAMISEMI majibu.

**NAIBU WAZIRI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA (MHE. MWITA M. WAITARA):** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili jana limeuliza naomba nirudie majibu ya Serikali kama ambavyo amesema Mheshimiwa Naibu Waziri yule wa Ujenzi, tumeshafanya tathimini kuangalia maeneo mbalimbali ambayo kwa kweli yameathirika na mvua na baadhi ya maeneo hayapitiki, tumeagiza watu wetu Meneja wa TARURA SO, tumeagiza Meneja wa Mikoa yote na Meneja Wilaya walete tathimini yao taarifa tumeshaipata tunaifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tuwahakikishie hivyo Waheshimiwa Wabunge na Waheshimiwa watanzania kwamba ndani ya muda mfupi sana maeneo yote ambayo hayapitiki kwa dharura, lakini tutaendelea kuwa tunaboresha ili kuimarisha barabara zetu katika maeneo hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaelekeze TANROAD Meneja wa TANROAD Mkoa wa Morogoro apitie maeneo ambapo Mheshimiwa Mbunge amezungumza na yako mambo ambayo unaweza kufanya ndani ya uwezo wao kwa bajeti ndogo iliyopo katika halmashauri na mikoa yetu, lakini yale maeneo makubwa ambayo ni changamoto kwao tumewaambia tuwapokee TAMISEMI ngazi ya taifa tuweze kuyafanyia kazi lengo ni kwamba barabara hizi zipitike wakati wote na huduma kwa jamii yetu iendelee kutolewa kama kawaida. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Khadija Nassir swali la nyongeza.

**MHE. KHADIJA NASSIR ALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kuniona, kufuatia mvua kubwa ambazo zinaendelea kunyesha nchini kumekuwa na uharibifu mkubwa sana wa miundombinu jambo ambalo limesababisha vifo kwa baadhi ya wananchi na kudhorota kwa shughuli za kiuchumi na za kijamii.

Je, Serikali ina mkakati gani maalum wa kuhakikisha kwamba baraka hii ya mvua inakuwa fursa na chachu ya maendeleo na siyo majanga kama ilivyo sasa hivi kwenye nchi yetu? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano majibu.

**NAIBU WAZIRI WA UJENZI, UCHUKUZI NA MAWASILIANO (MHE. ELIAS J. KWANDIKWA)**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza tunao utaratibu kawaida kama sehemu ya mkakati wa kushughulikia hali mvua zinavyokuwa nyingi, ndiyo maana katika bajeti ya mwaka huu unayoendelea kupitia Bunge lako Serikali ilitenga bilioni 8 zaidi ya bilioni 8 kwa ajili ya kumudu dharura zinavyojitokeza, kwa hiyo mkakati tuko nao.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mvua zimekuwa nyingi ndiyo maana tumeendelea kufanya utambuzi wa mahitaji hasa mvua zinavyoendelea, na hapa ninavyozungumza mpaka kufikia Januari tuna mahitaji ya shilingi bilioni 13.6 kwa ajili ya maeneo ya Mikoa 14 ambayo tumeitambua imekuwa na shida. Kwa hiyo, tunaendelea kupitia utaratibu wa kibajeti Serikali itafanya utaratibu wa kuona namna nzuri ya kutatua maeneo haya.

Mheshimiwa Naibu Spika, yako maeneo mengine yatahitaji mvua ikipungua ndiyo tuende tufanye marekebisho makumbwa, sasa hivi TARURA kushirikiana na *TANROAD* tunafanya utaratibu wa ku-*harmonize* yaani kufanya kazi kwa pamoja ili kutengeneza barabara mbadala kwenye maeneo ambayo yana shida ili wananchi waendelee kupata huduma ya barabara

mvua zikipungua tutarudi kufanya marejesho makubwa kwenye maeneo ambayo yamepata athari kubwa. Kwa hiyo, utaratibu upo wa kibajeti tutaendelea kuufuata kwa kuzingatia taratibu na sheria ili tuone tunafanya vizuri katika maeneo na kuwanusuru wananchi na hali hii ya mvua kubwa zilizoendelea kunyesha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Maji, Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Buberwa Kamala Mbunge wa Nkenge sasa aulize swali lake.

Na. 14

**Mradi wa Maji Kyaka – Bunazi**

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA** aliuliza:-

Je, ni lini mradi wa maji kwa ajili ya Kyaka – Bunazi utaanza kutekelezwa?

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodoras Buberwa Kamala, Mbunge wa Nkenge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika katika juhudi za kuboresha huduma ya maji katika Kata za Kyaka na Bunazi, Serikali ilibuni mradi wa maji ambao utawahudumia wananchi wa kata hizo. Usanifu wa mradi na taratibu za ununuzi wa Mkandarasi wa ujenzi wa mradi huo zimekamilika. Utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Kyaka-Bunazi umepangwa kutekelezwa katika mwaka 2020/2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, kazi kuu zilizopangwa kutekelezwa kwenye mradi huo ni ujenzi wa tekeo la maji litakalojengwa katika mto Kagera eneo la Rubale, ulazaji wa bomba kuu urefu wa kilomita 1.5, mtambo wa kutibu maji na Tanki la kuhifadhia maji lenye lita milioni mbili litakalojengwa katika eneo la Kituntu. Mradi huu ukimalika unatarajiwa kuhudumia jumla ya wakazi wote wa kata za Kyaka na Bunzai wapatao 64,470.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Balozi Dkt. Diodorus Kamala, swali la nyongeza.

**MHE. BALOZI DKT. DIODORUS B. KAMALA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, pamoja na shukurani za dhati kutoka kwa wananchi wa Wilaya ya Misenyi na Jimbo la Nkenge kwa mradi mkubwa wa maji ambao kwa mara ya kwanza sasa unaanza kutekelezwa, ninayo maswali mawili madogo ya nyongeza.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la kwanza; pamoja na ukweli kwamba mradi huu ni mkubwa lakini majibu yanaonyesha utatekelezwa katika bajeti ya Mwaka 2019/2020. Sasa katika kipindi hiki ambacho wananchi wanasubiri mradi huo mkubwa nini Serikali inafanya kuhakikisha maji yanaendelea kupatikana kwa uhakika ili wasipate tabu wakati wakisubiri mradi mkubwa?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili dogo; katika kikao changu cha wadau, wataalam waliniandalia taarifa nzuri na nikawaeleza wadau kuhusu Mradi wa aji ya Ruzinga lakini wadau wengi wakasema hapana Mheshimiwa unadanganywa, maji Ruzinga hayatoi.

Je, Mheshimiwa Naibu Waziri atakuwa tayari kufuatana na mimi ili twende kati ya Ruzinga ili tuone hizi fedha nyingi tunazopeleka tunafikiri maji yanatoka na hayatoki ili isije ikafika wakati mwingine ambao siyo muafaka wa kuuliza maswali kama haya twende pamoja anisaidie kutoa maelekezo ya Muarobaini wa matatizo hayo? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kiukweli amekuwa akifanya kazi kubwa sana katika Jimbo lake. Kitu ambacho nimhakikishie; mimi ni Naibu Waziri wa Maji, faraja yangu ni kuona Wanankenge wanapata maji safi na salama. Sasa nataka nimhakikishie baada ya Bunge tutafika na tukiona mradi ule ambao tumetoa fedha maji hayatoki tutamchukulia hatua Mhandisi wa maji pamoja na Mkandarasi ambae amepewa sehemu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kikubwa ambacho nataka kumweleza Mheshimiwa Mbunge ahadi ya utekelezaji wa mradi mkubwa ni ahadi ya Mheshimiwa Rais na watalaam wetu wameshafanya usanifu ninachotaka kumhakikishia, katika kipindi hiki ili wananchi waweze kupata huduma ya maji timu yetu imegundua kisima kikubwa sana katika Kijiji cha Igayaza, tutatekeleza mradi wa haraka ili wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji. Maji ni uhai na sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji hatupo tayari kupoteza uhai wa Wanakyaka. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mariam Kisangi, swali la nyongeza.

**MHE. MARIAM N. KISANGI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuuliza swali la nyongeza. Kwa kuwa matatizo wanayoyapata wananchi wa Nkenge pia yanawapata wananchi wa Kigamboni. Je, Serikali ina mkakati gani mahususi wa kuhakikisha chanzo cha maji cha visima vya Kimbiji na Mpera kinakamilika ili wananchi wa Kigamboni, Mbagala, Chamazi, Temeke na maeneo mbalimbali ya Jiji la Dar es Salaam waweze kupata maji safi na salama?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Mbunge kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa ufupi, hii ni Serikali ya Awamu ya Tano ikiahidi inatekeleza. Tumeshachimba visima zaidi ya 20 katika Kimbiji na Mpera na mpaka sasa tumeshamkabishi Mkandarasi kwa ajili ya uanzaji wa mradi wa Kigamboni ili wananchi wa Kigamboni waweze kupata huduma ya haraka. Kikubwa ambacho tunachotaka kumsisitiza Mkandarasi wa mradi ule aweze kufanyakazi kwa mujibu wa mkataba ili uweze kukamilika kwa wakati na wananchi wa Kigamboni na maeneo mengine waweze kupata huduma ya maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Esther Bulaya, swali la nyongeza.

**MHE. ESTHER A. BULAYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Naomba niulize swali dogo la nyongeza. Najua mradi wa Maji Bunda ni wa muda mrefu na nimeushughulikia sana, hilo halina ubishi. Najua tatizo sasa hivi siyo maji kutoka kwenye chanzo kule Nyabehu, tayari sasa hivi maji yanakuja. Tatizo kubwa ni mtandao wa kuhakikisha wananchi wengi wa Bunda Mjini wapate maji safi na salama. Sasa, ni lini Serikali watahakikisha wanasambaza mtandao mkubwa wa maji na kuunga mkono juhudi zangu kwa kutenga fedha za Mfuko wa Jimbo kuwasaidia kutandaza huo mtandao ili wananchi wa Bunda kwenye kata zote 14 wapate maji safi na salama, ni lini?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Esther Bulaya kama ifuatavyo:

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda atambue kwamba Serikali imefanya jitihada kubwa sana katika Jimbo lake la Bunda, tuna utekelezaji wa mradi zaidi ya bilioni 10, huo unaendana sambamba kabisa na utandazaji wa mtandao wa maji. Kikubwa ambacho ninachotaka kumhakikishia, Serikali hii ya Awamu ya Tano tutahakikisha kazi ile inakamilika kwa wakati na wananchi wake waweze kupata huduma hii muhimu sana ya maji.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Pauline Gekul, swali la nyongeza.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kunipa nafasi niulize swali moja la nyongeza. Mheshimiwa Naibu Waziri Mradi wa Maji wa Kata ya Sigino, Mheshimiwa Waziri alifika mwaka jana akaahidi kwamba wataalam wake watafika ndani ya siku 10 ili ule mradi uanze.

Naomba nifahamu hawa watalaam watafika ili wananchi wale wapate maji? Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nimwombe Mheshimiwa Mbunge kwa kazi kubwa anayoifanya tukutane basi baada ya Bunge ili tuweze kukutana na wataalam wetu na kuweza kuwaagiza haraka wafanye kazi. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na swali la Mheshimiwa Bonventura Desdery Kiswaga, swali lake litaulizwa kwa niaba na Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa.

Na. 15

**Kutumia Mtandao wa Maji Magu Kupeleka Ndagalu**

**MHE. RICHARD M. NDASSA (K.n.y. MHE. KISWAGA B. DESTERY)** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kutumia mtandao wa maji Magu kupeleka Tarafa ya Ndagalu, Kata za Shishani, Njinjinili, Kabila, Nkungulu, Ng'haya, Sukuma, Buhumbi na Mwamabanza zenye jumla ya vijiji 24?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji, naomba kujibu swali la Mheshimiwa Kiswaga, Mbunge wa Jimbo la Magu, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi wa Maji Magu Mjini ambao tayari umekamilika, una uwezo wa kuzalisha maji kiasi cha lita milioni 7.25 kwa siku, ukilinganisha na mahitaji ya sasa ya lita milioni 3.54 kwa wakazi wa Magu Mjini na Vijiji vya Kipeja, Sagani, Nyashimba na Ilungu. Hivyo Mradi huu una ziada ya maji ya lita milioni 3.71 kwa siku kwa sasa kutokana na ziada hiyo, Serikali kupitia Programu ya lipa kwa matokeo yaani *Programme for Results (P4R)* itajenga miundombinu ya usambazaji wa maji kutoka kwenye Mradi wa Magu mjini kupeleka kwa

baadhi ya vijiji vilivyopo tarafa ya Ndagalu ikiwa ni pamoja na Vijiji vya Misungwi, Kitongo, Lumeji, Buhimbi, Iseni, Nyang'hanga na Nyashoshi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kuwa azma ya upatikanaji wa maji katika vijiji vingine vya Tarafa ya Ndagalu inapatiwa ufumbuzi wa kudumu, Serikali itahakikisha kuwa imetenga fedha katika bajeti ya Mwaka 2020/2021 ili vijiji vilivyobaki viweze kupata huduma ya maji kupitia Mradi wa Ziwa Victoria.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mganga Ndassa, swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD M. NDASSA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba niishukuru sana Serikali kwa majibu yake mazuri hasa kukamilisha angalau kupeleka maji katika Wilaya ya Magu pale Magu Mjini.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali langu; kwa sababu muuliza swali la msingi amezungumzia vijiji kadhaa ikiwemo pamoja na Kijiji cha Kabila ambacho kina wakazi wengi sana. Ili kuondoa tatizo la ukosefu wa maji na Mheshimiwa Waziri anajua kabisa kwamba maji ni uhai, ni lini sasa angalau kwa kuanzia kabla ya Mradi mkubwa huu wa Maji ya Ziwa Victoria haujaanza angalau kwenda kufufua vile visima ambavyo vilikuwepo kama ambavyo tunavyofanya sasa kwenye eneo la Jimbo la Sumve pamoja na Magu, lakini pia kusafisha vile visima ambavyo vilikuwa vinafanya kazi. Sasa Serikali kwa nini sasa isifanye utaratibu wa kuchimba na kusafisha vile visima ambavyo vilikuwepo? Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa Ndassa kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge Mzee wangu, Mzee Ndassa sisi kama viongozi wa Wizara ya Maji tumeainisha Mikoa zaidi ya 17 yenye changamoto ya maji ikiwemo eneo la Mkoa wa Mwanza, lakini tumepata fedha kutokea *World Bank* na katika Mikoa hii 17 tumepeleka kila Halmashauri *1.3 billion* ikiwemo katika Jimbo lake la Sumve.

Nimwombe sana Mhandisi wa maji akae na Mheshimiwa Mbunge na mimi mwenyewe nipo tayari ili katika kuhakikisha fedha zile zinaelekezwa katika zile changamoto ambazo Mheshimiwa Mbunge amezianisha. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Oliver Semuguruka, swali la nyongeza.

**MHE. BONIFACE M. GETERE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru. Katika Jimbo la Bunda Vijijini kuna Mradi wa Maji Nyamuswa na kuna Mradi wa Maji Mgeta na Naibu Waziri ailifika kwenye maeneo hayo lakini mpaka sasa ile Kamati aliyoiunda kufuatilia shughuli hizo haijakwenda vizuri.

Je, Naibu Waziri yuko tayari sasa kushughulika na hilo jambo ili watu wa Nyamuswa na Mradi wa Mgeta-Nyangarangu wapate maji?

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, nadhani haya ni kati ya mambo yale aliyokuwa anazungumza Mheshimiwa Pius Msekwa jana. Mheshimiwa Naibu Waziri majibu kwa swali hilo.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nipo tayari. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Nape Nnauye, swali la nyongeza.

**MHE. NAPE M. NNAUYE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi niulize swali dogo la nyongeza. Pamoja na shukurani za wananchi wa Jimbo la Mtama kwa miradi kadhaa inayoendelea ya maji katika Jimbo hilo baada ya Mji wa Mtama kupewa hadhi sasa ya kuwa Halmashauri mahitaji ya maji yameongezeka sana katika Mji huu. Je, Serikali sasa iko tayari kwenye bajeti ya mwaka huu kutenga fedha kwa ajili ya kuboresha miundombinu na upatikanaji wa maji katika Mji huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji naomba kujibu swali la Mheshimiwa Mbunge, Kaka yangu Mheshimiwa Nape.

Mheshimiwa Nape anafanya kazi kubwa na nzuri na alishakuja katika Ofisi yetu ya Wizara ya Maji, tukakaa mimi, yeye, Waziri pamoja na Katibu Mkuu. Hakuna haja ya kusubiri mpaka bajeti fedha tumekwishatuma *1.3 billion* kwa ajili ya utekelezaji. Mheshimiwa Mbunge asimamie mradi ule uanze haraka sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Frank Mwakajoka, swali la nyongeza.

**MHE. FRANK G. MWAKAJOKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niulize swali la nyongeza. Mji wa Tunduma ni mji unaokua kwa kasi na kuna miradi karibuni miwili au mitatu inatekelezwa kwenye Mji wa Tunduma, lakini tangu imeanza kutekelezwa mpaka sasa hivi wananchi hawajaanza kupata maji ya uhakika na Mheshimiwa Waziri na Naibu Waziri pamoja wamekuwa wakiwapa tarehe kila wakati za kumaliza miradi hiyo.

Je, ni lini miradi hiyo itakamilika ili wananchi wangu wa Mji wa Tunduma waanze kupata maji safi na salama kwa wakati?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maji, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAJI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Maji kwanza nashukuru kuona Mheshimiwa Mbunge anakiri kwamba tunafanya kazi kubwa na ipo miradi ambayo tunaitekeleza katika Jimbo lake. Kikubwa ambacho ninachotaka nimhakikishie Mheshimiwa Mbunge, sisi kama viongozi wa Wizara tumeshabainisha miradi ambayo ipo katika hatua mbalimbali kwa ajili ya ukamilishaji. Tumepanga katika wiki hii ya maji itakuwa siyo wiki ya mapambio, ni wiki kwa ajili ya kuzindua miradi yote ya maji, kwa hiyo Wakandarasi wajipange katika kuhakikisha wana-*meet* zile *commitment* tulizoziweka ili wiki hii ya maji tuweze kuzindua miradi mingi ya maji.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tunakualika katika kuzindua miradi yetu ya maji. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, ukinialika na mimi nitakualika huko ambapo pengine hukupanga ratiba ya kwenda kwa sasa.

Waheshimiwa Wabunge, tunaendelea na Wizara ya Nishati, Mheshimiwa Fred Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busokelo sasa aulize swali lake.

Na. 16

**Visima Hatari Eneo Linalopakana na Gesi - Busokelo**

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE** aliuliza:-

Katika eneo linalopatikana gesi aina ya *carbondioxide (CO2)* kwenye Jimbo la Busekelo, Kijiji cha Mpata kuna visima ambavyo ni hatari kwa binadamu na viumbe hai wengine kwani huwa wanakufa wakivuta hewa ya sehemu hiyo:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kunusuru maisha ya binadamu na viumbe katika eneo hilo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati, majibu.

**NAIBU WAZIRI NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Nishati, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete, Mbunge wa Busekelo, kama ifuatavyo:-
Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kuwa katika Jimbo la Busekelo, katika Kijiji cha Mpata kuna visima vya gesi ya ukaa *(Carbondioxide)* vinavyomilikiwa na Kampuni ya Tanzania *Oxygen Limited.* Kampuni hiyo inamiliki leseni mbili za uchimbaji wa gesi ya ukaa ambazo ni *ML 139/2002* iliyotolewa tarehe 17/11/2002 na *ML 379/2009* iliyotolewa tarehe 21/08/2009. Kisima cha Mpata Kipo katika leseni Na. *ML 139/2002*.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo la Mpata kuna visima viwili. Kisima kimoja kilichimbwa na kimefunikwa madhubuti na Kampuni ya Tanzania *Oxygen Limited* ambayo inavuna gesi ya ukaa. Kisima cha pili kimetokana na nguvu za asili zilizosababishwa na mlipuko wa volkano na hivyo kupelekea uwepo wa kisima cha asili. Kutokana na uwepo wa kisima hicho kilichotokana na njia ya asili, tafiti za awali zinatoa tahadhari ya kisima hicho kikifunikwa kinaweza kutoa gesi hiyo kupitia njia nyingine na hivyo kuleta madhara yasiyotarajiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inaendelea kufanya ukaguzi wa mara kwa mara katika maeneo hayo ili kudhibiti athari inayoweza kutokea. Hatua za udhibiti zilizochukuliwa na Serikali kwa kushirikiana na *TOL* ni pamoja na kuweka vizuizi madhubuti, uzio na ulinzi wakati wote kwa watu na wanyama ili wasiweze kufika katika eneo la kisima sambamba na kuweka mabango ya tahadhari katika eneo hilo. Aidha, Serikali kwa kushirikiana na *TOL* inaendelea kutoa elimu kwa wananchi kuhusu hatari za gesi ya ukaa katika maeneo yanayozalishwa gesi hiyo. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Fredy Mwakibete, swali la nyongeza.

**MHE. FREDY A. MWAKIBETE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa fursa niweze kuuliza maswali mawili madogo ya nyongeza. Pamoja na juhudi nzuri za Serikali zilizofanywa pamoja na Kampuni hii ya Tanzania *Oxygen Limited* kuweza kuzuia baadhi ya wanyama watambaao pamoja na binadamu kwenda kwenye eneo hili la kisima ambacho mara nyingi miaka ya nyuma Wananchi na wanyama wengine walikufa kutokana na kuvuta gesi hii ya *carbondioxide*. Swali la kwanza; je, ni lini Serikali itaendelea kutoa elimu kwa wananchi ambao wanazunguka kisima hiki na kwa kuwa nguvu za asili za *volcano* bado zipo na *volcano* nii ni hai ili kuzuia madhara yatokanayo na kuvuta gesi hii ya *carbondioxide?*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa kuwa Serikali imeonesha nia njema kwa ajili ya kujenga viwanda hapa nchini lakini kumekuwa kuna changamoto kubwa kuingiza gesi hii ya *carbondioxide* ndani ya Nchi yetu ya Tanzania tukitambua kwamba *carbondioxide gas* inatumika katika mazingira ama kwenye vitu vingi ikiwemo vyakula pamoja na vinywaji ili visiharibike. Ni kwa kiwango gani Serikali itavutia zaidi wawekezaji kwenye maeneo mengine ambayo gesi hii ya *carbondioxide* bado haijaanza kuchimbwa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati, majibu.

**WAZIRI NISHATI**: Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nampongeza sana Mheshimiwa Naibu Waziri katika majibu ya msingi ya suala la Mheshimiwa Mwakibete, lakini vilevile nimpongeze sana Mheshimiwa Mwakibete kwa kufuatilia masuala haya ya matumizi ya *carbondioxide*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kwanza ni lini Serikali itaendelea kutoa elimu; Kampuni ya Tanzania *Oxygen* kwanza imetenga takribani dola milioni tano kila mwaka kawa ajili ya kutoa elimu katika maeneo yao ya leseni. Kwa hiyo shughuli za kutoa elimu zinaendelea, lakini sambamba na hilo Serikali kwa kushirikiana na Tanzania *oxygen* zimeweka timu mahususi kwa ajili ya mpangokazi wa kutoa elimu kila mwezi katika maeneo hayo. Kwa hiyo shughuli za utoaji wa elimu ni endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika suala la pili la kulinda soko la ndani; ni kweli, kwanza kuna nchi ambazo zinzalisha *carbondioxide* kama Tanzania, mathalani; DRC, Kenya na Nchi ya Msumbiji. Kwa Tanzania tunachofanya kwa sasa tumeunda timu mahususi kwa ajili ya kufanya tathmini ili kuangalia mahitaji ya ndani na uwezo tulionao ndani ya miezi mitatu, tukishajiridhisha kwamba uwezo wa ndani wa *carbondioxide* unatosha kuzalisha vinywaji kama soda pamoja na vinywaji vya bia, tutazuia kabisa *carbondioxide* kutoka nje badala yake tutumie viwanda vya ndani.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mipata swali la nyongeza.

**MHE. DESDERIUS J. MIPATA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kunipa nafasi. Vijiji vya Katani, Malongwe, Sintaling, Kana na vinginevyo viko katika Awamu ya III ya kupewa umeme mzunguko wa pili lakini mpaka sasa hatujapata. Je, ni lini mradi huu utaanza?

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli alivyozungumza Mheshimiwa Mbunge….

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Waziri wa Nishati kwa kuwa uko tayari kujibu lakini swali halina uhusiano na swali la msingi lilikuwa linahusu gesi. Mheshimiwa Naibu Waziri wa Madini majibu. *(Makofi)*

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu spika, nishukuru sana majibu yaliyotolewa upande wa Wizara ya Nishati lakini kwa kusisitiza kwa jinsi alivyouliza Mheshimiwa Atu sisi Wizara ya Madini kwa kushirikiana na TOL…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Malizia kabisa jina lake kwa sababu kule ukikatisha kule kwao anaweza ikajulikana kuna Mbunge mpya humu ndani. Mheshimiwa Fredy Atupele Mwakibete.

**NAIBU WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu spika, ahsante sana Mheshimiwa Atupele Mwakibete. Ni kwamba Wizara ya Madini kwa kushirikiana na Kampuni ya *Oxygen Limited* katika lile eneo ambalo linatoa ile hewa ya *carbondioxide* kampuni ya *TOL* wameweka sensa maalumu kwa ajili ya ku-*detect* hewa ile inapojitokeza kutambua mapema, na hewa hiyo inapojitokeza zile sensa zinatoa taarifa kwamba kuna hewa chafu inakuja na kwa kweli wanatoa taarifa katika maeneo yale kwa watu wanaozunguka maeneo yale kuweza kukaa mbali na lile eneo na kuhakikisha kwamba hapatokei tena vifo vinavyotokana na watu kupumua hewa hii ya ukaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kuna zile hatua za awali zimeshachukuliwa na kwa kweli Tanzania *Oxygen* kupitia leseni yao namba 139 ambayo imetolewa mwaka 2002 wako tayari sasa kuhakikisha kwamba wanakwenda katika uwekezaji na kuhakikisha kwamba wanakwenda kuitumia ile hewa ya *carbon dioxide* katika matumizi mbalimbali ambao yamepangwa ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu kwa swali alilouliza Mheshimiwa Mipata.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli maeneo ambayo ameyataja Mheshimiwa Mbunge yako katika mpango wa pili wa utekelezaji wa mradi wa *REA*, na kwa kweli katika eneo la Katani na Malongwe imeshaingia kwenye mpango huo na utekelezaji wake unaanza Februari mwaka huu kuanzia tarehe 28. Lakini kuna suala moja ambalo Mheshimiwa hajauliza kule Wampembe umbali takribani wa kilometa 68 kutoka Mjini ni eneo ambalo ni tengefu sana, eneo hili lilikuwa nalo liingie kwenye mpango wa *round* ya pili lakini badala yake tumeanza kuitekeleza kuanzia wiki iliyopita. Nimeomba nimpe taarifa Mheshimiwa Mbunge ili awape taarifa wananchi wake wananchi wa Wampembe ambao wanahitaji umeme kwa haraka sana ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Waheshimiwa tunaendelea na swali la Mheshimiwa Anna Richard Lupembe Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 17

**Kupeleka Umeme wa Gridi ya Taifa Katavi**

**MHE. ANNA R. LUPEMBE** aliuliza:-

Je, ni lini Serikali itapeleka umeme wa Gridi ya Taifa Mkoani Katavi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri na Nishati napenda kujibu swali la Mheshimiwa Dada yangu Anna Richard Lupembe Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Shirika la Umeme Nchini (*TANESCO*) inatekeleza Miradi mbalimbali ya kusafirisha umeme itakayohakikisha kuwa Mikoa yote nchini inaunganishwa katika gridi ya Taifa ikiwemo Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kwa sasa kupitia shirika la umeme nchini (*TANESCO*) inatekeleza Mradi wa ujenzi wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kilovoti 132 kutoka Tabora hadi Katavi kupitia Ipole na Inyonga yenye urefu wa kilomita 381 ili kuunganisha Mkoa wa Katavi katika gridi ya Taifa. Kazi hiyo pia itahusisha ujenzi wa vituo vya kupoza umeme wa msongo wa kilovoti 132/33 vya Ipole, Inyonga na Mpanda Mkoani Katavi. Gharama za mradi huu ni Shilingi bilioni 135.3**.**

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 11 Oktoba, 2019 Mheshimiwa Dkt. John Pombe Joseph Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliweka jiwe la msingi la ujenzi wa mradi huu katika eneo la Orio Mjini Mpanda. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni ujenzi wa vituo vya kupoza umeme vya Mpanda, Ipole na Inyonga pamoja na upimaji wa njia ya kusafirisha umeme kwa ajili ya tathmini ya mali za wananchi watakaopisha mradi. Kazi za ujenzi wa mradi huu zinatekelezwa kwa kutumia wataalam wa *TANESCO* kupitia kampuni tanzu ya *ETDCO*. Mradi huu unatarajiwa kukamilika kabla ya mwezi Mei, 2021.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali pia imeanza kutekeleza Mradi mkubwa wa njia ya kusafirisha umeme wa msongo wa kV 400, Iringa - Mbeya – Tunduma - Sumbawanga – Mpanda - Kigoma – Nyakanazi *(North West Grid)* yenye urefu wa kilomita 1,384. Mradi huu upo katika hatua mbalimbali za utekelezaji. Shughuli za ujenzi wa mradi huu zitaanza mwezi Mei, 2020 na zinatarajiwa kukamilika katika mwaka wa fedha 2022/2023.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anna Richard Lupembe swali la nyongeza.

**MHE. ANNA R. LUPEMBE:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwanza tunaishukuru sana Serikali wananchi wa Mkoa wa Katavi kwa kutuletea mradi mkubwa sana huu ambao utatusaidia katika Mkoa wetu wa Katavi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa kuwa mradi huu wa Mkoa wa Katavi ni mradi wa mkakati, Mkoa wa Katavi tunataka kujenga bandari na vilevile tunataka *standard gauge* inafika katika Mkoa wetu wa Katavi. Na mradi huu unaenda kwa kusuasua sana ninavyoongea sasa hivi nilikuwa naongea na Meneja wa *TANESCO* wa Mkoa wangu wa Katavi mradi unaenda kwa kusuasua, tunaomba tupate majibu mazuri lini mradi huu utaanza na utaisha lini ili kwa manufaa ya wananchi wa Katavi kwa sababu tuna malengo ya kupata viwanda ndani ya Mkoa wa Katavi tumechelewa sana tunataka viwanda ili tuweze kufaidika na Serikali yetu ya Awamu ya Tano? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na vilevile swali langu la pili kwa kuwa Mkoa wa Katavi kuna vijiji vingi sana na umeme wa *REA* bado haujawafika, ni lini umeme wa *REA* utatufikia katika vijiji vyetu? Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri, Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri katika eneo hili napenda pia nimpongeze Mheshimiwa Mbunge kwa kufuatilia mradi huu mahususi wa *North West Grid*. Kwanza ni lini mradi utaanza mradi umeshaanza kupeleka *Grid* ya Taifa katka maeneo ya Katavi na kwa hatua ya kwanza tumeanza na utekelezaji wa kuutoa umeme wa Grid kutoka Mjini Tabora kama ilivyosoma katika swali la msingi kupitia Ipole, Inyonga na hatimaye Mpanda. Umbali wa takribani kilomita 381 na utekelezaji umeanza na tunatarajia mradi kukamilika kabla ya mwezi Mei mwakani, kwa hiyo wananchi wa Katavi watakuwa wameshapatiwa umeme wa Grid kabla ya mwezi Mei Mwakani huo ni Awamu ya I ya utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Awamu ya II, mradi utaanza kutekelezwa kuanzia mwakani mradi ambao unatokea kimsingi Iringa, Mbeya, Sumbawanga na baadaye kutoka Sumbawanga, Mpanda na hatimaye Kigoma umbali wa takribani kilomita 1384 kwa ujumla wake mpaka Nyakanazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika awamu hii eneo hili litaanzwa kutekelezwa kwa maana nyingine mwanzo mwa mwaka lakini utaisha mwaka 2022. Mradi huu ni muhimu sana kwa sababu unaunganisha kati yetu na nchi ya Zambia kwa umeme wa kilovoti 400 na umeme utakapopatikana maeneo ya Katavi wananchi wa Katavi wataweza sasa kufanya shughuli za kiuchumi ikiwa ni pamoja na ujenzi wa viwanda. Kwa hiyo, nimwambie Mheshimiwa Mbunge kwa niaba ya wananchi wa Katavi wavute subira mradi wakati unatekelezwa na utakamilika kama nilivyotaja.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusiana na swali la pili kuhusu vijiji ambavyo havijapata umeme katika Mkoa mzima wa Katavi. Mkoa wa Katavi bado vijiji 132 havijapata umeme na vijiji vyote tumeviingiza kwenye mpango wa *REA* Awamu ya II unaoanza mwezi Februali hata hivyo vile vijiji ambavyo vinatekelezwa na mkandarasi kwa sasa vitakamilishwa vyote ifikapo mwezi Aprili mwaka huu 2020.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Joseph Mkundi swali la nyongeza.

**MHE. JOSEPH M. MKUNDI**: Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kumekuwa na tatizo kubwa sana la kukatika kwa umeme wakati mwingine kwa siku nzima au hata zaidi ya siku

kwenye visiwa vya UKerewe kila wakati mvua inaponyesha. Ningeomba Mheshimiwa Waziri awaambie wananchi wa Ukerewe ni lini tatizo hili litakoma ili wafurahie huduma ya umeme kama yalivyo maeneo mengine nashukuru sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli eneo la Ukerewe kwa mwezi mmoja uliopita umeme ulikuwa umekatika sana umesababishwa na sababu moja tu, wavuvi wanaovua kutoka eneo la Kisolia ambapo ni mwanzo wa kuingilia kutoka Bunda kuelekea Lugenzi wamekuwa mara nyingi sana wakikata nyaya wakati wa uvuvi. Lakini nyaya zile zimekuwa zikitikiswa pia wakati wa mvua inapoambatana na upepo, kwa hiyo, ni kweli maeneo ya Ukerewe yamekuwa yakipata changamoto kwa kukatika kwa umeme kipindi hiki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hatua tulizochukua kwa niaba ya Mheshimiwa Mbunge na wananzegwa wananchi wa Ukerewe ni kwamba kwanza tumeanza kujenga kebo ya kutoka Kisolia kwenda Lugenzi ambapo ni kilomita nne na tume-commit shilingi bilioni 375 na ujenzi umeanza tutafunga kebo tutaipitisha juu ili wavuvi waache kuzigusa na hivyo kutakuwa na umeme muhimu sana kwa maeneo hili. Kwa hiyo, wananchi wa Ukerewe wavumilie kipindi cha wiki mbili zinazofuata mradi utakamilika ili umeme uwe ni uhakika zaidi kwa maeneo ya UKerewe.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipe nafasi kidogo kwa sababu ni suala la Ukerewe nitoe tangazo kwa wananchi sio wa Ukerewe peke yake ingawa Mheshimiwa Mbunge hajaliuliza, kumekuwa na changamoto kwa wananchi wa Ukerewe hasa watumiaji wadogo wa umeme kutozwa shilingi 2500 kwa *unit* kinyume na utaratibu na sheria ya umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda nitoe tangazo kwa wananchi wa Ukerewe wasikubali kutoa shilingi 1000 kwa *unit* kwa sababu wananchi wote wa Ukerewe ni sawa na Watanzania wengine ambao wanatumia *unit* 75 ambao wanatakiwa walipe shilingi 100 *per unit* badala ya 2500 *per unit*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tangazo hili Mheshimiwa Mbunge anifikishie, lakini nimuombe Mheshimiwa Mkuu wa Wilaya ya Ukerewe alisimamie na Meneja wa *TANESCO* alisimamie ili mwananchi yoyote atakayepatikana akitozwa hivyo kupitia kwa mkandarasi basi atoe taarifa mara moja na Serikali ichukue hatua dhidi ya watu ambao sio wazalendo kwa kitendo hicho ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante Mheshimiwa Willy Qambalo swali la nyongeza.

**MHE. WILLY Q. QAMBALO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, mkandarasi Nipol *group* anayefanya usambazaji wa umeme katika Mkoa wa Rushu hususani Wilaya ya Karatu kazi yake ya usambazaji ni ndogo sana, hivi sasa pamoja na kwamba muda wake wa ukandarasi unakaribia kuisha lakini bado vijiji vingi vya Kata za Bugeri, Kansai Endamarieki havijafikiwa na umeme. Nini kauli ya Serikali juu ya mkandari huyo ambaye anasuasua?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Nishati majibu.

**NAIBU WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kazi za ujenzi wa mradi wa *REA* Awamu ya III mzunguko wa kwanza zinaendelea na mkandarasi Nipol anafahamu kabisa hivi karibuni tulifanya kikao cha wakandarasi wote na kwamba tumewaambia kwamba ifikapo tarehe 30 Juni, 2020 mradi utakuwa umekamilika na watakabidhi vijiji vyote vitakuwa vimejengewa miundombinu ya umeme na kazi ya kuwasambazia wateja itaendelea.

Kwa hiyo, nimuombe Mheshimiwa Mbunge baada ya kipindi cha maswali na majibu tuonane ili tuweze kuzungumza zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie tu usimamizi umeimarishwa na ni muagize mkandarasi Nipol kwa niaba ya Waziri wa Nishati kwamba azingatie *dead line* iko pale pale na aitaongezwa muda wowote kwa wakandarasi wote nchini lazima wakamilishe tarehe 30 Juni, 2020 ili uunganishaji pamoja na miundombinu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Martha Umbulla swali la nyongeza.

**MHE. MARTHA J. UMBULLA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niipongeze Serikali kwa kusambaza umeme maeneo mengi katika nchi yetu lakini najua kipaumbele moja wapo cha Serikali ni kulenga zile Taasisi zenye kutoa huduma za jamii kama shule, zahanati nakadhalika. Shule ya sekondari ya Bama iliyoko Kata ya Nangwa Wilayani Hanang licha ya kuomba kwa muda mrefu hadi leo juhudi za kuomba huo umeme haujazaa matunda. Ni nini tatizo ambalo linasababisha sekondari hiyo isipate umeme hadi leo?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Nishati majibu.

**WAZIRI WA NISHATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nimshukuru Mheshimiwa Mbunge kwa swali lake la nyongeza Mheshimiwa Martha. Kwanza nimpongeze kwa sababu amefuatilia sana kuhusu shule hii, lakini nieleze tu shule hii ipo karibu sana na umeme takribani nusu ya kilomita na tumekuwa tukifuatilia sana halmashauri ile iweze kulipia ili umeme uweze kuingia kwenye hiyo shule ya sekondari. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbunge nashukuru sana kwa kukumbushia hili lakini na mimi nitoe maelekezo wa Mkurugenzi wako na Mwenyekiti wa Halmashauri alipe gharama za kuunganishiwa umeme ili shule hiyo ipate umeme.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitumie nafasi hii kwa Waheshimiwa Wabunge kwa niaba ya Wakurugenzi na Wenyeviti wa Halmashauri zote nchini wahakikishe wanatenga fedha mahususi kwa ajili ya kuingiza umeme kwenye Taasisi za Umma, hapa tuna maana shule, vituo vya afya, zahanati na Taasisi nyingine. Imekuwa ni changamoto kubwa sana tunapokwenda maeneo yale unakuta shule ipo karibu umeme lakini halmashauri haijalipia. Basi nitoe rai hiyo ili wafanye hivyo ziweze kuunganishiwa umeme na shule ambazo ziko mbali hata kama kijijini hatujapeleka umeme sisi tutapeleka umeme mahususi kwa ajili ya hizo shule za sekondari na vituo vya afya. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri kwa kuzingatia miradi mikubwa ambayo mnatekeleza sasa hivi kama Serikali ya kuleta umeme mwingi umeme utakapokuwa mwingi nadhani upande wa *TANESCO* waangalie namna wanaweza kumuwekea mtu umeme halafu walipe kwa kutumia *bill* kama ambavyo umeme hawezi kupata bila kulipa. Kwa hiyo atakavyokuwa analipa umeme analipa na huduma ambayo nyie mlishaipeleka pale.

Waheshimiwa Wabunge tunaendelea na Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Mheshimiwa Vedasto Edigar Ngombale Mbunge wa Kilwa Kaskazini swali lake litaulizwakwa niaba na Mheshimiwa Bobali.

Na. 18

**Zoezi la Kupeleka Mifugo Mikoa ya Kusini**

**MHE. HAMIDU H. BOBALI (K.n.y. MHE. VEDASTO E. NGOMBALE**) aliuliza:-

Zoezi la kupeleka mifugo Mikoa ya Kusini limeleta madhara makubwa kwa mazingira na wananchi kwa ujumla kwa sababu ya kukosa maandalizi kabla ya utekelezaji wake:-

(a) Je, Serikali iko tayari kujenga Malambo ili kunusuru tatizo la maji kwa mifugo hiyo?

(b)Je, Serikali iko tayari kuondoa mifugo ambayo ipo katika maeneo ambayo hayakupangwa kwa ajili ya mifugo kutokana na mipango ya matumizi bora ya ardhi katika Kata ya Mifola, Kandawale na Somanga?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mheshimiwa Waziri wa Mifugo na Uvuvi naomba kujibu maswali ya Mhe. Vedasto Edgar Ngombale Mbunge wa Kilwa Kaskazini kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mujibu wa ugetuaji wa Madaraka, kumradhi mnamo mwaka 2006 Serikali iliamua kuondoa makazi, shughuli za kilimo na za mifugo katika bonde la Ihefu ambalo lilikuwa linaendelea kukauka hivyo kuathiri upatikanaji wa maji ya kutosha kwa ajili ya uzalishaji wa umeme. Kabla ya kuondoa mifugo katika maeneo hayo, Ofisi ya Makamu wa Rais ilifanya kikao na Wakuu wa Mikoa ya Pwani, Lindi, Mtwara na Ruvuma kuwaomba waainishe maeneo ambayo yanaweza kutumika kupokea mifugo hiyo. Baada ya kikao hicho Wakuu wa Mikoa hiyo walionesha utayari wa kupokea mifugo katika Mikoa yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatua iliyofuata ilikuwa ni kuweka mpango wa matumizi bora ya ardhi ya vijiji ambapo katika Mkoa wa Lindi jumla ya vijiji 69 vilitengeneza mpango wa matumizi bora ya ardhi, na jumla ya Hekta 215,343.34 zilitengwa kwa ajili ya malisho. Serikali pia ilijenga josho na kituo cha kupokea mifugo katika kijiji cha Marendego kilichoko Wilaya ya Kilwa ambapo mifugo ilikuwa inapokelewa na kupatiwa huduma za uogeshaji kabla ya kwenda kwenye vijiji vilivyoandaliwa kupokea mifugo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Sera ya Ugatuaji wa Madaraka, wajibu wa kutoa huduma kwa wafugaji kama vile maji (ujenzi wa mabwawa na malambo) pamoja na majosho ni jukumu la halmashauri husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara iko tayari kushirikiana na halmashauri zenye changamoto kubwa ya ukosefu wa vyanzo vya maji kwa ajili ya mifugo kutegemeana na upatikanaji wa fedha. Katika mwaka 2019/2020, Wizara imepanga kukarabati malambo 6 katika Mikoa ya Manyara, Pwani, Simiyu, Arusha, Geita na Tabora na kuchimba visima virefu 50 katika maeneo yenye mifugo mingi na yaliyotenga maeneo ya malisho ikiwemo Mkoa wa Tunduru-Ruvuma.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Mujibu wa Sheria ya Matumizi Bora ya Ardhi Na. 6 ya Mwaka 2007, vijiji pia vinayo Mamlaka ya kutunga Sheria ndogo ya kusimamia utekelezaji wa mipango waliojipangia. Kwa sababu hiyo basi, vijiji husika vinao uwezo wa kuondoa mifugo katika maeneo ambayo hayakutengwa kwa ajili ya malisho. Hata hivyo, Wizara imeunda timu ya kutatua migogoro kati ya wafugaji na watumiaji wengine wa ardhi. Aidha, Wizara iko tayari kutumia timu hiyo kwenda jimbo la Kilwa Kaskazini ili kushirikiana na halmashauri katika kutatua tatizo hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Bobali swali la nyongeza.

**MHE. HAMIDU H. BOBALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa fursa kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Kwa bahati wakati mifugo inahama inakwenda Mkoa wa Lindi Mheshimiwa Naibu Waziri aliyekuwa anajibu alikuwa Mkuu wa Wilaya kule Kilwa na wakati mwingine akikaimu nafasi ya Mkuu wa Mkoa, kwa hiyo, jambo hili analifahamu vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tatizo lililopo ni kwamba, mifugo iliyokuja wakati ule na leo imekuwa mingi kama ime-*double* kwa hiyo, Mkoa kama wa Lindi umezidiwa na idadi ya mifugo. Swali la msingi Mheshimiwa Mbunge ameuliza kwamba, je, Serikali ipo tayari kuandaa mpango

mwingine wa kuhakikisha mifugo ile inapungua kwa sababu, sasa hivi ukataji wa misitu umekuwa mkubwa kulingana na idadi ya mifugo ambayo tunayo? Kwa hiyo, hilo swali la kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kuna malambo Serikali walijenga katika maeneo haya ya wafugaji, mfano hata pale Jimboni kwangu Mchinga katika eneo la Ktomanga limejengwa lambo kubwa la zaidi ya milioni 300, lakini kwa mwaka wa tatu sasa lambo lile halitumiki kwa sababu tu linahitaji ukarabati wa fedha wa shilingi milioni 22 na kwenye bajeti ya Halmashauri ya mwaka huu ya 19 na 20 tumeomba tupatiwe milioni 22 ili lambo lile lifanyiwe ukarabati na wale wafugaji waweze kupata huduma zao. Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kututhibitishia kwamba, hii milioni 22 wataitoa kwa kuwa ipo kwenye bajeti ili tuweze kutoa huduma kwa wafugaji waliopo maeneo yale? Nashukuru.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mifugo na Uvuvi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MIFUGO NA UVUVI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Bobali, Mbunge wa Mchinga, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kwanza Mkoa wa Lindi umezidiwa na je, Serikali ina mipango gani ya kuhakikisha kuwa inapunguza mifugo ile iliyozidi pale katika Mkoa wa Lindi. Serikali imefanya jitihada kadhaa, moja ya jitihada ni katika kuhakikisha kwamba, wafugaji wanavuna mifugo yao. Katika kuvuna mifugo hii ni pamoja na ile jitihada ya makusudi ya kuanzisha machinjio za kisasa.

Kwa upande wa Mkoa wa Lindi, Lindi Manispaa imejengwa na inaendelea kujengwa machinjio ya kisasa itakayorahisisha na kuwapa fursa wafugaji wetu waweze kuvuna mifugo yao na kwenda kuiuza katika machinjio ile na hatimaye kuweza kupata faida kwa upande wa wafugaji wenyewe, lakini kwa upande wa nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile Serikali inao mpango madhubuti wa kuhakikisha kuwa inaboresha ufugaji huu, ili kusudi kuweza kufanya ufugaji wenye tija. Ufugaji ambao utamfanya mfugaji awe na mifugo michache, lakini yenye kumpa faida kubwa zaidi kuliko kuwa na makundi makubwa ya mifugo ambayo tija yake wakati mwingine inakuwa ni ndogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili Mheshimiwa Bobali ameeleza kuwa liko lambo katika Mji wa Mchinga ambalo lambo lile halitumiki na tayari wameshaliweka katika bajeti. Naomba nimhakikishie kuwa, Mheshimiwa Bobali pindi pesa hizi zitakapopatikana sisi kama Serikali tuko tayari kuboresha huduma za mifugo, hivyo, tutalichukua jambo hili na kulitekeleza.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana, Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Kilimo. Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 19

**Mfereji wa *Muo Irrigation Scheme***

**MHE. ESTER M. MMASI** aliuliza:-

Mfereji wa *Muo Irrigation Scheme (MUU)* ni mradi wa Umwagiliaji uliopata fedha takribani Shilingi milioni 248 mnamo mwaka 2018.

Je, kwa nini Serikali haioni umuhimu wa kukamilisha mradi huu kwa faida ya wakazi wa Old Moshi Mashariki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua umuhimu wa uendelezaji wa Skimu ya Umwagiliaji Muo kwa ajili ya shughuli za kiuchumi kwa wananchi wa *Old Moshi* na Taifa kwa ujumla. Aidha, kwa kuzingatia mahitaji na umuhimu wa uendelezaji wa Skimu ya Umwagiliaji ya Muo Serikali mpaka kufikia mwaka wa fedha 2019/2020 tumeshapeleka jumla ya shilingi milioni 261 kwa ajili ya ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, fedha hizo zilitokana na Mfuko wa *Local Government Capital Development Grant* jumla ya Shilingi za Kitanzania milioni 51 kwa ajili ya kusakafia mfereji mkuu umbali wa mita 200. Mfuko wa Umwagiliaji wa Wilaya *(District Irrigation Development Fund)* jumla ya Shilingi za Kitanzania milioni 200 kwa ajili utandikaji wa mabomba kutoka kwenye chanzo cha maji, progamu ya kuendeleza kilimo wilaya jumla ya shilingi milioni 10 kwa ajili ya kuendeleza utandikaji wa mabomba.

Mheshimiwa Naibu Spika, mpaka sasa kazi zifuatazo zilizokwishatekelezwa ni pamoja na ujenzi wa banio kwenye chanzo cha mfereji mkuu umekamilika. Utandikaji na ufungaji wa mabomba *class B* umbali wa kilometa sita kati ya kilometa nane umekamilika. Ujenzi wa matenki mawili ya kurekebisha msukumo wa maji umekamilika. Ujenzi wa chemba ya kufunika kwenye sehemu ya banio na ujenzi wa mfumo wa hewa katika mabomba umekamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, mwezi Septemba, 2019, Serikali ilituma wataalam wake katika skimu ya Muo kwa lengo la kubaini changamoto zilizopo na kuanisha mikakati na mahitaji ya kuendeleza skimu hiyo. Changamoto zilizobainishwa ni pamoja na kuwepo kwa hitaji jipya la kubadilishwa matumizi ya chanzo cha maji kwa matumizi ya maji ya kunywa badala ya maji ya umwagiliaji na kuwepo ongezeko la shughuli za ujenzi katika skimu hiyo kusababisha kupungua kwa eneo la kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia changamoto hizo Serikali imepanga kuitisha mkutano wa wadau kwa ajili ya kujadili na kupata ufumbuzi wa changamoto hizo. Aidha, baada ya makubaliano ya mkutano wa wadau kuhusu kubadilisha matumizi au la ya chanzo cha maji Serikali itaendelea kutafuta fedha za kibajeti kutoka vyanzo mbalimbali kwa ajili ya uendelezaji wa skimu hiyo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Michael Mmasi, swali la nyongeza.

**MHE. ESTER M. MMASI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Mheshimiwa Naibu Waziri. Hata hivyo, ikumbukwe kwamba, Skimu ya Muo ilipitishwa kwenye bajeti ya mwaka 2009 na mwaka 2010, lakini ni kweli mpaka mwaka 2018 shilingi milioni 261 zilikuwa zimekwishatolewa, lakini haitoshi tunaambiwa kwamba, katika kilometa nane za mraba kilometa sita tayari zilikuwa zimeshasambazwa mabomba yenye mioundombinu ya kiumwagiliaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Waziri atakubaliana na mimi kwenye ile tume waliyoituma Septemba, 2019 ubadhirifu katika mradi ule ulionekana. Nasema hivi kwa sababu moja, watakumbuka kwenye ule mradi mabomba yalitakiwa kufukiwa chini kwa nchi mbili kwenda chini, lakini ukienda kwenye mradi mabomba asilimia 90 yaliyolazwa pale yako juu kabisa yanaonekana na yanapasuliwa na wanyama, yanavuja ni kwamba, umepoteza tija.

Mheshimiwa Naibu Spika, haitoshi. Katika Mradi wa Muo Skimu fedha za Serikali zimetolewa, lakini pia ile Kamati ya Kusimamia Maji ya Kata haikuwahi kuidhinisha mkandarasi alipwe, lakini pamoja na kwamba, Vijiji vyote Suduni, Kikarara, Mahoma na Kidia hawajapata

maji hata kijiji kimoja, lakini mkandarasi alilipwa maji mpaka leo hayajatoka. Swali langu kwa Serikali kwa kuwa, baadhi ya mikoa tumeona wakandarasi wakiwajibishwa, je, ni kwa nini hatuoni umuhimu wa kumwajibisha mkandarasi huyu ambaye mpaka leo ameshindwa kukaa kwenye matakwa ya kimkataba?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili; kwa majibu haya ya Serikali na hasa nikianza kusoma *statement* ya kwanza, *opening statement* ya Mheshimiwa Naibu Waziri anasema, "*Serikali inatambua umuhimu wa uendelezaji wa Skimu ya Umwagiliaji wa Muo*", lakini huku chini tunaambiwa Serikali imefika mahali inaona kuna kila sababu sasa ya ku-*divert* mradi badala ya *Muo Scheme* iende kukidhi haja ya wakulima wa mazao ya migomba wakulima wetu kule Moshi, lakini pia na wale wamama wanaolima mbogamboga tunaona leo tubadilishe mradi tukafanye ni mradi wa kwa ajili ya kukidhi mahitaji ya maji kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukumbuke huu mradi hasa tulipotaka sisi ni kwa ajili ya umwagiliaji, ili kipato cha watu wetu kiweze kuinuka, lakini sasa kwa majibu haya ya Serikali, swali, je, Serikali inataka kutuambia kwa kuwa sisi watu wa Kilimanjaro tumekuwa na meneo madogo basi ni hatupaswi kushiriki kwenye masuala mazima ya kilimo? Kama ni hivyo basi naomba leo tusimame pale mbele tuwambie wananchi wa *Old Moshi* Mashariki kwamba, Serikali imekataa msishiriki kwenye masuala ya kilimo kwa kuwa ardhi yenu ni ndogo. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya nyongeza ya Mheshimiwa Ester Mmasi, Mbunge wa Viti Maalum, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la kwanza la kujua kwamba, ni kwa nini Serikali hatuchukui hatua stahiki kwa mkandarasi ambaye amefanya kazi chini ya kiwango; kwanza nataka nimhakikishie kwamba, Serikali tulishaanza kuchukua hatua ya kwanza kubadilisha huo muundo kwa ajili ya kuweka wakandarasi wa umwagiliaji katika ngazi ya wilaya, lakini pia tulituma tume maalum kwa ajili ya kufanya tathmini ya miradi yote ya umwagiliaji nchini pamoja na mradi huu. Taarifa tayari tunazo na taarifa tumeshazifikisha kwa TAKUKURU kuanza kuchukua hatua kwa wakandarasi wote waliofuja fedha za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili anataka kusema kwamba, kwa nini Serikali sasa tunataka tubadilishe matumizi ya mradi ule kutoka mradi wa umwagiliaji kwenda mradi wa maji ya kunywa. Kwanza nataka nimwambie Mheshimiwa Mbunge sio Serikali wenye nia hiyo, baada ya Serikali kutuma timu ya wataalam kwenda kubainisha mahitaji ya sasa ya ule mradi, hili hitaji limetoka kwa watumiaji wenyewe, watu wa Moshi. Wakasema sasa kwa sasa hivi eneo limepungua sana na nyumba wamejenga mpaka wengine wanakaribia kwenye chanzo ndio maana wanataka kwamba, kubadilisha matumizi badala ya kutumia kilimo cha umwagiliaji wafanye ule mradi kwa ajili ya maji ya kunywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ndio maana kwa hekima ya Serikali tumeamua badala ya kuliamulia tuandae mkutano wa wadau wote ili tukutane kwa pamoja ili tuone sasa kipaumbele cha watu wa hapo ni nini, bado wana nia ya mradi wa umwagiliaji au wanataka maji ya kunywa. Baada ya mkutano ule ndio tutapanga nini cha kufanya kutokana na kipaumbele cha wananchi wenyewe kwa sababu, Serikali hii ni shirikishi, lazima tuwashirikishe wananchi wenyewe katika maamuzi sahihi ya maendeleo yao.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge niwakumbushe tena maswali ya nyongeza yawe mafupi.

Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Buyungu, sasa aulize swali lake.

Na. 20

**Ukarabati wa Skimu ya Umwagiliaji – Kakonko**

**MHE. *ENG.* CHRISTOPHER K. CHIZA** aliuliza:-

Mwaka 2005 Serikali ilikamilisha ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Itumbiko, lakini banio lake limeharibika na kusababisha Skimu nzima kushindwa kufanya kazi; aidha, Serikali kupitia Mfuko wa *Food Aid Counterpart Fund* ilipata shilingi milioni 300 ili kujenga miundombinu ya umwagiliaji katika Kijiji cha Gwanumpu lakini mradi huo hauendelei licha ya kutengenewa fedha za utekelezaji.

(a) Je, lini Serikali itakarabati banio la Skimu ya Umwagiliaji ya Itumbiko ili kuokoa miundombinu inayoendelea kuharibika na kuwasaidia wananchi kuendelea kulima ?

(b) Je, ni kwa nini Serikali imeshindwa kuwasiliana na Mkurungenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kakonko ili kufuatilia fedha za *Food Aid Counterpart Fund* ambazo zimekosa wafuatiliaji?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA)** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Kilimo, napenda kujibu swali la Mheshimiwa *Engineer* Christopher Kajoro Chiza, Mbunge wa Jimbo la Buyungu, lenye sehemu (a) na (b), kama ifuatavyo:-

(a) Mheshimiwa Naibu Spika, Skimu ya Umwagiliaji ya Itumbiko ina jumla ya hekta 230 na inategemewa na wakazi zaidi ya 339. Skimu hiyo imejengwa mara ya kwanza mwaka 2004 kwa fedha kutoka Mfuko wa Maendeleo ya Umwagiliaji Wilaya kwa kiasi cha shilingi milioni 340 ambazo zilitolewa kwa awamu mbili. Aidha, kutokana na uharibifu wa miundombinu uliotokana na mafuriko mwaka 2017/2018 Serikali itatuma wataalam wake kufanya tathmini ya kina ili kubaini athari zilizotokea na kuainisha gharama za ukarabati zinazohitajika kwa ajili ya ukarabati na uendelezaji wa Skimu hiyo ya Itumbiko.

(b) Mheshimiwa Naibu Spika, katika Wilaya ya Kakonko Serikali inatekeleza ujenzi wa Skimu ya Umwagiliaji ya Gwanumpu iliyopo Kijiji cha Gwanumpu, Kata ya Gwanumpu, yenye hekta 139 kwa kushirikiana na Serikali ya Japan, kupitia shirika lake, kupitia Mradi wa *Food Aid Counterpart Fund* kwa gharama ya Sh.358,302,000. Aidha, jumla ya Sh.248,570,000 zimetolewa katika awamu ya kwanza na ya pili na Sh.109,732,000 zitatolewa kutegemeana na utekelezaji wa mradi huo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali kupitia Tume ya Taifa ya Umwagiliaji inafuatilia kwa ukaribu utekelezaji wa ujenzi wa Skimu ya Gwanumpu kwa ushirikiano na Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko. Mwezi Disemba mwaka 2019 wataalam wa Tume ya Taifa ya Umwagiliaji wakishirikiana na wataalam wa Halmashauri ya Wilaya ya Kakonko walipitia upya tathmini ya awali iliyofanyika na kubainisha gharama za ujenzi kwa wakati huu na kuziwasilisha katika shirika la *Food Aid Counterpart Fund* kwa ajili ya kupata fedha za ujenzi huo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa *Engineer* Christopher Chiza, swali la nyongeza.

**MHE. *ENG.* CHRISTOPHER K. CHIZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nina kila sababu za kuishukuru Serikali si kwa majibu tu, lakini kwa utekelezaji wa vitendo. Kwa mfano katika Skimu ya Itumbiko, Mkurugenzi Mtendaji wa Wilaya ya Kakonko, Ndugu Masumbuko, ameshirikiana sana

na wananchi na mimi mwenyewe na tayari maji yameanza sasa kuingia katika mfereji mkuu na banio limetengenezwa, lakini bado tunahitaji miundombinu mingine ikiwemo barabara za kutoa mazao mashambani zitengenezwe.

Pia nashukuru Tume ya Umwagiliaji imenipa taarifa kwamba, shilingi milioni 109 kutoka *Food Aid Counterpart Fund* zimepatikana kwa ajili ya kutekeleza Mradi wa Umwagiliaji wa Gwanumpu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa hiyo, nina swali moja tu la nyongeza; kwa kuwa, wakati tunaanzisha miradi hii ya Itumbiko na Gwanumpu kwenye *package* hiyo tulikuwa na Mradi wa Umwagiliaji wa Nyamtukuza ambao uko katika mpaka wa Wilaya ya Kakonko na Ngara na mradi huu ulitarajiwa kunufaisha Kata za Kumbuga katika Wilaya ya Ngara na Kata ya Nyamtukuza katika Wilaya ya Kakonko na tayari Serikali imeshaweka fedha nyingi, lakini mradi umetelekezwa hautekelezwi na sababu zinazotolewa hazitoshelezi kwa sababu ni zile za mabishano tu kwamba, nani autekeleze, ni Ngara au Kakonko? Ni Kagera au ni Kigoma? Je, Mheshimiwa Naibu Waziri yuko tayari sasa kuingilia kati ili mradi huu nao utengewe fedha ili utekelezwe na wananchi wa Ngara na wa Kakonko waweze kunufaika na mradi huu?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa kilimo, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA KILIMO (MHE. OMARY T. MGUMBA):** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana. Napenda kujibu swali moja la nyongeza la Mheshimiwa Christopher Chiza, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nichukue nafasi hii kwa niaba ya Serikali, tunampongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa juhudi zake kutekeleza miradi hii. Alitenga fedha za Jimbo kwa ajili ya kushirikiana na wananchi wake kusaidiana na Serikali kuendeleza skimu hii aliyoisema.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili kwenye swali lake la msingi nataka nimweleze kwamba, niko tayari kuingilia kati kwa sababu, nia ya Serikali ni kupeleka maendeleo kwa wananchi wake, mradi cha muhimu kwamba, watu wa Kagera ni Watanzania, watu wa Kigoma ni Watanzania, ilimradi mradi huu tuumalize kwa wakati upeleke maendeleo kwa wananchi wetu na waweze kunufaika na Serikali yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini la mwisho, sio kwa umuhimu, nataka nimwombe Mheshimiwa Mbunge, hela kama alivyosema ziko tayari, lakini kuna changamoto ndogo tu kutoka wale viongozi wa skimu, waharakishe mchakato ule wa kupata watia saini, ili hela zile ziweze kuingizwa kwenye akaunti yao haraka iwezekanavyo.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, Mbunge wa Viti Maalum, sasa aulize swali lake.

Na. 21

**Kukipa Usajili wa Kudumu Chuo Cha *VETA* – Karatu**

**MHE. CECILIA D. PARESSO** aliuliza:-

Wilaya ya Karatu ilipata mfadhili wa kujenga Chuo cha *VETA* na ujenzi umekamilika toka mwaka 2017 na tayari majengo yote yamekabidhiwa kwa Halmashauri.

Je, ni lini sasa Serikali itakipa Chuo hicho usajili wa kudumu pamoja na mahitaji mengine kama ilivyo katika vyuo vingine?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia, majibu.

**NAIBU WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Tekonolojia, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, vyuo vinavyotoa mafunzo ya ufundi stadi nchini husajiliwa kupitia Mamlaka ya Elimu na Mafunzo ya Ufundi Stadi *(VETA)*. Utaratibu wa kuomba usajili huhusisha kujaza fomu inayopatikana katika tovuti ya *VETA* na kwenye Ofisi zote za Kanda za *VETA*. Ofisi za kanda hukagua vyuo vilivyoomba na kupewa usajili wa awali *(Preliminary Registration)*. Hii ni hatua ya mwanzo kuelekea kupata usajili kamili.

Mheshimiwa Naibu Spika, usajili kamili hutolewa baada ya kufanyiwa tathmini ambayo inahusisha kutimiza vigezo ambavyo ni chuo kuwa na mfumo wa uendeshaji unaosimamiwa na Bodi ya Wakurugenzi au ya Wadhamini pamoja na menejimenti yenye sifa stahiki za kitaaluma. Chuo kuwa na miundombinu stahiki kwa mujibu wa viwango na vigezo vilivyowekwa. Chuo kuwa na vifaa na mitambo ya kufundishia kwa mujibu wa vigezo vilivyowekwa na chuo kuwa na Walimu wenye sifa stahiki za kitaaluma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Tarehe 26 Novemba mwaka 2019, Chuo cha VETA Karatu kilipewa fomu ya kujitathmini ili kijaze na kuwasilisha ofisi za VETA Kanda ya Kaskazini kwa ajili ya kufanyiwa ukaguzi wa mwisho ili kipate Usajili Kamili yaani *Full Registration* kwa mujibu wa taratibu za usajili. Hata hivyo, Halmashauri ya Wilaya ya Karatu haijarejesha fomu hii, ili iweze kupatiwa usajili wa kudumu na kuanza kudahili wanafunzi.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Cecilia Daniel Paresso swali la nyongeza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi niweze kuuliza maswali mawili ya nyongeza, kwa kuwa Sera ya Elimu ni kuwa na VETA katika kila Wilaya na kwa kuwa Wilaya ya Karatu tumeshaonesha mfano huo wa kuwa na VETA kupitia Wafadhili wetu na ni ukweli kwamba kutokana na mapato ya ndani ya halmashauri siyo rahisi kukiendesha Chuo hiki Je, Serikali sasa iko tayari kukichukua Chuo hiki na kukiendesha?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kwa kuwa Wafadhili hao mpaka sasa wanaendelea kutoa fedha za uendeshaji na wanaendelea kujenga baadhi ya miundombinu, na kwa kuwa wanaweza kukoma wakati wowote Je, Serikali sasa kupitia Wizara iko tayari katika Bajeti ya mwaka unaokuja 2020/2021 kutenga fedha kwa ajili ya uendeshaji wa Chuo hiki?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ni kweli kama anavyosema Mheshimiwa Mbunge kwamba inawezekana kabisa kwamba katika mazingira ambayo halmashauri au basi Mamlaka ya Serikali za Mitaa inashindwa kuendesha VETA kuna uwezekano mkubwa wa halmashauri hiyo kuweza kuipa VETA na VETA ikaweza ikabeba majukumu yote ya uendeshaji pamoja na gharama zote ambazo zinahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wangu ni kwamba kama Halmashauri ya Karatu inaona kwamba kwa sasa haiwezi kuendesha Chuo hiko kikamilifu na kutimiza malengo yake kinaweza kikaomba VETA iweze kuimiliki na hivyo kuiendesha moja kwa moja na kuondoa changamoto ambazo wanazipata.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili kuhusu kwamba kama inawezekana fedha zikatengwa katika Bajeti inayokuja kwa ajili ya Chuo hiko baada ya wafadhili kuanza kushindwa

kumalizia. Ushauri wangu ni kwamba ni vigumu kwa sasa VETA au Wizara kuipangia fedha kwa sababu inachukuliwa kwamba bado ni Chuo cha Serikali za Mitaa katika maana kwamba bado ni Chuo cha halmashauri kwa hiyo wakitaka fedha zitengwe na Serikali Kuu ni lazima kwanza waanze utaratibu ule wa kuipeleka VETA.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga Mbunge wa Mlimba sasa aulize swali lake.

Na. 22

**Hitaji La Chuo cha Ufundi Mlimba**

**MHE. SUSAN L. KIWANGA** aliuliza:-

Jimbo la Mlimba lina wahitimu wengi wa Shule za Msingi na Sekondari ambao wanabaki majumbani kila mwaka:-

Je, ni lini Serikali itajenga Chuo cha Ufundi ili vijana hao waweze kupata Ufundi Stadi ili wajiajiri?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia naomba kujibu swali la Mheshimiwa Susan Limbweni Kiwanga Mbunge wa Mlimba kama ifuatavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali inatambua uhitaji wa Vyuo vya Ufundi Stadi katika kuendeleza vijana wake ili waweze kushiriki kikamilifu katika harakati za maendeleo ya nchi yao. Katika kutimiza lengo hili, Serikali imejiwekea mkakati madhubuti wa kuendeleza elimu ya ufundi katika ngazi mbalimbali. Hivyo, Serikali inaendelea na juhudi za kutafuta fedha kwa ajili ya kujenga Vyuo hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kutekeleza mkakati huu wa kuendeleza elimu ya ufundi, Serikali imejipanga kuhakikisha kuwa kila wilaya na mkoa unakuwa na chuo cha ufundi stadi ili kupanua fursa kwa vijana wetu. Kwa mwaka wa fedha 2019/2020, Serikali kwa kupitia Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatumia shilingi bilioni 40 kujenga vyuo 25 vya VETA katika ngazi ya Wilaya ambapo sasa hivi vipo katika hatua mbalimbali za ujenzi. Aidha, kwa Jimbo la Mlimba na wilaya nyingine, Serikali inafanya juhudi ya kutafuta fedha kwa ajili ya kuhakikisha mkakati wa kuwa na VETA kila Wilaya unakamilika.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Susan Kiwanga swali la nyongeza.

**MHE. SUSAN L. KIWANGA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante majibu ya Waziri ni kama vile ya kukopi na ku-*paste* sasa nimeuliza swali kama Mbunge wa Halmashauri ya Mlimba pamoja na kuwa kuna halmashauri nyingine zimeshaanza kupata hizo hela na zinajengwa lakini kila mtu analia na pale panapo mbana. Sasa Halmashauri ya Mlimba yaani kwa miaka mitatu mfululizo wanafunzi waliomaliza Kidato cha Nne takribani milioni nne laki nane na themanini na saba wako mtaani ukiachilia mbali wa darasa la saba. Sasa na pale Mlimba katika Kituo cha Mpanga Utengule kuna majengo kabisa yapo kwa hiyo Serikali haiwezi kuwa na gharama kubwa kwenda kujenga majengo mengi.

Je, kwa nini Serikali isiende kwenye Kituo hiko cha Mpanga kwenda kukiboresha ili wanafunzi hao wanaozagaa mtaani waanze pale baada ya kujenga majengo makubwa hayo tunayosubiri kwa miaka mingi na watoto wanazidi kupotelea mtaani? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, je, Serikali ina mpango gani sasa wa kuboresha hizo Shule za Sekondari au za Msingi kuwepo na Kitengo cha Ufundi ili hawa wanafunzi hata kama wakifeli kuingia darasa la juu wawe tayari wamepata miundombinu ya kiufundi katika maeneo haya katika Shule zote Tanzania? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Elimu, Sayansi na Teknolojia majibu.

**NAIBU WAZIRI WA ELIMU, SAYANSI NA TEKNOLOJIA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza kuhusu kama jibu langu ni la kukata na kupaka yaani *cut and paste* naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba hata swali ambalo ameniuliza nalo siyo jipya sana linaulizwa mara nyingi kwa hiyo majibu yanakuwa ni yale yale siyo kwamba lenyewe ndiyo limeanza kuulizwa leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuhusiana kama inawezekana Serikali kutoa fedha ili kuendeleza Kituo ambacho tayari kipo ili kiwe Chuo cha VETA naomba tu nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba kama kuna Taasisi ambayo tayari inatumika na inaonekana inafaa kuwa VETA bila kuvunja matumizi au kuondoa matumizi ya sasa Serikali iko tayari kufikiria lakini ni baada vilevile ya kufanya tathmini ya kuhakikisha kuwa inafaa kwa ajili ya kuachwa Chuo cha VETA.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake kuhusu Serikali kuboresha au kuanzisha mafunzo ya Ufundi katika Shule zote naomba nimuhakikishie Mheshimiwa Mbunge kwamba tayari kuna Mpango madhubuti wa kuboresha baadhi ya Shule zetu za Ufundi lakini kwa sasa jitihada kubwa tunaweka katika kuanzisha Vyuo vya VETA kila Wilaya kuliko kila Shule ya Sekondari kuwa Shule ya Ufundi kwa sababu vilevile ina mahitaji makubwa hasa ikichukuliwa kwamba tunahitaji kuwa na Walimu wa kutosha.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa tunaendelea na Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Mheshimiwa Richard Philip Mbogo Mbunge wa Nsimbo sasa aulize swali lake.

Na. 23

**Hitaji la Huduma za Madaktari Bingwa - Katavi**

**MHE. RICHARD P. MBOGO** aliuliza:-

Huduma za matibabu ya madaktari bingwa zipo katika kanda zote isipokuwa kanda za Magharibi na Kusini:-

Je, ni lini Serikali itapeleka huduma hizo Mkoani Katavi ili kusaidia wananchi wa Kanda ya Magharibi?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**NAIBU WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto naomba kujibu swali la Mheshimiwa Richard Philip Mbogo Mbunge wa Nsimbo kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Hospitali ya Mkoa wa Katavi kuna uhitaji wa Madaktari bingwa 24 kulingana na ikama na kwa sasa kuna Madaktari Bingwa wawili. Madaktari hao ni Madaktari

bingwa wa Watoto na Wanawake. Ili kukabiliana na changamoto hii, Serikali imepanua wigo wa mafunzo kwa ajili ya Madaktari bingwa. Lengo la Serikali ni kuwa na Madaktari bingwa angalau wawili wawili katika fani za magonjwa ya kina mama, watoto, magonjwa ya dharura, mifupa, usingizi na upasuaji. Wataalamu hawa watakapomaliza mafunzo watapangiwa katika Hospitali za Rufaa za Mikoa ikiwa ni pamoja na Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha, Serikali ina kusudio la kujenga Hospitali ya Kanda ya Magharibi Mkoani Tabora ambayo inategemewa kuhudumia wakazi wa Mikoa ya Rukwa, Katavi, Tabora pamoja na Kigoma.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Richard Mbogo swali la nyongeza.

**MHE. RICHARD P. MBOGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa majibu ya Serikali lakini pia naomba nipongeze Serikali wakati wa ziara ya Mheshimiwa Rais mwaka jana mwezi wa kumi Mkoa wa Katavi Mheshimiwa Waziri mwenye dhamana Mheshimiwa Ummy aliweza kukagua Hospitali tunayojenga ya Mkoa na kuongeza fedha za ujenzi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ningependa kupata majibu ya Serikali je, ni lini tena ujenzi wa Hospitali yetu ya Mkoa wataongeza fedha ili kuweza kuikamilisha kwa wakati na huduma ziweze kupatikana kwa wananchi wa Mkoa wa Katavi? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, ili kuipunguzia mzigo Hospitali yetu ya Mkoa ambayo inajengwa na kwa msingi tunahitaji Ujenzi wa Vituo vya Afya viongezeke kwa maeneo ya mbali ili kusogeza huduma kwa wananchi wetu hususani Kata ya Ugala ambayo ni km 80 kutoka Mpanda Mjini.

Je, ni lini Serikali tena itatuongezea fedha ili tuweze kufanya ujenzi wa Kituo cha Afya kwenye Kata ya Ugala? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Waziri wa Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto majibu.

**WAZIRI WA AFYA, MAENDELEO YA JAMII, JINSIA, WAZEE NA WATOTO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana napenda kujibu swali la Mheshimiwa Richard Mbogo Mbunge wa Nsimbo, swali la kwanza ni lini tutakamilisha ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Mkoa!

Mheshimiwa Naibu Spika, nimthibitishie Mheshimiwa Mbogo lakini na Wabunge wote wa kutoka Katavi mwezi huu tumeongeza shilingi bilioni nukta moja kwa ajili ya kuendelea na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa ya Katavi na timu yangu ilikuwa kule Katavi Mpanda na ni matarajio yetu kabla ya mwezi wa sita tutakuwa tumemaliza Jengo la OPD, Jengo la *Maternity* pamoja na maabara ili tuweze kutoa huduma kwa wakazi wa Mkoa wa Katavi.

Mheshimiwa Naibu Spika, swali lake la pili kuhusu ujenzi wa Kituo cha Afya ni Sera yetu ya Afya kuhakikisha kwamba tunajenga Vituo vya Afya, Zahanati na Hospitali za Halmashauri. Lakini tunataka kubadilisha kidogo Sera, Sera ya Afya ambayo tunaiandika sasa hivi tunasema Serikali itajenga Miundombinu ya kutoa huduma za Afya katika ngazi zote kwa kuzingatia vigezo vikubwa vitatu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kigezo cha kwanza Jiografia ya eneo husika, kigezo cha pili, idadi ya watu na kigezo cha tatu ni mzigo wa magonjwa katika eneo husika. Kwa hiyo, Mheshimiwa Mbogo nakubaliana na wewe Kituo cha Afya kwa sababu eneo lako liko mbali na Kituo cha Afya ambacho kipo kwa hiyo tutakuweka katika vipaumbele vyetu kuhakikisha tunajenga Kituo cha Afya kwa kushirikiana na wenzetu wa Ofisi ya Rais TAMISEMI. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Waheshimiwa wabunge tunaendelea na Wizara ya Viwanda na Biashara Mheshimiwa Catherine Valentine Magige Mbunge wa Viti Maalum sasa aulize swali lake.

Na. 24

**Kulinda Biashara za Wazalishaji wa Ndani**

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE** aliuliza:-

Je, Serikali ina mkakati gani wa kulinda biashara za wazalishaji wa ndani ili kuwajengea uwezo kuelekea uchumi wa Viwanda?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Viwanda na Biashara naomba kujibu swali la Mheshimiwa Catherine Valentine Magige, Mbunge wa Viti Maalum kama ifuatavyo:-

Mheshimwia Naibu Spika, katika kuhakikisha biashara za wazalishaji wa ndani zinalindwa, Serikali imeweka mikakati mbalimbali ya Kisera, Kisheria na Kiutendaji. Mikakati hiyo ni pamoja na kuwawekea mazingira wezeshi wafanyabiashara wa ndani ili waweze kuzalisha bidhaa zenye ushindani katika soko; kuandaa na kutekeleza Mpango wa Kuboresha Mfumo wa Udhibiti wa Biashara Nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kutoza kodi kwenye bidhaa zinazoingia nchini katika kiwango cha asilimia 10 kwa bidhaa ghafi na asilimia 25 kwa bidhaa zilizo tayari kutumiwa na mlaji. Aidha, viwango hivyo vinaweza kutozwa asilimia zaidi ya 25 kulingana na umuhimu wa bidhaa ili kulinda viwanda vya ndani. Kwa mfano, katika mwaka 2018/2019, Serikali iliongeza kodi kwenye mafuta ya kupikia yanayoingizwa nchini na kuweka vibali na leseni za udhibiti na usimamizi kwa baadhi ya bidhaa zinazoagizwa kutoka nje ya nchi kama vile vibali vya kuagiza sukari, mtindi, mitumba na magunia au viroba vinavyotumika kufungashia bidhaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa upande wa marumaru, utafiti uliofanywa na Wizara ya Viwanda na Biashara kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania ulipendekeza Kiwango cha Ushuru wa Forodha kwa marumaru zinazoingizwa kutoka nje ya nchi kiongezwe kutoka asilimia 25 na sasa hadi kufikia asilimia 35. Dhumuni kuu la kuongeza ushuru huo ni kuongeza tofauti ya bei ili kuvilinda viwanda vya ndani dhidi ya bidhaa zinazotoka nje ya Jumuiya ya Afrika Mashariki na Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika.

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali imeendelea kuimarisha Vituo vya Pamoja Mipakani yaani *One Stop Border Post* katika maeneo ya kuingiza bidhaa nchini. Aidha, udhibiti na ukaguzi umeimarishwa katika Viwanja vya Ndege na Bandari ili kudhibiti bidhaa za magendo, bidhaa hafifu na bandia kuingizwa nchini.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Catherine Magige swali la nyongeza.

**MHE. CATHERINE V. MAGIGE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru pamoja na majibu mazuri ya Mheshimiwa Naibu Waziri, nina maswali madogo mawili ya nyongeza, kwa kuwa hivi karibuni kumekuwa na malalamiko ya Viwanda vya ndani kukosa masoko kikiwemo na Kiwanda cha marumaru. Je, nini Mkakati wa Serikali kuhakikisha Viwanda vya ndani vinapata masoko ya uhakika? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, kwa kuwa kumekuwa na malalamiko ya bidhaa nyingi zisizo na ubora kuingizwa katika Nchi yetu. Je, ni nini Mkakati wa Serikali kuhakikisha bidhaa ambazo hazina ubora yaani bidhaa feki hazingii katika nchi yetu? *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara majibu.

**NAIBU WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika kuhakikisha kwamba Viwanda vya ndani vinapata masoko ya uhakika ikiwemo hivi vya marumaru kama ambavyo umesema ni kweli kabisa kama ambavyo nimejibu kwenye jibu la msingi ni kwamba marumaru zinazozalishwa nchini sasa hivi ni takribani mita za mraba 32.4 milioni na matumizi yetu ni takribani mita za mraba 30 milioni lakini unakuta bado ni kwamba bidhaa kama hizo zimeendelea kuingia toka nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kutokana na kwamba Viwanda hivi vinatumia malighafi takribani asilimia 95 ambazo zinapatikana hapa nchini kimsingi tunastahili kuvilinda ili viweze kuhakikisha kwamba vinapata masoko.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ni kama ambavyo nimesema kwamba tutaongeza Kodi kwa hizo bidhaa zinazotoka nje ili kuhakikisha kwamba hizi za ndani zinakuwa na bei yenye ushindani. Hata hivyo, napenda kutoa angalizo kwa wenye Viwanda hivyo pamoja na wenye Viwanda wengine, si tu kwamba kwa sababu Serikali imeamua kuongeza Kodi kwenye hizo bidhaa wao sasa wakae tu bila kufanya majukumu yao ya msingi ikiwemo kuandaa *business strategies* nzuri na *marketing strategies* ili kuweza kuwafahamisha watumiaji juu ya ubora wa bidhaa zao ili hayo hatuyaendekeza sana kwa sababu tungependa pia walaji wapate bidhaa zilizo nzuri na wanazozitaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, vilevile kuhusu bidhaa feki kupitia *TBS*, *TBS* imeendelea kufanya ukaguzi kwa bidhaa zote zinazotoka nje ya nchi na hata zile za ndani kwa mfano kuanzia mwaka 2015 mpaka sasa ni kwamba jumla ya sampuli sabini na nne elfu mia sita tisini na saba zimefanyika na kuzitambua bidhaa ambazo zimefikia viwango vinavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, kwa bidhaa zinazotoka nje zinakaguliwa kutoka huko nje kabla hazijaingizwa na hata zikitokea kwamba hazikukaguliwa nje tunakagua hapa nchini.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe watanzania kuzingatia Viwango ambavyo vinastahili. Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Mheshimiwa Waziri wa Viwanda na Biashara majibu.

**WAZIRI WA VIWANDA NA BIASHARA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa nafasi hii, kwanza nimpongeze Mheshimiwa Naibu Waziri kwa majibu mazuri lakini pia nimpongeze Mheshimiwa Catherine Magige kwa swali zuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika na Waheshimiwa Wabunge, mkakati wa Serikali sio tu kulinda viwanda vya ndani, lakini pia mkakati wa Serikali ni kusaidia viwanda vya ndani na wafanyabishara waweze kufanya biashara nje ya nchi, ndani ya *SADC*, Jumuiya ya Afrika na hivi sasa tunafanya uchambuzi wa kuhakikisha nchi yetu inajiandaa vizuri na Soko la Pamoja la Afrika yaani *Africa Continental Free Trade Area*.

Kwa hiyo mpango wa *Blue Print,* hivi sasa Serikali tumeanda Muswada kwa ajili ya kuja hapa Bungeni, Muswada ambao utasaidia kuweka mazingira ya kirafiki kwa Watanzania kufanya biashara si tu ndani lakini kwenye bara la Afrika na maeneo mengine ya dunia.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo mkakati wetu ni kulinda viwanda vya ndani lakini pia kuvipa fursa ya kufanya biashara za kimataifa. Nashukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Kuvipa fursa kufanya biashara za kimataifa lakini pia biashara ndani ya nchi kwa kuzingatia hivyo hivyo vigezo, maana sisi wenyewe tukiwa tunataka matumizi ya maeneo yetu yatumie bidhaa za nje maana yake hatuzitaki za ndani. Sasa nje zitakubalikaje kama sisi wenyewe hatuzikubali. Kwa hiyo tuweke viwango vya juu hata sisi tuweze kuzitumia bidhaa hizo hizo.

Wizara ya Maliasili na Utalii, Mheshimiwa Zuberi Mohamed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, sasa aulize swali lake.

Na. 25

**Lango la Utalii wa Picha – Pori la Akiba Selous**

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA** aliuliza:-

Mwelekeo wa Serikali kwa sasa ni kuimarisha utalii wa picha badala ya utalii wa uwindaji kwenye Mapori yetu ya Akiba nchini: -

Je, Serikali haioni umuhimu wa kuwa na lango la utalii wa picha kwenye Pori la Akiba la Selous kwenye Ukanda wa Kusini kwenye Wilaya za Tunduru na Liwale?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII** alijibu:-

Mheshimiwa Naibu Spika**,** naomba kujibu swali la Mheshimiwa Zuberi Mohammed Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Niabu Spika, Serikali ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Mheshimiwa Dkt. John Joseph Pombe Magufuli, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa kupitia Wizara ya Maliasili na Utalii imendelea na jitihada za kupanua wigo wa mazao ya utalii kulingana na rasilimali zilizopo. Mazao hayo ni pamoja na utalii wa uwindaji, utalii wa picha, utalii wa utamaduni na utalii wa fukwe na namna ambayo itanufaisha Taifa na Watanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika utekelezaji wa azma hiyo, tarehe 26 Julai, 2019, Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mhe. Dkt. John Joseph Pombe Magufuli akiwa katika ziara yake ya kikazi kwenye uzinduzi wa Mradi wa Kufua Umeme wa Maji wa Nyerere, alitoa maelekezo kwa Wizara ya Maliasili na Utalii kuwa sehemu ya Pori la Akiba Selous ipandishwe hadhi kwa kuanzisha Hifadhi Taifa Nyerere. Azimio la kuanzisha Hifadhi ya Taifa Nyerere lilipitishwa na Bunge lako Tukufu kwenye kikao cha tarehe 9 Septemba, 2019 na kuridhiwa na Mheshimiwa Rais kwa *GN. No.* 923 ya mwaka 2019. Kwa mujibu wa Sheria, shughuli za utalii zinazoruhusiwa kwenye hifadhi za Taifa ni zile za kuangalia na kupiga picha tu na uwindaji hauruhusiwi.

Mheshimiwa Spika, napenda kumfahamisha Mheshimiwa Mbunge kuwa, kufuatia kuanzishwa kwa Hifadhi ya Taifa Nyerere, Wilaya za Tunduru na Liwale ni miongoni mwa wilaya zitakazonufaika na fursa za moja kwa moja za utalii wa picha katika maeneo hayo. Aidha, tathmini itafanyika ili kuona sehemu ya kuweka lango la kuingilia katika Hifadhi ya Taifa ya Nyerere itaweza kuwekwa kuendeleza utalii.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Zuberi Kuchauka, swali la nyongeza.

**MHE. ZUBERI M. KUCHAUKA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ya kuuliza maswali mawili ya nyongeza. Awali ya yote, niishukuru Serikali kwa kuliona hili na kupandisha hadhi Hifadhi ya Selous, lakini baada ya kupandisha hadhi au baada ya Serikali kuimarisha uhifadhi katika hifadhi zetu suala la wanyamapori limekuwa ni shida sasa hivi, hasa wanyama kama tembo. Wanyama hawa sasa hivi wanasumbua kwenye maeneo yetu na niliuliza swali hapa kuhusiana na Serikali kuleta Muswada pengine kupata fidia wakasema haiwezekani, lakini bado suala la kifuta machozi hakipatikani. Je, Serikali ipo tayari kutupatia fedha hizi mapema iwezekanavyo?

Mheshimiwa Naibu Spika, Wizara ya Maliasili inapozungumzia utalii Kanda ya Kusini, bado napata changamoto. Mwaka jana tumepata fedha kuendeleza utalii Kanda ya Kusini, lakini Wizara hii inapozungumzia Kanda Kusini wanazungumzia Morogoro, Mbeya na Iringa, lakini Mkoa wa Lindi, Mtwara na Songea hautajwi. Je, Serikali kwa upande wake inapozungumzia kukuza utalii ukanda wa kusini unaamanisha mikoa ipi? Ahsante sana.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri Maliasili na Utalii, majibu.

**NAIBU WAZIRI MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Kuchauka, Mbunge wa Liwale, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza naomba kumpongeza sana Mheshimiwa Mbunge kwa namna ambavyo amekuwa akifuatia haki za wananchi wake hasa wanaoathirika na matatizo ya kuharibiwa kwa mali zao na kuhatarisha usalama wao na wanyama waharibifu kama tembo. Nilifanya naye ziara kwenye jimbo lake na tulifanya mikutano takriban mitatu na tulizungumza na wananchi hasa kwenye mgogoro wao wa mpaka na Selous.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni kweli kwamba tuliahidi hapa tutaleta marekebisho ya kanuni, kanuni zipo lakini Wizara yetu inazipitia upya ili kanuni hizo zinapokwenda kulipa fidia hiyo fidia iwe angalau na thamani kulingana na uharibifu uliofanywa kwa sababu zimekuwa za muda mrefu. Kanuni hizo zimekuwa ziko tayari na Mheshimiwa Waziri hivi karibuni alikuwa amealika wadau kuzipitia na mara baada ya wadau kupitia, tutazitangaza na zitaanza kutumia. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge ni kweli awali zilikuwa malipo yake ni kidogo, lakini tumezipita.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kuchelewa kwa kifuta jasho suala hili linahusisha taratibu na taratibu zinaanzia kwenye halmashauri yenyewe kwenye vijiji. Wataalam wetu wa vijiji wa kilimo wanapaswa kulifanya suala hili kwa haraka kwa kulipeleka kwa Afisa Wanyamapori wa Wilaya na baadaye linafika kwenye *level* yetu ya Wizara na kwa sababu ni la nchi zima, mara nyingi tumekuwa tukiangalia *first in, first out*. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, ni suala la utalii kusini, ni kweli imekuwepo tafsiri kwamba unaposema utalii kusini unamaanisha Lindi, Ruvuma na Mtwara, lakini tunapozungumzia kwenye Mradi wa *REGROW* ni utalii wa Nyanda za Juu Kusini. Sasa hivi Wizara yetu ipo katika hatua za mwisho za kuandaa utaratibu ambao tutafanya mkutano tena kama tulivyofanya na watu wa Nyanda za Juu Kusini ili kufungua utalii wa kusini kwa maana ya Mikoa ya Lindi, Mtwara na Ruvuma. Kwa hiyo nimwondoe wasiwasi Mheshimiwa Mbunge hatujasahau eneo hili, tunalifanyia kazi na Wizara inashirikisha wataalam kutoka vyuo vikuu mbalimbali katika kuangalia maeneo ambayo yanaweza kutuletea mafanikio ya haraka ikiwa ni pamoja na kufungua milango ya mikoa hii yote ambayo inapakana na bahari na hasa katika maeneo ambayo tuna mali kale nyingi kama maeneo ya Mikindani na Kilwa. Nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tumalizie, Mheshimimwa Waziri kwa kifupi.

**WAZIRI WA MALIASILI NA UTALII:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Pamoja na majibu mazuri na Mheshimiwa Naibu Waziri, napenda kuongezea majibu kwenye sehemu ya swali la Mheshimiwa Zuberi Kuchauka kwamba tunapozungumzia utalii Kanda ya Kusini, hatuzungumzii utalii wa Kanda ya Kusini ambayo ipo kwenye nyanda ya juu peke yake, tunazungumzia kusini kwa ujumla wake. Mradi wa *REGROW* pamoja na ku-*include* na pori la Akiba la Selous la zamani na sasa Nyerere *National Park* ambayo ipo kusini *proper* huku lakini pia imejikita kutengeneza Mji wa Iringa kama kama *hub* ya utalii, lakini mradi huu upo kwenye awamu hii ya kwanza awamu ya pili utatanua maeneo zaidi kwenye upande wa Kanda ya Kusini upande huo wa akina Mheshimiwa Zuberi Kuchauka.

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo kuna miradi mingine mikubwa inayoendelea kule ikiwepo Mradi wa *SECAD* lakini pia ikiwemo mradi wa kukifanya Kisiwa cha Kilwa Kisiwani ile malikale iliyopo pale kama kivutio cha kipekee. Pale tumewaelekeza *TAWA* ambao kwa sasa tumewapa dhamana ya kuwaendeleza utalii kwenye eneo hili Kilwa Kisiwani, wanunue boti ya kitalii ambayo itakuwa ya *first class* na *business class,* lakini pia wawekeze kwenye *lodge* ya kitalii ambayo itakuwepo katika eneo hilo la kisiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kuna mradi mkubwa utakuja pale kama wananchi watatoa ushirikiano, kuna zaidi ya trilioni moja itawekezwa pale katika eneo la fukwe zilizopo pale kusini kuanzia Kilwa mpaka Msimbati na hivyo tunaamini utalii wa fukwe unaweza ukakua kwa kiasi kikubwa sana katika eneo lile kama wananchi watatoa ushirikiano ili tuweze kuilinganisha Hifadhi ya Taifa ya Nyerere na fukwe zilizopo pale kusini. Ahsante.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante. Wizara ya Mambo ya Ndani ya Nchi, Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge wa Temeke, sasa alize swali lake.

Na. 26

**Kukarabati Gereza la Keko**

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA** aliuliza:-

Je, Serikali ina mpango gani wa kukarabati gereza la Keko ambalo miundo mbinu yake imechakaa sana?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI** alijibu: -

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, napenda kujibu swali la Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, Mbunge Wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Gereza la Keko ni moja ya magereza yaliyojengwa wakati wa mkoloni, hivyo hata miundombinu yake imekuwa ni ya muda mrefu inayohitaji ukarabati. Hata hivyo, Serikali imekuwa ikifanya jitahada za ukarabati kulingana na fedha inavyopatikana.

Mheshimiwa Naibu Spika, aidha katika mwaka wa fedha 2016/2017, Serikali ilifanya ukarabati wa mfumo wa maji taka kwa kuchimba mashimo ya kuhifadhia majitaka baada ya mashimo yaliyokuwepo kuzidiwa kutokana na idadi kubwa ya wahalifu waliomo ndani ya gereza hilo.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Abdallah Ally Mtolea, swali la nyongeza.

**MHE. ABDALLAH A. MTOLEA:** Mheshimiwa Naibu Spika, swali hili naliuliza kwa mara ya pili, niliuliza kwa mara kwanza kwama 2016 na Serikali kweli ni sikivu ilifanya ukarabati mdogo mwaka 2016/2017. Hata hivyo, ukarabati huo haukumaliza tatizo kwa sababu bado maji taka yanachirizika kutoka gerezani kwenda kwenye makazi ya watu na ni hatari zaidi kwa kipindi hiki cha mvua ambayo maeneo hayo mengi yamefurika na maji ya mvua. Kwa hiyo kuna hatari kubwa ya kutokeza magonjwa ya mlipuko.

Je, Serikali ipo tayari sasa kama hatuwezi kujenga mashimo ya kutosha basi tuzibe zile njia zisitiririshe maji kwenda kwenye makazi ya wananchi?

Mheshimiwa Naibu Spika, swali la pili, gereza hili ni gereza *VIP* ni gereza ambalo limejengwa kwa upekee sana ukifananisha na magereza mengine, ndio maana huhifadhiwa watu maarufu au wenye kesi kubwa kubwa, je, Serikali haioni kuna haja sasa ya kulitazama gereza hili kwa jicho lingine ili watenge fedha za kutosha kwa ajili ya kufanya ukarabati wa gereza lote kwa pamoja?

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Naibu Waziri wa Mambo ya Ndani ya Nchi, majibu.

**NAIBU WAZIRI WA MAMBO YA NDANI YA NCHI:** Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kujibu maswali mawili ya Mheshimiwa Mtolea, Mbunge wa Temeke, kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nimpongeze wakati ule alivyoleta hoja yake ya changamoto ya gereza hili na yeye ameona uungwana wa kuipongeza Serikali kwa kutilia maanani yale aliyoeleza hapa Bungeni na tukayafanyia kazi. Nimhakikishie kwamba kama ambavyo tumefanya kipindi kile na haya ambayo ameyazungumza sasa hivi na yenyewe tatayachukua ili tuweze kuyafanyia kazi.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tumefika mwisho wa kipindi chetu cha maswali. Naleta kwenu matangazo ya wageni tulionao Bungeni siku ya leo. Tutaanza na wageni waliopo jukwaa la Mheshimiwa Spika.

Wapo wageni saba wa Mheshimiwa Spika kutoka Jijini Dar es Salaam, ambao ni ndugu Senzo Mazingiza ambaye ni Mtendaji Mkuu wa Klabu Bingwa ya Soka Nchini, Simba *Sports Club,* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia ndugu Haji Sunday Manara, De La Boss Msemaji Bora wa Vilabu vya Mpira, haya ngoja nimalizie kusoma Msemaji Bora wa Vilabu vya Mpira wa Miguu Duniani na Msemaji wa Mabingwa wa Nchi, Simba *Sports Club*. *(Makofi/Vigelegele)*

Haya tunaye pia ndugu Hashim Mbaga ambaye ni Mkurugenzi wa Wanachama na Matawi ya Simba *Sports Club* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Belinda Paul ambaye ni Meneja wa Miradi Simba, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia ndugu Betty Mgimba ambaye ni pia *Head* wa *Institution Bank and Liabilities, Equity Bank*, karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia Benedict Mwinula ambaye ni Meneja wa Miradi - *Equity Bank* karibu sana. *(Makofi)*

Tunaye pia ndugu Winland Mmbando ambaye ni Meneja Mikopo wa *Equity Bank,* Tawi la Dodoma karibu sana.(*Makofi*) (*Vigelegele)*

Wageni wengine wanne wa Mheshimiwa Spika ni kutoka *Maisha Care Foundation* ambao ni ndugu Taner Yildiz, karibu sana. Yupo pia Dkt. Salum Twahir. Yupo pia

ndugu Buddy Amour karibu sana, yupo pia ndugu Msafiri Angalieni Mpendu, karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge tunao pia wageni mbalimbali wa Waheshimiwa Wabunge, lakini kwa kuzigatia muda tuliobaki nao tuwatambuwe uwepo wao wote wasimame tuwaone. Wageni wote wa Waheshimiwa Wabunge karibuni sana. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge ninayo pia matangazo mawili; lipo tangazo linalotoka kwa Mwenyekiti wa wa Jumuiya wa Mtakatifu Thomas Moore, Bunge. Mheshimiwa Shally Raymond, anawatangazia Wabunge wote kwamba siku ya leo saa saba kamili kutakuwa na Ibada, baada ya kuahirisha Bunge, jengo la Pius Msekwa ghorofa ya pili. Kwa hiyo Waheshimiwa Wabunge mnakaribishwa sana kwenye ibada hiyo.

Pia kuna tangazo kutoka kwa Mwenyekiti wa Tawi la Simba, Bunge Mheshimiwa Rashid Shangazi, anawatangazia Waheshimiwa Wabunge wote kwamba mnaalikwa kwenye sherehe ya ufunguzi rasmi wa Tawi la Simba *Sports Club* Bunge (wekundu wa mjengoni) leo mchana mara baada kuahirishwa kwa kikao cha Bunge. Sherehe hizo zitafanyika mbele ya lango kuu la kuingilia viwanja vya Bunge.

Waheshimiwa Wabunge mnaalikwa hata wale ambao sio Wanachama wa Simba *Sports Club* na Mheshimiwa Spika jana alimtaja mahsusi Mheshimiwa Mkuchika kwamba anakualika sana kwamba yeye ndiye mgeni rasmi. Pia alimtaja Mheshimiwa Antony Mavunde kama Mbunge mwenyeji wa Dodoma mjini kwamba mnatarajiwa kuwepo hao kupokea wageni. *(Makofi)*

Baada ya kusema haya Waheshimiwa Wabunge, tutaendelea na ratiba iliyopo mbele yetu. Katibu!

**NDG. PAMELA PALLANGYO – KATIBU MEZANI:**

## HOJA ZA KAMATI

### TAARIFA ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2019

### NA

### TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2019

**NAIBU SPIKA**: Waheshimiwa Wabunge tutaanza na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka Mbunge wa Same Mashariki.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA – MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kukushukuru kwa kunipa nafasi ya kuwasilisha taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (*PAC*) kwa mwaka 2019. Pia nichukue nafasi hii kuwatakia Spika, Naibu Spika, Wabunge wote heri ya mwaka mpya.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia napenda nishukuru sana kwamba leo bosi wetu Manara yupo hapa kushuhudia nikisoma ripoti hii ya *PAC* aone tunavyosimamia fedha za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya kwanza kwa mujibu wa kanuni ya 117, kifungu kidogo cha 15 ya kanuni ya kudumu za Bunge toleo la Januari, 2016 naomba kuwasilisha taarifa

ya mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali, *PAC* kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2019 na kuliomba Bunge lako tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili. Pia niombe kwamba taarifa yangu yote iingie kwenye *Hansard*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mwaka 2019 *PAC* ilipokea na kujadili taarifa ya *CAG* kuhusu ukaguzi wa hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za jumla ya mafungu 41 ya Serikali Kuu na 28 ya Mashirika ya Umma. Aidha kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya miradi ya maendeleo kwa upande wa utekelezaji wa maazimio ya Bunge kamati imeridhishwa na utekelezaji wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya pili uchambuzi, uchambuzi wa taarifa ya *CAG* kwa mafungu mahsusi ya Serikali Kuu ya Mashirika ya Umma uliibainisha mambo yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Uchambuzi wa hali ya ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (*TRA*), pamoja na jitihada kubwa zilizofanywa na *TRA*, katika kukusanya mapato ya Serikali uchambuzi wa *CAG* kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2018 umebaini changamoto kadhaa ambazo zinapunguza kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kamati za kiutendaji zinazochangia changamoto za kiutendaji zinazochangia na kushusha kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali ya *TRA* pamoja ni hizi zifuatazo:-

(i) Kuchelewa kufanyika usuluhisho wa madeni ya kodi (*weaknesses in the process of reconciliation of Tax receivables);*

(ii) Kutofanyika kwa usahihi wa ukadiriaji wa kodi ya zuio (*withholding tax*) na ushuru wa stempu (*stamp duty);*

(iii) Uwepo wa madeni ya ki-kodi ya muda mrefu yasiyokusanywa;

(iv) Ucheleweshaji usiokuwa na tija wa maamuzi ya rufaa za ki-kodi suala hili limejitokeza katika bodi ya rufaa za kodi *TRAB*, Baraza la Rufaa za kodi *TRAT* na Mahakama ya rufaa ya Tanzania;

(v) Ufuatiliaji hafifu wa madeni ya kodi;

(vi) Kutofanyika kwa mapitio ya kina ya miamala ya kifedha makampuni ya kimataifa (*inadequate review of related part transactions of multinational companies*);

(vii) Dosari katika usimamizi wa makusanyo ya kodi katika viwanja vya ndege;

(viii) *TRA* kutowasilisha kwa wakati mapato inayokusanya kwa niaba ya taasisi nyingine za Serikali;

(ix) Dosari katika usimamizi wa kodi zinazotakiwa kukusanywa kutokana na mafuta yanayoingizwa hapa nchini na yanasafirishwa nchi za nje.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na changamoto zilizobainishwa hapo juu uchambuzi wa kamati umebainisha kiasi cha mapato ambayo hayakukusanywa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 kama yanavyofafanuliwa katika jedwali 2.1 la taarifa hii ambayo ziko kwenye *tab* zenu wote

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa usimikaji wa mifumo muhimu ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za bandari kati ya mwaka 2010 mpaka 2019. Katika mwaka 2010 hadi

2019 *TPA* waliingia jumla ya mikataba 12 na wametumia kiasi cha *euro* milioni 8.1 dola za Marekani milioni 15.6 na kiasi cha shilingi milioni 694.1 kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na usimikaji wa mifumo fedha hizi ni takribani shilingi bilioni 57.6.

Mheshimiwa Naibu Spika, mchanganuo wa malipo na kampuni zilizopewa kazi ya usimikaji mifumo kati ya mwaka 2010 hadi 2019 na kiasi cha kazi walizotekeleza umefafanuliwa katika jedwali namba 2 la taarifa yetu ambayo iko kwenye *tab* zenu. Kamati inasisitiza kukamilika kwa mifumo hiyo ambayo imetumia gharama kubwa hadi sasa

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokuwepo kwa makubaliano ya mkopo kati ya mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF)* na Chuo Kikuu cha Dodoma na kupungua kwa mtaji wa mfuko.

Mheshimiwa Naibu Spika, uchambuzi wa kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *(NHIF),* kwa mwaka unaoishia tarehe 30 Juni, 2018 ilibainika kuwa *NHIF* hawakuwa na mkataba wa mkopo wa kimaandishi (*written law agreement*) na Chuo Kikuu cha Dodoma. Mkopo unaohusika ni ule unaohusu ujenzi wa hospitali ya Benjamin Mkapa.

Mheshimiwa Naibu Spika, mkopo huo ulitolewa kwa maelekezo kwamba kutatolewa dhamana ya Serikali *(Government Guarantee)* hata hivyo hadi Bodi na Menejimenti ya *NHIF* inafika mbele ya kamati dhamana hiyo ilikuwa haijatolewa hadi kufika tarehe 30 Juni, 2017 deni la mkopo huo lilifikia jumla ya shilingi bilioni 82.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto za utendaji katika Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO),* kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30 2018 *CAG* alishindwa kutoa maoni ya ukaguzi katika Shirka la Madini la Taifa yaani alikuwa ana *disclaim of opinion*, jambo hili limeendelea sambamba na kuongezeka kwa hasara ya Shirika kutoka shilingi milioni 715.6 ilipokuwa Juni, 2017 hadi shilingi milioni 2.4 Juni 2018 ongezeko hilo ni karibu mara tatu katika kipindi cha mwaka mmoja.

Mheshimiwa Naibu Spika, masuala ya msingi yaliyosababisha *STAMICO* kupata hati husika ya ukaguzi, ni kama ifuatavyo:

(a) Kutojumuisha kwa taarifa za hesabu za kampuni tanzu za *STAMIGOLD* Ltd ya Kyerwa T Co. Ltd katika hesabu jumuifu za *STAMICO*. Jambo hili ni kinyume na kanuni namba 10 ya kanuni za uandaaji wa hesabu kimataifa. Ni kwa msingi huo hali halisi ya mali na madeni ya kampuni hizo tanzu haujulikani hadi sasa.

(b) Suala la pili katika *STAMICO* ni kuwa thamani ya jumla ya shilingi bilioni 33 ambayo ni thamani ya uwekezaji uliofanywa na *STAMICO* katika kampuni tanzu haina uhalisia. *CAG* alishindwa kupata uthibitisho wa kutosha wa thamani hiyo kutokana na kutokuwepo na taarifa sahihi za uwekezaji

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na dosari hizo za kiuwekezaji hali ya ufanisi wa STAMICO imekuwa ni changamoto kubwa

Mheshimiwa Naibu Spika, Dosari katika usimamizi wa ujenzi wa vyuo vya uwalimu katika fungu 46 Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia, kamati imefanya uchambuzi wa kina wa miradi ya ukarabati na ujenzi kwa mwaka 2017/2018 na kubaini dosari ambazo zinaweza kuisababishia Serikali kutopata thamani halisi ya fedha miradi hiyo na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo:

(a) Mradi wa ujenzi wa bwalo katika Chuo cha Ualimu Punguso;

(b) Mradi wa ujenzi wa ukarabati wa Chuo cha Ualimu Kitangali;

(c) Mradi wa ujenzi wa ukarabati wa Chuo cha Ualimu Shinyanga.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama uchambuzi wa kamati ulivyotanabaisha Wizara ya Elimu Sayansi na Teknolojia inatakiwa kuongeza jitihada za usimamizi wa mikataba, ucheleweshaji wa utekelezaji wa mikataba unaongeza gharama za ujenzi na kusababishia Serikali hasara kubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokamilika kwa muda mrefu wa baadhi ya miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), kamati imebaini uwepo wa miradi kadhaa ya NHIC ambayo imesimama kwa muda mrefu na hivyo kuwepo kwa viashiria vya Serikali kupata hasara siku zijazo. Mradi wa kwanza ni wa nyumba 711-1 uliopo Kawe Dar es Salaam wenye thamani ya shilingi bilioni 142.55.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mradi huu umesimama tangu mwanzo wa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Mradi mwingine ni wa ujenzi wa *Victoria Palace* wenye thamani ya shilingi bilioni 34.14 mradi huu umesimama tangu mwaka 2017 ambapo pamoja na kusimama *CAG* alibaini ongezeko la gharama kwa zaidi ya shilingi bilioni 6.86 ambalo anakiri hazikutolewa maelezo ya msingi.

Mheshimiwa Naibu Spika, mradi mwingine ni wa nyumba 711-2 ambao upo eneo ya Kawe Dar es Salaam wenye thamani ya shilingi bilioni 103 mradi huu umesimama tangu mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha, hadi mradi huu unasimama ulikuwa umetekelezwa kwa kiasi cha 30% na kutumia jumla ya shilingi bilioni 34.7.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni dhahiri kuwa utekelezaji wa miradi hiyo ulianza bila kufanyiwa upembuzi wa kina hali iliyosababisha gharama za miradi kuongezeka. Aidha, kuna viashiria vya kutowajibika ipasavyo kwa uliokuwa uongozi wa *NHC* katika kuhakiki gharama za miradi hiyo. Hata hivyo kuna umuhimu wa kuangalia namna bora ya kukamilisha miradi hiyo ili kuepusha hasara kubwa ambayo *NHC* itapata hapo baadaye hasa kama mradi huu utasitishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi ya Wakala wa Majengo *(TBA)*. Wakala wa Majengo Tanzania *TBA* ilipewa majukumu ya ujenzi wa majengo ya taasisi mbalimbali za Serikali, kwa mikataba yenye gharama za takriban shilingi bilioni 24. Uchambuzi wa kamati umebaini na kuthibitisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa miradi husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika kushughulikia hoja ya *TBA* kutokamilisha miradi kwa wakati kamati ilibaini dosari zifuatazo ambazo ndiyo sababu za kutokuwepo na ufanisi wa kutosha katika wakala husika.

(a) Katika baadhi ya miradi vifaa vya ujenzi vilivyotolewa havikuwa vimepimwa na Wahandisi wa miradi kwa kuzingatia makisio ya gharama za ujenzi (*BOQ*).

(b) Kuhamishwa kwa vifaa vya ujenzi kutoka mradi mmoja kwenda mradi mwingine.

(c) Upungufu mkubwa wa wataalamu na vifaa kwa mfano kamati ilibaini kuwa miradi miwili ilikuwa inasimamiwa na mratibu mmoja kwa wakati mmoja. Aidha, katika miradi mingi vifaa vya ujenzi vilikuwa vinachangiwa kwa wakati mmoja

Mheshimiwa Naibu Spika, uwekezaji uliofanywa na *NSSF* katika hisa za Vodacom unaotoa faida kidogo sana ukilinganisha na dhamana za Serikali. Taarifa ya *CAG* imebainisha kuwa mnamo tarehe 5 Aprili 2017 *NSSF* iliomba ridhaa ya BOT ili kuwekeza katika hisa za Vodacom ambazo faida yake ilikuwa chini ukilinganisha na dhamana za Serikali. Hata hivyo kabla ya ridhaa kuhusika kutolewa na BoT tarehe 10 Aprili 2017, bodi ya *NSSF* iliidhinisha mfuko kutumia kiasi cha shilingi bilioni 40 katika kuwekeza katika ununuzi wa hisa za Vodacom bila ya kupata kibali cha BoT.

Mheshimiwa Naibu Spika, mnamo tarehe 20 Aprili 2017 Benki Kuu ilikataa kuidhinisha uwekezaji huo kwa msingi kuwa faida itakayopatikana ni ndogo sana ukilinganisha na faida ambayo *NSSF* ingepata kwa kununua dhamana za Serikali. Mathalani endapo *NSSF* wangewekeza kwenye dhamana za muda mfupi (*treasury bills*) zingetoka faida ya 15% na zile za muda mrefu *bonds* kwa miaka 5 zingetoa faida ya 17.2% tofauti na faida ya 2% tu wanayopata kwa hisa za Vodacom.

(a) Mapendekezo kuhusu hali ya ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania TRA, Bunge linaazimia kwamba, Serikali iziboreshe na kuziongezea uwezo bodi ya rufaa za kodi na baraza la vifaa vya kodi kwa kuteua wenyeviti, makamu wenyeviti na wajumbe wa kutosha ili kuziwezesha taasisi hizi kufanya vikao vya kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati. Aidha, Serikali itoe bajeti ya kutosha kwa ajili ya taasisi hizi ili zifanye kazi zake kwa wakati na kwa ufanisi. Hatua hizi itasaidia kupunguza milundikano wa kesi za kodi zilizokaa muda mrefu bila kuhitimishwa.

(b) *TRA* iongezewe uwezo na ujuzi wafanyakazi wote wanaohusika na ukaguzi na ukadiriaji wa kodi kupitia mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa kukadiriwa kodi kwa usahihi.

(c) Serikali iongeze jitihada katika ukusanyaji wa kodi ambazo hazijalipwa na walipa kodi. Jambo hili linaweza ufanikiwa kwa kuboresha na kuiongezea uwezo kitengo cha ukusanyaji wa madeni na mikakati ya kuhakikisha kuwa kodi zote zinakusanywa kwa wakati badala ya kufanyiwa makadirio uthamini hivyo kuzuia ulimbikizaji baada ya kufanyiwa makadirio au uthamini hivyo kuzuia ulimbikizaji wa kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokamilika kwa usimikaji wa mifumo muhimu ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za TPA. Bunge linaazimia kwamba Serikali itumie taasisi ya umma ya wakala mtandao *e-government* kusimamia na kuratibu shughuli zinazoendelea za uwekezaji mifumo ya *TPA*. Jambo hili litasaidia kuweka uwajibikaji na kupunguza gharama ambazo Serikali imekwishaingia hadi sasa.

(d) Kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)* kwa kadri atakavyoona inafaa kufanya ukaguzi wa ufanisi (*performance audit*) wa shughuli zinazohusu ununuzi na usimikaji wa mifumo katika taasisi za umma. Ukaguzi huu utakuwa muhimu ili kutoa mwongozo na ushauri kwa taasisi za umma katika manunuzi ya mifumo ili kuepuka gharama.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya *NHIF*.

(a) Bunge linaazimia kwamba bodi ya wakaguzi ya *NHIF* na bodi ya wakaguzi wa hospitali ya Benjamin Mkapa wafatilie kwa karibu Serikalini suala la makubaliano ya kimaandishi ya mkopo wa ujenzi wa hospitali ya Benjamin Mkapa ili kufunga hoja husika.

(b) Kuhusu mtaji wa mfuko *NHIF* ihakikishe kunakuwepo na mwenendo mzuri wa mfuko kwa kuongeza udhibiti na ufuatiliaji wa kiwango cha madai ya huduma ili kuepuka madai hewa ambayo yanaathiri shughuli za mfuko.

(c) *NHIF* iendelee kufanya tafiti mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwekeza asilimia fulani ya michango ya wanachama ili uwekezaji huo uje kusaidia malipo ya huduma za afya kwa wanachama pindi watakapostaafu au Wabunge ambao hawataweza kurudi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utendaji wa Shirika la Madini la Taifa *(STAMICO)* Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali kupitia Ofisi ya Msajili *(TRO)* wa Hazina iimarishe usimamizi wa karibu wa *STAMICO* ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya shughuli za utendaji wa kila siku wa Shirika hilo; Serikali ifanye mapitio ya mikataba yote ambayo *STAMICO* imeingia na Kampuni Tanzu ili kuhakikisha makubaliano katika mikataba yanatekelezwa ipasavyo na masharti hasi yanaondolewa; na *STAMICO* ifanye uthamini wa mali zake ili kutambua thamani halisi ya mali za Kampuni kwa sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba la Taifa *(NHC)*; Bunge linaazimia kwamba:-

(a) Serikali iangalie namna bora ya kuiwezesha *NHC* kukamilisha Miradi ambayo ilikuwa katika hatua za mwisho za utekelezaji ili kupunguza hasara ambayo tayari imepatikana; na

(b) Serikali iendelee na uchunguzi wa kina wa Miradi yote ya *NHC* ili kubaini dosari zilizopo katika Miradi husika. Miradi mingi imebainika kuwa ilitekelezwa kwa gharama zisizo halisia na usimamizi wake haukuwa na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kutokamilika kwa wakati kwa Miradi ya *TBA* Bunge linaazimia kwamba:-

(a) *TBA* waboreshe na kuimarisha Kitengo cha Usimamizi wa Utekelezaji; na

(b) TBA watengeneze utaratibu wenye ufanisi wa udhibiti wa mifumo ya ndani katika utekelezaji wa Miradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii *(NSSF);* Bunge linaazimia kwamba:-

Serikali ichunguze suala hili na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Dosari za Usimamizi wa Mikataba katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia. Bunge linaazimia kwamba:-

Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iimarishe Kitengo chake cha usimamizi wa Mikataba ya ujenzi. Aidha, majengo yote ambayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi yakamilike na taarifa zitolewe kwa CAG.

Mheshimiwa Naibu Spika, hitimisho, shukurani; napenda kutumia fursa hii kumshukuru Spika na wewe binafsi Naibu Spika kwa kazi nzuri ambayo mmeifanya pamoja na Wenyeviti wote Bunge kwa kusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa uadilifu na weledi Mkubwa. Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge, Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa Shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova.

Mheshimiwa Spika, mwisho, Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, pamoja na Mhasibu Mkuu wa Serikali *(ACGEN)* Ndugu Francis Mwakapalila na Msajili wa Hazina *(TR)*, Ndugu Athuman Mbutuka. Aidha, naishukuru Kurugenzi ya Usimamizi wa Mali za Serikali *(DGAM)* kwa kuendelea kuisadia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza na wale ambao hawakusikiliza pia nafikiri watasoma kwenye *tablet*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**TAARIFA YA SHUGHULI ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI (PAC) KWA MWAKA 2019 - KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

(*Inatolewa chini ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016)*

**IKISIRI**

Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ina dhima kubwa kwa mujibu wa Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kushughulikia maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara, Idara, Wakala na Mashirika ya Umma. PAC imekuwa ikitekeleza wajibu wake huo kwa kutumia [1]Taarifa za Ukaguzi za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG).

Chimbuko la Taarifa hii linatokana na masharti ya Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Taarifa imechambua kwa kina utekelezaji wa shughuli za Kamati kwa kuzingatia majukumu ya Kikanuni ya Kamati ya PAC kwa kipindi cha mwaka 2019.

Kamati imebainisha maeneo kadhaa ambayo yana changamoto za matumizi ya fedha za umma. Maeneo hayo ni pamoja uwepo wa kiasi kikubwa cha kodi kisichokusanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) kutokana sababu kadhaa kama vile ukadiriaji wa kodi usiokuwa na uhalisia pamoja na uwepo wa mashauri mbalimbali ya kikodi ambayo hayakamiliki kwa wakati. Aidha, dosari nyingine ni pamoja na usimamizi usioridhisha wa Mikataba hasa ya ujenzi na ukarabati katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia hali inayosababisha ongezeko la gharama za ujenzi na hivyo kusababisha hasara kwa Serikali.

[1] Rejea Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016

Maeneo mengine ambayo Kamati imebainisha uwepo wa viashiria vya hasara katika rasilimali za Umma ni pamoja na ucheleweshaji wa kukamilika Miradi katika Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Shirika la Nyumba la Taifa (NHC). Ucheleweshaji huo umesababisha ongezeko kubwa la gharama za Miradi na kutofikiwa kwa malengo kwa Miradi husika. Aidha, Kamati imebainisha changamoto za ufanisi na utendaji katika Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) na pia kutokuwepo kwa Mkataba wa kimaandishi *(Written loan agreement)* kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Chuo Kikuu cha Dodoma unaohusu ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa.

Kamati imetoa mapendekezo mahsusi katika maeneo yenye matumizi mabaya ya fedha za umma ikiwa ni pamoja kuishauri Serikali kuboresha na kuziongezea uwezo Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi kwa kuteua Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa kutosha ili kuziwezesha Taasisi hizi kufanya vikao vya kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati. Aidha, Kamati imependekeza kwa TRA kuongeza uwezo na ujuzi kwa wafanyakazi wote wanaohusika na ukaguzi na ukadiriaji wa kodi kupitia mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa kukadiriwa kodi kwa usahihi.

Kwa upande wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO), Kamati imeshauri Serikali kupitia Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) iimarishe usimamizi wa karibu

wa STAMICO ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya shughuli za utendaji wa kila siku wa Shirika hilo. Aidha, Serikali ifanye mapitio ya mikataba yote ambayo STAMICO imeingia na Kampuni Tanzu ili kuhakikisha makubaliano katika Mikataba yanatekelezwa ipasavyo na masharti hasi yanaondolewa.

Kwa upande wa Shirika la Nyumba la Taifa (NHC), Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Fungu – 46 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Kamati imependekeza kuimarisha Vitengo vya usimamizi wa Miradi ili kuepuka ongezeko la gharama lililotokana na kutokuwepo kwa usimamizi wenye ufanisi. Aidha, Kamati, imetoa mapendekezo kuhusu maboresho ya msingi katika Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF), Mamlaka ya Bandari Tanzania (TPA) na pia hatua za kuchukua kwa uwekezaji uliofanywa na NSSF katika ununuzi wa hisa za Vodacom.

**SEHEMU YA KWANZA**

## 1.0 MAELEZO YA JUMLA

### 1.1 Utangulizi

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Kanuni ya 117 (15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, naomba kuwasilisha Taarifa ya Mwaka ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC), kuhusu shughuli zilizotekelezwa kwa mwaka 2019 na kuliomba Bunge lako Tukufu liipokee na kuijadili inavyostahili.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka 2019, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) ilipokea na kujadili Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018, naomba kulijulisha Bunge lako Tukufu kuwa maelezo yanayotolewa katika Taarifa hii yanatokana na Hesabu zilizokaguliwa kama zilivyowasilishwa katika Taarifa hiyo ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali.

### 1.2 Majukumu ya Kamati

**Mheshimiwa Spika,** Shughuli za Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali zilizingatia majukumu yake yaliyoainishwa katika Kifungu cha 14 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Majukumu hayo ni:-

a) Kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara za Serikali yaliyoainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali;

b) Kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yaliyokwishatolewa na Kamati hiyo yenye lengo la kuondoa matatizo hayo; na

c) Kutoa mapendekezo na Ushauri kwa Wizara za Serikali kuhusu matumizi mazuri ya fedha za umma ili kupunguza matumizi mabaya ya fedha za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Msingi wa majukumu hayo unatokana na Taarifa ya hesabu zilizokaguliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kama ilivyobainishwa katika Kifungu cha 16 cha Nyongeza ya Nane ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016.

### 1.3 Muhtasari wa Matokeo ya Utekelezaji wa Shughuli za Kamati


**Mheshimiwa Spika**, Shughuli za Kamati kwa mwaka 2018/2019, zililenga kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Wizara na Mashirika ya Umma kama yalivyobainishwa katika Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2018. Aidha, shughuli hizo zilikusudia kufuatilia

utekelezaji wa mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali (PAC) mwezi Januari, 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa kuzingatia Ibara ya 143 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977, kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2018 Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) alifanya ukaguzi wa jumla ya Taasisi[2] 263 za Serikali Kuu ikijumuisha Wizara na Idara zinazojitegemea 65, Wakala 33, Mifuko maalum 16, Sekretarieti za Mikoa 26, Taasisi nyingine 42, Vyama vya Siasa 26, Bodi za Mabonde ya Maji 14 na Balozi 41. Ukaguzi ulihusisha pia Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), Hesabu Jumuifu za Taifa *(Consolidated accounts)*, ukaguzi wa malipo tarajali ya pensheni na kaguzi maalum. Mchanganuo wa Taasisi zilizokaguliwa ni kama unavyoonekana katika Chati Na. 1.1-hapa chini:-

[2]Rejea ukurasa xix wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018.

**Chati Na. 1.1 Mgawanyo wa Taasisi za Serikali Kuu zilizokaguliwa mwaka 2018.**





***Chanzo:*** **Taarifa ya CAG kwa ukaguzi wa Serikali Kuu kwa mwaka wa fedha unaoshia tarehe 30 Juni, 2018.**

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Mashirika ya Umma, Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali alikaguwa na kutoa Taarifa ya jumla ya Mashirika ya Umma 122 pekee ikilinganishwa na Mashirika 150 yaliyokaguliwa kwa mwaka 2017.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilifanikiwa kuchambua na kujadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za jumla ya Mafungu 41 ya Serikali Kuu na 28 ya Mashirika ya Umma. Aidha, Kamati ilipata fursa ya kutembelea baadhi ya Miradi ya maendeleo ikiwamo ya ujenzi wa ofisi, barabara, soko, stendi ya mabasi Dodoma na uwekezaji katika Miradi ya ujenzi wa nyumba za kibiashara, Dar es Salaam. Mchanganuo wa Mafungu yaliyojadiliwa na Kamati kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018 umechambuliwa katika chati 2.1 hapa chini:-

**Chati Na. 2.1: Mafungu yaliyojadiliwa na Kamati kwa mwaka 2019**




***Chanzo:* Uchambuzi wa Kamati kwa mafungu mbalimbali kwa mwaka 2019**

**Mheshimiwa Spika,** Jumla ya mafungu sitini na tisa yalifika mbele ya Kamati kwa ajili ya kujadiliwa. Aidha, Maafisa Masuuli na Wenyeviti wa Bodi za Taasisi husika walihojiwa na Kamati kuhusu Taarifa za hesabu zao.

### 1.3.1 Utekelezaji wa Mapendekezo yaliyotolewa na Kamati ya Hesabu za Serikali kipindi kilichopita

**Mheshimiwa Spika**, Kwa mujibu wa Taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali iliyowasilishwa Bungeni tarehe 01 Februari, 2019 jumla ya mapendekezo tisa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali yaliridhiwa na kuwa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa lengo la kufuatilia utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotolewa kipindi kilichopita, mapema mwezi Aprili 2019, Kamati ilipokea majibu ya Serikali kuhusu utekelezaji wa Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Matokeo ya uhakiki wa utekelezaji wa Maazimio ya Bunge yaliyotokana na Taarifa ya PAC kwa kiasi kikubwa yamebainisha kwamba, Serikali imezingatia ushauri na maelekezo ya Bunge. Kamati imepitia azimio moja baada ya lingine na kuridhika na hali ya utekelezaji. Jambo hili ni muhimu na la kujivunia kama mojawapo ya mafanikio ya Bunge lako tukufu. Mapitio ya utekelezaji wa Maazimio hayo kwa muhtasari ni kama ifuatavyo: -

a) Kuhusu uhakiki wa Mfuko Mkuu wa Serikali; Majibu ya Serikali yamebainisha hatua kadhaa zilizochukuliwa baada ya ukahiki wa Mfuko Mkuu wa Serikali kama ilivyokuwa imependekezwa na Kamati. Hatua hizo ni pamoja na:-

i. Maboresho ya mfumo wa kihasibu na mapato ya Serikali [3](IFMS);

[3] Maboresho kutoka EPICOR 9.05 kwenda EPICOR 10

ii. Maboresho ya mfumo wa ulipaji mishahara kwa njia ya Kielektroniki (GSPP);
iii. Kuunganishwa kwa mfumo kwa kukusanya mapato ya Serikali (GePG) na Taasisi mbalimbali za Serikali ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya utendaji wa mfumo wa Akaunti Jumuifu ya Hazina (TSA); na

iv. Serikali imeihakikishia Kamati kuwa itaendelea kuzingatia Sheria ya Bajeti katika utekelezaji wa shughuli zake za kila siku.

b) Kuhusu uwekezaji usio na tija uliofanywa na Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF), Serikali iliifahamisha Kamati kuwa Miradi yote iliyotekelezwa na NSSF na kuwa na dosari katika utekelezaji wake ipo chini ya uchunguzi wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU). Kwa msingi huo, hatua za kisheria zitachukuliwa pindi uchunguzi utakapokamilika. Aidha, kwa Miradi saba ambayo Kamati ilikuwa imebainisha kuwa na dosari za utekelezaji, maelezo ya Serikali yameainisha mikakati kadhaa ambayo mingi imelenga katika mbinu ya kupunguza hasara iliyokwishajitokeza hapo awali *(Loss reduction strategy)* ili kuokoa fedha za Wanachama zilizokuwa zimewekezwa katika maeneo hayo.

c) Kuhusu Ukaguzi Maalum wa Ubia kati ya Shirika la Maendeleo la Taifa (NDC) na Kampuni ya IETL ambapo Kamati ilipendekeza kufanyike mapitio ya [3]Mkataba wa Mradi huo ambao haukuwa na maslahi mapana kwa Taifa. Ufafanuzi wa Serikali katika eneo hili ni kuwa, kuliundwa Kamati maalum ya Wataalam ili kujadiliana na Mwekezaji husika ili kurejesha fedha zote ambazo Taarifa ya CAG ilibaini zililipwa kimakosa. Pamoja na jitihada hizo, Serikali inatathmini hali ya kiutendaji ya NDC *(Corporate Valuation)* kubainisha uwezo wa rasimali watu na fedha katika utekelezaji wa dila na dhima ya Shirika hilo.

d) Kuhusu madeni sugu ya matrekta yaliyokopeshwa na Shirika la Uzalishaji Mali la Suma (SUMA – JKT), ufafanuzi na utekelezaji wa Serikali umebainisha kuwa hadi kufikia mwezi Aprili 2019, jumla ya **shilingi 7,920,927,213** zilikuwa zimekusanywa. Aidha, kufuatia maagizo ya Mheshimiwa Rais kuwa wadaiwa wote wa SUMA – JKT wawe wamelipa madeni yao ndani ya siku thelathini kuliwezesha ukusanyaji wa deni la **shilingi 2,326,784,200**.

e) Kuhusu mikopo chechefu katika Benki ya maendeleo ya TIB, Serikali imetoa ufafanuzi kuwa kwa wakopaji wa jumla ya **shilingi bilioni 89** walipewa notisi ya kutakiwa kurejesha mikopo yao

kama Bunge lilivyoazimia. Changamoto kubwa kwa suala la mikopo chechefu ni kuwa wakopaji wanakimbilia Mahakamani na kuomba zuio la mali zao kukamatwa hivyo kukwamisha jitihada za urejeshaji wa mikopo kupitia dhamana za wadaiwa.

f) Kuhusu malipo ya resheni wa watumishi wasio Askari pamoja na malipo kwa mtoa huduma[5] ambaye hakutoa huduma, majibu ya Serikali yamefafanua kuwa uchunguzi wa masuala hayo ulikamilika 07/03/ 2019 na kupelekwa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka (DPP) kwa hatua zaidi. Aidha, Kamati ilipata Taarifa kuwa mojawapo ya mashauri hayo tayari limefikishwa Mahakamani ili haki iweze kutendeka.

g) Kuhusu deni ambalo TBA walikuwa wamechukua mkopo katika Benki ya CRDB na kuonekana uwepo wa vipengele vyenye masharti hasi kwa Serikali, Kamati imefahamishwa kuwa mkopo husika wa **shilingi 3,626,896,766** umesitishwa kama Bunge lilivyoazimia. Aidha, "*commitment fee*" ya asilimia mbili ambayo ilikuwa moja ya sharti hasi katika mkopo huo ilisitishwa.

[4] Joint Venture Agreement and Shareholders Agreement

[5] Rejea Mkataba wa Giva Justice

h) Kuhusu madeni ya TANESCO, TPDC, SONGAS na PAET, Kamati ilipata maelezo ya Serikali kupitia kwa Ofisi ya Msajili wa Hazina (TRO) ambapo kwa kupitia majadiliano ya kiutawala madeni hayo yameanza kulipwa. Mathalani, hadi kufikia tarehe 31 Januari, 2019 kupitia mazungumzo husika, TIB iliweza kukusanya **Dola za Marekani Milioni 4.4** kutoka TPDC. Hivyo, Kamati ina imani kuwa madeni haya yataendelea kupungua kadri muda unavyoendelea.

i) Mwisho, kuhusu hoja ya Mkataba wa Ubia kati ya Jeshi la Polisi na Mwekezaji wa eneo la Osterbay Dar es Salaam, majibu ya Serikali yamefafanua kuwa Timu ya Wataalamu iliyoundwa na Serikali imekamilisha kazi yake ya mapitio ya Mkataba na majadiliano na Mwekezaji husika. Aidha, utekelezaji wa makubaliano umeanza kufanyika ikiwa ni pamoja na makabidhiano ya nyumba za **Askari 330** za **Maafisa 23** Kituo cha Polisi Oysterbay zilizojengwa na Mwekezaji. Kamati inategemea makubaliano yote yatakamilika kwa wakati ili kuendelea kuongeza uwajibikaji katika usimamizi wa fedha na rasilimali za umma.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na utekelezaji wa Maazimio ya Bunge ambao umefanyika kwa kiasi kikubwa kama ilivyofafanuliwa hapo awali, Kamati inaendelea kusisitiza umuhimu wa Serikali kukamilisha kwa haraka hoja zote ambazo bado zipo kwenye uchunguzi na kuchukua hatua stahiki.

**Mheshimiwa Spika,** Masuala ya hoja za ukaguzi katika NSSF, Jeshi la Polisi Fungu 28, NDC, madeni ya SUMA - JKT na madeni ya TIB yamechukua muda mrefu kukamilika. Katika kipindi chote cha miaka minne ya uhai wa Kamati hii, tumesisitiza sana masuala ya kiuwajibikaji katika Taasisi za Umma. Hata hivyo, kumekuwa na dosari za kuchukua hatua kutokana na kutokamilika kwa uchunguzi pale panapokuwa na tuhuma mbalimbali za ubadhirifu. Hivyo ni muhimu Serikali ikaweka nguvu zaidi katika eneo hilo ili kutokwamisha uwajibikaji katika matumizi ya fedha za umma.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA MATOKEO YA UTEKELEZAJI

### 2.1 Maelezo ya Jumla Kuhusu Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika**, Ili kubainisha maeneo yenye matatizo ya matumizi mabaya ya fedha za umma na kwa kuzingatia Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Kaguzi mahususi za Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, vigezo vya msingi vilitumika kuainisha maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilijielekeza katika kubainisha thamani ya pesa iliyotumika katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa *(Value for money criteria),* uzingatiaji wa bajeti, kiasi cha matumizi ikilinganishwa na mahitaji halisi, matokeo ya Taarifa za Kaguzi Maalum zilizofanyika hivi karibuni na umakini katika matumizi yaliyoripotiwa na kukaguliwa.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na vigezo hivyo, Kamati pia ilijielekeza kwa kuangalia hali ya Kujirudia rudia kwa hoja za ukaguzi katika Taasisi husika, uzingatiaji wa Mamlaka halali za kuidhinisha matumizi ya fedha, uzingatiaji wa Sheria, Kanuni na taratibu za matumizi ya fedha za umma na kuwepo kwa Kumbukumbu na nyaraka zinazopaswa kutunzwa kwa ushahidi wa matumizi kama zilivyohitajiwa na CAG.

### 2.2 Uchambuzi

**Mheshimiwa Spika,** Kufuatia vigezo na mambo ya msingi niliyoyataja hapo awali, uchambuzi wa Taarifa ya CAG kwa mafungu mahususi ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma ulibainisha mambo yafuatayo: -

#### 2.2.1 Uchambuzi wa Hali ya Ufanisi katika Utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**Mheshimiwa Spika,** Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ndio chombo kilichopewa jukumu la msingi la kisheria kukusanya kodi mbalimbali hapa Nchini. Kama inavyoeleweka, kwa miaka ya karibuni TRA imepiga hatua kubwa katika kuongeza ufanisi wa kiutendaji ikiwa ni pamoja na kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato na ongezeko la mapato ya Serikali. Hatua hii imesaidia kuongeza mapato na hivyo kuwezesha utekelezaji wa Miradi mikubwa ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na jitihada kubwa zinazofanywa na TRA katika kukusanya mapato ya Serikali, uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG kwa hesabu zinazoishia tarehe 30 Juni, 2018 umebaini changamoto kadhaa za ambazo zinapunguza kasi ya ukusanyaji wa mapato stahiki ya Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto zinazochangia na kushusha kasi ya ukusanyaji wa mapato ya Serikali katika TRA ni pamoja na hizi zifuatazo:-

1. Kuchelewa kufanyika usuluhishi wa madeni ya kikodi *(Weakness in the process of reconciliation of tax receivables)*;

2. Kutofanyika kwa usahihi kwa ukadiriaji wa kodi ya zuio *(Withholding tax)* na ushuru wa stempu *(Stamp duty)*;

3. Uwepo wa madeni ya kikodi ya muda mrefu yasiokusanywa;

4. Ucheleweshaji usio kuwa na tija wa maamuzi ya rufaa za kikodi[6]. Suala hili limejitokeza katika Bodi ya Rufaa za Kodi (TRAB), Baraza la Rufaa za Kodi (TRAT) na Mahakama ya Rufaa Tanzania;

5. Ufuatiliaji hafifu wa madeni ya kikodi;

6. Kutofanyika kwa mapitio ya kina ya miamala ya kifedha ya Makampuni ya Kimataifa *(inadequate review of related party transactions of multinational companies)*;

7. Dosari katika usimamizi wa makusanyo ya kodi katika viwanja vya Ndege;

8. TRA kutowasilisha kwa wakati mapato inayokusanya kwa niaba ya Taasisi nyingine za Serikali;

9. Dosari katika usimamizi wa kodi zinazotakiwa kukusanywa kutokana na mafuta yanayoingizwa hapa Nchini na yanayosafirishwa kwenda Nje ya Nchi; na

10. Dosari katika mfumo wa TANCIS hivyo kusababisha baadhi ya kodi kutokusanywa kwa bidhaa zinazosafirishwa Nje ya Nchi kupitia hapa Nchini.

---

[6]Jumla ya mashauri 817 ya kikodi yalikuwa hayajashughulikiwa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na changamoto zilizobainishwa hapo juu, uchambuzi wa Kamati umebainisha kiasi cha mapato ambayo hayakukusanywa hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2018 kama inavyofafanuliwa katika jedwali Na. 2.1 hapa chini: -

**Jedwali Na. 2.1 Mapato ambayo hayakukusanywa na TRA kutokana na dosari mbalimbali**

| **Idara ya Kikodi *(Tax department)*** | **Kodi isiyokusanywa kutokana na dosari za kiutendaji *(Inefficiency issues)*** | **Kodi isiyokusanywa kutokana na dosari za ukadiriaji *(Potential revenue not assessed)*** | **Kodi isiyokusanywa *(Potential revenue uncollected)*** | **Jumla** |
|---|---|---|---|---|
| Idara ya Kodi za Ndani *(Domestic revenue department)* | TZS. 76,404,212,066.38 | TZS.142, 477,308.83 | TZS. 80,858,621,763.81 | TZS.157, 405,311,139.02 |
| Idara ya Walipa kodi wakubwa *(large taxpayers department)* | TZS. 41, 935,256,752.75 NA USD 21,048,320.00 | TZS. 6, 598,419,473.52 NA USD 2, 746,634 | TZS. 5, 277,301,337.31 | TZS. 53,810,977,563.58 USD 23,794,954.00 |
| Idara ya Ushuru na forodha *(Customs and excise department)* | TZS. 696,304,219,416.58 | TZS. 1,890,092,298.91 | TZS. 87,856,823,935.06 | TZS. 788,215,480,248.77 NA USD 25,000 |

***Chanzo: Taarifa ya CAG ya Ukaguzi wa TRA kwa Mwaka wa Fedha Unaoishia Juni 30, 2018***

**Mheshimiwa Spika,** Kama jedwali 2.1 linavyofafanua hapo juu, kiasi kikubwa cha fedha za kodi kilikuwa kimehojiwa na CAG na kilikuwa haikajakusanywa hadi mwaka wa fedha unaoishia Juni 30, 2018. Ni kwa msingi huo Kamati inaendelea kuisisitiza TRA kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa kodi na kuzingatia weledi wa hali ya juu ili kuongeza ufanisi wa kiutendaji.

### 1.1.1 Kutokamilika kwa Usimikaji wa Mifumo Muhimu ya Uendeshaji na Usimamizi wa Shughuli za Bandari kati ya Mwaka 2010 – 2019

**Mheshimiwa Spika,** Mifumo ya usimamizi wa shughuli za Bandari ni nguzo muhimu katika udhibiti na usimamizi wa mapato yanayotokana na Bandari. Uwepo wa mifumo thabiti unaweza kusaidia ongezeko la mapato ambayo kwa sasa yanakuwa kwa wastani wa 8.7 kwa mwaka.

| Na. | Jina la Kampuni | Mwaka wa Mkataba | Kiasi cha Mkataba | Kiwango cha Kazi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | M/S SAAB PHAEROS BVDA | 2010 | EURO 127,750 | Ulikamilika |
| 2. | M/S SOFT TECH CONSULTANTS LIMITED | 2010 | TZS. 694,142,960 | Haukukamilika, ulisitishwa |
| 3. | M/S SAAB PHAEROS BVDA | 2014 | EURO 227,000 | Ulikamilika |
| 4. | M/S SAAB PHAEROS BVDA | 2014 | EURO 5,041,533 | Haukukamilika, ulisitishwa |
| 5. | M/S BUSINESS CONEXION | 2014 | USD 1,064,211 | Ulikamilika |
| 6. | M/S BUSINESS CONEXION | 2014 | USD 175,053 | Upo katika hatua za kukamilika |

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi suala la mifumo katika TPA kati ya mwaka 2010 hadi 2019. Kati kipindi hicho, TPA waliingia jumla ya Mikataba kumi na mbili yenye thamani ya kiasi cha **Euro 8,159,761.67 Dola za Marekani 15,625,546** na kiasi cha **shiling**i **694,142,960** kwa ajili ya shughuli zinazohusiana na usimikaji wa mifumo. Fedha hizi ni takribani **shilingi 57,566,143,400**.

**Mheshimiwa Spika,** Mchanganuo wa malipo na Kampuni zilizopewa kazi ya usimikaji mfumo kati ya mwaka 2010 hadi 2019 na kiasi cha kazi walizotekeleza umefafanuliwa katika Jedwali Na. 2.2 hapa chini: -

**Jedwali 2.2: Kampuni zilizopewa kazi ya usimikaji mifumo kati ya mwaka 2010 – 2019**

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 7. | M/S AMANDI HOLDING | 2014 | USD 6,314,576 + USD 1,436,319 | Mradi Unatumika bado |
| 8. | M/S SAAB PHAEROS BVDA | 2018 | EURO 117,148.23 | Ulikamilika |
| 9. | M/S TWENTY THIRD CENTURY SYSTEMS | 2015 | USD 6,635,387.16 | Upo katika hatua ya kufungwa |
| 10. | M/S SAAB TECHNOLOGIES BVBA | 2019 -2020 | EURO 233,935.44 | Ulikamilika |
| 11. | SAP EAST AFRICA LIMITED | 2019- 2021 | USD 997,647.04 | 50% kazi inaendelea |
| 12. | M/S SAAB TECHNOLOGIES BVBA | 2019- 2021 | EURO 2,412,395.00 | 32% kazi inaendelea |

***Chanzo:* Taarifa ya TPA kwa Kamati ya Tarehe 23 Januari, 2020**

**Mheshimiwa Spika,** Kama jedwali Namba 2.2 hapo juu linavyofafanua, Hoja ya Kamati katika suala hili ni kusisitiza umuhimu wa kukamilisha zoezi la usimikaji mifumo kwa wakati ili kuondoa mianya ya upotevu wa mapato ya Serikali. Aidha, kukamilika kwa usimikaji wa mifumo hiyo ni muhimu ili kupata thamani halisi ya fedha kwa malipo yaliyokwishafanyika kati ya mwaka 2010 hadi 2019.

**Mheshimiwa Spika,** Ni muhimu Serikali ikaangalia jambo hili kwa umakini ikiwa ni pamoja kuitumia Taasisi ya Serikali ya Wakala Mtandao *(E – Government)* kusimamia shughuli hizo ili kuepuka gharama kuongezeka.

### 1.1.2 Kutokuwepo kwa Makubaliano ya Mkopo kati ya Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) na Chuo Kikuu cha Dodoma na Kupungua kwa Mtaji wa Mfuko

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati katika taarifa ya hesabu zilizokaguliwa za Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF) kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018 ilibainika kuwa NHIF hawakuwa na Mkataba wa mkopo wa kimaandishi *(Witten loan agreement)* na Chuo Kikuu cha Dodoma. Mkopo unaohusika ni ule unaohusu ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa.

**Mheshimiwa Spika,** Mkopo huo ulitolewa kwa maelekezo kwamba kutatolewa dhamana ya Serikali *(Government guarantee)*. Hata hivyo, hadi Bodi na Menejimenti ya NHIF inafika mbele

ya Kamati[1], dhamana hiyo ilikuwa haijatolewa. Hadi kufikia tarehe 30 Juni, 2017, deni la mkopo huo lilifikia jumla ya **shilingi 82,736,176,217**.

**Mheshimiwa Spika,** Pamoja na uwepo wa jitihada za Bodi ya NHIF kufuatilia suala hilo Serikalini, lakini hadi sasa halijapata ufumbuzi. Hivyo ni muhimu hoja hii ikafanyiwa kazi kwa haraka ili kuhakikisha uwekezaji huo mkubwa na muhimu uliofanyika unaonekana dhahiri katika vitabu vya hesabu za NHIF kwa kuzingatia taratibu za kihasibu na Sheria za Nchi.

**Mheshimiwa Spika,** Hoja ya pili katika NHIF ni kupungua kwa mtaji wa Mfuko kunakotokana na kuongezeka kwa gharama za malipo ya matibabu na udanganyifu unaofanywa na watoa huduma za afya. Pamoja na kuongezeka kwa makusanyo ya michango kila mwaka, taarifa ya CAG ilibaini kuwa gharama za matibabu inazotolewa kwa wachangiaji wa hiyari[2] ni kubwa ukilinganisha na mapato yanayokusanywa kutoka kwa Wanachama hao.

**Mheshimiwa Spika,** Hivyo ni muhimu NHIF ikaendelea kuboresha taratibu za uchangiaji ili kuongeza mtaji wa Mfuko ili kuendana na ongezeko kubwa la gharama za matibabu pamoja na kuchukua hatua za kudhibiti malipo hewa na kudhibiti gharama za matibabu kutoka kwa watoa huduma wa afya.

### 1.1.3 Changamoto za Utendaji katika Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

**Mheshimiwa Spika,** Kwa mwaka wa fedha ulioishia Juni 30, 2018 CAG alishindwa kutoa maoni ya ukaguzi katika Shirika la Madini la Taifa (*Disclaimer of opinion)*. Hii ni mojawapo ya hati ya ukaguzi ambayo hutolewa pindi Mkaguzi anaposhindwa kupata taarifa za muhimu za kukamilisha ukaguzi wake na hivyo kukwazwa kwa mawanda ya ukaguzi. Jambo hili limeenda sambamba na kuongezeka kwa hasara ya Shirika kutoka **shilingi 715, 621, 000** (Juni, 2017) hadi **shilingi 2,387,167,000** (Juni, 2018).

**Mheshimiwa Spika,** Masuala ya msingi yaliyosababisha STAMICO kupata hati husika ya ukaguzi ni kama ifuatavyo:-

a) Kutojumuishwa kwa taarifa za hesabu za Kampuni Tanzu za STAMIGOLD Limited na *Kyerwa Tin Company Limited* katika hesabu jumuifu za STAMICO. Jambo hili ni kinyume na Kanuni [3]Namba 10 ya Kanuni za uandaaji wa hesabu kimataifa. Ni kwa msingi huo, hali halisi ya mali na madeni ya Kampuni hizo tanzu haijulikani hadi sasa.

b) Suala la pili katika STAMICO ni kuwa thamani ya jumla ya **shilingi bilioni 33** ambayo ni thamani ya uwekezaji uliofanywa na STAMICO katika Kampuni tanzu haina uhalisia. CAG alishindwa kupata uthibitisho wa kutosha wa thamani hiyo kutokana na kutokuwepo na taarifa sahihi za uwekezaji.

**Mheshimiwa Spika,** Kutokana na dosari hizo za kiuwekezaji, hali ya ufanisi wa STAMICO imekuwa ni changamoto kubwa. Uchambuzi wa Kamati umebaini kuwa, hadi sasa STAMICO imeshindwa kubaini iwapo inapata hasara au faida katika uwekezaji iliofanya katika mgodi wa *Buckreef Gold Company Limited*. Uwekezaji huu ulianza tangu mwaka 2011. Kutokutambua faida au hasara kutokana na uwekezaji wa hisa katika mgodi huo ni kinyume na matakwa ya Kanuni za Kimataifa za Ukaguzi [4](IAS) na hivyo kukwamisha jitihada za kuongeza faida kwa Serikali.

**Mheshimiwa Spika,** Uchambuzi wa Kamati ulibaini pia kuwa STAMICO ilikuwa haijafanya tathmini ya makubaliano baina yake na Kampuni ya Tanzanite One Mining Company ili kubaini

[1] Rejea Kikao cha Kamati na Bodi na Menejimenti ya NHIF cha tarehe 28 Agosti, 2019 - Dodoma
[2] Wanachama wa hiyari ni Wanachama wa Mfuko ambao hawapo katika mfumo rasmi wa ajira kama Watoto walio chini ya miaka 18, watumishi wa madhehebu ya kidini, Wajasiriliamali katika vikundi na Wanafunzi.
[3] IFRS 10
[4] IAS 28

iwapo makubaliano yao ni ya uendeshaji wa pamoja wa mgodi *(Joint operation)* au ni makubaliano ya ubia *(Joint venture)*. Ikumbukwe kwamba, matakwa ya Kanuni za uandaaji wa hesabu kimataifa [5](IFRS) yanaelekeza masuala hayo mawili yatolewe taarifa tofauti ili kutoa taswira halisi ya ufanisi wa Kampuni. Ni kwa msingi huo, taswira ya ufanisi wa STAMICO haiko bayana.

**Mheshimiwa Spika,** Changamoto nyingine inayokwaza ufanisi wa STAMICO ilikuwa ni kwa Shirika hilo kushindwa kutambua asilimia 10 ya thamani ya uwekezaji wake katika Kampuni ya Itetemia. Kwa STAMICO kushindwa kutambua jambo hili, kunaashiria kwamba STAMICO haipati faida stahiki zinazotokana na shughuli za uchimbaji zinazofanywa na Kampuni ya Itetemia Mining Company. Aidha, jambo hili pia linaenda kinyume na matakwa ya Kifungu cha 39 cha Kanuni za Ukaguzi za Kimataifa [6](IAS).

### 1.1.4 Dosari katika Usimamizi wa Ujenzi wa Vyuo vya Ualimu katika Fungu 46 - Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) imebainisha dosari kubwa katika usimamizi wa shughuli za ujenzi na ukarabati wa majengo katika vyuo mbalimbali vya Ualimu hapa Nchini. Shughuli hizo za ukarabati zimekuwa zikitekelezwa na Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia – Fungu 46.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imefanya uchambuzi wa kina wa Miradi hiyo ya ukarabati na ujenzi kwa mwaka 2017/2018 na kubaini dosari ambazo zinaweza kuisababishia Serikali hasara na kutopata thamani halisi ya fedha. Miradi hiyo na ufafanuzi wake ni kama ifuatavyo: -

#### a) Mradi wa Ujenzi wa Bwalo katika Chuo cha Ualimu Mpuguso

Mkataba wa Mradi huu uliingiwa kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Kampuni ya *M/S Lukolo Company Limited* kwa Mkataba Namba ME-024/CTR/HQ/2015-2016/11 lot 2 wenye thamani ya **shilingi 3,814,349,468** kwa ajili ya ujenzi na ukarabati wa chuo cha Ualimu Mpuguso.

Hadi mwezi Novemba, 2019 ambapo CAG alienda kufanya uhakiki wa Mradi alibaini kuwa Mkandarasi hakuwa katika eneo la kazi na hakuna kazi iliyokuwa inafanyika. Jambo hili linaashiria kutochukuliwa kwa hatua za haraka na uongozi wa Wizara ili kuondoa mkwamo katika ujenzi na ukarabati wa majengo husika hivyo kusababisha hasara kwa Serikali Aidha, kuchelewesha ujenzi kutokana na dosari za usimamizi kumesababisha ongezeko la gharama za ujenzi.

#### b) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Ualimu Kitangali

Katika Mradi huu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliingia Mkataba na Kampuni ya *G.E Engineering Construction Limited*, Mkataba wenye Namba ME-024/CTR/HQ/2015 kwa gharama za **shilingi 2,167,873,042.** Mradi huu ulihusisha ujenzi wa nyumba za watumishi saba na Bwalo la Wanafunzi na ulitakiwa kukamilika katika kipindi cha miezi 20.
Hata hivyo, uhakiki wa CAG uliofanyika mwezi Novemba 2018 ulibaini ucheleweshaji wa ujenzi wa Mradi husika. Mathalani, ilibainika kuwa ujenzi wa nyumba za watumishi ulichukua zaidi ya [7]miezi tisa ya ziada kinyume cha Mkataba. Dosari hizi kwa kiasi kikubwa zilitokana na usimamizi duni wa Wizara katika utekelezaji wa Mradi husika.

#### c) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Chuo cha Ualimu Shinyanga

[5] IFRS 11 (Joint Agreements)
[6] IAS 39 (Financial Instruments: Recognition and Measurement)
[7] Rejea Kifungu 17.1 cha General Conditions of the Contract (GCC)

Taarifa ya ukaguzi inabainisha kuwa, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iliingia Mkataba na Kampuni ya *M/S AFRIQ Engineering and Construction Co. Ltd* wenye gharama ya **shilingi 4,891,555,788** mnamo mwaka 2015/2016. Mkataba huo wenye Namba ME-024/CTR/HQ/2015-2016/13(LOT2) ulikuwa ni kwa ajili ya ujenzi wa majengo sita ikihusisha madarasa mawili, mabweni mawili, maktaba, ukumbi wa mihadhara, ukarabati wa mabweni na jiko.

Mradi huu ulianza tarehe 22 Agosti, 2016 na ulitakiwa kukamilika ndani ya kipindi cha wiki themanini (tarehe 04 Aprili, 2018). Hata hivyo, hadi wakati wa ukaguzi, mwezi Novemba, 2018 Mradi ulikuwa umezidisha wiki ishirini na nane za utekelezaji na ulikuwa umetekelezwa kwa asilimia sitini tu. Jambo hili linaendelea kudhihirisha mapungufu katika usimamizi wa Mikataba katika Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia.

**Mheshimiwa Spika,** Kama uchambuzi wa Kamati unavyotanabaisha hapo juu, Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia inatakiwa kuongeza jitihada za usimamizi wa Mikataba. Ucheleweshaji wa utekelezaji wa Mikataba unaongeza gharama za ujenzi na kuisababishia Serikali hasara.

#### 1.1.5 Kutokamilika kwa Muda Mrefu kwa Baadhi ya Miradi ya Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**Mheshimiwa Spika,** Shirika la Nyumba la Taifa (NHC) lina dhima kuu ya kujenga nyumba za biashara na makazi na kisha kuziuza hapa Nchini. Masuala ya msingi ambayo NHC hutakiwa kuzingatia katika uwekezaji ni pamoja na marejesho ya mtaji uliotumika kuwekeza (ROI)[8], muda wa marejesho ya uwekezaji na masuala mengineyo ya kiuchumi kwa wakati husika.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati imebaini uwepo wa Miradi kadhaa ya NHC ambayo imesimama kwa muda mrefu na hivyo kuwepo kwa viashiria vya Serikali kupata hasara siku zijazo. Mradi wa kwanza ni wa nyumba (711-1) uliopo Kawe – Dar es Salaam wenye thamani ya **shilingi bilioni 142.55**. Mradi huu umesimama tangu mwanzoni mwa mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Mradi mwingine ni wa ujenzi wa Victoria Palace wenye thamani ya **shilingi bilioni 34.14.** Mradi huu umesimama tangu mwaka 2017, ambapo pamoja na kusimama CAG alibaini ongezeko la gharama kwa zaidi ya **shilingi bilioni 6.86** ambalo anakiri hazikutolewa maelezo ya msingi[9].

**Mheshimiwa Spika,** Mradi mwingine ni wa nyumba (711-2) ambao upo eneo la Kawe – Dar es Salaam wenye thamani ya **shilingi bilioni 103**. Mradi huu umesimama tangu mwaka 2017 kutokana na ukosefu wa fedha. Hadi Mradi huu unasimama ulikuwa umetekelezwa kwa kiasi cha asilimia thelathini na kutumia jumla ya **shilingi bilioni 34.7**.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ilipata fursa ya kutembelea Miradi hiyo mitatu na kuona hali halisi ya utekelezaji wake. Hali ya Miradi hiyo sio ya kuridhisha kwa sasa ukizingatia ukweli kwamba imesimama kwa muda mrefu.

**Mheshimiwa Spika,** Kwa upande wa Miradi na (711-1) na (771 – 2), uwezekano wa NHC kupata hasara endapo itavunja Mkataba na Wakandarasi ni kubwa. Mathalani, taarifa ya CAG inafafanua kuwa NHC watalazimika kuwalipa Wakandarasi **shilingi bilioni 99.99** kama gharama za kuvunjwa Mkataba. Aidha, NHC watalazimika kurejesha **shilingi bilioni 2.6** kwa Wateja waliokwishaanza kulipia manunuzi ya nyumba hizo hapo awali.

**Mheshimiwa Spika,** Ni dhahiri kuwa utekelezaji wa Miradi hiyo ulianza bila kufanyika upembuzi wa kina hali iliyosababisha gharama za Miradi kuongezeka. Aidha, kuna viashiria vya kutowajibika ipasavyo kwa uliokuwa uongozi wa NHC katika kuhakiki gharama za Miradi hiyo. Hata hivyo, kuna umuhimu wa kuangalia namna bora ya kukamilisha Miradi hiyo ili kuepusha hasara kubwa ambayo NHC inaweza kupata hapo baadaye.

---

[8] Return on Investment (ROI)

[9] Rejea aya ya 4 ya Taarifa ya CAG kuhusu Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018 Uk. 147.

**Mheshimiwa Spika,** Kamati inasisitiza umuhimu wa kuangalia mkakati bora wa kukwamua Miradi hiyo kwa kulenga kupunguza hasara ambayo tayari imepatikana *(Loss reduction strategy)*.

### 1.1.6 Ucheleweshaji wa Utekelezaji wa Miradi ya Wakala wa Majengo Tanzania (TBA)

**Mheshimiwa Spika,** Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) ilipewa majukumu ya ujenzi wa majengo na Taasisi mbalimbali za Serikali kwa mikataba yenye gharama za takribani **shilingi 24,068,482,278**[10]. Uchambuzi wa Kamati umebaini na kuthibitisha ucheleweshaji wa utekelezaji wa Miradi husika.

**Mheshimiwa Spika,** Katika kushughulikia hoja ya TBA kutokamilisha Miradi kwa wakati, Kamati ilibaini dosari zifuatazo ambazo ndio sababu za kutokuwepo na ufanisi wa kutosha katika Wakala husika:-

a) Katika baadhi ya Miradi, vifaa vya ujenzi vilivyotolewa havikuwa vimepimwa na Wahandisi wa Miradi kwa kuzingatia makisio ya gharama za ujenzi (BOQ)[11]. Tafsiri ya jambo hili ni kwamba, thamani ya gharama zilizokuwa zinatolewa katika Miradi mingi ya TBA hazikuwa zinaakisi kazi iliyokuwa imefanyika hivyo kuleta ugumu wa kufanyika malipo kwa wakati.

b) Kuhamishwa kwa vifaa vya ujenzi kutoka Mradi mmoja kwenda Mradi mwingine. Jambo hili limesababisha ucheleweshaji wa kukamilika Miradi mingi kwa muda uliopangwa.

c) Upungufu mkubwa wa wataalamu na vifaa. Kwa mfano, Kamati ilibaini kuwa Miradi miwili ilikuwa inasimamiwa na Mratibu mmoja kwa wakati mmoja. Aidha, katika Miradi mingi vifaa vya ujenzi vilikuwa vinachangiwa kwa wakati mmoja.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG imebainisha baadhi ya Miradi ambayo TBA imeshindwa kukamilisha kwa wakati. Mfano ni Mradi wa ujenzi wa nyumba za "*Magomeni quarters*" wenye thamani ya **shilingi bilioni 20** na Mradi wa ujenzi wa nyumba za Askari Magereza - Ukonga Dar es Salaam wenye thamani ya **shilingi bilioni 10**. Katika Mradi wa nyumba za Askari Magereza Ukonga, Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania aliamua Mradi huo utekelezwe na Jeshi baada ya TBA kushindwa kuutekeleza ipasavyo.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi hiyo miwili ilianza kutekelezwa tarehe 01 Oktoba, 2016 na mwezi Machi, 2017 mtawalia. Aidha, Miradi yote miwili ilitakiwa kukamilika tarehe 15 Februari, 2018 na tarehe 05 Juni, 2018 mtawalia.

**Mheshimiwa Spika,** Mwezi Januari, 2019 uhakiki wa CAG katika Miradi husika ulibaini dosari kadhaa. Mathalani, katika Miradi yote ilibainika hali ya utekelezaji wa Miradi ilikuwa katika hatua ya kuweka zege katika ghorofa ya kwanza na ya nne. Hali hii ilikwenda kinyume na Mkataba kwani kwa kipindi hicho muda wa utekelezaji wa Miradi husika ulikuwa umekwishakamilika.

**Mheshimiwa Spika,** Miradi mingine inayotekelezwa na TBA na ambayo ina dosari za utekelezaji ni pamoja na ujenzi wa Ofisi ya Mkuu wa Mkoa Songwe, Makao Makuu ya TANROADS - Dodoma, Jengo la Tume ya Maadili - Dodoma, Jengo la Tume ya Uchaguzi – Dodoma, Jengo la Halmashauri ya Mji – Tarime, Jengo la Halmashauri ya Wilaya – Butiama na ujenzi wa Hospitali ya Rufaa – Geita.

### 1.1.7 Uwekezaji Uliofanywa na NSSF Katika Hisa za Vodacom Unaotoa Faida Ndogo Ukilinganisha na Dhamana za Serikali

[10] Rejea Ukurasa wa 140 wa Taarifa ya CAG kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu kwa Mwaka wa Fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018.
[11] Bill of Quantities

**Mheshimiwa Spika,** Mwongozo[12] wa Uwekezaji katika Mifuko ya Hifadhi ya Jamii unaelekeza kwamba, Mifuko iwekeze katika maeneo ambayo faida zake ni kubwa kuliko hati fungani (Dhamana) za Serikali. Aidha, kwa maeneo ambayo faida yake ni ndogo kuliko dhamana za Serikali, Mfuko husika utatakiwa kupata idhini ya Benki Kuu ya Tanzania (BOT) kabla ya kuwekeza katika maeneo hayo.

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya CAG imebainisha kuwa mnamo tarehe 05 Aprili, 2017 NSSF iliomba ridhaa ya BOT ili kuwekeza katika hisa za Vodacom ambazo faida yake ilikuwa chini ukilinganisha na dhamana za Serikali. Hata hivyo, kabla ya ridhaa husika kutolewa, tarehe 10 Aprili, 2017 Bodi ya NSSF iliidhinisha Mfuko kutumia kiasi cha **shilingi bilioni 40** katika kuwekeza katika ununuzi wa hisa za Vodacom bila ya kupata kibali cha BOT.

**Mheshimiwa Spika,** Mnamo tarehe 20 Aprili, 2017, BOT ilikataa kuidhinisha uwekezaji huo kwa msingi kuwa faida itakayopatikana ni ndogo ukilinganisha na faida ambayo NSSF ingepata kwa kununua dhamana za Serikali. Mathalani, endapo NSSF wangewekeza kwenye dhamana za muda mfupi *(Treasury bills)* zingetoa faida ya **15%** na zile za muda mrefu *(Bonds)* kwa miaka mitano zingetoa faida kwa **17.92%**

**Mheshimiwa Spika,** Faida zilizofafanuliwa hapo juu ni tofauti na faida ya **2%** ambayo NSSF inapata kwa mwaka kwa kuwekeza katika hisa za Vodacom. Kwa msingi huo, uwekezaji husika ulikiuka mwongozo wa uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii na una athari katika kutengeneza faida kwa Shirika.

**SEHEMU YA TATU**

## 2.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

### 2.1 Maelezo ya jumla

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na uchambuzi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu ukaguzi wa Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha unaoishia tarehe 30 Juni, 2018, Kamati ina maoni na mapendekezo kama ifuatavyo: -

### 2.2 Maoni

**Mheshimiwa Spika**, Maoni ya Kamati yanazingatia jukumu la Bunge kuwa chombo mahsusi cha usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kwa mantiki hiyo, Kamati ina maoni yafuatayo: -

**Mheshimiwa Spika,** Kamati ina maoni kuwa, kwa Maazimio ya Bunge kwa Taarifa ya Kamati ya mwaka uliopita, Serikali imefanya jitihada kubwa kutekeleza ushauri na Maazimio ya Bunge. Pamoja na jitihada zinazoendelea kuchukuliwa na Serikali, ni muhimu ushauri na mapendekezo ya Kamati za Bunge yakaendelea kuzingatiwa na Serikali ili kuondoa mianya yote ya upotevu wa fedha za umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Aidha, Kamati inaendelea kusisitiza kuwa, ni muhimu Taasisi za Serikali zikafanyia kazi kwa wakati hoja za ukaguzi zinazokuwa zimeibuliwa na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG). Jambo hili lifanyike sambamba na uchukuaji wa hatua za kisheria na kinidhamu kwa wahusika wanaokuwa wamethibitika kuhusika kwa namna moja au nyingine katika ubadhirifu wa fedha za umma.

### 2.3 Mapendekezo

[12] Kifungu cha 9(1) na (2) cha Mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Jamii wa Mwaka 2015.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati yametolewa kwa kuzingatia ukubwa wa athari ya hoja inayohusika, matokeo yenye kuambatana na hoja husika, uwezekano wa hoja kujirudia na hatua zinazotakiwa kuchukuliwa kushughulikia hoja husika [13]*(Risk levels)*.

**Mheshimiwa Spika,** Mapendekezo ya Kamati ni yale yanayolenga hoja zenye athari ya juu *(High risk issues)* na hivyo kuhitaji utekelezaji wa haraka ili kuondoa matumizi yasiofaa ya fedha za umma katika Taasisi za Serikali.

### 2.3.1 Kuhusu Hali ya Ufanisi wa Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA)

**KWA KUWA,** Kamati imefafanua kuhusu dosari za kiutendaji *(Inefficiency issues)* katika Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) pamoja na ucheleweshaji wa maamuzi ya rufaa za kodi Bodi na Baraza husika;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zimesababisha kutokukusanywa kwa mapato stahiki ya kodi kama yalivyofafanuliwa katika jedwali Na. 2.1;

**KWA HIVYO BASI,** Ili kuongeza ufanisi wa makusanyo ya kodi, Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali iziboreshe na kuziongezea uwezo Bodi ya Rufaa za Kodi na Baraza la Rufaa za Kodi kwa kuteua Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na Wajumbe wa kutosha ili kuziwezesha Taasisi hizi kufanya vikao vya kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati. Aidha, Serikali itoe bajeti ya kutosha kwa ajili ya Taasisi hizi ili zifanye kazi zake kwa wakati na kwa ufanisi. Hatua hizi zitasadia kupunguza mlundikano wa kesi za kodi zilizokaa muda mrefu bila kuhitimishwa;

b) TRA iwaongezee uwezo na ujuzi wafanyakazi wote wanaohusika na ukaguzi na ukadiriaji wa kodi kupitia mafunzo mbalimbali yatakayowawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi na hivyo kuongeza mapato ya Serikali kwa kukadiriwa kodi kwa usahihi; na

c) Serikali iongeze jitihada katika ukusanyaji wa kodi ambazo hazijalipwa na Walipa kodi. Jambo hili linaweza kufanikiwa kwa kuboresha na kukiongezea uwezo Kitengo cha ukusanyaji wa madeni na mikakati ya kuhakikisha kuwa kodi zote zinakusanywa kwa wakati baada ya kufanyiwa makadirio au uthamini hivyo kuzuia ulimbikizaji wa kodi.

### 2.3.2 Usimikaji wa mifumo muhimu ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za TPA

**KWA KUWA,** Kamati imebainisha changamoto ya kukamilika kwa wakati mchakato wa usimikaji mifumo muhimu ya usimamizi na uendeshaji wa shughuli za TPA;

**NA KWA KUWA,** Kutokamilika mwa mifumo hiyo kunaweza kutoa mianya ya upotevu wa mapato muhimu kwa Taifa;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali itumie Taasisi ya Umma ya Wakala Mtandao *(E – Government)* kusimamia na kuratibu shughuli zinazoendelea za uwekaji mifumo ya TPA. Jambo hili litasaidia kuweka uwajibikaji na kupunguza gharama ambazo Serikali imekwishaingia hadi sasa; na

b) Kumuomba Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG) kwa kadri atakavyoona inafaa, kufanya ukaguzi wa ufanisi *(Performance audit)* wa shughuli zinazohusu ununuzi na usimikaji wa mifumo katika Taasisi za Umma. Ukaguzi huu utakuwa muhimu ili kutoa

[13] Grouping of different risks according to their estimated cost of likely impact, likelihood of occurrence and countermeasures required

mwongozo na ushauri kwa Taasisi za Umma katika manunuzi ya mifumo ili kuepuka gharama zisizo za lazima kwa siku zijazo.

### 2.3.3 Mfuko wa Taifa wa Bima ya Afya (NHIF)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha kutokuwepo kwa makubaliano ya kimaandishi ya mkopo *(Written loan agreement)* wa **shilingi 82,736,176,217** kati ya NHIF na Chuo Kikuu Dodoma kuhusiana na ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa, pamoja na kupungua kwa hali ya mtaji wa Mfuko;

**NA KWA KUWA,** Kutokuwepo kwa makubaliano hayo ni dosari ya kiuhasibu katika Hesabu za Mfuko, na pia kupungua kwa hali ya mtaji kunaathiri uwezo wa kifedha wa Mfuko kutekeleza wajibu wake wa Kisheria;

**KWA HIYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Bodi ya Wakurugenzi ya NHIF na Bodi ya Wakurugenzi ya Hospitali ya Benjamini Mkapa wafuatilie kwa karibu Serikalini suala la makubaliano ya kimaandishi ya mkopo wa ujenzi wa Hospitali ya Benjamini Mkapa ili kufunga hoja husika;

b) Kuhusu mtaji wa mfuko, NHIF ihakikishe kunakuwepo mwenendo mzuri wa Mfuko, kwa kuongeza udhibiti na ufuatiliaji wa kiwango cha madai ya huduma ili kuepuka madai hewa ambayo yanaathiri shughuli za Mfuko; na

c) NHIF iendelee kufanya tafiti mbalimbali za kuboresha huduma zake ikiwa ni pamoja na kuangalia uwezekano wa kuwekeza asilimia fulani ya michango ya wanachama ili uwekezaji huo uje kusaidia malipo ya huduma za afya kwa wanachama pindi watakapostaafu.

### 2.3.4 Kuhusu Utendaji wa Shirika la Madini la Taifa (STAMICO)

**KWA KUWA,** Taarifa ya Ukaguzi katika Shirika la Madini la Taifa (STAMICO) imebainisha dosari kubwa za kiutendaji ikiwa ni pamoja na CAG kutoa " *disclaimer of opinion*" katika Hesabu za Shirika;

**NA KWA KUWA,** Dosari hizo zimesababisha Serikali kutopata faida stahiki kama gawio na kodi mbalimbali kutoka kwa STAMICO na Kampuni zake Tanzu;

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) Serikali kupitia Ofisi ya Msajili (TRO) wa Hazina iimarishe usimamizi wa karibu wa STAMICO ikiwa ni pamoja na kufanya tathmini ya shughuli za utendaji wa kila siku wa Shirika hilo;

b) Serikali ifanye mapitio ya Mikataba yote ambayo STAMICO imeingia na Kampuni Tanzu ili kuhakikisha makubaliano katika Mikataba yanatekelezwa ipasavyo na masharti hasi yanaondolewa; na

c) STAMICO ifanye uthamini wa mali zake ili kutambua thamani halisi ya mali za Kampuni kwa sasa.

### 2.3.5 Shirika la Nyumba la Taifa (NHC)

**KWA KUWA,** Taarifa ya CAG imebainisha uwepo wa Miradi mingi iliyo chini ya NHC ambayo imeshindwa kukamilika kwa wakati;

**NA KWA KUWA,** Kutokamilika kwa Miradi hiyo kumeongeza gharama za ujenzi na kuisababishia Serikali hasara kubwa, kutopatikana kwa thamani halisi ya fedha iliyowekezwa na pia kuwepo kwa uwezekano wa NHC kushtakiwa na Wakandarasi;

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba: -

a) Serikali iangalie namna bora ya kuiwezesha NHC kukamilisha Miradi ambayo ilikuwa katika hatua za mwisho za utekelezaji ili kupunguza hasara ambayo tayari imepatikana; na

b) Serikali iendelee na uchunguzi wa kina wa Miradi yote ya NHC ili kubaini dosari zilizopo katika Miradi husika. Baadhi ya Miradi imebainika kuwa ilitekelezwa kwa gharama zisizo halisia na usimamizi wake haukuwa na ufanisi.

### 2.3.6 Kutokamilika kwa wakati kwa Miradi ya TBA

**KWA KUWA,** Kamati imebainisha hali ya kutokamilika kwa wakati kwa Miradi inayotekelezwa na TBA hapa Nchini;

**NA KWA KUWA,** Kutokamilika kwa Miradi hiyo kunaisababishia Serikali hasara kwa kuongeza gharama za ujenzi na kuwanyima Wateja fursa za kutumia Miradi husika kwa wakati mwafaka;

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba:-

a) TBA waboreshe na kuimarisha Kitengo cha usimamizi wa utekelezaji wa Miradi ili kuhakikisha miradi yote inaanza na kukamilika kwa kuzingatia muda uliokubalika Kimkataba; na

b) TBA wabuni utaratibu wenye ufanisi wa udhibiti wa mifumo ya ndani katika utekelezaji wa Miradi hasa katika eneo la matumizi ya fedha, vifaa vya ujenzi na rasilimali watu ili kuharakisha utekelezaji wa Miradi.

### 2.3.7 Shirika la Taifa la Hifadhi ya Jamii (NSSF)

**KWA KUWA,** Uchambuzi wa Kamati katika Taarifa ya CAG ulibaini kuwa uwekezaji wa NSSF katika hisa za Vodacom haukuzingatia mwongozo wa Uwekezaji wa Mifuko ya Hifadhi ya Jamii;

**NA KWA KUWA,** Uwekezaji huo unatoa riba ndogo kuliko riba inayotolewa na dhamana za Serikali hivyo kuikosesha NSSF mapato stahiki;

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba, Serikali ifanye uchunguzi wa kina wa suala hili na kuchukua hatua stahiki kwa kuzingatia matokeo ya uchunguzi.

### 2.3.8 Usimamizi wa Mikataba ya Ujenzi katika Wizara ya Elimu , Sayansi na Teknolojia

**KWA KUWA,** Kamati imebaini mapungufu katika usimamizi wa shughuli za ujenzi na ukarabati wa vyuo vya Ualimu unaotekelezwa katika Fungu – 46 Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia;

**NA KWA KUWA,** Mapungufu hayo yamesababisha ongezeko la gharama za ujenzi na hivyo kuisababishia Serikali hasara na pia kutofikiwa kwa malengo ya Wizara;

**KWA HIVYO BASI,** Bunge linaazimia kwamba; Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia iimarishe Kitengo cha usimamizi wa Mikataba ya ujenzi na ukarabati. Aidha, majengo yote ambayo yapo katika hatua mbalimbali za ujenzi yakamilike na taarifa zitolewe kwa CAG.

## SEHEMU YA NNE

## 3.0 HITIMISHO

### 3.1 Shukurani

**Mheshimiwa Spika,** Taarifa ya Kamati imefafanua kwa kina changamoto na dosari mbalimbali yaliyojitokeza katika Hesabu za Serikali Kuu na Mashirika ya Umma kwa mwaka wa fedha wa 2017/2018 na kutoa mapendekezo ya namna ya kuondoa mapungufu hayo kwa lengo la kuhimiza uwajibikaji katika matumizi ya fedha za Umma.

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kutumia fursa hii kukushukuru wewe binafsi kwa uongozi wako makini ambao umeiwezesha Kamati yangu kutekeleza majukumu yake bila vikwazo kwa kutoa maelekezo na miongozo thabiti pale Kamati ilipohitaji msaada wako. Aidha, namshukuru Naibu Spika Mhe. Dr. Tulia Ackson pamoja na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kukusaidia kuongoza Bunge letu kwa ufanisi.

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru wajumbe wote wa Kamati ya Bunge ya Hesabu za Serikali kwa kutekeleza majukumu ya Kamati hii kwa uadilifu na weledi mkubwa.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kuwatambua Wajumbe hao kama ifuatavyo: -

1. Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb - **Mwenyekiti**
2. Mhe. Aeshi Khalfan Hilary, Mb **- M/Mkiti**
3. Mhe. Felister Aloyce Bura, Mb
4. Mhe. Dkt. Shukuru Kawambwa, Mb
5. Mhe. Dkt. Hadji Hussein Mponda, Mb
6. Mhe. Jamal Kassim Ali, Mb
7. Mhe. Hussein Abraham Makungu, Mb
8. Mhe. Livingstone Joseph Lusinde, Mb
9. Mhe. Musa Bakari Mbarouk, Mb
10. Mhe. Stanslaus Shing'oma Mabula, Mb
11. Mhe. Hassan Elias Masala, Mb
12. Mhe. Ignas Aloyce Malocha, Mb
13. Mhe. Ali Salim Khamisi, Mb
14. Mhe. Omar Mohamed Kigua, Mb
15. Mhe. Khadija Nassir Ali, Mb
16. Mhe. Mariam Nassoro Kisangi, Mb
17. Mhe. Maida Hamad Abdallah, Mb
18. Mhe. Josephine Tabitha Chagula, Mb
19. Mhe. Abdallah Haji Ali, Mb
20. Mhe. Aysharose Ndogholi Matembe, Mb
21. Mhe. Juma Hamad Omar, Mb
22. Mhe. Allan Joseph Kiula, Mb
23. Mhe. Rashid Abdallah Shangazi, Mb
24. Mhe. Rhoda Edward Kunchela, Mb
25. Mhe. Kiswaga Boniventura Destery, Mb
26. Mhe. Joyce Bita Sokombi, Mb
27. Mhe. Anatropia Lwehikila Theonest, Mb
28. Mhe. Oliver Daniel Semuguruka, Mb

**Mheshimiwa Spika,** Napenda kumshukuru Katibu wa Bunge Ndugu Stephen Kagaigai kwa ushauri wake kwa Kamati pale alipotakiwa kufanya hivyo. Natoa Shukurani kwa Idara ya Kamati za Bunge kwa kuratibu shughuli za Kamati, kupitia kwa Mkurugenzi Ndugu Athuman Hussein, Mkurugenzi Msaidizi Ndugu Michael Chikokoto, Makatibu wa Kamati Ndugu Erick Maseke na Ndugu Wilfred Magova.

**Mheshimiwa Spika,** Mwisho Kamati inatambua na kuthamini ushirikiano mkubwa ilioupata kutoka kwa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, Charles Kichere, Mhasibu Mkuu wa Serikali (AcGen) Ndugu Francis Mwakapalila na Msajili wa Hazina (TR) Ndugu Athuman Mbutuka. Aidha naishukuru Kurugenzi ya Usimamizi wa mali za Serikali (DGAM) kwa kuendelea kuisadia Kamati katika utekelezaji wa shughuli zake kwa weledi na ufanisi.

**3.2 Hoja**

**Mheshimiwa Spika,** Nawashukuru Waheshimiwa Wabunge wote kwa kunisikiliza. Naomba kutoa Hoja.

Mhe. Naghenjwa Livingstone Kaboyoka, Mb
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA**
**HESABU ZA SERIKALI (PAC)**
29 Januari, 2020

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Hoja imeungwa mkono, Mheshimiwa Kaboyoka kwa sababu unaenda kukaa ungekunywa kabisa maji.

Mheshimiwa Abdallah Chikota, Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwa niaba ya Mwenyekiti ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mitaa *(LAAC),* naomba kuwasilisha Bungeni maoni na mapendekezo ya Kamati kuhusu taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Hesabu za Serikali za Mitaa kwa mwaka wa fedha Ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Wasilisho hili ni kwa mujibu wa kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kwa sababu za muda, naomba uniruhusu kuwasilisha Taarifa hii kwa Mhutasari lakini Wajumbe wote pamoja na *Hansard* waichukue Taarifa Kuu kama ilivyopakiwa katika Vishikwambi (*tablets*).

Mheshimiwa Naibu Spika, Taarifa hii imegawanyika katika Sehemu Kuu Tatu. Sehemu ya Kwanza ipo katika Ukurasa wa 1- 7 wa Taarifa Kuu. Sehemu hii inatoa utangulizi kuhusu Chimbuko la Kamati ya *LAAC*, shughuli zilizotekelezwa, Orodha ya Wadau na Mafanikio yaliyopatikana katika kutekeleza shughuli za *LAAC*. Sehemu hii inahusika na uongozi wa LAAC tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997, inaelezwa pia kuwa tangu kuanzishwa kwake mwaka 1997, *LAAC* imeongozwa na Wenyeviti Saba ambao ni: Mheshimiwa Stephene Galinoma, Mheshimiwa Warid Kaborou, Mheshimiwa Mgana Msindai, Mheshimiwa Wilbroad Slaa, Mheshimiwa Agustino Mrema, Mheshimiwa Rajab Mbarouk na sasa Mheshimiwa Vedastor Ngombale, Mbunge wa Kilwa Kaskazini.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Pili ya Taarifa hii i ipo Ukurasa wa 8-26 ya Taarifa Kuu. Sehemu hii inahusu Masuala matatu yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la kwanza ni kuhusu hali halisi ya Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Serikalini. Suala hili limefafanuliwa katika Ukurasa wa 8-11 wa Taarifa Kuu. Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati Serikalini ni wa kuridhisha. Hali kadhalika Ushirikiano kati ya *LAAC* na Ofisi ya Rais, TAMISEMI (Serikali za Mitaa) ni mzuri. *LAAC* inasisitiza kuwa ahadi za Serikali kuhusu utekelezaji wa Mapendekezo yaliyosalia zinapaswa kutekelezwa kwa vitendo ili kuimarisha nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na ubora wa huduma kwa wananchi katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusu hali halisi ya utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mamlaka ya Serikali ya Mitaa. Sehemu ya pili ya taarifa yetu inaelezea pia kuhusu hali halisi iliyopo katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Hali hii imefafanuliwa katika Hali hii imefafanuliwa katika Ukurasa wa 11-12 wa Taarifa Kuu. Changamoto kubwa iliyopo katika utekelezaji na ubora wa kazi katika baadhi ya miradi ya maji na ujenzi wa vyumba vya madarasa, nyumba za Walimu na zahanati. Miradi mingi ya maji haikamiliki kwa wakati wakati miradi ya ujenzi inatekelezwa chini ya viwango kutokana na usimamizi usioridhisha.

Pia kuna kukiukwa kwa taratibu za manunuzi katika baadhi ya Halmashauri mathalani katika Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma-Ujiji, Wilaya ya Songea na Shinyanga. Taarifa Kuu imefafanua zaidi kuhusu changamoto zilizopo kwenye miradi hii katika halmashauri hizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Sehemu ya Tatu ya Taarifa yetu inahusu Maoni na Mapendekezo ya Kamati kuhusiana na Hoja mbalimbali za Ukaguzi. Sehemu hii inapatikana katika Ukurasa wa 27-35 wa Taarifa Kuu ikiwa na Mapendekezo katika maeneo tisa (9) yaliyochambuliwa katika sehemu hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya pili kama nilivyosema inahusu Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi, Uchambuzi huu upo katika Sehemu ya Pili ya Taarifa Kuu katika Ukurasa wa 23-26. Hoja zilizochambuliwa zinahusu masuala tisa (9) yafuatayo:-

Mheshimiwa Naibu Spika, Suala la kwanza ni Halmashauri kutopatiwa kiasi stahiki cha fedha za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kutoka Hazina. Katika mahojiano na Mamlaka ya Serikali za Mitaa ilibainika kwamba kiasi cha ruzuku ya fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida kinachopelekwa na Serikali Kuu katika Halmashauri na kufanyiwa ukaguzi na *CAG* ni kidogo ikilinganishwa na kiasi cha fedha hizo ambacho Hazina inadai kuwa imepeleka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, kuna kutofautiana kwa takwimu kati ya Hazina, Ofisi ya CAG na Ofisi ya Rais TAMISEMI. Hali hii inaathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri. Aidha, hali hii inaibua migongano katika vyombo vya usimamizi wa fedha za umma mathalani Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi, Wizara ya Fedha na Mipango (Hazina) na Ofisi ya Rais, TAMISEMI. Hii ni kwa sababu chombo kimoja kinakuwa na taarifa tofauti na kingine mbele ya Kamati ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la pili ni kuhusu Halmashauri kutokukusanya kikamilifu mapato ya ndani mbali na kuwa na makadirio ya chini ya viwango vya makusanyo, Halmashauri nyingi hazifikii malengo hayo. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Halmashauri zote nchini zilitarajia kukusanya kiasi cha bilioni 687 kutoka katika vyanzo vya mapato yao ya ndani lakini zilikusanya jumla ya shilingi bilioni 553 tu. Hii ni sawa na asilimia 71 ya makadirio Kwa maana kwamba 29% ya mapato hayo haikukusanywa. Wastani wa jumla ya mapato yote ya Serikali za Mitaa hauzidi 1% ya mapato yote ya ndani ya Serikali. Bila ya ruzuku ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa nchini haziwezi kuendesha shughuli zake hata kwa mwezi mmoja. Sababu zinazochangia udhaifu huo zimeelezwa kwa kina katika Ukurasa wa 15 na 16 wa Taarifa Kuu. Baadhi yake ni hizi zifuatazo:-

(a) Utaratibu wa Serikali Kuu kuhodhi vyanzo vya uhakika vya mapato vilivyoko katika Mamlaka za Serikali za Mitaa mathalani kodi ya majengo na ushuru wa mabango ya biashara mbalimbali ambavyo kwa sasa vinakusanywa na *TRA*, ushuru wa maegesho ya magari unaokusanywa na *TARURA* na kodi ya ardhi inayokusanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(b) Utaratibu wa Serikali Kuu kutozirejeshea Halmashauri hizo kiasi stahiki cha cha gawio la mapato yanayokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali vilivyoko katika maeneo yao;

(c) Kukosekana kwa uaminifu miongoni mwa Watendaji wa Halmashauri wanaokusanya mapato hayo; na

(d) Uduni wa mtandao wa mawasiliano *(internet)* katika Halmashauri zilizo katika mikoa ya pembezoni mathalani Mkoani Ruvuma na Kigoma ambao unaathiri ufanisi wa mashine za kukusanyia mapato kwa njia za kieletroniki *(PoS)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tatu ni ambalo limechambuliwa ni Halmashauri kutozingatia Miongozo hii ya Matumizi ya Fedha. Zipo baadhi ya Halmashauri zisizozingatia Miongozo hii. Kwa mfano katika Ukurasa wa 19 na 20 wa Taarifa Kuu tumeonesha Jedwali la Mifano ya namna Halmashauri za Wilaya za Mkalama, Songea, Singida, Makete, Shinyanga, Iringa na Manispaa ya Kigoma-Ujiji zilivyokiuka Miongozo hii. Pamoja na hatua zingine, ni muhimu Ofisi ya Rais, TAMISEMI ikajiimarisha zaidi katika kufuatilia na kutathmini utendaji wa Halmashauri kwa kila mkoa na nchi nzima ili kuboresha nidhamu ya matumizi za fedha za umma na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne, ni Upotevu wa mapato ya Halmashauri kutokana na uzembe wa Idara za Afya katika kujaza *form* za madai ya Bima ya Afya. Kamati ya *LAAC* imebaini kuwa kutokana na Watendaji katika Idara za Afya kujaza vibaya fomu za bima za afya, Halmashauri nyingi zimekuwa hazirejeshewi madai yao kutoka *NHIF*. Hivyo zinapata hasara ya huduma za afya zinazozitoa kwa wagonjwa wanaotumia bima hizo. Hoja hii ipo katika Halmashauri nyingi ingawa Jedwali Na.5 katika Ukurasa wa 22 wa Taarifa Kuu linaonesha mifano michache tu. Hali hii isipotafutiwa ufumbuzi itakomaa na kuwa mwanya mkubwa wa upotevu wa mapato katika Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano, ni Upotevu wa Mapato ya Halmashauri kutokana na Malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani *(VAT)* na kodi ya zuio. Hali hii huongeza gharama za utekelezaji wa miradi kwa sababu kuna kiasi kikubwa cha fedha huelekezwa kwenye malipo ya *VAT* badala ya kuwa gharama halisi za utekelezaji wa mradi.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la sita, ni upungufu wa Watumishi katika Idara mbalimbali za Halmashauri. Halmashauri mbalimbali nchini zinakabiliwa na uhaba wa Watumishi katika kada mbalimbali. Kada iliyoathiriwa zaidi ni Waalimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari, Walimu wa shule za Msingi, Wauguzi, Wakaguzi wa Ndani, Wahasibu na Wahandisi (Ujenzi). Hali hii inachangia sana katika kudorora kwa ufanisi wa huduma mbalimbali za afya, elimu, ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ile inayotumia *force accounts* na kuhitaji usimamizi mkubwa na wa karibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la saba, ni madai ya fedha Kutokana na stahili mbalimbali za Watumishi Serikalini na Madiwani. Yapo madai ya fedha zinazotokana na stahili mbalimbali za Watumishi Serikalini na Madiwani katika Halmashauri mbalimbali. Watumishi wana madai ya fedha za uhamisho, likizo na malimbikizo ya mishahara. Pia Waheshimiwa Madiwani wanadai posho za mwezi na vikao mbalimbali vinayoendeshwa kisheria katika mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ukosaji wa malipo hayo unaathiri morali na ufanisi katika kazi zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nane ni baadhi ya Halmashauri kuwa na Ofisi Kuu katika maeneo yasiyo yao kijiografia na kiutawala. Hali hii ipo katika Halmashauri za Wilaya za Iringa, Tarime, Mbogwe, Kondoa na Sumbawanga. Kwa tafsiri ya Kamati yetu ya *LAAC*, huko ni kujitenga na watu ambao Halmashauri hizo zinawatumikia na ni kuongeza gharama za utendaji na utawala kusikokuwa na ulazima. Kwa hili tunampongeza Mheshimiwa Rais wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania kwa sababu hivi karibuni ametoa maagizo kwamba halmashauri hizi zote ziwe na ofisi zao katika maeneo ya kijiografia na kiutawala. Tunampongeza sana Mheshimiwa Rais.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tisa, ni baadhi ya Halmashauri kutokupeleka michango ya kisheria ya kila mwezi ya malipo ya uzeeni ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Katika baadhi ya Halmashauri (Mfano; Halmashauri za Wilaya za Songea, Mafia, Busega pameanza kuibuka utamaduni wa kutokupeleka michango ya malipo ya uzeeni ya Watumishi katika Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii. Utamaduni huu usipokemewa ni mzigo na hasara kubwa kwa Halmashauri zenyewe na Watumishi husika pindi watakapostaafu kazi. Halmashauri zitadaiwa madeni pamoja na kiasi kikubwa cha riba.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu ya tatu, ya taarifa yetu inahusu maoni na mapendekezo. Mapendekezo yafuatayo yanatolewa kufuatia Uchambuzi Uliofanyika katika Sehemu ya Pili ya Taarifa Kuu. Kabla ya kusoma Mapendekezo haya, naomba niwakumbushe Wajumbe kuwa katika Taarifa Kuu kuna maelezo ya awali ya Mwenyekiti ambayo ni Sehemu ya Taarifa ya Kamati. Ninashauri Maelezo hayo yasomwe na kuzingatiwa na Serikali kwa ajili ya maboresho katika Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pendekezo la kwanza inahusu kutofautiana kwa takwimu na upatikanaji wa fedha kutoka Hazina. *LAAC* inapendekeza mambo mawili (2) yafuatayo:-

Kwanza, Wizara ya Fedha na Mipango, Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Ofisi ya Ukaguzi wafanye usuluhisho wa pamoja kuhusu sababu zinazosababisha kutokea kwa tatizo hili. Taarifa ya Majadiliano hayo ya Pamoja iwasilishwe mbele ya *LAAC* mapema kabla ya kuanza kwa Vikao vya Uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa za mwaka 2018/2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pili agizo lingine ni Serikali iwe inatoa ipasavyo kiasi cha fedha kinachokuwa kimetengwa na Bunge kwa ajili ya shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida katika taasisi mbalimbali nchini ikizingatiwa kuwa utaratibu huo unakuwa umetungiwa Sheria mahsusi ya Fedha kwa kila mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu Halmashauri kutokukusanya ipasavyo mapato yake ya ndani, *LAAC* inapendekeza mambo yafuatayo:-

(a) Mosi, dhana ya kuibua vyanzo vipya vya mapato itekelezwe kikamilifu katika ngazi zote za Serikali, kwa maana ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Dhana hii ikitekelezwa kwa ustadi na kwa vitendo itaziwezesha Serikali za Mitaa kubakia na vyanzo vya uhakika vya mapato ambavyo kwa sasa vimechukuliwa na Serikali Kuu.

(b) Serikali Kuu ijielekeze pia katika kutoa ushauri wa kitaalam na usimamizi katika mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Idara za Serikali zinazohusika na ukaguzi na ufuatiliaji zijizatiti kufuatilia hali halisi ya ukusanyaji wa mapato katika mifumo ya kielektroniki ili kuongeza ufanisi na kudhibiti mianya ya upotevu.

(c) Serikali itumie ipasavyo fursa ya kuwepo kwa Mkongo wa Taifa ili kuboresha mawasiliano ya *internet* kwa maeneo yaliyo pembezoni mwa nchi ili kuwezesha *PoS* kufanya kazi kwa ufanisi;

(d) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe Vitengo vya Ukaguzi wa ndani pamoja na Vitengo vya Sheria; Vitengo vya Manunuzi na Uhasibu ili masuala yanayohusu ukusanyaji na utumiaji wa fedha yafanyike kwa utaalam kwa kuzingatia sheria, kanuni na miongozo iliyopo;

(e) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziongeze ubunifu katika vyanzo vya mapato na kuhuisha kiasi cha tozo, kodi na ushuru unaotozwa katika vyanzo hivyo ili kuvutia wateja; na

(f) Mabaraza ya Madiwani yapewe mafunzo ya usimamizi wa mapato na matumizi ya fedha za umma katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tatu ilikuwa ni baadhi ya halmashauri kutozingatia miongozo ya manunuzi ya umma. Kamati ya *LAAC* inapendekeza kwamba Mfumo wa Manunuzi ya Umma kwa njia ya Mtandao uimarishwe na kutumiwa katika taasisi zote za Serikali nchini. Watumishi watakaobainika kukiuka taratibu zilizowekwa kwa mujibu wa sheria bila ya kuwa na sababu za msingi wawajibishwe.

Aidha, Kamati inapendekeza pia kwamba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi iombwe kufanya Ukaguzi Maalum katika Hesabu za Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 katika Halmashauri za Manispaa ya Kigoma Ujiji na Wilaya ya Songea ili kubaini sababu na wahusika katika ukiukwaji mkubwa wa matumizi ya fedha za umma uliobainika katika Taarifa za Hesabu za Halmashauri hizo.

Mheshimiwa Naibu Spika, hapa kuna matumizi makubwa sana ya fedha ambazo hazijawasilishwa benki, halmashauri inakusanya lakini inafanya matumizi kabla fedha hazijaenda benki. Ndiyo maana tumemuomba *CAG* afanye *special audit* katika halmashauri hizi mbili, Kigoma Ujiji na ile Halmashauri ya Wilaya ya Songea.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la nne lilikuwa ni upungufu wa watumishi katika Kada mbalilimbali zilizopo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Ombwe hili lina madhara hasi katika viwango vya huduma na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa ile inayotumia *force accounts*. Ni vyema Serikali ikatafuta namna ya kuziba ombwe hili kwa kuajiri watumishi wa kada husika.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala la tano lilikuwa ni madai ya posho za madiwani na watumishi wa Serikali na changamoto zake katika ufanisi wa utendaji wao. Kamati ya *LAAC* inashauri kuwa madeni haya yawekewe utaratibu madhubuti wa kuyakusanya, kuyahakiki mapema katika vituo vyao vya kazi ili yaweze kulipwa. Kamati inaomba madeni ya Waheshimiwa Madiwani yalipwe mapema kabla ya Mabaraza ya Madiwani hayajavunjwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, itakuwa ni ukiukwaji wa haki endapo Mabaraza ya Madiwani yatavunjwa na madiwani wataenda kwenye mchakato wa uchaguzi wakati wanadai stahili zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya sita ni upotevu wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na Uzembe katika ujazaji wa fomu za Bima ya Afya (*NHIF*). Kamati inashauri kwamba Serikali itoe elimu kwa watumishi wake juu ya ujazaji bora wa fomu hizi lakini pia ibuni mbinu madhubuti ya kudhibiti udanganyifu katika kujaza fomu hizi ili huduma za afya zizidi kuwa bora na endelevu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya saba ilikuwa baadhi ya halmashauri kuwa na ofisi katika maeneo yasiyo yao Kijografia na Kiutawala. Kamati inapendekeza kwamba kila halmashauri na iwezeshwe kuwa na ofisi zake kuu ndani ya maeneo yake ya kijografia na kiutawala ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa wananchi wake. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya nane ilikuwa upotevu wa mapato ya halmshauri kutokana na malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani na kodi ya Zuio. Ofisi ya Rais-TAMISEMI izisimamie kikamilifu halmashauri kuhakikisha kuwa hazilipi *VAT* kwa wakandarasi wanaotekeleza miradi ambayo ina msamaha wa kodi hiyo. Hoja ya tisa ni baadhi ya halmashauri kutokupeleka michango ya kisheria ya kila mwezi ya malipo ya uzeeni ya watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii. Kamati inapendekeza kwamba Ofisi ya Rais-TAMISEMI na mifuko husika ya Hifadhi za Jamii ziongeze juhudi za kuzisimamia halmashauri ili kuhakikisha kuwa michango hiyo inalipwa kwa wakati. Aidha, Wakurugenzi Watendaji watakaobainika kuzembea wawajibishwe kwa uzembe huo kwa sababu ni wajibu wao kuchangia michango hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya *LAAC* inamshukuru Mheshimiwa Spika kwa miongozo na ridhaa mbalimbali zilizowezesha utekelezaji wa bora wa shughuli zake za kamati. Pia tunakupongeze wewe Naibu Spika na Wenyeviti wote wa Bunge kwa kwa miongozo yao katika nyakati mbalimbali. Aidha, tunamtakia Mheshimiwa Mussa Zungu, Mbunge aliyekuwa Mwenyekiti wa Bunge utekelezaji mwema wa majukumu yake mapya ya Uwaziri.

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ya *LAAC* pia inaishukuru Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge chini ya Katibu wa Bunge Bwana Stephen Kagaigai kwa ufanisi wake katika kupanga, kutafiti, kushauri, kuratibu na kufuatilia vema utekelezaji wa shughuli za Kamati. Tunawapongeza sana Watendaji wake ambao ni Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndugu Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndg. Dismas Muyanja, Dickson M. Bisile na Ndugu Waziri Kizingiti.

Mheshimiwa Naibu Spika, shukrani za kipekee ziifikie Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (*NAO*) chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndugu Charles E. Kichele kwa ufafanuzi mahiri wa hoja za ukaguzi na kwa mahusiano mema na kamati yetu. Tunaishukuru pia Ofisi ya Katibu Mkuu Wizara ya Fedha na Mipango (HAZINA), Ofisi ya Rais–TAMISEMI na Watendaji wote wa Serikali ambao kwa namna moja au nyingine wameiwezesha Kamati ya *LAAC* kutekeleza majukumu yake kikamilifu.

Aidha, ninaomba kutoa shukrani pia kwa Asasi mbalimbali za Kiraia, vyombo vya habari na wananchi kwa ujumla kwa ushirikiano wao. Nitoe shukrani kwa wajumbe wa kamati ambao orodha yake ipo lakini kwa sababu ya muda naomba orodha yote iingie kwenye hansard.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja; naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki mapendekezo ya Kamati ya *LAAC* juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2018 ili mapendekezo hayo sasa yawe Maazimio ya Bunge.

**MHUTASARI WA MAONI NA MAPENDEKEZO KUHUSU TAARIFA YA MDHIBITI NA MKAGUZI MKUU WA HESABU ZA SERIKALI KATIKA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA WA FEDHA ULIOISHIA TAREHE 30 JUNE, 2018 – KAMA ILIVYOWASILISHWA MEZANI**

**MAELEZO YA AWALI YA MWENYEKITI**

***Mheshimiwa Spika****, mnamo mwaka 2016, nilipata fursa ya kuwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC). Nawashukuru sana Wabunge wenzangu walionichagua, Watumishi wa Bunge waliotuhudumia, Serikali na Wadau mbalimbali wa ndani na nje ya nchi walioshirikiana nasi. Kutoka kwao, nimejifunza kuhusu shughuli za Bunge na maisha ya Bunge kwa ujumla, ufanisi wa kazi Bungeni na nje ya Bunge. Nimejifunza kuhusu muundo wa Serikali za Mitaa nchini, utendaji wake na mifumo yake ya kifedha, wajibu wa CAG na uhusiano wake na Bunge. Zaidi nimejifunza kuhusu umuhimu wa Kamati za Kudumu za Bunge katika kurahisisha utekelezaji wa Shughuli za Bunge kwa kina zaidi.*

***Mheshimiwa Spika,*** *kupitia nafasi hii, nimeshuhudia mabadiliko yenye tija katika nidhamu ya matumizi ya fedha za umma na kuimarika kwa utoaji wa huduma mbalimbali kwa jamii katika Halmashauri. Halmashauri zilizo nyingi kwa sasa zinafanya jitihada za kuboresha mifumo ya ukusanyaji, uhifadhi na utumiaji wa fedha za umma. Kuna mwamko wa Wananchi kushiriki katika shughuli za maendeleo na kufanyakazi kwa juhudi na maarifa. Kuna ongezeko la shule za umma za msingi na sekondari. Ingawa bado hazitoshi ikilinganishwa na idadi ya Watoto. Kuna ongezeko la zahanati na vituo vya afya, huduma za fedha na shughuli za kibiashara kwa wananchi, umeme, ulinzi na usalama wa raia na mali zao. Hali hii imejidhihirisha pia kufuatia*

*kupungua kwa hoja za Ukaguzi na kuongezeka kwa idadi ya Hati Safi za Ukaguzi katika Halmashauri kwa kila mwaka. Nafurahi kuwa nimekuwa sehemu muhimu ya mafanikio haya.*

***Mheshimiwa Spika,*** *Wakati wa kujadili hoja za Ukaguzi katika Halmashauri, nimebaini kuwa juhudi za pamoja zinatakiwa katika maeneo mbalimbali. Kwa mfano: Upatikanaji wa huduma za maji safi na salama haukidhi mahitaji ya Wananchi katika kuchochea shughuli mbalimbali za maendeleo majumbani, mashambani na viwandani. Huduma za kifedha mathalani mikopo kwa Wajasiriamali zina riba kubwa kiasi cha kutowasaidia Wajasiriamali kuchangia ipasavyo katika ukuaji wa uchumi wa Halmashauri na Taifa kwa ujumla. Vyanzo vya uhakika vya mapato ya ndani ya Halmashauri vimechukuliwa na Serikali Kuu kiasi cha kuongeza zaidi utegemezi wa Halmashauri katika Serikali Kuu. Kiasi cha fedha za maendeleo hakipelekwi katika Halmashauri kwa namna kinavyopitishwa na Bunge hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi hiyo. Katika baadhi ya maeneo Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani ni dhaifu kiasi cha kuathiri udhibiti wa ndani wa matumizi ya fedha za umma na udhibiti wa vihatarishi mahala pa kazi. Baadhi ya Halmashauri zina upungufu mkubwa wa Watumishi kiasi cha kuathiri usimamizi wa shughuli mbalimbali za maendeleo hasa zile zinazotumia force accounts.*

***Mheshimiwa Spika****, Nafurahi pia kwamba nimekuwa miongoni mwa Watanzania walioziona changamoto hizo na kupaza sauti. Nawakaribisheni sana Wabunge wote, Serikali, Wanataaluma, Waandishi wa Habari, AZAKI, Wadau mbalimbali wa Maendeleo, na Wananchi kwa ujumla tuisome na kuielewa vema Taarifa hii kisha kushiriki katika utekelezaji wa mapendekezo yake kila mmoja kwa nafsi, sehemu na uwezo wake.*

Vedasto E. Ngombale, Mb.
**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**

## SEHEMU YA KWANZA

### 1.0 MAJUKUMU YA KAMATI NA UTEKELEZAJI WAKE

### 1.1 MAELEZO YA JUMLA

**Mheshimiwa Spika**, Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa (LAAC) iliundwa mwaka 1997 baada ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Mashirika ya Umma (POC) kugawanywa katika Kamati mbili (LAAC na PAC). Msingi wa majukumu yanayotekelezwa na LAAC ni Ibara ya 96(2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano (1977) na yamefafanuliwa zaidi katika Kanuni za Kudumu za Bunge Toleo la Januari, 2016 kuwa ni: kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa kwa mujibu wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali, kutoa na kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake Serikalini. Serikali za Mitaa ni ngazi za kiutawala za utekelezaji wa shughuli za Serikali katika Wilaya, tarafa, kata, vijiji na vitongoji nchini[1].

Halmashauri ni vyombo vya uratibu, upangaji na usimamizi wa shughuli za maendeleo katika ngazi hizo. Vyombo hivi, vina wajibu pia wa kuratibu mapato, matumizi na upatikanaji huduma mbalimbali za jamii katika ngazi hizo. Hadi kufikia Januari 2020, Tanzania Bara ina jumla ya Halmashauri 185 kwa mgawanyo wa Majiji (6), Manispaa (20), Miji (22) na Wilaya (135)[2]. Kwa sasa, LAAC inashughulikia Taarifa za Hesabu zilizokaguliwa Halmashauri 185 za Tanzania Bara. Katika kutekeleza jukumu hilo tangu mwaka 1997 hadi 2020 (Bunge la Kumi na Moja), LAAC imeongozwa na Wenyeviti Saba Wafuatao:

(1) Mwaka 1997- 1998- Mhe. Stephene J. Galinoma (CCM - Kalenga).
(2) Mwaka 1999- 2000- Mhe. Warid A.Kaborou (CHADEMA - Kigoma Mjini).
(3) Mwaka 2000- 2008- Mhe. Mgana I. Msindai (CCM - Iramba Mashariki).
(4) Mwaka 2008- 2010- Mhe. Wilbroad P. Slaa (CHADEMA - Karatu).
(5) Mwaka 2011- 2013- Mhe. Augustine L. Mrema (TLP - Vunjo).
(6) Mwaka 2013- 2015- Mhe. Rajab M. Mbarouk (CUF- Ole, Pemba)
(7) Mwaka 2016- 2020- Mhe. Vedasto E. Ngombale (CUF - Kilwa Kaskazini).

**Mheshimiwa Spika**, baada ya Utangulizi huo, naomba kwa mujibu wa Kanuni ya 117(15) ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016, kuwasilisha Taarifa ya Maoni na Mapendekezo ya LAAC kuhusu Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 juni, 2018 kuhusiana na mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

### 1.2 MUUNDO WA TAARIFA

**Mheshimiwa Spika**, Taarifa hii imegawanyika Sehemu Kuu Tatu. **Sehemu ya Kwanza** inafafanua msingi wa Kikatiba wa kuwepo kwa LAAC na Kamati nyingine za Bunge, Muundo wa Taarifa, shughuli zilizotekelezwa na LAAC kwa Mwaka 2019; na Wadau waliohusika katika utekelezaji wa shughuli hizo. **Sehemu ya Pili** ni Uchambuzi wa Hoja za Ukaguzi wa Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Sehemu hii inaweka msingi wa Mapendekezo yanayotolewa katika **Sehemu ya Tatu**.

Aidha, Taarifa hii ina maelezo ya Awali ya Mwenyekiti wa Kamati kuhusiana na halihalisi aliyoiona katika matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini katika kipindi chote cha Uongozi wake (2016- 2020). Ni muhimu kwa Wadau kuisoma, kuielewa na hata kuifanyia kazi Sehemu hii kama Sehemu ya Taarifa nzima.

[1] Ibara ya 145 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977).
[2] OR- TAMISEMI (2019). Taarifa ya Mapato ya Vyanzo vya Ndani vya Halmashauri kwa mwaka wa fedha 2017/18

### 1.3 SHUGHULI ZILIZOTEKELEZWA

**Mheshimiwa Spika**, Majukumu ya LAAC hutekelezwa katika namna mbalimbali za Kibunge ikiwemo Vikao vya Mahojiano na Wadau, Ziara za Ukaguzi wa miradi ya maendeleo, na mafunzo ya usimamizi wa fedha za umma. Baada ya kupokea Taarifa ya Ukaguzi wa CAG, LAAC huchambua Halmashauri moja baada ya nyingine ili kubaini Halmashauri zenye matatizo sugu ya matumizi mabaya ya fedha za umma. Halmashauri zinazobainika huitwa kwa ajili ya kujibu hoja za Ukaguzi. Baadhi ya Halmashauri hufanyiwa ziara za Ukaguzi wa ufanisi wao katika kutekeleza miradi mbalimbali ya maendeleo. Baadhi ya Halmashauri zilizobainika kufanya vizuri huitwa pia mbele ya Kamati ili zitoe uzoefu wao kuhusu sababu za mafanikio yao.

Katika Mwaka 2019, LAAC imejadili Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. LAAC imefanya ziara katika jumla ya miradi **Ishirini (20)** ya maendeleo na kushiriki Semina **Nane (8)** za kujenga uwezo katika kushughulikia taarifa za ukaguzi. Aidha, LAAC iliweza kuhoji jumla ya Halmashauri **Sabini na Tatu (73)** kati ya Halmashauri 185 zilizokaguliwa na CAG.

**Mheshimiwa Spika,** katika kutekeleza majukumu yake, LAAC imenufaika sana na teknolojia ya Bunge Mtandao (e- Parliament) uliyoiasisi Bungeni. Kabla ya teknolojia hii, mjumbe mmoja wa LAAC alikuwa analazimika kupekuwa na kusoma wastani wa kurasa 300 za Vitabu vya Halmashauri wakati wa Mahojiano na Wadau. Kwa sasa Wajumbe huenda moja kwa moja kwenye Hoja inayojadiliwa kwa kubofya katika vishikwambi. Hata hivyo, LAAC inaona kuwa teknolojia hii itawasaidia zaidi Wabunge endapo watapewa fursa ya kutumia vishikwambi kusoma taarifa mbalimbali za Bunge mahali popote wanapokuwa badala ya kulazimika kuwepo katika maeneo ya Bunge tu ili kusoma taarifa hizo!

### 1.4 WADAU KATIKA SHUGHULI ZA KAMATI

**Mheshimiwa Spika**, mdau Mkuu katika utekelezaji wa shughuli za LAAC ametajwa katika Nyongeza ya Nane, Sehemu ya Nne, Fasili ya 16 ya Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016 kuwa ni Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi. Hii ni kwa sababu maoni na mapendekezo ya LAAC hujengwa katika misingi ya Taarifa za Ukaguzi unaotekelezwa na Ofisi hiyo.

Wadau wengine ni Kamati zingine za Kudumu za Bunge. Hii ni kwa sababu yapo baadhi ya masuala ambayo LAAC hulazimika kuyajadili na Kamati nyingine ili kupata ufumbuzi wa kina. Wananchi pia ni Wadau muhimu kwa sababu Bunge ni Chombo chao cha Uwakilishi. Wadau wengine ni Serikali Kuu na Serikali za Mitaa nchini kwa sababu ndiyo vyombo vinavyohusika katika masuala ya mapato na matumizi yanayohojiwa na LAAC. Mabunge rafiki duniani yanajumuishwa katika kundi la Wadau kwa sababu kuna utaratibu wa kubadirishana uzoefu katika usimamizi wa fedha za umma katika mabunge mbalimbali. Wadau wengine ni Washirika katika Maendeleo, Vyombo vya Habari na Asasi za Kiraia (CSOs).

### 1.5 MAFANIKIO KUTOKANA NA SHUGHULI ZA KAMATI

(a) LAAC imechochea ongezeko la Hati Safi za Ukaguzi kwa kuzihimiza Halmashauri kujibu Hoja za Ukaguzi kwa Wakati. Kwa Mfano, Hati zenye shaka zimepungua kutoka 113 katika mwaka wa fedha 2014/15 na kushuka hadi saba (7) kwa mwaka 2017/2018;

(b) LAAC imechochea uchangiaji katika Vikundi vya Maendeleo kwa akina Mama (4%), Vijana (4%) na Watu wenye Ulemavu (2%) kufanyika kwa mujibu wa Sheria badala ya hiari katika Halmashauri;

(c) LAAC imeendelea kuzihimiza Halmashauri nchini kuboresha mifumo ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ili zijiimarishe kiuchumi. Kutokana na Hoja hii, tarehe 21 Januari, 2020 OR- TAMISEMI ilitangaza kukabidhi jumla ya PoS 7,227 kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato kwa njia ya kielektroniki;

(d) LAAC imechangia kuimarika kwa mawasiliano ya kazi kati ya OR- TAMISEMI na Bunge kupitia vikao na ziara mbalimbali;

(e) LAAC imechangia kuimarika kwa mawasiliano ya kazi kati ya Bunge na Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi na Ofisi zingine za umma zinazoshiriki katika shughuli za Kamati; na

(f) LAAC imeimarisha ushirikiano wake na Vyombo vya Habari nchini.

(g) LAAC imechangia ushauri wake mara kwa mara katika kuanzishwa rasmi kwa mamlaka ya maji safi, maji taka na usafi wa mazingira vijijini(RUWASA) inayowajibika kusimamia utekelezaji wa miradi ya maji vijijini.

## SEHEMU YA PILI

### 2.0 UCHAMBUZI WA HOJA ZA UKAGUZI KWA MWAKA 2017/2018

### 2.1 MAELEZO YA JUMLA

Msingi wa Taarifa hii ni hoja za Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Hesabu za Mamlaka za Serikali za Mitaa Tanzania Bara kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Katika Mwaka huo, jumla ya Halmashauri 185 zilikaguliwa. Kati ya Halmashauri hizo, Halmashauri 176 zilipata Hati Safi za Ukaguzi, Halamshauri 7 zilipata Hati zenye Shaka. Halmashauri 1 (Manispaa ya Kigoma Ujiji) ilipata Hati Isiyoridhisha. Aidha, Halmashauri 1 ya Wilaya ya Nyangh'wale ilipata Hati Mbaya ya Ukaguzi kwa sababu iliwasilisha kwa CAG taarifa zisizojitosheleza mapato na matumizi yake ya fedha.

### 2.2 UTEKELEZAJI WA MAPENDEKEZO YA KAMATI SERIKALINI

**Mheshimiwa Spika**, jukumu la msingi la Bunge ni kuisimamia na kuishauri Serikali katika kutekeleza wajibu wake kwa Wananchi[3]. Kamati za Kudumu za Bunge ikiwemo LAAC ni vyombo vya Kikatiba vilivyoundwa na Bunge kwa ajili ya kurahisisha utekelezaji wa shughuli zake[4]. Shughuli za Kamati zipo pia kwa mujibu wa Katiba[5] na zimefafanuliwa zaidi katika Kanuni za Kudumu za Bunge, Toleo la Januari, 2016. Kila Kamati ya Kudumu ya Bunge inao wajibu wa kufuatilia utekelezaji wa mapendekezo yake Serikalini.

**Mheshimiwa Spika**, hali halisi ya utekelezaji wa Mapendekezo ya LAAC katika Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2017 ulikuwa ni wa kuridhisha ingawa kuna Masuala kadhaa ya Msisitizo ambayo yametolewa mapendekezo zaidi katika Sehemu ya Tatu ya Taarifa hii. Maeneo hayo yanahusu ukusanyaji wa mapato ya ndani, uhaba wa Watumishi katika Halmashauri, udhaifu wa Vitengo vya Ukaguzi wa ndani na madai ya Watumishi Serikalini. LAAC inashauri kuwa maelezo na ahadi za Serikali zitekelezwe

[3] Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)
[4] Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)

[5] Ibara ya 96 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)

kikamilifu kwa nia ya kuziimarisha Serikali za Mitaa katika matumizi ya fedha za umma na utoaji wa huduma kwa Wananchi. Jedwali Namba 1 linaonesha majibu wa Serikali kwa kila hoja iliyotolewa na LAAC.

**Jedwali Na. 1**: Utekelezaji wa Mapendekezo ya Kamati (2016/17)

| S/N | PENDEKEZO LA KAMATI | UTEKELEZAJI WA SERIKALI |
|---|---|---|
| 1 | Serikali ifanye maboresho katika mifumo ya udhibiti wa ndani wa Halmashauri ili kuongeza mapato na matumizi bora ya fedha za umma | Hadi kufikia Agosti, 2019 Halmashauri 101 zimeunda Kamati za Ukaguzi kwa ajili ya kuongeza udhibiti wa ndani. |
| 2 | Serikali iboreshe upatikanaji wa fedha za maendeleo katika Halmashauri ili kurahisisha utekelezaji wa miradi. | Serikali inaendelea kutoa fedha za maendeleo kutoka HAZINA kulingana na makusanyo. |
| 3 | Halmashauri zihimizwe na kusimamiwa ipasavyo katika kufanya manunuzi ya umma kwa mujibu wa Sheria. | Kwa sasa pameanzishwa mfumo wa manunuzi ya umma kwa njia ya kielektroniki (TANePs) ambapo kila taasisi ya umma zikiwemo Halmashauri zitapaswa kuzingatia. |
| 4 | Halmashauri ziongeze juhudi katika kuboresha upatikanaji wa mapato ya ndani ili ziweze kuboresha huduma kwa Wananchi | Juhudi mbalimbali zinafanyika ikiwemo kuzihimiza Halmashauri kubuni vyanzo vipya vya mapato na kutumia mashine za kielektroniki kwa nia ya kuondoa ubadhirifu na upotevu wa mapato. |
| 5 | Serikali ihakikishe kuwa Halmashauri zinajibu Hoja za Ukaguzi kwa Wakati | Sekretarieti za Mikoa zimeboresha usisimamizi katika Vikao vya Halmashauri katika kila Mkoa. |
| 6 | Halmashauri zichangie kikamilifu 10% ya maendeleo ya jamii katika Vikundi vya Wanawake na Vijana | Kwa sasa uchangiaji katika vikundi hivi ni kwa mujibu wa Sheria kufuatia marekebisho ya Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (1982) ya Mwaka 2018 ambapo kwa mujibu wa Kifungu cha 37 (1) Vikundi vya Wanawake vitapata 4%, Vijana 4% na Watu wenye Ulemavu watapata 2%. |
| 7 | Serikali iweke utaratibu mahsusi wa kuharakisha mchakato wa kutunga Sheria Ndogo za Halmashauri ili kuharakisha matumizi ya Sheria hizo. | OR- TAMISEMI ipo katika hatua za kusimika mfumo wa kielektroniki kwa ajili ya kupokea rasimu za Sheria Ndogo kutoka katika Halmashauri mbalimbali nchini. |
| 8 | Mali zilizothibitishwa kuwa zimechakaa ziondolewe katika Vitabu vya Halmashauri ili kuondoa Hoja za Ukaguzi zisizo za lazima katika Halmashauri hizo. | Kupitia Barua AD.34/35/01/6 ya tarehe 17 Mei, 2019 HAlmashauri zote nchini zimeelekezwa kuondoa mali chakavu katika vitabu vya hesabu zao kwa mujibu wa Sheria. |

**Chanzo**: *Taarifa ya Mwaka ya LAAC Bungeni kwa Mwaka wa Fedha Ulioishia tarehe 30 Juni 2017 na Majibu ya OR- TAMISEMI katika Vikao vya LAAC.*

## 2.3 HALI HALISI KATIKA UTEKELEZAJI WA MIRADI YA MAENDELEO 2017/2018

Katika kushughulikia Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa za Halmashauri kwa Mwaka wa fedha wa 2017/2018, LAAC ilitembelea jumla ya Halmashauri 11 zifuatazo: Jiji la Mwanza,

Manispaa za Musoma, Ilemela na Bukoba, Miji ya Tarime na Kahama, Wilaya za Tarime, Ukerewe, Ngara, Mbogwe, Karagwe. Kamati ilijielekeza katika kuona ufanisi uliopo katika utekelezaji wa miradi ya Elimu, Ujenzi, Afya na maji na kubaini kuwa:

(a) Miradi inayotumia *force account* inahitaji usimamizi wa kitaalam zaidi kutoka kwenye Idara zinazohusika na ujenzi katika halmashauri husika ili iweze kutekelezwa kwa viwango. Kwa sasa hali iliyobainika ni kwamba miradi inayotekelezwa kwa mfumo huu inakabiliwa na changamoto ya usimamizi mdogo wa kitaalam kiasi cha kuathiri ubora wa miradi hiyo.

(b) Katika baadhi ya Halmashauri miradi ya ujenzi haikukamilishwa kwa wakati hivyo kuongeza gharama za ujenzi kwa mujibu wa Mikataba. Kwa mfano, ingawa Kamati haikupata gharama halisi, katika Halmashauri ya Manispaa ya Musoma ujenzi wa barabara za mjini ulicheleweshwa kiasi kusababisha ongezeko kubwa la gharama.

(c) Katika Halmashauri mbalimbali, miradi ya maji haikamilishwi kwa wakati hivyo kufanya Wananchi waendelee kupata adha ya kukosa huduma ya maji. Kwa mfano katika Halmashauri ya Manispaa ya Ilemela Mradi wa Maji wa Nyatula- -Igombe na Kugusumbu haukukamilika kwa wakati ingawa Mkandarasi alilipwa fedha zote za utekelezaji. Aidha, katika Wilaya ya Ukerewe kuna shida katika miradi ya maji ya Vijiji vya Bwasa na Kigola ambapo miradi hiyo inaonekana kuwa imekamilika, na Mkandarasi amelipwa fedha zote ila maji hayatoki.

## 2.4 HOJA ZILIZOBAINIKA KATIKA ZIARA NA VIKAO

Kwa msingi wa Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa mwaka ulioishia 30 Juni, 2018, LAAC ina Hoja Tisa (9) zifuatazo kuhusiana na nidhamu ya mapato na matumizi ya fedha za umma katika Serikali za Mitaa nchini:

### 2.4.1 Halmashauri kutopatiwa kiasi stahiki cha fedha za Maendeleo na Matumizi ya Kawaida kutoka HAZINA.

**Mheshimiwa Spika**, Katika mahojiano na Mamlaka mbalimbali za Serikali za Mitaa nchini, ilibainika kwamba kiasi cha fedha za maendeleo na matumizi ya kawaida kinachopelekwa na Serikali katika Halmashauri na kufanyiwa ukaguzi na NAOT ni kidogo ikilinganishwa na kiasi cha fedha hizo ambacho HAZINA inadai kuwa imepeleka. Hata hivyo, Kamati iliendelea na mahojiano katika hoja hii kwa kuzingatia Taarifa ya Hesabu zilizokaguliwa na NAOT kwa sababu zilizingatia Mizania ya hesabu zilizofungwa na kutangazwa kwa umma na Mamlaka zenyewe kwenye vyombo mbalimbali vya habari. Hali hii inaonesha kuwa fedha zinazotengwa na Bunge hazipelekwi kikamilifu katika maeneo yanayokusudiwa hivyo kuathiri utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika maeneo hayo. Aidha, hali hii inaibua migongano katika usimamizi wa fedha za umma miongoni mwa vyombo vya usimamizi mathalani NAOT, Wizara ya Fedha na Mipango (HAZINA) na OR- TAMISEMI. Hii ni kwa sababu Chombo kimoja kinakuwa na taarifa tofauti na kingine katika Halmashauri moja mbele ya LAAC.

**Jedwali Na. 2:** Mfano wa Halmashauri zilizopata Fedha Pungufu kutoka HAZINA

| HALMASHAURI | FEDHA ZA MAENDELEO (bilioni) | | FEDHA ZA MATUMIZI YA KAWAIDA | |
|---|---|---|---|---|
| | ZILIPELEKWA | HAZIKUPE LEKWA | ZILIPELEKWA | HAZIKUPE LEKWA |
| Manispaa ya Kigamboni | 17.9 | 4.9 | 19.75 | 4.4 |
| Manispaa ya Morogoro | 29.9 | 2.24 | 47.9 | 9.4 |
| Wilaya ya Malinyi | 3.1 | 0.411 | 8.7 | 2.8 |
| Wilaya ya Kasulu | 3.4 | 6.03 | 19.6 | 18.5 |
| Wilaya ya Mkalama | 5.5 | 0.637 | 11.4 bln | 3.05 |

**Chanzo**:*Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC, Okt, 2019.*

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina maoni kwamba Wizara ya Fedha, OR- TAMISEMI na NAOT wanapaswa kujadiliana sababu za tofauti hizi na mwelekeo sahihi unaopaswa kuzingatiwa ili kuondoa mkanganyiko huo na athari zake katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Halmashauri husika. **Jedwali Na.1** hapo juu linaonesha mifano michache tu lakini hali hii ipo katika Halmashauri kadha wa kadha nchini.

### 2.4.2 **Halmashauri kutokukusanya Kikamilifu Mapato yao ya Ndani**

**Mheshimiwa Spika**, Baba wa Taifa, Hayati, Mwl. Julius Kambarage Nyerere, Rais wa Kwanza wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania alipata kusema: "…***Serikali isiyokusanya kodi ni mufilisi***"[6]. Halmashauri nchini hazijaweza kukusanya mapato yao ya ndani kikamilifu. Zina utegemezi mkubwa kifedha katika Serikali Kuu. Mapato yao ya ndani hayafiki 10% ya fedha zote zinazotumika katika kila mwaka wa fedha[7]. Mbali na kuwa na Makadirio ya chini ya viwango vya makusanyo, Halmashauri nyingi hazifikii malengo katika makusanyo ya mapato hayo. Katika mwaka wa fedha wa 2017/2018, Halmashauri zote nchini zilitarajia kukusanya kiasi cha Tsh. 687 bln kutoka katika vyanzo vya mapato yao ya ndani. Hata hivyo, zilikusanya kiasi cha Tsh.553 bln ambayo ni sawa na 81 ya matarajio. Asilimia 29 sawa na Tsh. 134 bln haikukusanywa[8]. Wastani wa jumla ya mapato yote ya Serikali za Mitaa hauzidi 1% ya mapato yote ya ndani ya Serikali. Bila ya ruzuku ya Serikali Kuu, Serikali za Mitaa nchini haziwezi kuendesha shughuli zake hata kwa mwezi mmoja. Katika mahojiano na halmashauri mbalimbali, LAAC imejifunza kuwa udhaifu katika kukusanya mapato ya ndani unachangiwa na sababu zifuatazo:

(a) Utaratibu wa Serikali Kuu kuhodhi vyanzo vya uhakika vya mapato vilivyoko katika Mamlaka za Serikali za mitaa mathalani kodi ya majengo na ushuru wa mabango ya biashara mbalimbali ambavyo kwa sasa vinayokusanywa na TRA, ushuru wa maegesho ya magari unaokusanywa na TARURA, na kodi ya ardhi inayokusanywa na Wizara ya Ardhi, Nyumba na Maendeleo ya Makazi;

(b) Utaratibu wa Serikali Kuu kutozirejeshea Halmashauri hizo kiasi stahiki cha cha gawio la mapato ynayokusanywa kutoka katika vyanzo mbalimbali vilivyoko katika Halmashauri;

(c) Uduni wa mtandao wa mawasiliano (internet) katika Halmashauri zilizo katika mikoa ya pembezoni mathalani Mkoani Ruvuma na Kigoma unaathiri ufanisi wa mashine za kukusanyia mapato kwa njia za kieletroniki (PoS);

(d) Baadhi ya Watumishi kukosa uaminifu wa kurejesha mapato wanayoyakusanya kutoka katika vyanzo mbalimbali na wengine kukosa utaalam au kuwa Wazembe katika kukusanya mapato hayo;

(e) Kukosekana kwa tathmini ya kina na ufuatiliaji katika ufanisi wa mifumo ya ukusanyaji wa mapato; na

(f) Baadhi ya Halmashauri Watendaji wake hawajazielewa vema sura na tabia za Halmashauri zao (Council Environmental Profiles) hivyo kutozibaini ipasavyo fursa za kiuchumi zilizomo katika mazingira yao badala yake wamezidi kutegemea vyanzo vya zamani kama vile kilimo na mifugo tu!

[6] Ibara ya 62 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)

| HALMASHAURI | MWAKA WA FEDHA | MAOTEO | MAKUSANYO HALISI | NAKISI |
|---|---|---|---|---|
| Wilaya ya Bumbuli | 2017/2018 | 848,683,066/= | 592,683,066/= | 255,693,934/= |
| Wilaya ya Mtwara | 2017/2018 | 2,623,475,923/= | 2,288,941,838/= | 232,223,162/= |
| Wilaya ya Busega | 2017/2018 | 1,598,393,000/= | 1,144,677,000/= | 453,716,000/= |
| Manispaa ya Shinyanga | 2017/2018 | 2,200,000,000/= | 2,050,844,893/= | 149,155,105/= |
| Wilaya ya Mkalama | 2017/2018 | 1,013,000,000/= | 884,511,457/= | 128,488,543/= |
| Wilaya ya Meatu | 2017/2018 | 3,211,545,535/= | 1,792,720,509/= | 1,418,825,026/= |

[7] Ibara ya 96 (1) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)
[8] Ibara ya 96 (2) ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania (1977)

**Jedwali Na. 3: :** Baadhi ya Halmashauri ambazo hazikukusanya Kikamilifu Mapato ya Ndani

**Chanzo**: *Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC, Oktoba, 2019*

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina maoni kuwa udhaifu wa Halmashauri katika kukusanya mapato yake ya ndani huzifanya halmashauri hizo zishindwe kutoa huduma za msingi kikamilifu. Aidha, udhaifu huu, huongeza zaidi utegemezi wa Halmashauri hizo kifedha kwa Serikali Kuu. Hali hii huifanya Serikali Kuu kuwa na mzigo mzito wa majukumu kuanzia katika ngazi ya kimataifa, kitaifa na katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Hivyo, kwa kuwa LAAC imebainisha sababu za makusanyo madogo, ni vema Serikali kwa ujumla wake ikaona umuhimu wa kuzitafutia sababu hizo ufumbuzi.

### 2.4.3 **Halmashauri kutozingatia Miongozo ya Matumizi ya Fedha**

**Mheshimiwa Spika,** nidhamu ya matumizi ya fedha za umma ni muhimu kwa ajili ya taasisi kupata tija inayokusudiwa. Baadhi ya Miongozo hiyo nchini ni: *Sheria ya Fedha za Umma (2001) pamoja na Marekebisho yake, Sheria ya Fedha za Serikali za Mitaa (1982) pamoja na Marekebisho yake*, *Sheria ya Manunuzi ya Umma (2004) pamoja na Marekebisho yake, Memoranda ya Usimamizi wa Fedha katika Serikali za Mitaa (2009) na Mwongozo wa Ofisi ya Rais- TAMISEMI wa Usimamizi wa Fedha katika Serikali za Mitaa*. Uchambuzi wa LAAC umebaini kuwa kuna changamoto katika baadhi ya Halmashauri katika kutekeleza Miongozo hii. Kwa mfano: Katika Halmashauri za Wilaya za Mkalama, Songea, Singida na Makete Vitengo vya Ukaguzi wa Ndani na Kamati za Ukaguzi hazifanyi zao kikamilifu kutokana na kutokuwa na bajeti mahsusi au vitendea kazi kama vile kompyuta na gari.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina maoni kuwa ni muhimu kwa kila Halmashauri na taasisi zingine za umma nchini kuzingatia taratibu zilizopo nchini katika matumizi ya fedha za umma. Ni muhimu pia OR- TAMISEMI ikajiimarisha zaidi katika kufuatilia na kutathmini utendaji wa Halmashauri kwa kila Mkoa na nchi nzima ili kuboresha nidhamu ya matumizi za fedha za umma na upatikanaji wa huduma kwa wananchi.

**Jedwali Na. 4: Baadhi ya Halmashauri ambazo Hazikuzingatia Miongozo**

| HALMASHAURI | HOJA | KIASI CHA FEDHA | MWONGOZO AMBAO HAUKUZINGATIWA |
|---|---|---|---|
| Halmashauri ya Manispaa ya Kigoma Ujiji. | Manunuzi ya bidhaa na huduma mbalimbali kwa kutumia masurufu | 41,935,000/= | LGFM (2009), Order No. 39(2) |
| | Manunuzi ya Bidhaa mbalimbali bila kuwepo Ushindani wa Wazabuni | 40,830,000/= | PPA (2011) Kifungu cha 64(1) |
| | Ukodishaji wa eneo la Kibirizi bila kuwepo na Ushauri wa Kisheria na bila kupata Kibali cha Wizara Mama (OR-TAMISEMI) uliopelekea pia mali zenye thamani ya Tsh. 676,999,999/= kutoonekana katika Vitabu vya fedha vya Halmashauri na kukosekana kwa Taarifa ya Kitaalam juu ya Manunuzi ya Vifaa vya utekelezaji wa Mradi huo. | 676,999,999/= | LGFM (2009), Order No. 58(2) |
| | Manunuzi ya Huduma mbalimbali yasiyothibitishwa na nyaraka zozote | 47,276,687/= | LGFM (2009), Order No. 34(1) |
| | Manunuzi yenye nyaraka pungufu. | 142,645,921/= | LGFM (2009), Order No. 8(2)C |
| Wiaya ya Mkalama | (a) Manunuzi ya huduma na bidhaa mbalimbali bila ya kudai risit ya EFD zilinunuliwa.<br><br>(b) Mkandarasi *Luneco Investiment Co Ltd* alilipwa fedha zote za utekelezaji wa Mradi wa Maji wa Nyahala, Kiasi cha kabla Mradi huo haujakamilika. Mpaka sasa Vituo 10 tu vinatoa maji kati ya Vituo 16. | 243.3mil<br><br>Tsh. 905.2 mil | Kanuni ya 28(1) ya Sheria ya Kodi, The Income Tax (EFD) Regulations, 2012. |
| Wilaya ya Songea | Kuchukua fedha katika akaunti ya amana bila kufuata taratibu na kuzitumia katika manunuzi ambayo hayakuidhinishwa Bodi ya Wazabuni. Mpaka sasa fedha hizo hazijarejeshwa. | Tsh. 63.mil | |
| Wilaya ya Makete | Ilifanya manunuzi ya huduma mbalimbali ambayo | Tsh. 38.85 mil | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | hayakuidhinishwa na Bodi ya Zabuni. | | |
| Wilaya ya Shinyanga | Mkandarasi Halem *Construction Co Ltd* mwenye Mkataba Na. LGA/114/2013-2014/NRWSSP/W22 aliyetekeleza Mradi wa Maji katika Kijiji cha Mwakitolyo alilipwa fedha zaidi ya kiwango cha makubaliano katika Mkataba. | Tsh. 46.5 mil | Mkataba wa Kazi husika |
| Wilaya ya Iringa | Mkandarasi *RJR Construction Co ltd* amelipwa kiasi cha Tsh. 1.311 bln kati ya Tsh. 1.94 bln anazopaswa kulipwa kwa ajili ya ujenzi wa mabwawa ya maji katika Vijiji vya Isupilo- Itengulinyi na Kijiji cha Lumuli kupitia Mkataba Na. LGA/023/2013-14/W/027A wakati kazi yenyewe imekamilika kwa 45% tu. | Tsh.1.311 biln | Mkataba wa Kazi husika |

**Chanzo**: *Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC, Oktoba, 2019*

2.4.4 **Upotevu wa mapato ya Halmashauri kutokana na uzembe wa Idara za Afya katika kujaza form za madai ya Bima ya Afya.**

Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini hupata dawa na vifaa tiba kwa ajili ya binadamu kutoka katika Bohari Kuu ya Madawa Nchini (MSD). Dawa hizo hutumika kwa wagonjwa mbalimbali ikiwemo wale wanaotumia bima za afya za Shirika la Taifa la Bima ya Afya (NHIF). Kutokana na udhaifu katika kujaza fomu za bima za afya, Halmashauri nyingi zimekuwa hazirejeshewi madai yao kutoka NHIF hivyo kupata hasara ya huduma za afya zinazozitoa kwa Wagonjwa wanaotumia bima za NHIF.

**Mheshimiwa Spika**, hoja hii ipo katika Halmashauri nyingi ingawa Jedwali lifuatalo linaonesha mifano michache tu. Kamati ina maoni kuwa hali hii isipotafutiwa ufumbuzi ni mwanya mkubwa wa upotevu wa mapato katika Halmashauri.

**Jedwali Na. 5:** Mfano wa Halmashauri zilizopata Hasara kutokana na ujazaji Mbaya wa Fomu za Bima ya Afya kwa wagonjwa

| HALMASHAURI | KIASI KINACHODAIWA HADI KUFIKIA JUNI 2018 (000,000) | MKAKATI WA KUREJESHEWA FEDHA HIZO |
|---|---|---|
| Manispaa Kinondoni | 12.6 | - |
| Manispaa ya Masasi | 36.914 | - |
| Wilaya ya Kasulu | 215.608 | - |
| Manispaa ya Shinyanga | 9.4 | - |

**Chanzo:** *Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC, Oktoba, 2019.*

**Mheshimiwa Spika,** LAAC ina maoni kuwa endapo juhudi za makusudi za kurekebisha udhaifu huu hazitachukuliwa, upotevu wa mapato ya Mamlaka ya Serikali za Mitaa nchini kupitia

mwanya huu utaendelea kukua na kuchangia zaidi katika kuzorotesha uwezo wa Halmashauri kifedha na kiutoaji wa huduma za afya.

### 2.4.5 Upotevu wa Mapato ya Halmshauri kutokana na Malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi ya Zuio

**Mheshimiwa Spika**, Uchambuzi wa Ripoti ya taasisi ya WAJIBU kuhusiana na Mamlaka za Serikali za mitaa na miradi ya maendeleo kwa mwaka 2017/18, jumla ya Tsh. 12 bln zililipwa na Halmashauri mbalimbali kwa Wakandarasi kama malipo ya ongezeko la thamani wakati wa kutekeleza miradi ya afya, elimu, uchukuzi na maji. Malipo hayo hayakustahili kufanyika ndiyo maana baadhi ya Halmashauri zimeanza michakato ya kuwadai Wakandarasi waliolipwa fedha hizo. Katika hali ya kawaida, fedha hizo zingetumika kukamilisha miradi hiyo kwa wakati na gharama nafuu kulinga na MoU zake. Kwa mfano, katika Mwaka wa fedha 2017/2018, Halmashauri ya Wilaya ya Mkalama haikupata kiasi cha Tsh. 13 mil ilichopaswa kulipwa kama Kodi ya Zuio kutoka kwa Wakandarasi Waliojenga vyumba vya madarasa vya shule mbalimbali za Sekondari na zahanati.

### 2.4.6 Upungufu wa Watumishi katika Idara mbalimbali za Halmashauri

Uchambuzi wa LAAC katika maelezo na taarifa mbalimbali zilizotolewa na Halmashauri katika Vikao unaonesha kuwa Halmashauri mbalimbali nchini zinakabiliwa na uhaba mkubwa wa Watumishi katika Kada mbalimbali. Kada iliyoathiriwa zaidi ni Waalimu wa Sayansi katika Shule za Sekondari na Msingi, Wauguzi, Wakaguzi wa Ndani, Wahasibu na Wahandisi (Ujenzi). Hali hii inachangia sana katika kudorora kwa ufanisi wa huduma mbalimbali za afya, elimu, ukusanyaji wa mapato na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo hususani ile inayotumia *force accounts* na kuhitaji usimamizi mkubwa na wa karibu.

**Jedwali Na. 6:** Mifano ya Halmashauri zenye Upungufu wa Watumishi

| Halmashauri | Idadi inayoombwa | Idadi Iliyopatikana | Upungufu |
|---|---|---|---|
| Wilaya ya Meatu | 654 | 296 | 358 |
| Wilaya ya Mtwara | 821 | 86 | 735 |
| Manispaa Kigoma Ujiji | 1166 | - | 1166 |
| Wilaya ya Kasulu | 802 | - | 802 |
| Wilaya ya Shinyanga | 739 | - | 739 |
| Wilaya ya Kilwa | 908 | 183 | 725 |

***Chanzo**: Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC 2019.*

**Mheshimiwa Spika**, tatizo hili lipo katika Halmashauri zote nchini ingawa **Jedwali Na. 6** linaonesha mifano michache tu. LAAC ina maoni kuwa Raslimali watu ndiyo msingi wa kila jambo linapangwa na kutekelezwa Serikalini. Jitihada katika kuhimiza matokeo katika utendaji (Results Based Performance) tunapaswa kuhimiza pia uwepo wa raslimali watu kwa idadi na ubora unaostahili ili tuweze kunufaika zaidi.

### 2.4.7 Madai ya Fedha Kutokana na Stahili Mbalimbali za Watumishi Serikalini na Madiwani

**Mheshimiwa Spika**, yapo madai ya fedha zinazotokana na stahili mbalimbali za Watumishi Serikalini na Madiwani katika Kata mbalimbali. Watumishi hususani Waalimu wana madai ya fedha za uhamisho, likizo na malimbikizo ya mishahara. LAAC ina maoni kuwa ufanisi wa Watumishi unategemea sababu mablimbali ikiwemo uwezo kitaaluma, mazingira mazuri ya kazi yanayoruhusu matumizi ya taaluma na ujuzi wao, ujira stahiki, na mambo mengine yaliyo halali kwao kuyafanya au kufanyiwa.

**Mheshimiwa Spika**, kutowalipa Watumishi stahili zao kwa wakati siyo jambo la motisha. Kuna athiri morali na ufanisi katika kazi. Hivyo, ni vyema kuipatia ufumbuzi ili kuepusha madhara yanayoweza kujitokeza katika katika maeneo mbalimbali ya huduma wanazozitoa Watumishi na Madiwani hao. Kutokana na kushuka kwa morali wa kazi tunaweza kuona madhara katika viwango vya huduma za afya, viwango vya kujua kusoma na kuandika miongoni mwa watoto mashuleni, viwango vya miradi ya maendeleo inayosimamimiwa na Watumishi hao, viwango vya usafi wa miji na majiji, viwango vya mipango miji, idadi ya kesi ambazo Serikali inashindwa mahakamani, na viwango vya ushiriki wa wananchi katika shughuli za maendeleo.

### 2.4.8 Baadhi ya Halmashauri kuwa na Ofisi Kuu katika Maeneo yasiyo yao Kijografia na Kiutawala

Katika uchambuzi wa Taarifa za Halmashauri mbalimbali, LAAC imebaini kuwepo kwa Halmashauri ambazo Ofisi zake ziko nje ya maeneo yao ya kijiografia na kiutawala. Halmashauri hizo zinatekeleza majukumu yao nje ya maeneo ambako watu wao wa kuwahudumia wanapatikana. Hivyo, zinaendeleza majengo na miundombinu mingine ya kiofisi nje na maeneo hayo na, zinaongeza gharama za uendeshaji wa Halmashauri kwa kigezo cha umbali.

Kwa mfano; Halmashauri za Wilaya za Iringa, Tarime, Mbogwe, Kondoa na Sumbawanga Ofisi zao zipo ndani ya Halmashauri zingine kijiografia na kiutawala. Huko ni kujitenga na Watu ambao Halmashauri hizo zinawatumikia na ni kuongeza gharama za utendaji na utawala kusikokuwa na ulazima. Ni muhimu kila Halmashauri iwe na Ofisi zake katika maeno yake ya kijografia na kiutawala ili kurahisisha utoaji wa huduma.

### 2.4.9 Baadhi ya Halmashauri kutokupeleka Michango ya Kisheria ya Kila Mwezi ya Malipo ya Uzeeni ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii.

**Mheshimiwa Spika**, katika baadhi ya Halmashauri (Mfano; Halmashauri za Wilaya za Songea, Mafia, Busega na Meatu) pameanza kuibuka utamaduni wa kutokupeleka michango ya malipo ya uzeeni ya Watumishi katika Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii. Utamaduni huu usipokemewa ni mzigo na hasara kubwa kwa Halmashauri zenyewe na Watumishi husika pindi watakapostaafu kazi. Halmashauri zitadaiwa madeni hayo ikiwa ni pamoja na kiasi kikubwa cha riba. Kamati inaona ni vyema OR- TMISEMI na Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii zikaongeza juhudi za kuzisimamia Halmashauri ili kuhakikisha kuwa zinalipa michango hiyo kwa wakati.

**Mheshimiwa Spika**, Sehemu ya Pili ya Taarifa hii imebainisha athari kwa kila hoja iliyochambuliwa. Katika Sehemu ya Tatu, LAAC inatoa mapendekezo ambayo ni muhimu Serikali ikayazingatia kwa ajili ya kuleta maboresho katika Serikali za Mitaa.

## SEHEMU YA TATU

## 3.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

**Mheshimiwa Spika**, Mapendekezo yafuatayo yanatolewa kufuatia Uchambuzi wa wa Hoja mbalimbali za CAG katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018. Uchambuzi huo umefanyika katika Sehemu ya Pili ya Taarifa hii.

### 3.1 MAPENDEKEZO KWA KILA HOJA YA KAMATI

(1) **Kuhusu Mwenenendo wa upatikanaji wa fedha kutoka HAZINA na athari zake katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini**.

**Mheshimiwa Spika,** hoja hii inagusa utekelezaji wa Sheria ya Fedha inayotungwa na Bunge kila Mwaka wa fedha, inagusa ufanisi wa Mamlaka za Serikali za Mitaa katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo kwa Wananchi na inagusa uhusiano wa Mamlaka mbalimbali za Serikali (Wizara ya Fedha na Mipango, OR- TAMISEMI na NAOT) na Bunge katika kusimamia mapato na matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Hivyo, LAAC inapendekeza mambo mawili (2) yafuatayo yafanyike ili hoja iweze kufungwa: -

(a) Wizara ya Fedha na Mipango, OR- TAMISEMI na NAOT wafanye majadiliano ya pamoja kuhusu sababu zinazosababisha kutokea kwa hali hiyo. Taarifa ya Majadiliano hayo ya Pamoja iwasilishwe mbele ya LAAC mapema kabla ya kuanza kwa Vikao vya Uchambuzi wa Hesabu zilizokaguliwa za Mamlaka za Serikali za Mitaa za Mwaka 2018/2019.

(b) Serikali iwe inatoa ipasavyo kiasi cha fedha kinachokuwa kimetengwa kwa ajili ya shughuli za maendeleo na matumizi ya kawaida katika taasisi mbalimbali nchini ikizingatiwa kuwa utaratibu huo unakuwa umetungiwa Sheria mahsusi ya fedha kwa kila mwaka husika.

(2) **Halmashauri kutokukusanya ipasavyo mapato yake ya ndani**.

**Mheshimiwa Spika**, Kutokana na umuhimu wa Hoja hii katika maendeleo ya Wananchi, LAAC inapendekeza mambo Sita (6) yafuatayo ambayo yakitekelezwa kwa ufanisi yatasaidia kuongeza mapato na kuboresha huduma katika Serikali hizo na nchi kwa ujumla:

(a) Dhana ya kuibua vyanzo vipya vya mapato itekelezwe kikamilifu katika ngazi zote za Serikali kwa maana ya Serikali Kuu na Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Dhana hii ikitekelezwa kwa ustadi na kwa vitendo itachangia sana kusitishwa kwa utaratibu uliopo sasa ambao Serikali Kuu imechukua vyanzo vya uhakika vya mapato vilivyopo katika Serikali za Mitaa. Vyanzo hivyo ni kama vile kodi ya majengo (property tax), kodi ya ardhi (land rent), ushuru wa mazao ya kimkakati, na Kodi ya mabango ya biashara.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina maoni kuwa endapo Serikali Kuu itajielekeza katika kuboresha mazingira ya utalii, nishati, usafiri na usafirishaji, viwanda na biashara mbalimbali za kimataifa ili kupata ushuru na kodi zinazotokana na shughuli hizo, Serikali za Mitaa zitapata uhakika wa kukusanya mapato yao ya ndani.

(b) Serikali Kuu ijielekeze pia katika kutoa ushauri wa kitaalam na usimamizi katika mikakati ya ukusanyaji wa mapato ya ndani ya Mamlaka za Serikali za Mitaa. Aidha, LAAC inashauri kuwa Idara za Serikali zinazohusika naUkaguzi na Ufuatiliaji zijizatiti kufuatilia hali halisi ya mapato katika mifumo ya kielektroniki

ya ukusanyaji wa mapato na kulinganisha mapato halisi yanayowekwa Benki kwa lengo la kudhibiti mianya ya upotevu.

**Mheshimiwa Spika**, Pendekezo hili litatekelezwa kwa upana na ubora zaidi endapo Idara zinazohusika na Ukaguzi na Ufuatiliaji wa fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa katika OR-TAMISEMI zitaimarishwa na kuwezeshwa kifedha ili zitekeleze kikamilifu wajibu huo.

(c) Baadhi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini hususani zile zilizoko katika maeneo ya mipakani (mipaka ya Tanzania na Msumbiji, Zambia, Rwanda, DRC na Burundi) zinatoa utetezi kuwa kukosekana kwa mawasiliano madhubuti ya mtandao katika maeneo yao kunaathiri ukusanyaji wa mapato kwa njia za kielektroniki. LAAC inaona ni vyema Serikali ikaitumia fursa ya kuwepo kwa Mkongo wa Taifa wa Mawasiliano ya Mtandao kuimarisha mawasiliano ya aina hiyo katika maeneo yaliyopo pembezoni mwa nchi.

**Mheshimiwa Spika**, endapo Pendekezo hili litatekelezwa litaziongezea Halmashauri husika ufanisi katika kukusanya mapato kwa njia za kielektroniki kwa kutumia mashine za **PoS** ambazo Serikali ipo kuzisambaza.

(d) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziimarishe Vitengo vya Ukaguzi wa ndani, Sheria, Manunuzi na Uhasibu ili masuala yanayohusu ukusanyaji na utumiaji wa fedha yafanyike kwa utaalam zaidi. Kwa sasa idadi ya Watumishi, viwango va bajeti na Ufanisi wao katika maeneo hayo hauridhishi na unachangia mdororo katika ukusanyaji na utumiaji wa fedha za umma kwa ujumla. Vitengo hivi viwezeshwe pia katika eneo la mafunzo kuhusiana na mifumo ya usimamizi wa fedha na mifumo mingine ya usimamizi wa shughuli za Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini. Zipewe vitendea kazi mathalani gari kwa ajili ya Ukaguzi na Kompyuta kwa ajili ya shughuli za Kiofisi.

**Mheshimiwa Spika**, endapo Pendekezo hili litatekelezwa kikamilifu, udhibiti wa ndani na nidhamu ya matumizi ya fedha za umma katika Halmashauri vitaimarika.

(e) Mamlaka za Serikali za Mitaa ziongeze ubunifu katika vyanzo vya mapato na kuhuisha (review) kiasi cha tozo/kodi/bei/ushuru unaotozwa katika vyanzo hivyo ili kuvutia Wateja. Kwa sasa zipo huduma zinazotolewa kwa bei kubwa kiasi cha kuwatisha Wateja. Aidha, Mamlaka hizo zitumie ipasavyo uimara wa vitengo vilivyotajwa katika kipengele (d) hapo juu ili kudhibiti ipasavyo matumizi ya mapato yanayokusanywa kutokana na ushuru, tozo, ada za leseni na vyanzo vingine[9]; na

(f) Pamoja na mambo mengine ya Utendaji, Mabaraza ya Madiwani yapewe mafunzo ya Usimamizi wa Mapato na Matumizi ya Fedha za Umma katika maeneo yao; yahimizwe kuwa vichocheo na Waangalizi Madhubuti wa Mapato na Matumizi katika Halmashauri zao. Katika baadhi ya Halmashauri Wanatajwa baadhi ya Madiwani kuwa vikwazo katika ukusanyaji wa mapato katika maeneo yao.

(3) **Baadhi ya Halmashauri kutozingatia Miongozo ya Manunuzi ya umma**.

Katika hoja hii, LAAC inapendekeza kwamba Mfumo wa Manunuzi ya Umma kwa njia ya Mtandao (TANePS) uimarishwe na kutumiwa katika taasisi zote za Serikali

nchini. Watumishi wataobainika kukiuka taratibu za manunuzi ya umma zilizowekwa kwa mujibu wa Sheria bila ya kuwa na sababu za msingi wachukuliwe hatua za Kisheria za kiuwajibikaji.

[9] WIPA: Ripoti ya Uwajibikaji; Mamlaka za Serikali za Mitaa na Miradi ya Maendelo 2017- 18, Uk.6

**Mheshimiwa Spika**, inapendekezwa pia kwamba Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAOT) iombwe kufanya Ukaguzi Maalum katika Hesabu za Mwaka wa Fedha ulioishia tarehe 30 Juni, 2018 katika Halmashauri za Manispaa ya Kigoma Ujiji na Wilaya ya Songea ili kubaini sababu na Wahusika katika ukiukwaji mkubwa wa manunuzi na matumizi ya Fedha za Umma kwa ujumla uliobainika katika Taarifa za Hesabu za Halmashauri hizo kwa CAG na LAAC.

(4) **Upungufu wa Watumishi katika Kada mbalilimbali zilizopo katika Utumishi wa Mamla za Serikali za Mitaa na athari zake katika ufanisi wa Mamlaka hizo**.

**Mheshimiwa Spika,** idadi kubwa ya Watumishi wa Umma katika Kada mbalimbali walioondolewa Serikalini kufuatia zoezi la kuondoa Watumishi hewa. LAAC anaunga mkono utekelezaji wa zoezi hilo. Lakini ni dhahiri pia kuwa kufuatia utekelezaji wa zoezi hilo, pamekuwa na ombwe (vaccum) katika Kada zilizokuwa zimejazwa na Watumishi hao. Ombwe hili lina madhara hasi katika kasi na viwango vya huduma na usimamizi wa miradi mbalimbali ya maendeleo hasa ile inayotumia *force accounts*.

**Mheshimiwa Spika**, ni vyema Serikali ikaona uwezekano wa kutoa ajira kwa ajili ya kuziba ombwe hilo na kuongeza ufanisi kwa Watumishi hao. Pendekezo hili liende sanjari na maboresho katika mazingira ya kazi na stahili za Watumishi hao ili taifa liweze kunufaika ipasavyo kutokana na idadi na utaalam wao katika nyanja mbalimbali.

(5) **Madai ya Posho za Madiwani na Watumishi wa Serikali na Changamoto zake katika ufanisi wa utendaji wao**.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC ina maoni kuwa Madiwani ni kiungo muhimu sana kati ya Serikali na Wananchi hasa katika kutekeleza miradi ya maendeleo na shughuli zingine za ulinzi na usalama katika Kata zetu. Hali kadhalika Watumishi wa Serikali ndiyo watekelezaji na wasimamizi Wakuu wa Sera na Mipango mbalimbali ya Serikali kwa Wananchi. Hivyo, ni vyema wakawa wanalipwa stahili zao kwa wakati ili kuwatia moyo na ufanisi wa kazi wanazozifanya. Kwa mfano, Watumishi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chamwino peke yake wanaidai Serikali kiasi cha Tsh. 1.3 bn[10] kutokana na stahili mbalimbali. Hali kama hii huibua manung'uniko miongoni mwao kiasi cha kushusha morali wa kazi na tija.

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inashauri kuwa madeni haya yawekewe utaratibu madhubuti wa kuyakusanya na kuyahakiki mapema katika vituo vyao vya kazi ili yaweze kulipwa kwa wakati.

(6) **Upotevu wa mapato ya Mamlaka za Serikali za Mitaa kutokana na Uzembe katika ujazaji wa Form za Bima ya Afya (NHIF**).

**Mheshimiwa Spika**, Hoja ya Ukusanyaji wa Mapato na udhibiti wa matumizi yake imejadiliwa kwa kiasi kikubwa hapo juu. LAAC inashauri kwamba Serikali itoe elimu kwa Watumishi wake juu ya ujazaji bora wa formu hizi lakini pia ibuni mbinu

madhubuti ya kudhibiti udanganyifu katika kujaza formu hizo ili huduma za afya zizidi kuwa bora na endelevu.

[10] Taarifa (Briefing) ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali katika Vikao vya LAAC tarehe 15 Jan 2020

(7) **Baadhi ya Halmashauri kuwa na Ofisi Kuu katika Maeneo yasiyo yao Kijografia na Kiutawala**

**Mheshimiwa Spika**, kwakuwa kila Halmashauri ina mipaka yake ya kijiografia na utawala, LAAC inapendekeza kwamba kila Halmashauri ielekezwe au iwezeshwe kuwa na Ofisi zake Kuu ndani ya maeneo yake ya kijografia ili kurahisisha utoaji wa huduma kwa Wananchi.

(8) **Upotevu wa Mapato ya Halmshauri kutokana na Malipo ya Kodi ya Ongezeko la Thamani (VAT) na kodi ya Zuio**

**Mheshimiwa Spika**, kwa sababu VAT na Kodi ya Zuio (withholding tax) ni kodi za kisheria, LAAC inapendekeza kwamba OR - TAMISEMI isimamie kikamilifu Halmashauri kwa nia ya kuhakikisha kuwa Halmashauri hizo zinatekeleza matakwa hayo ya Sheria kwa kukusanya ipasavyo kodi hizo.

(9) **Baadhi ya Halmashauri kutokupeleka Michango ya Kisheria ya Kila Mwezi ya Malipo ya Uzeeni ya Watumishi katika Mifuko ya Hifadhi za Jamii.**

**Mheshimiwa Spika**, kama ilivyoelezwa hapo awali, katika baadhi ya Halmashauri pameanza kuibuka utamaduni wa kutokupeleka michango ya malipo ya uzeeni ya Watumishi katika Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii. Kamati inapendekeza kwamba OR- TMISEMI na Mifuko husika ya Hifadhi za Jamii ziongeze juhudi za kuzisimamia Halmashauri ili kuhakikisha kuwa michango hiyo inalipwa kwa wakati. Aidha, Wakurugenzi Watendaji watakaobainika kuzembea wawajibishwe kwa uzembe huo.

## 3.2 SHUKRANI

**Mheshimiwa Spika**, LAAC inakushukuru kwa Miongozo na ridhaa mbalimbali ulizokuwa ukizitoa na kuwezesha shughuli zake kutekelezwa kwa ufanisi. Tunakushukuru na kukupongeza zaidi kwa historia na manufaa uliyoyaweka kwa kuanziasha na kuhimiza matumizi ya Bunge Mtandao (e-Parliament). Tunamshukuru pia Naibu Spika wa Bunge Dkt. Tulia Ackson na Wenyeviti wote wa Bunge kwa Miongozo yao katika nyakati mbalimbali.

Aidha, tunaishukuru Sekretarieti ya Ofisi ya Bunge kwa ufanisi wake katika kupanga, kutafiti, kushauri, kuratibu na kufuatilia vema utekelezaji wa shughuli za Kamati Chini ya Katibu wa Bunge Bw. Stephen Kagaigai. Hivyo, naomba shukrani zangu zimfikie Kaimu Mkurugenzi wa Idara ya Kamati za Bunge Ndg. Michael Chikokoto na Makatibu wa Kamati Ndg. Dismas Muyanja, Ndg. Dickson M. Bisile; na Ndg. Waziri Kizingiti.

**Mheshimiwa Spika**, naomba kutoa shukrani za kipekee kwa Ofisi ya Taifa ya Ukaguzi (NAO) chini ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali Ndg. Edward Kichele kwa ufafanuzi mahiri wa hoja za ukaguzi na kwa mahusiano mema ya kazi kwa ujumla katika wakati wote tuliotekeleza jukumu hili. Tunaishukuru pia Ofisi ya Katibu Mkuu- Wizara ya Fedha na Mipango (HAZINA), Ofisi ya Rais –TAMISEMI na Watendaji wengine wote wa Serikali ambao kwa namna moja ama nyingine wameiwezesha LAAC kutekeleza majukumu yake kikamilifu. Aidha, ninaomba kutoa shukrani pia kwa Asasi mbalimbali za Kiraia, Vyombo vya Habari na Wananchi kwa Ujumla kwa ushirikiano wao katika kutoa taarifa za matumizi ya fedha katika Mamlaka za Serikali za Mitaa nchini.

**Mheshimiwa Spika,** Wajumbe Wafuataao ndiyo waliounda Kamati ya LAAC na kuandaa Taarifa hii. Nawashukuru sana kwa ushirikiano, na ninaomba kuwatambua kwa majina yao kama ifuatavyo:

| | | | |
|---|---|---|---|
| (1) | Mhe. Vedasto Ngombale (Mb) | - | Mwenyekiti |
| (2) | Mhe. Abdallah D. Chikota (Mb) | - | Makam Mwenyekiti |
| (3) | Mhe. Ahmed Ally Salum (Mb) | - | Mjumbe |
| (4) | Mhe. Azza H. Hamad (Mb) | - | Mjumbe |
| (5) | Mhe. Conchesta Rwamlaza (Mb) | - | Mjumbe |
| (6) | Mhe. Ezekiel M. Maige (Mb) | - | Mjumbe |
| (7) | Mhe. Faida Mohamed Bakar (Mb) | - | Mjumbe |
| (8) | Mhe. Alex R. Gashaza (Mb) | - | Mjumbe |
| (9) | Mhe. Juma K. Hamad (Mb) | - | Mjumbe |
| (10) | Mhe. Leah J. Komanya (Mb) | - | Mjumbe |
| (11) | Mhe. Martin M. Msuha (Mb) | - | Mjumbe |
| (12) | Mhe. Prof. Norman S. King (Mb) | - | Mjumbe |
| (13) | Mhe. Rose K. Sukum (Mb) | - | Mjumbe |
| (14) | Mhe Tauhida C. Gallos (Mb) | - | Mjumbe |
| (15) | Mhe. Anastazia J. Wambura (Mb) | - | Mjumbe |
| (16) | Mhe. Cecilia D. Pareso (Mb) | - | Mjumbe |
| (17) | Mhe. Dkt. Godwin A. Mollel (Mb) | - | Mjumbe |
| (18) | Mhe. Edward F. Mwalongo (Mb) | - | Mjumbe |
| (19) | Mhe. Eng. Christopher K. Chizza (Mb) | - | Mjumbe |
| (20) | Mhe. Mangungu A. Issa (Mb) | - | Mjumbe |
| (21) | Mhe. Mary P. Chatanda (Mb) | - | Mjumbe |
| (22) | Mhe. Seif Ungando Ally (Mb) | - | Mjumbe |
| (23) | Mhe. Selemani J. Zedi (Mb) | - | Mjumbe |
| (24) | Mhe. Tunza I. Malapo (Mb) | - | Mjumbe |
| (25) | Mhe. Yussuf K. Makame (Mb) | - | Mjumbe |
| (26) | Mhe. Zainab M. Bakar (Mb) | - | Mjumbe |

**3.3 HOJA**

**Mheshimiwa Spika**, Naomba sasa Bunge lako Tukufu lipokee, lijadili na kuyaafiki Mapendekezo ya LAAC juu ya Taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kuhusu matumizi ya fedha za umma katika Mamlaka za Serikali za Mitaa kwa Mwaka wa Fedha ulioishia Tarehe 30 Juni, 2018 ili Mapendekezo hayo sasa yawe Maazimio ya Bunge.

**Mheshimiwa Spika,** Naomba kutoa Hoja.

………………………………………..
Vedasto Edgar Ngombale (Mb).

**MWENYEKITI**
**KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU**
**ZA SERIKALI ZA MITAA (LAAC)**
……Januari, 2020.

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Wajumbe wa Kamati sijui hawapo humu ndani au na wenyewe. *(Kicheko)*

Hoja imeungwa mkono tutaendelea na utaratibu wetu nimeshaletewa hapa majina kwa mujibu wa kanuni zetu vyama vyote vimeshaleta hapa majina. Kwa hivyo tutaanza na Mheshimiwa George Malima Lubeleje atafutiwa na Mheshimiwa Allan Kiula, Mheshimiwa Ali Salim Khamis ajiandae.

**MHE. GEORGE M. LUBELEJE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia hoja hizi mbili, Kamati ya Hesabu za Serikali Kuu na Serikali za Mitaa. Niwapongeze wenyeviti na pamoja na wajumbe wa kamati hizi mbili. Vilevile, nimpongeze Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais- TAMISEMI anafanya kazi nzuri sana na hizi halmashauri nyingi ameshazitembelea. Hivi karibuni amegawa mashine za kukusanyia mapato 7227 kwa ajili ya kuboresha ukusanyaji wa mapato katika halmashauri. Ni kweli halmashauri zilinunua mashine lakini mashine nyingi zilichakachuliwa kwa hiyo walikuwa hawakusanyi mapato ya kutosha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Serikali za Mitaa ni Serikali kamili, ukisoma Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania Ibara ya 145 na 146 inatambua kwamba Tanzania kutakuwa na Serikali za Mitaa. Hapo zamani hazikuwa kwenye Katiba lakini sasa zinatambulika kikatiba. Serikali za Mitaa zinakusanya mapato na mapato ya ndani ndiyo uhai wa kila halmashauri za mitaa lakini halmashauri nyingi wanategemea ruzuku na ruzuku ya Serikali ni kidogo sana. Vyanzo vingi vya mapato vyenye kero vilifutwa kwa sababu vilikuwa ni kero sana kwa wananchi na TAMISEMI au Serikali iliahidi kuwapa ruzuku Serikali za Mitaa ili kuwaongezea mapato ili waweze kutekeleza miradi ya maendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la kusikitisha Serikali haitoi ruzuku ya kutosha kwa halmashauri hata zile fedha ambazo zimetengwa kwa ajili ya kusaidia halmashauri hazitolewi zote. Kwa hiyo, utakuta miradi mingi imekwama, sasa hivi ukienda kila halmashauri kuna maboma, majengo ya zahanati yamekwama, majengo ya shule yamekwama. Kwa mfano katika Jimbo langu la Mpwapwa tuna zahanati tatu ambazo zimekwama mpaka sasa, zahanati ya Mugoma sasa miaka kumi haijakamilika, zahanati ya Mzase miaka kumi haijakamilika lakini kama halmashauri wangekuwa wanakusanya mapato ya kutosha na Serikali ingekuwa inatoa ruzuku ya kutosha hayo majengo yangeweza kukamilika.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu kudhibiti; katika utaratibu wa *Local Authorities* kuna Kamati ya Fedha na Mipango na Uongozi, hawa ndiyo wanaodhibiti mapato na matumizi ya halmashauri za wilaya. Bahati mbaya sana fedha nyingi za halmashauri zinakusanywa lakini hazifiki kwenye Mfuko Mkuu wa Halmashauri, kwa hiyo, zinatumika sana bila sheria ya fedha ambayo inahusika. Nilikuwa nashauri kwamba halmashauri zidhibiti mapato na matumizi na fedha zote zinazokusanywa zisitumike kabla hazifika kwenye Mfuko Mkuu wa Halmashauri na kupelekwa benki.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni kuhusu ulipaji wa posho za madiwani. Posho za madiwani ni haki yao, ni suala la kisheria, siyo kwamba halmashauri ni hiari hapana lakini kuna madiwani hawalipwi vizuri. Utakuta kuna halmashauri nyingine hazijalipa posho sasa ni miezi 12, miezi 14 hawajalipwa, na hizi posho ndiyo zinalipa deni la madiwani waliokopa kwenye vyombo vya fedha NBC, NMB na CRDB. Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI wahimize hawa wakurugenzi wamalize haya madeni kabla ya mwezi wa sita la sivyo kwa kuwa madiwani wamekopa kwenye mabenki, udiwani ukishakwisha hawataandama tena halmashauri kwa sababu halmashauri ndiyo waliowadhamini hawa madiwani. Kwa hiyo, mabenki yatawaandama madiwani, watakamatiwa mali zao madiwani, ni jambo ambalo ni baya sana kwa kweli. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, Mheshimiwa Waziri uagize halmashauri zako zote walipe posho hizi na walipe madeni ya Waheshimiwa Madiwani au benki ili wasikamatiwe mali zao baada ya udiwani kwisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la mwisho ni kodi ya majengo *(property tax)*. *Property tax* mimi sipingi, *TRA* wakusanye *property tax* ninachosema basi angalau wasikae mwaka mzima (miezi 12) *TRA* ndiyo wagawe fedha hizi kwenye halmashauri, angalau miezi sita *TRA* wakishakusanya angalau miezi sita waanze kuzigawa fedha hizi kweye halmashauri, wasisubiri miezi 12. Halmashauri za Wilaya, Manispaa, Majiji wana miradi yao, miradi haiwezi kusubiri fedha zibaki mpaka miezi 12 ndiyo zigawanywe kwenye halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana na naunga mkono hoja hizi zote mbili na naendelea kuzipongeza hizi kamati wanafanya kazi nzuri sana na sasa hati chafu zimepungua. halmashauri nyingi na Serikalini, Mashirika, Wizara nyingi zinapata hati safi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana.

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Allan Kiula atafuatiwa na Mheshimiwa Ali Salim Khamis, Mheshimiwa Felister Bura ajiandae.

**MHE. ALLAN J. KIULA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipatia nafasi niweze kuchangia kwenye kamati hizi mbili ambazo leo ndiyo siku yetu ya kuwasilisha ripoti. Kwanza kabisa niwapongeze wenyeviti wa kamati hizi mbili kwa kazi kubwa waliofanya ya kutuongoza. Jambo la pili nimpongeze *CAG* kwa kazi kubwa aliyofanya kwa sababu kazi yetu imekuwa nyepesi kwani wao walifanya kazi kwa weledi wakatushirikisha na sisi tukatembea kwenye hoja ambazo waliziandaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya hapo nipitie maeneo machache, eneo la kwanza ambalo nimeona ni muhimu kupitia ni suala la ukusanyaji wa mapato ambalo linafanywa na Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA)*. Hoja za *TRA* zimeelezwa katika kitabu ambacho mwenyekiti ameweza kukiwasilisha hapa kwenye ripoti hiyo. Kamati inachosisitiza ni kwamba *TRA* ni roho ya Serikali, ni roho ya nchi na bila mapato bajeti yetu tunayoipitisha inakuwa ni bajeti ambayo haiwezi kutekelezeka. Kwa hiyo, *TRA* ni chombo ambacho tunakitegemea sana kiweze kukusanya mapato na mapato hayo yagharamie bajeti ya Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama ndivyo basi hayo mapungufu ambayo tumeyaona ya (*outstanding taxes)* kodi nyingi kutokukusanywa yanatakiwa kufanyiwa kazi. Hapa linahitajika suala la weledi, suala la uadilifu na suala la kufanya kazi kwa bidii. Kukusanya kodi ni kazi kubwa lakini wakiwa na watumishi wenye weledi kazi hiyo itafanyika na mara zote tumekuwa tukiona suala la mlundikano wa rufaa kwenye Mabaraza ya Rufaa. Kamati ndiyo tumesema kwamba Bunge liazimie kwamba hizo kesi zimalizike na fedha au kodi iliyofungwa huko iweze kukusanywa.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo kama ipo kodi ambayo inaonekana haiwezi kukusanyika na ili vitabu vya *TRA* viweze kukaa sawa, basi hizo kodi zifanyiwe utaratibu wa kuweza kufutwa. Kwa mfano juzi tulipata wasilisho la kusudio la kufuta kodi ambayo inatokana na ile ada ya magari ya kila mwaka. Kwa hiyo, TRA wanayo kazi kubwa ya kuweza kuhakikisha kwamba wanarekebisha mahesabu yao lakini na kodi wanaikusanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo la pili ambalo ningependa kulizungumzia ambalo tumelizungumza kwenye kamati yetu ni suala la Wakala wa Majengo (TBA). Hilo jambo ni kubwa sana, katika kupitia mahesabu yao na katika kuzungumza na *TBA* yenyewe tumeona kwamba wana miradi mingi ambayo haijakamilika na hata katika utendaji wao tunaona miradi mingine

sasa wanaanza kunyang'anywa zinapewa taasisi nyingine. Hilo ni jambo ambalo linaashiria alama nyekundu kwa maana ya kwamba iko changamoto inabidi itatuliwe hapa. Pamoja na hayo yote, tunachoshauri pia labda hao *TBA* sasa wasipewe kazi nyingine mpaka wamalize hizi kazi zilizopo. *(Makofi)*

Nafikiri hilo litakuwa ni jambo kubwa na ni jambo zuri na ni jambo ambalo linaleta heshima kwa *TBA* yenyewe, lakini kama wameshika miradi midogo midogo na miradi haimaliziki hiyo haiwezi kuwa na sura nzuri kwa Taifa lakini pia hatuwezi kufuatilia matumizi mazuri ya fedha za Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Shirika la Nyumba *(National Housing Corporation)* na yenyewe kuna miradi mingi ambayo haijakamilika na miradi hiyo imesimama. Tumetembelea baadhi ya miradi kama ilivyoelezwa kwenye ripoti na tunaona sasa kwamba pesa ya umma au shirika lenyewe linakwenda kupoteza pesa nyingi. Miradi hiyo iliyosimama bado wakandarasi wako kwenye *site* na wakandarasi hao kwenye *site* wanalipwa pesa bila kufanya kazi. Sasa hatima ya *National Housing* ni nini? Hilo ndilo swali la kujiuliza, kwa hiyo tunaomba Serikali iingilie kati iweze kuona namna bora ya kuhakikisha kwamba baadhi ya miradi inakamilika, sio miradi yote ichaguliwe miradi ya kipaumbele ambayo inaweza ikamaliziwa na hizo nyumba zikauzwa au zikapangishwa kutokana na mpango ambao wao wameweka. Sasa hilo ni jambo muhimu sana kwa sababu hizo nyumba zitageuka kuwa magofu.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeona Serikali imetoa pesa nyingi kukarabati vyuo vya ualimu, tunaipongeza Serikali kwa kutoa pesa lakini pesa hizo nazo zimekwenda kwa utaratibu wetu wa *force account*. Sasa tunaona liko tatizo kidogo la usimamizi, jambo hilo ni kubwa, wasimamizi wanatakiwa wasimamie ili pesa isiweze kupoteza. Nia ya Serikali ni nzuri, lakini pesa zikienda tija hiyo isipoonekana na yenyewe inakuwa ni changamoto kubwa kwa sababu pesa ya Serikali ambayo ni kodi haiwezi kupotea hivi hivi. Kwa hivyo tunasisitiza kwamba pale ambapo tunaona usimamizi haukufanyika vizuri ambao hawakusimamia vizuri wachukuliwe hatua kwa sababu pia inakatisha tamaa kuona kwamba pesa zinatolewa halafu kazi iliyokusudiwa haifanyiki kikamilifu. Tunawapongeza na Wizara wamejitahidi kufanya kadiri walipoweza isipokuwa kwenye eneo la usimamizi.

Mheshimiwa Naibu Spika, Bandari tumeiona na yenyewe wamejitahidi, kwa nyakati tofauti bandari sasa hivi inafanya kazi kubwa tunaona pesa nyingi zinaingia na walitoa gawio juzi tuliona lakini suala la mifumo inabidi liandaliwe, mifumo iliyopo iweze kukamlishwa ili waweze kufanya kazi kwa ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo machache ya kuchangia, naunga mkono hoja au wasilisho letu chini ya Mwenyekiti wetu mama Kaboyoka. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ally Salum Khamis atafuatiwa na Mheshimiwa Felista Bura, Mheshimiwa Anatropia Theonest ajiandae.

**MHE. ALI SALIM KHAMIS:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante. Awali ya yote nimshukuru Mwenyezi Mungu kutujalia leo kuweza kuwasilisha ripoti zetu mbili hizi, lakini pia nikushukuru wewe Mheshimiwa Naibu Spika kunipa fursa hii na nitangulie kuwapongeza Wenyeviti wa Kamati kwa kazi nzuri ambayo wamefanya na leo wameweza kuwasilisha taarifa hizi hapa kwa ajili ya utekelezaji.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo nina mambo mawili tu ya kuchangia kwenye Kamati zetu mbili hizi na la kwanza ni suala la bandari. Suala la bandari tukichukua kumbukumbu nyingi ambazo zimepita huko nyuma ni jambo la kwanza ambalo Mheshimiwa Rais alitilia mkazo na nguvu nyingi kwa ajili ya kuhakikisha kwamba bandari inafanya kazi zake kwa weledi. Pia

Mheshimiwa Waziri Mkuu na yeye alichukua jitihada hizo ili pia kuhakikisha kwamba bandari inafanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, bandari ni uchumi wa nchi katika Taifa letu ama Taifa lingine lolote lile duniani. Leo ukiangalia Dubai ukiacha masuala ya mafuta jambo kubwa ambalo wanalitegemea katika kuendesha nchi yao ni bandari na wanapokea mizigo mingi kutoka sehemu mbalimbali na kusafirisha mizigo mingi na kuongezea pato lao la Taifa kwa nchi yao. Kwa hiyo ni muhimu na sisi sasa kuona kwamba bandari ni sehemu ya kuweza kukuza uchumi wa nchi yetu na kuonekana kwamba ni mahali pazuri pa kuweza kukusanya mapato ili kuleta ufanisi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nayasema haya kwa sababu kwa mujibu wa taarifa yetu ambao tumewasilisha hapa toka mwaka 2010 mpaka mwaka 2019 bandari inahangaika kuweka mifumo ya kieletroniki kwa ajili ya kukusanya mapato na kupatikana uhalisia ni mapato kiasi gani ambayo yanapatikana. Gharama kubwa ambayo imetumika zaidi ni kwamba zaidi ya bilioni 57 zimeshatumika kwa ajili ya kuweka hiyo mifumo lakini bila mafanikio. Sasa tuombe kwamba Serikali kama nilivyotangulia kusema Mheshimiwa Rais alifanya juhudi kubwa, lakini katika eneo hili la bandari mpaka leo kwenye masuala haya ambayo ni muhimu ya ukusanyaji wa mapato hayajakamilika ili kupata ufumbuzi wa mfumo sahihi wa kuweza kutoa takwimu sahihi na mapato sahihi ambayo yanakusanywa kwenye bandari.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kama ambavyo Kamati imeshauri naona sasa ifike mahali kwamba bandari iweze kufikia mwisho kwa ajili ya kuweza kuokoa fedha za walipa kodi ili kuweza kuweka mifumo sahihi na ambayo itaweza kutoa takwimu sahihi za mapato yanayopatikana katika bandari yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili ambalo nimekusudia kuchangia leo na nilimwona Mheshimiwa Waziri wa Fedha hapa muda si mrefu na nina imani yupo na Naibu Waziri yupo. Kuna jambo ambalo ni muhimu kulielekeza kwake Mheshimiwa Waziri wa Fedha na jambo hili linahusiana na Shirika letu la Ndege ambalo mara ya mwisho katika ukaguzi wa mwisho ambao umefanyika 2018/2019, Mkaguzi ameonesha tahadhari ya Shirika letu la Ndege kwenda kwenye hatari ya kufilisika kama madeni ambayo yapo hayatalipwa. Sasa Serikali imechukua jukumu la kwamba watalipa hayo madeni ili kuhakikisha kwamba Shirika linafanya kazi zake upya na kutengeneza faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nimwombe Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye yupo hapa kwamba hii *commitment* ambayo Serikali imekubali kuchukua juu ya Shirika la Ndege basi itekelezwe kwa wakati ili shirika lisije likapata matatizo kama yale ambayo yametokea huko awali na ukizingatia sasa hivi uwekezaji ambao umeshafanyika ni zaidi ya trilioni moja na nusu kwa ajili ya kulirudisha shirika hili ili liweze kufanya kazi kwa mafanikio.

Mheshimiwa Naibu Spika, la pili, mwaka 2016/2017 na 2017/2018 nilitoa ushauri hapa kwa Mheshimiwa Waziri wa Fedha ambaye alileta hoja mezani na nikasema kwamba kuanzishwa shirika ni jambo jema na tukakubali kwamba shirika hili litasaidia nchi, lakini tukatoa mawazo kwamba tunahitaji uweledi kwenye hili shirika. Najua kwamba wapo wataalam kwenye hili Shirika la Ndege Tanzania wanafanya kazi vizuri lakini utaalam wao una kikomo yaani unafika mahali lazima upate usaidizi kutoka kwa wataalam ambao wamebobea katika biashara hizi za ndege ili kulinyanyua shirika liweze kufanya kazi zake vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano, leo ukiangalia shirika letu la ndege la *Air Tanzania* limeshindwa hata kuanzisha safari za kutoka aidha, Dar es Salaam- Nairobi au Dar es Salaam – Zanzibar – Nairobi mpaka huu muda ambao tunazungumza. Leo *Jomo* Kenyata *Airport* ni *hub* katika Afrika Mashariki katika masuala ya kibiashara iwe ya ndege na mambo mengine, lakini

hadi leo shirika letu halijaweza kwenda Nairobi, lakini ukiangalia Kenya *Airways* wanakuja mara saba kwa siku Dar es Salaam pamoja na Zanzibar.

Mheshimiwa Naibu Spika, hii inaonesha kwamba sasa tunahitaji wataalam waliobobea zaidi katika masuala haya ili kulifanya shirika liweze kufanya kazi zake kibiashara zaidi na kuweza kuleta faida katika shirika hilo na hasa ukizingatia kwamba mwaka 2017/2018 shirika limepata hasara ya bilioni 10 baada ya *tax,* lakini 2018/2019 limepata hasara ya bilioni 16. Kwa hiyo badala ya hii hasara kupungua inaongezeka sasa na *nature* ya biashara hii maana yake leo ukipata hasara bilioni 10, mwakani ipungue ili mwisho wa siku iweze ku-*recover* ile *loss* na iweze kutengeneza faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa namwomba Mheshimiwa Waziri wa Fedha kwa sababu yeye ndio ambaye alileta hoja ya kulisimamia shirika hili na nina imani kwamba *commitment* ya Serikali kwamba wamekubali kulisimamia na ili shirika liweze kuendelea vizuri basi, sasa wakati umefika kwa Serikali kufikiria kutafuta mtaalam mbobezi katika masuala haya ya biashara ya ndege ili aweze kulisaidia Shirika la *Air* Tanzania.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikupe mfano wa pili mdogo tu, *Air* Tanzania imeanza kuja Dodoma na inakuja mara mbili kwa siku, lakini baada ya kuanzishwa hii *route* ya kuja Dodoma kwa sababu ya *potentially* ya biashara ya ndege utakuwa leo *Precision Air* anakuja mara tatu kwa siku wakati mwingine mara nne Dodoma na ndege zinajaa. Sasa wapi tunafeli tuna matatizo wapi ili tuone kwamba shirika tunalisaidia liweze kujiendesha kibiashara zaidi na liweze kwenda kwenye ushindani wa biashara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa badala ya kwamba sisi tulianzisha shirika ili tuweze kupata faida matokeo yake tunatengenezea watu njia kuwafanya watajirike zaidi katika hii biashara na sisi tunabaki kuwa tunawafuata wao nyuma. Kwa hiyo haya ni mambo ambayo yanaonesha kwamba pamoja na kazi nzuri ambayo wanafanya wataalam wetu lakini wanahitaji utaalam wa ubobezi ili kuwatoa hapa waliko kwenda kwenye *stage* nyingine.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, nikushukuru kwa kunipa fursa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Mheshimiwa Felister Bura atafuatiwa na Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, Mheshimiwa Martin Msuha ajiandae.

**MHE. FELISTER A. BURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kukushukuru sana kwa kunipa nafasi hii adimu ya kuchangia katika Bunge lako Tukufu. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa afya aliyonijalia siku ya leo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue fursa hii kuipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano wa usimamizi wa matumizi ya fedha za umma. Kabla ya Serikali ya Awamu ya Tano tulikuwa tunaona kurasa ripoti ya *PAC* na ripoti ya *LAAC* zilikuwa na kurasa zaidi ya 100, lakini kwa sasa ukiangalia taarifa iliyoletwa na Kamati hizi mbili unaona jinsi matumizi yalivyodhibitiwa na Serikali na fedha za umma zinatumika ipasavyo. Ukitaka kushuhudia hali hiyo Bunge lako Tukufu lilitoa maazimio kwa Serikali na maazimio hayo yametekelezwa kwa kiasi kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe tu mfano kwamba, Serikali imeboresha mfumo wa ulipaji kwa Mfuko Mkuu wa Serikali, lakini Serikali pia imeboresha mfumo wa ulipaji mishahara, kuondoa mishahara hewa, vile vile akaunti jumuishi Serikali imeboresha. Kamati yetu kipindi kilichopita tuliiomba Serikali kuona namna ya ukusanyaji wa madeni na hasa madeni ya SUMA JKT ambayo ilikopwa na watu binafsi. Tumeona mpaka mwezi wa sita mwaka 2018, Serikali imeweza kukusanya bilioni saba na milioni mia tisa. Pia tumeona madeni chechefu ya *TIB*

yameanza kukusanywa. Hii inaonesha jinsi Serikali ilivyo makini sasa kusimamia matumizi ya fedha za umma, naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano. Serikali pia imehakikishia Kamati kwamba itaendelea kuzingatia Sheria ya Bajeti na kwa utekelezaji wa shughuli mbalimbali za umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo *CAG* ameona upungufu kwa mashirika aliyokagua kati ya mashirika 150 amekagua mashirika 122, lakini kati ya mashirika hayo aliyokagua ameona upungufu, kama walivyosema wenzangu lakini nianze na *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO CAG* ameshindwa kutoa maoni yake kutokana na kasoro ambazo ni kubwa zilizoonekana katika shirika hili. Katika shirika hili la *STAMICO* shirika limepata hasara ya bilioni mbili na milioni 387 na hasara hii imetokana na nini, hasara hii imetokana na kutojumuishwa taarifa ya makampuni tanzu ya *STAMICO*. *STAMI Gold Limited* na Kyelwa *Tin Company* ambayo hesabu jumuishi ya mashirika haikujumuishwa kwenye taarifa ya hesabu ya *STAMICO*. Pia hali halisi ya madeni ya mashirika haya, lakini hali halisi ya madeni ya *STAMICO,* pia uwekezaji wa bilioni 33 ya uwekezaji *STAMICO* katika kampuni hizi sio wa uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* haijafanya tathmini ya uwekezaji au ya makubaliano yake kati yake na *Tanzania One Mining* na kama ni uendeshaji wa pamoja au kama ni *joint venture*. Kwa hiyo haya yamefanya *CAG* asitoe maoni. Niiombe Serikali imeweza kudhibiti mambo mengi kwa mashirika ya umma imeweza kudhibiti matumizi mabaya kwa mashirika ya umma na hata kwa halmashauri zetu itupie jicho *STAMICO* na kusimamia haya ambayo *CAG* ameyaona kwa *STAMICO*. Pia *STAMICO* iliweka asilimia 10 ya uwekezaji kwa kampuni ya Itetemia, *STAMICO* haijawahi kupata faida stahiki. Kwa hiyo niiombe Serikali iangalie namna ya kuisaidia *STAMICO*.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia tulikagua *National Housing, National Housing* kazi yake ni kujenga na kuuza majengo hapa nchini na imejenga majengo mengi katika halmashauri zetu, lakini kuna uwekezaji uliofanywa pale Kawe, uwekezaji wa nyumba 711 kwa *site* ya kwanza. Hata hivyo, mpaka sasa ule uwekezaji umesimama na umesimama kwa sababu Shirika la Nyumba la Taifa halina fedha za kuendesha ile miradi, lakini pia tumeona miradi ya pale eneo la Victoria pia kuna miradi mikubwa ambayo *National Housing* ilianza kujenga ni vitega uchumi lakini mpaka sasa miradi ile imesimama.

Mheshimiwa Naibu Spika, nina wasiwasi kwamba wale wakandarasi waliokuwa wanajenga zile nyumba watakuja kuleta hasara kwa *National Housing* kwa sababu watadai fedha. Wamesimama ujenzi sio kwamba wao wameshindwa kazi, wamesimama ujenzi kwa sababu hakuna fedha za kuendeleza ujenzi. Kwa hiyo wao wanahesabu kila siku faida, kila siku hasara wanayoipata kila siku wanachaji kwa *National Housing* na hizi fedha *National Housing* walizikopa sio kwamba ni za kwao na kule walikokopa kila siku riba inaingia.

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Serikali iamue kukwamua *National Housing* tusiache lile shirika letu zuri ambalo limefanya kazi nzuri kwa muda mrefu likapata hasara ambayo haitaweza kumudu kulipa na tumeona kama Serikali haitawasaidia bilioni 99 kwa ripoti ya *CAG* tuliyoipata watatakiwa kuwalipa wakandarasi.

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumze pia juu ya *TPA* au juu ya bandari tumeona hali halisi ya bandari ilivyo. Nawashukuru na kuwapongeza kwamba walitoa gawio Serikalini bilioni 168, walitoa Serikalini, nawapongeza sana, lakini kitu ambacho ni shida pale ni usimikaji wa mifumo ya uendeshaji na usimamizi wa shughuli za bandari. Bandari ni shirika ambalo tunalitegemea kuisaidia Serikali katika mapato, lakini kama mifumo haieleweki na mifumo yenyewe imeshagharimu bilioni 57 lakini mpaka leo haijakamilika. Niiombe Serikali isaidie na kuisimamia bandari ili mifumo hii ikakamilike kwa wakati.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala la *UDOM, UDOM* waliingia mkataba na Bima ya Afya kwamba Bima ya Afya wajenge Hospitali ya Benjamini Mkapa na mimi kama mwakilishi wa wananchi wa Dodoma naishukuru sana Serikali kwa ujenzi wa hospitali ya Bima ya Afya, wengi wanapata huduma pale na huduma inayopatikana pale maeneo mengine inawezekana haipatikani. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, BIMA waliambiwa na Serikali kwamba watapewa dhamana ya Serikali kufidia lile deni mpaka leo dhamana ya Serikali haijatoka. Mimi nilidhani ni kitu rahisi tu kwa Serikali kutoa dhamana ya kwake kwa mfuko wa Bima ya Afya. Kwa hiyo, niiombe Serikali, deni hili linazidi kukua kwa sababu ni muda mrefu sasa na mimi kama mkazi wa Dodoma naishukuru sana Serikali kupata hospitali ya Benjamin Mkapa. Lakini basi watoe dhamana kwa ule mfuko maana mfuko huu ni mfuko unaowatibu wenye uwezo na wasio na uwezo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Naipongeza sana Serikali ya Awamu ya Tano kwa kusimamia vizuri matumizi ya fedha za umma na kwa kuchukua hatua za haraka pale ambapo inaonekana kwamba kuna ufujaji wa pesa. Naunga mkono ripoti za Kamati zote mbili. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Anatropia Lwehikila Theonest, atafuatiwa na Mheshimiwa Martin Msuha, Mheshimiwa Leah Komanya ajiandae.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, nitoe mchango wangu kwenye Kamati yetu ya *PAC* ambayo pia ni Mjumbe. Nieleze masikitiko yangu na ya Kamati kwa utendaji usioridhisha wa *TRA*. Mwenyekiti amewasilisha vizuri sana na mimi nitaeleza pamoja na mambo mengine nitaeleza moja kati ya changamoto ambazo tulielezwa. *TRA* imekuwa na ufuatiliaji hafifu wa madeni ya kikodi, *TRA* kutofanyika mapitio ya kina ya miamala ya fedha ya makampuni mbalimbali ya Kimataifa. Na dosari katiika ukusanyaji wa makusanyo ya kodi katika viwanja vya ndege. *TRA* kutowasilisha kwa wakati mapato inayokusanya kwa niaba ya taasisi nyingine. *TRA* ina ucheleweshaji usio na tija wa maamuzi ya rufaa ya kikodi, uwepo wa madeni ya muda mrefu yasiyokusanywa. Huo ni mfano wa uozo mwingi ulioko *TRA*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huo ni mfano wa changamoto *TRA* inayosababishia watu wengine. *TRA* inaposhindwa kukusanya kodi inatengeneza msururu wa kuleta changamoto kwa wananchi wadogo wadogo ambao wamekuwa wakiteswa na kukamatwa kwa ajili ya kuchangia michango mbalimbali. Utaambiwa michango ya zahanati, michango ya shule, michango ya shule za kata, shule za misingi, watoto wanakaa chini kwa sababu ya watu wazembe ambao wako *TRA*. Sina uhakika kama ile bahati mbaya au ni makusudi, kwa sababu kama tunaweza tukaajiri watu ambao tunadhani hawana uwezo maana yake hatutaki kukusanya hela ya kutosha na tunazidi kuwaletea changamoto wananchi wetu wa chini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa katika *auditing query* za *CAG* kwa mwaka 2017/2018. Ameonesha kuna zaidi ya bilioni 974 kitengo cha kukusanya kodi za ndani yaani *domestic revenue department* kulikuwa na dosari alihoji *CAG* wapi kilipo kiwango cha zaidi ya bilioni 679 na *TRA* waliweza ku-*verify* kiasi cha bilioni 56 tu lakini kwa walipa kodi wakubwa *(large tax payers) CAG* alihoji kiwango cha bilioni 607 ikiwa ni pamoja na $ milioni 24 ambayo ni sawa kama na zaidi ya milioni 500. Hizi ukiziweka pamoja unapata kiwango cha shilingi bilioni 974 kama nilivyokwisha eleza awali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hizo hela zote zimekuwa zinahojiwa kwa mwaka 2017/2018. Hizo hela ungeziweka pamoja kwa kiwango cha kujenga zahanati moja kwa shilingi milioni 244

ingejenga zaidi ya zahanati 3,600. Tutakuwa hapa tunasema wanawake wanakufa kwa kujifungua, watoto wanakaa chini, watoto wanapata mimba kwa kutembea umbali mrefu kufuata elimu katika maeneo kadha wa kadha kumbe tuwasababishia sisi changamoto kwa kuweka watu katika taasisi wasioweza kukusanya kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini wakati mwingine najiuliza pengine hawa watu sio kwamba wana uwezo hafifu au inafanywa makusdi.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, taarifa.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia kuna taarifa. Mheshimiwa Dkt. Ashatu Kijaji!

**T A A R I F A**

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kumpa Taarifa mzungumzaji kwamba afahamu kwamba katika kipindi ambacho *TRA* imeimarika kiutendaji, kifanisi ni kipindi hiki na ndiyo maana mwezi wa 12, 2019 tumekusanya zaidi ya trilioni 1.976. Kwa hiyo, naomba alifahamu hilo huku akitambua hayo yalioneshwa kwenye Taarifa ya *CAG,* 2017/2018 ambayo Serikali tumeshaifanyia kazi kwa kiwango kikubwa na ndiyo maana tumeimarisha ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, wanapojadili aweze tu kusema sasa wapi tuboreshe zaidi kwa sababu madeni mengi tayari tumeshayakusanya mpaka sasa. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Antropia Theonest unapokea Taarifa hiyo?

**MHE ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, siipokei lakini nasikitika kwamba anakataa hata Taarifa ya *CAG.* Moja kati ya changamoto ambayo tutapata kama Serikali ni pamoja na kutotaka kushauriwa au kusikiliza watu wengine wanasema nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni mjumbe wa Kamati…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Anatropia, ngoja tuiweke vizuri kwa sababu Taarifa ambayo Bunge inajadili ni ya 2017/2018 kwa hivyo kwa mujibu wa Kanuni zetu Taarifa uliyokuwa unapewa ni ya kuhusu maboresho yaliyokuja baada ya hiyo Taarifa kutoka. Una uhuru Kikanuni wa kukubali au kukataa lakini sasa sio hoja tena ya Waziri kwamba labda anakataa kupokea unachotoa mapendekezo. Alikuwa anakutaarifu yale ambayo Serikali imeshafanya mpaka sasa. Mheshimiwa Anatropia endelea na mchango wako.

**MHE. ANATROPIA L. THEONEST:** Mheshimiwa Naibu Spika, katika mwaka 2017/2018 ni bajeti ya kwanza kuwa na *deficit* ya 19.7 *almost* asilimia 20 ya kukadiria ambacho hakitekelezeki kwa *almost* asilimia 20 kwa maana watu wana *expectations* au wanajua vyanzo vya mapato lakini hawaendi kukusanya fedha. Ni bajeti ya kwanza kuwa na nakisi kubwa ambayo ilikadiriwa bila kukusanywa. Nadhani Waziri ana nafasi ya kujibu na atasaidia ni namna gani hizo changamoto ataweza kuzitatua katika kipindi kinachokuja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu ya pili ambayo ililetwa kwenye Kamati ni juu ya kitu kinaitwa *immigration. Immigration* imeshaongelewa humu ndani zaidi ya mara moja na naiongelea imeletwa kwenye kamati yetu na imesababisha fungu husika kupata hati isiyoridhisha. Mtambo ulionunuliwa kwa ajili ya *e-passport* haukuwahi kuwa *recognized* kwamba ulinunuliwa shilingi ngapi, *tender* ilifanyika wapi? Ulikuwa na gharama gani? Lakini mkataba unahusu nini. Ametumbuliwa juzi Mheshimiwa Kangi Lugola kwa sababu amesaini mkataba

ambao haukuletwa Bungeni. Nataka yeyote aniambie hapa, mkataba uliongiwa kwa ajili ya kuleta mtambo wa *immigration* uliletwa Bungeni? *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa Mbunge hapa, uliletwa? Kama tunaamua kufanya haki, tusifanye *double standard*. Huo mkataba sisi kama Kamati tume-*demand* uletwe na tuliwafukuza waliokuja kwenye Kamati na jibu walilokuja nalo walisema haya maswali yanahusu usalama, usalama hauwezi kuwa kichaka cha kuingizia hasara Serikali hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kitu ambacho bado kina-*shock,* mtambo wenyewe hauko *secure, CAG* alituambia mtambo hauko *secure*. Mtu anaweza kuwa nyumbani kwake akawa anachapisha *visa,* yuko China au kokote anatoa tu *Visa* sehemu yoyote. Kwa hiyo, sasa ni lazima mjue athari ambayo mnalisababishia Taifa letu kama tunaamua kufichaficha mambo chini ya kapeti. *(Makofi)*

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Kengele ya pili imeshagonga Mheshimiwa. Ahsante sana. Mheshimiwa Martin Msuha, atafuatiwa na Mheshimiwa Leah Komanya, Mheshimiwa Cecilia Paresso ajiandae.

**MHE. MARTIN M. MSUHA:** Mheshimiwa Naibu Spika ahsante sana kwa kunipa nafasi na mimi niweze kuchangia hoja zilizoko mezani. Nitachangia Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Na mimi nianze kuchukua fursa kwa kumpongeza sana Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali kwa kazi kubwa anayoendelea kuifanya ya kuzifikia Halmashauri zote 185 kwa maana ya ukaguzi na Taarifa yake ndiyo msingi kwa kazi za Kamati yetu ya *LAAC*. Nitakuwa na maeneo makubwa mawili tu ya kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la kwanza ni mfuko wa wanawake, vijana na walemavu. Eneo la pili ni la uhaba mkubwa wa watumishi katika Mamlaka za Halmashauri zetu nchini. Katika eneo ambalo limekuwa likijionesha kama lina udhaifu mkubwa kwenye halmashauri zetu ni madeni ya mfuko wa wanawake, vijana na walemavu. Halmashauri zetu zilikuwa hazipeleki michango hiyo kwa wakati kwa miaka kadhaa iliyopita lakini niipongeze Serikali ilisikia mapendekezo ya Kamati kwa kutengeneza sheria ambayo sasa imeifanya halmashauri zetu kuchangia kwa lazima katika mfuko huu.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na sheria hii, madeni ya nyuma yalikuwa ni mzigo mkubwa kwa halmashauri zetu lakini pia Kamati iliona ifike na mapendekezo ya kufuta madeni ambayo yalikuwepo kabla ya kutungwa kwa sheria hii mwaka 2018.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue tena fursa nyingine kuipongeza Serikali kwa kufuta madeni hayo ambayo yalikuwa ni makubwa sana kwa halmashauri zetu. Mwaka 2019, Serikali ilikuja na *regulations* za jinsi ya kutoa mikopo kwenye vikundi vya akina mama, vijana na walemavu. Moja ya kifungu katika Kanuni hizi inaihitaji vikundi kurejesha baada ya miezi mitatu. Baada ya kuwa wamepata mkopo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimekutana na changamoto kwenye baadhi ya vikundi ambavyo vimepata mkopo na kushindwa kurejesha baada ya miezi mitatu kwa maana ya kutokana na asili ya biashara ambayo wanakwenda kuifanya. Kanuni hii imezichukulia vikundi vyote kana kwamba vinakwenda kufanya biashara inayofanana. Kwamba watakwenda kupeleka bidhaa sokoni ambazo ziko tayari lakini kumbe kuna vikundi vingine vinakwenda kuwekeza kwenye biashara ambayo inahitaji kuanza kuzalisha baada ya muda mrefu kidogo, pengine miezi sita au mwaka.

Mheshimiwa Naibu Spika, mfano, nilikutana na kikundi kimoja ambao wao wanakwenda kuwekeza kwenye ulimaji wa matunda na mbogamboga kwa kutumia kitalu nyumba mpaka kupita miezi mitatu ambayo sheria inahitaji waanze kurejesha walkuwa bado wapo kwenye ujenzi wa kitalunyumba na wanahitaji kwa mujibu wa Kanuni hii ya 10 waanze kurejesha mkopo huo. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali wakiangalie kifungu hiki, waweze kuvitenga vile vikundi katika ma-*group*. Vile vikundi ambavyo vinakwenda kufanya biashara *straight away* viwe na muda wake na vile ambavyo vina uwekezaji wa m uda mrefu viangaliwe ni kipindi gani vianze kurejesha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Mwenyekiti, ushauri mwingine sheria hii inahitaji halmashauri ziendelee kuchangia kipindi chote *indefinitely* na lengo ni kutengeneza mfuko ambao utakuwa ni *revolving*. Ziko halmashauri zetu zingine zina makusanyo makubwa sana ya ndani, kuzifanya zichangie asilimia 10 kwenye mfuko huu kunatengeneza fedha nyingi sana ambazi zitakuwa zinaweza zikalea matumizi mabaya baadaye. Kwa hiyo, tulikuwa tunashauri Serikali iangalie namna ya kujenga mfuko huu. Iweke labda miaka mitano halmashauri zichangie hizo asilimia 10 kufikia labda miaka mitano, halmashari hizi ambazo zina mapato makubwa zinakuwa zimeshatengenza mfuko mkubwa ambao unaweza kujiendesha. Baada ya hapo hizo asilimia 10 zielekezwe kwenye matumizi mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la pili ambalo nilihitaji kuchangia ambalo pia limejionesha kwa kiasi kikubwa kwenye vitabu vya Halmashauri zetu ni uhaba mkubwa sana wa watumishi katika Mamlaka za Serikali za Mitaa. Wakati fulani tunajiuliza kama halmashauri hizi zinaweza kuendeshwa kwa uhaba huo mkubwa wa watumishi, kwa mfano kule kwenye halmashauri yangu ya Wilaya ya Mbinga tuna uhaba wa walimu wa shule ya msingi wapatao 971 lakini watumishi Sekta ya Afya ni zaidi ya 400, huo ni uhaba. Wakati fulani tunajiuliza ni lini Serikali iliamua kufanya utafiti wa kiwango cha huduma ambazo zinatolewa kwa uhaba huo wa watumishi.

Mheshimiwa Naibu Spika, labda wakati fulani Serikali ijiulize kama Serikali za Mitaa zinaweza kujiendesha kukiwa na uhaba huu mkubwa wa watumishi, hizo ikama zilitengenezwa kwa uhalisia wa mahitaji ya hizo Halmashauri zetu? Labda hiyo inaweza ikatuletea ufafanuzi kwamba hayo ma-*gap* ya watumishi ni halisia au ni hesabu tu ambazo zilitengenezwa bila kuzingatia uhalisia.

Mheshimiwa Naibu Spika, uhaba huo unasababisha nafasi nyingi pia za Wakuu wa Idara kukaimiwa. Katika Taarifa za *CAG* zilizopita zinaonekana kwamba kuna madeni makubwa ya watumishi waliokuwa wanakaimu kwenye nafasi mbalimbali, unaweza kukurta mtumishi anadai mpaka milioni 50. Halmashauri moja inadaiwa milioni 400, 500 kutokana na posho za kukaimu nafasi mbalimbali za Ukuu wa Idara. Kwa hiyo, tunaishauri Serikali ifanye upekuzi mapema ili kuondokana na madeni ambayo si ya lazima wakati mwingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine hili la uhaba wa watumishi kwa mfano kule kwenye Halmashauri yetu ya Mbinga umefanya majengo mengi ambayo yamekamilika ya zahanati yasiweze kufunguliwa kwa wakati ni kutokana na uhaba wa watumishi wa Idara ya Afya kwa mfano zahanati ya Lukiti ambayo imepewa jina la Martin Mtonda Msuha haijafunguliwa kwa sababu ya uhaba wa watumishi. Zahanati ya kijiji cha Longa, zahanati ya Matuta na Kijiji na Ruanda. Zahanati hizi zote zimekamilika lakini hakuna watumishi wa kwenda kuanza kutoa huduma katika maeneo hayo. Kwa hiyo, nguvu za Serikali na za wananchi zimebaki hazitumiki ipasavyo kwa sababu ya kutosa watumishi wanaohitajika wa Idara ya Afya. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo la mwisho kwa sababu muda bado ninao, nichukue nafasi hii kuipongeza Serikali kwa kuona kuwa ukusanyaji wa mapato ya ndani umekuwa ni

changamoto kwa Halmashauri zetu na hivyo basi kutokana na hamashauri zetu kutokukusanya mapato ya kutosheleza matumizi yao imesababisha halmashauri nyingi kubadilisha matumizi. Halmashauri nyingi zimekuwa zikikopa kutoka kwenye akaunti ya amana ili kukidhi mahitaji yake ya ndani. Jambo hili limesababishwa na kutoweza kukusanya mapato yao ya ndani kikamilifu. Niipongeze Serikali imeliona hili, juzi hapa wamegawa mashine za kukusanyia mapato zipatazo 7,229 ambazo zimesambazwa nchi nzima kwenye Halmashauri yetu. Ni imani yetu sasa mashine hizi zitasimamiwa vizuri na TAMISEMI kwa maana ya kwamba zile *controls* walizoweka ili wale watumishi wasiwe wanachezea tena zile mashine kuziweka *offline* wakati wakiwa wanaendelea na makusanyo itafanyika hivyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini uhaba huu wa fedha za ndani umesababisha pia madeni makubwa sana kwa madiwani wetu. Madiwani wetu hawajalipwa posho kwa muda miezi mingi karibu Halmashauri nyingi nchini. Kwa hiyo, naishauri pia Serikali iangalie namna ya kufanya uchambuzi wa madeni ambayo madiwani wetu wanadai tunavyoeleka kukamilisha miaka mitano ya kipindi chetu cha utawala.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo naomba kuunga mkono Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa lakini pia Kamati ya *PAC.* Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Leah Komanya, atafuatiwa na Mheshimiwa Cecilia Paresso, tutamalizia na Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. LEAH J. KOMANYA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru kwa kunipatia nafasi. Pia nimshukuru Mwenyezi Mungu kwa kunipa kibali niweze kuchangia katika hoja hizi mbili.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishukuru kwa kipindi chote nilichokuwa Bungeni katika awamu hii nimeweza kuhudumu Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa. Mengi nimejifunza, mengi nimeyaona kumekuwa na mabadiliko katika halmashauri zetu katika utendaji kazi. Kumekuwa pia na mabadiliko katika usimamizi wa miradi, miradi imeongezeka tofauti na tulivyokuwa tunaanza.

Mheshimiwa Naibu Spika, pia Halmashauri katika kujinasua katika ukusanyaji wa mapato pia kumekuwepo na miradi ya kimkakati. Niipongeze Serikali ya Awamu ya Tano, Serikali ya Chama cha Mapinduzi chini ya uongozi wa Mheshimiwa Dkt. Magufuli kwa kuziwezesha Halmashauri zetu kupata miradi mikubwa ya kimkakati kwa mfano soko la Job Ndugai hapa Dodoma, stendi ya basi, soko la Morogoro na miradi mingine iliyopo katika mikoa mingine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuwepo kwa miradi ya mikakati kutatengeneza sasa mazingira ya kuwezesha ukusanyaji mzuri wa kodi kwa ajili ya Halmashauri. Kubwa pale niombe kuwepo na mikakati mizuri ya uendeshaji ili kuwe na tija katika ukusanyaji wa mapato na tija katika kutoa huduma kwa wananchi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kufuatia ripoti yetu kumekuwa na tatizo kubwa upande wa mafao ya watumishi, tofauti na tulivyokuwa tunaanza Kamati hakukuwa na matatizo ya michango ya watumishi katika mifuko yao ya mafao lakini kwa sasa kasi inakuwa kubwa sana ya mafao ya watumishi kutokupelekwa katika mifuko yao hususan kwa watumishi wa Halmashauri wanaolipwa na mapato ya ndani. Naomba hili kama Mwenyekiti wa Kamati alivyosoma jambo hili likemewe kabisa kwa sababu michango ni midogo lakini riba inaenda kuongezeka kwa kasi kubwa mpaka inazielemea Halmashauri kuweza kulipa mafao hayo na kusababisha watumishi wanaostaafu kupata shida.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda pia nichangie upande wa Halmashauri kutokukusanya kikamilifu mapato yao. Katika taarifa zetu Halmashauri nyingi zimeshindwa kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato kutokana na sababu mbalimbali za kimiundombinu na hali ya hewa. Moja ya sababu zilizotajwa ni uduni wa mtandao wa mawasiliano *(internet)* kwa kutumia zile mashine zetu za kukusanyia mapato. Sisi kama Kamati Halmashauri nyingi zilizofika katika Kamati zilionekana mapato hayakuweza kuwasilishwa Halmashauri wakati wa ukaguzi wa *CAG*, lakini baadaye yalionekana lakini pia yalisababisha kushuka kwa asilimia ya ukusanyaji wa mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na changamoto zilizo katika mashine hizi, sababu hii haimuondoi Mweka Hazina wa Halmashauri ya Wilaya kusimamia ukusanyaji wa mapato kwa kufuata sheria na kanuni za fedha za Serikali za Mitaa. Kwa sababu misimu ya ukusanyaji wa mapato inajulikana, unajua ni msimu gani upo juu lakini Mweka Hazina amekaa tu ofisini eti anasubiri mtandao usome. Kuna vigezo vingi vya kuangalia, anaweza kuangalia kwenye taarifa ya mapato na matumizi, anaona haipandi lakini umekuwa kama ni mwanya wa fedha hizi kutumika kwa matumizi mengine kabla hazijafikishwa Halmashauri. (*Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niipongeze Serikali kupitia TAMISEMI imeweza kutoa mashine za kukusanyia mapato 7,227 ambazo zimewekewa udhibiti zaidi na mashine hizi zinaonekana pia hazitakidhi mahitaji ya Halmashauri zilizopo. Ushauri wangu napenda kutokana naupungufu uliopo katika mashine zilizopo sasa hivi, Serikali ifanye utaratibu wa kuzitoa katika mzunguko zile mashine kwa sababu zifuatazo:-

Kwanza hazijulikani ziliponunuliwa, hakukuwa na mzabuni mmoja kwa hiyo udhibiti wa hizi mashine haukuwepo. Kuendelea kuwepo katika mzunguko zinaendelea kukusanya fedha ambazo haziingii katika mapato ya Halmashauri.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pia kupitia mashine hizi mpya zilizoletwa zitasababisha sasa kuwe na*control* ya mnunuzi Halmashauri fulani atajulikana *POS* yake iko Halmashauri fulani. Kwa hiyo, ushauri mkubwa ziondolewe katika mzunguko.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kama wenzangu walivyochangia nataka kuchangia kuhusu madai ya watumishi wa Halmashauri zetu za Serikali. Pamoja na juhudi zinazofanywa na Serikali za kulipa madeni ya watumishi lakini kumekuwepo na malimbikizo makubwa ya madeni ya watumishi katika halmashauri zetu. Kwa mfano, Halmashauri ya Chamwino kwa madai ya watumishi ni shilingi bilioni 1.3; Sumbawanga bilioni 1.3; na Halmashauri ya Meatu bilioni 1.5. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na kuwa Serikali inafanya uhakiki, ushauri wangu ambao nataka kuutoa, kama kuna watumishi ambao hawastahili kulipwa basi taarifa zirudishwe ili Halmashauri ziweze kupunguza katika madeni yaliyopo katika hesabu zao. Pia, Serikali iwe na mkakati wa makusudi wa kulipa madeni ya watumishi. Ushauri mwingine madeni mengine yanasababishwa na mishahara kwa ajili ya ule mfumo wa *Lawson*uidhinishaji wake ni mdogo, kwa hiyo inasababisha kutengeneza malimbikizo ya mishahara ambayo hayastahili yangeweza kulipwa katika mishahara kusiwepo na usumbufu wa watumishi kudai madeni yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, madeni yanayotokana na watumishi kukaimu kwa muda mrefu yamekuwa ni mengi hususan kwa watumishi wasio na barua za kutoka TAMISEMI ndio wanatengeneza madeni hayo.

Mheshimiwa Naibu Spika, pamoja na hayo nashukuru kwa mazuri yanayofanywa. Nakushukuru na naunga mkono hoja. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Cecilia Paresso atachangia dakika tano, atafuatiwa na Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. CECILIA D. PARESSO:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia ripoti ya *LAAC* na mimi pia ni mjumbe.

Mheshimiwa Mwenyekiti, kati ya mwaka 1998 na mwaka 2008 ilifanyika *reforms* kubwa sana kwenye *Local Government* na ilitumia fedha nyingi. *Reforms* hizo zilielekeza kuwajengea uwezo watumishi kwa maana ya Mkurugenzi na timu yake na menejimenti kwa ujumla lakini pia *reforms*hizo ziliwajengea uwezo Madiwani katika kusimamia fedha za Halmashauri zinazoletwa katika Halmashauri zao na *reforms* hizi zilitumia fedha nyingi kama nilivyoeleza.

Mheshimiwa Mwenyekiti, Serikali ya Awamu ya Tano ilipoingia madarakani kwa kweli imeonesha kabisa kutokuzithamini *Local Government* kwanza kwa uteuzi tu uliofanyika wa ma-*DED* tumeona ma-*DED* walioteuliwa kwa kiwango kikubwa wengi hawana uwezo, hawakutoka kwenye mfumo wa *Local Government. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, huko nyuma utaratibu uliokuwa unatumika kutokana na hizo *reforms*zilizofanyika, Mkurugenzi alikuwa anateuliwa ni mtumishi wa Serikali za Mitaa ambaye amehudumu kwa kipindi kisichozidi miaka mitano anaenda kuteuliwa kushika hiyo nafasi. Hii maana yake ni kwamba alitakiwa awe anazielewa Serikali za Mitaa, ajue kusimamia fedha vizuri, aielewe Serikali za Mitaa kwa ufanisi zaidi, lakini sasa hivi watendaji walioteuliwa kwa kweli hawana uwezo wowote.

Mheshimiwa Naibu Spika, haya ndiyo yanayosababisha tunaona *Local Government* leo hata miradi kwanza miradi yenyewe inayotekelezwa vipaumbele vinavyowekwa havifikiwi na wala havifanyiki kwa sababu ya upungufu huo. Pia *reforms* zile zilijenga uwezo kwa Madiwani, leo Madiwani wetu kwanza hata baadhi ya Halmashauri vikao havikai, hakuna fedha. vikao havifanyiki, Kamati za Fedha hazisimamii ipasavyo hata hizo fedha kidogo zinazopelekwa kwenye *Local Government. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nadhani tufike mahali kama nchi kama utawala wa awamu fulani unafanya mambo wa kadha wa kadha. Mfano, kama tulifanya *reforms* kwenye tawala zilizopita huko nyuma, utawala unaokuja hauna budi kurithi na kuhakikisha inaendeleza yale ambayo yaliendelezwa na utawala uliopita na sio kupindisha. Nadhani uzalendo wa nchi hii ni pamoja na kuyaenzi na kuyatekeleza yalifanyika kwenye awamu zilizopita na kuendeleza na si kuharibu ama kufanya ambavyo haitakiwi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tumeongea toka tunaanza Bunge hili na sasa tunaelekea ukomo wa Bunge hili. Tumeeleza jinsi ambavyo Serikali za Mitaa zimenyang'anywa mapato ya uhakika ambayo kwa kiwango kikubwa ndio yalikuwa yanasaidia kuwepo na uhai wa Serikali za Mitaa.

Leo wamenyang'anya vyanzo vya uhakika, mambo hayaendi kwenye Serikali za Mitaa, tutaendelea kuwataka Serikali kuhakikisha kwanza vyanzo vya uhakika kwenye *Local Government* vinarudishwa, waziachie Halmashauri zikusanye mapato/hizo fedha ili iweze kuendeleza miradi katika maeneo yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ni hiki kitu kinachoitwa *force account;* Serikali inaisemea sana na kuipigia chapuo, lakini mimi naona kutakuwa kuna shida kubwa sana mbeleni. Hizi *force account* miradi inayotekelezwa kwa*force account* inaenda kutekelezwa kwa kiwango kikubwa na hao mafundi ambao watateuliwa kwa utaratibu unaokuwepo lakini hatuangalii ubora wa majengo yanayojengwa kwa *force account. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawataka wasimamizi kwa maana ya Mainjinia wa Wilaya wakasimamie lakini tuna mainjinia wangapi kwenye wilaya moja wakasimamie miradi hii kuangalia ubora wa majengo yanayojengwa? Mainjinia wenyewe hawatoshi, utakuta kwenye wilaya moja labda kuna miradi minne ama mitano inayojengwa kwa *force account* halafu unataka injinia mmoja kwenye Halmashauri kwa sababu pia tuna upungufu mkubwa sana kwenye Halmashauri, unataka injinia huyohuyo mmoja akasimamie, hivi ufanisi wa miradi hii uko wapi?.

Mheshimiwa Naibu Spika, tunapokwenda mbele watakuja kuona miradi ya *force account* majengo yanaanguka tu hovyo hovyo kwa sababu hayajajengwa kitaalam, hayana usimamizi wa kila siku, tunawaachia hao mafundi sanifu ambao kwa kweli hawakidhi vigezo wanaenda wanazitazama hatuwaachii mainjinia, kwanza hatuna lakini haipati usimamizi wa kutosha kuhakikisha kwamba miradi hii kwa kweli inasimamiwa inavyotakiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nizungumzie suala la miradi ya mikakati. Kuna fedha nyingi sana zinakopwa kwa ajili ya miradi ya mkakati. Mfano hapa Dodoma…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umeisha Mheshimiwa, zilikuwa dakika tano, ahsante sana. Nilisema tutamalizia na Mheshimiwa Alex Gashaza.

**MHE. ALEX R. GASHAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi hii ili nami niweze kuchangia kwenye Taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa na Kamati ya *PAC*.Kwanza nianze kwa kumshukuru Mwenyezi Mungu ambaye amenipa nafasi ili kuweza kusimama kwa ajili ya kuchangia. Pili, nichukue nafasi hii kuishukuru Serikali kwa utekelezaji wa miradi mingi katika Halmashauri zetu. Miundombinu katika Sekta ya Afya na Sekta ya Elimu tumeona kazi iliyofanyika, tunaipongeza Serikali. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo maeneo ambayo nitapenda kusisitiza kama ambavyo tumeweza kuyaeleza katika taarifa yetu, baadhi ya Halmashauri na niseme kwa wingi zaidi ya asilimia 50 kuna maeneo ambayo yamepelekea kuweza kupata hoja za ukaguzi kwa mfano eneo la ku-*dispose* mali za Serikali kwenye Halmashauri zetu hususan magari chakavu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hizi hoja zimekuwa zikijirudia mara kwa mara na hazipatiwi ufumbuzi, lakini katika kutafakari kwa kina tumekuja kugundua kwamba yawezekana kuna changamoto hususan katika suala zima la sheria ya ku-*dispose* mali hizi, kwa sababu inachukua muda mrefu kwanza kukamilisha mchakato huu wa ku-*dispose* na hata Halmashauri wanapoanza *initiative* za kuandika barua kwa ajili ya kuomba kibali, kibali kinachelewa.

Mheshimiwa Naibu Spika,vile vile tumekuja kugundua kwamba pengine Halmashauri kwa sababu wao ndio wanapaswa kumgharamia Mhakikimali Mkuu wa Serikali au timu yake inayokuja kufanya *assessment,* basi Halmashauri wanaona hakuna sababu kwa sababu wanagharamikia baada ya kuuza fedha zinaenda Hazina na sio lazima kwamba zirudi kwa ajili ya kusaidia ama kununua gari nyingine kwa ajili ya ku-*replace* kwenye Halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, nipendekeze kwamba katika kipengele hiki ni vizuri tukaangalia kama kikwazo ni sharia, basi tuone namna gani ambavyo unaweza ukaletwa Muswada kwa ajili ya kurekebisha sheria hii ili kuwaondolea mzigo mkubwa Halmashauri ambao wanaamua sasa kuacha magari yanakuwa *grounded* na Serikali inaendelea kupata hasara.

Mheshimiwa Naibu Spika, sehemu nyingine ya pili ni kuhusu miradi hii inayotekelezwa na *force account* na hii inatokana na upungufu wa watumishi ambao wapo katika Halmashauri zetu. Serikali naipongeza kwamba wanaonesha jitihada za kuongeza watumishi hususan kwenye Sekta ya Elimu na Afya lakini kwenye upande wa uhandisi bado kasi ya kupeleka/kuajiri watumishi hao ni ndogo kiasi kwamba sasa usimamizi wa miradi hii ambayo inakuwa ikitekelezwa kwenye Halmashauri zetu inakuwa ni shida. Wapo ma-*engineer* na*technicians* ambao wapo mitaani hebu na wenyewe sasa kutokana na umuhimu kwamba Serikali inapeleka fedha nyingi kwa ajili ya kutekeleza miradi hii basi tuongeze pia idadi ya kuajili wataalam katika maeneo haya ili kusudi tuweze kupima ile *value for money. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hii ukijaribu kuangalia wakati tunatekeleza miradi ya MMEM mwaka 2000/2001, tulikuja kukutana na changamoto hii kwamba tulianza kujenga madarasa kwa wingi maeneo yote nchi nzima lakini kwa sababu usimamizi ulikuwa ni mdogo tumejikuta kwamba madarasa mengi yaliyojengwa leo hayatamaniki wakati ni muda mfupi. Kwa hiyo, ili tusiendelee kufanya makosa yaleyale ndio maana nashauri kwamba Serikali tuongeze idadi ya kuajiri hususan wataalam katika sekta hii ya uhandisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikielekea kwenye upande wa makusanyo, niipongeze Serikali kupitia Wizara ya TAMISEMI kwamba kwa sehemu kubwa kwa kweli wamefanya kazi kubwa baada ya kupeleka *POS* 7,227 kwenye Halmashauri zetu. Kupeleka *POS*ni jambo moja lakini pia kukusanya mapato inavyotakiwa ni jambo lingine kwa sababu unaweza ukapeleka *POS* lakini *POS* zile wakazi-*locate* kwenye vyanzo ambavyo sio *reliable* yaani vyanzo ambavyo havina mapato ya kutosha na zile *POS* zingine ambazo zimekuwepo na zimekuwa zikifanya udanganyifu zinapelekwa kwenye vyanzo vile ambavyo ndio kuna makusanyo makubwa na kukawepo na *leakage* kama ambavyo tumefanya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nishauri kama ambavyo Mbunge aliyechangia Mheshimiwa Komanya alisema kwamba ni afadhali zile *POS* ambazo zilikuwa zikitumika ambazo udhibiti wake sio rahisi basi zitolewe na Halmashauri hizi kwa sababu bei ya kununua *POS* hizi ambazo sasa zimedhibitiwa na kisasa bei imeshuka karibu kwa asilimia 75, basi walazimishwe kununua hizi *POS* mpya ambazo ni rahisi kuzidhibiti na hatimaye iwe rahisi sasa kuweza kuzungumza mfumo mzima wa makusanyo ili Halmashauri ziweze kuongezewa makusanyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie kwa kusisitiza kwenye upande wa stahiki za Madiwani. Tunamalizia muda lakini wapo Madiwani katika maeneo mengi wanadai Halmashauri zao posho zao lakini pia hata makato ambayo yamekuwa yakikatwa kwenye mikopo yao haipelekwi kwenye mabenki lakini pia hata huduma ya bima wamekuwa wakikatwa lakini hazipelekwi.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, muda uliobaki ni mdogo, tuombe kwamba Waziri mwenye dhamana na Serikali waweze kufuatilia kuhakikisha kwamba kwenye Halmashauri Madiwani hawa wasiondoke na madeni, wakati mwingine inakuwa ni ngumu kuweza kuja kudai baada ya kuwa wamemaliza muda wao. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilikuwa na hayo ya kuchangia na naunga mkono taarifa hizi za Kamati ya *LAAC* na Kamati ya *PAC*. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana Waheshimiwa tumefika mwisho wa kipindi chetu cha kwanza kwa siku ya leo, lakini naomba niwakumbushe hasa Wajumbe wa Kamati hizi mbili wanavyochangia hapa ndani waweze kutuongoza vizuri kwenye haya maazimio ambayo wametuletea maana ndio taarifa za Kamati zote mbili zipo hapa na Waheshimiwa Wabunge wamezisikia Wenyeviti wakisoma hapo.

Sasa ninavyoisikiliza michango ni kama inabishana na wote ni Wajumbe wa Kamati huko huko. Wapo Wajumbe wa Kamati wanaoneka kusema kuna maboresho makubwa sana, taarifa zimekuwa nzuri na hati chafu zimepungua ama kama zinaelekea kuisha hivi, zipo chache na wakati huohuo wengine wanaonesha kwamba hakuna kitu kimefanyika katika hii miaka yote. Sasa tuliongoze Bunge vizuri kwenye kufanya maamuzi baadaye leo maana kazi zinafanywa kwenye ngazi za Kamati halafu Wabunge wengine wanakuja kushirikishwa tukiwa hapa sasa Wajumbe wa Kamati watuongoze vizuri.

Waheshimiwa Wabunge nitasoma baadhi ya majina yatakayochangia mchana halafu wengine tutawasoma wakati huo. Mheshimiwa Yussuf Salim Hussein, Mheshimiwa Anastazia Wambura, Mheshimiwa Peter Msigwa, Mheshimiwa Khadija Nassir, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, Mheshimiwa Suleiman Zedi na Mheshimiwa Ritta Kabati. Tutaendelea kuwasoma kadri tutakavyokuwa tunaendelea.

Kwa sasa nasitisha shughuli za Bunge mpaka saa kumi na moja kamili jioni leo.

*(Saa 7.00 Mchana Bunge lilisitishwa mpakaSaa 11.00 Jioni)*

*(Saa 11.00 Jioni Bunge lilirudia)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa tukae.

**NDG. MOSSY LUKUVI – KATIBU MEZANI:**

**HOJA ZA KAMATI**

**TAARIFA ZA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI KWA MWAKA 2019 NA**

**TAARIFA YA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI ZA MITAA KWA MWAKA 2019**

*(Majadiliano Yanaendelea)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, tutaanza na Mheshimiwa Anastazia Wambura, atafuatiwa na Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, Mheshimiwa Selemani Zedi ajiandae.

**MHE. ANASTAZIA J. WAMBURA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi hii ya kuchangia, kuwa mchangiaji wa kwanza jioni hii. Nashukuru sana na nitangulie kumshukuru Mwenyezi Mungu kwa zawadi yake ya uhai na kwa mema mengi ambayo ametujalia katika Bunge letu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii pia kuwapa pole Watanzania wenzetu ambao wamekumbwa na maafa ya mafuriko na nimuombe pia Mwenyezi Mungu aiepushe nchi yetu na majanga ya aina hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Spika pamoja na Bunge letu kwa kazi nzuri ambayo tumeifanya jana ya kuwaenzi Maspika wastaafu. Kwa kweli ni kazi moja nzuri sana na ya kihistoria; naomba tujipongeze. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kipekee kabisa napenda pia kuishukuru Ofisi ya Spika kwa kuboresha vishikwambi, vimeboreshwa sana na vishikwambi hivi Kamati zetu zimeweza pia kutumia kwa kufanyia kazi za Kamati na vimefanya kazi nzuri sana. Na ukichukulia kwa mfano Kamati ya *LAAC* tulikuwa tunabeba vitabu vikubwa sana, vinaweza vikafika karibu kilo tatu au

zaidi ambavyo vilikuwa vinatutesa sana, lakini kwa vishikwambi hivi sasa tumeepukana na hiyo adha, kwa hiyo tunashukuru sana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kuunga mkono taarifa za Kamati ya *LAAC* ambayo ni Kamati yangu, ni Mjumbe wa Kamati ya *LAAC,* lakini pia Kamati ya *PAC,* naunga mkono taarifa zao, au taarifa zetu kwa asilimia 100. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza niseme ninachozungumza ninaongezea tu pale ambapo Kamati ya *LAAC* imezungumza kupitia Makamu Mwenyekiti wetu, kwa hiyo mimi ntaongezea kiasi fulani. Na nianze kusema kwamba katika maendeleo ya halmashauri au katika maendeleo ya Taifa kwa ujumla, cha kwanza kabisa ni lazima tuwe na rasilimali watu, lakini watu hawa tunaowasema ni lazima wawe ni watu wenye uwajibikaji wa kuridhisha. Lakini pia tunahitaji kitu kingine ambacho ni rasilimali fedha pamoja na vile vingine ambavyo alikuwa akivisema Hayati Baba wa Taifa; ardhi, siasa safi, uongozi bora, lakini mimi ntazungumzia hivi vitu viwili; rasilimali watu na rasilimali fedha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa tukienda katika halmashauri zetu tumekuwa na changamoto kubwa sana katika ukusanyaji wa mapato, na hili linatokana na baadhi ya watumishi kutokuwa waaminifu na vitu ambavyo vimekuwa vikitumika, zile nyenzo ambazo ni mashine za *POS,* watumishi hawa wamekuwa wakitumia *POS* bandia, mashine za *POS* bandia, lakini vilevile wakati mwingine wamekuwa wakizima *data,* na kuna wakati pia wanazitumia kwa matumizi tofauti na yale ambayo yamekusudiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niseme tu naipongeza sana Wizara ya TAMISEMI inayosimamiwa na Mheshimiwa Waziri Jafo na Naibu Mawaziri wake kwa uamuzi ambao wamechukua hivi karibuni. Uamuzi huu ni wa kuleta mashine mpya za *POS* ambazo zimeboreshwa vizuri sana. Mambo kama haya ambayo wamekuwa wakiyafanya hayawezekaniki katika mashine hizi mpya. Kwa hiyo, wameleta na wamesambaza mashine ambazo ni zaidi ya 7,000 katika halmashauri zote, mashine ambazo zimeboreshwa, ni za kisasa na zina *identification* yake kabisa, hawawezi wakatumia mashine bandia.

Mheshimiwa Naibu Spika, na kikubwa zaidi niseme tu kwamba tunapaswa kumpongeza sana Mheshimiwa Jafo na ofisi yake kwa jinsi ambavyo wamepunguza gharama za kuleta hizi mashine. Wameleta mashine kwa gharama ya asilimia 30 ya ile gharama ambayo ilikuwa ikitumika mwanzoni kununua mashine hizohizo. Kwa hiyo, tunapaswa wote kujifunza na kuiga uzalendo huu ambao wenzetu wametumia.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuyasema hayo niseme tu hivi karibuni halmashauri nyingi zimepunguza uwezekano wa kuwa na hati chafu, halmashauri zenye hati chafu ni chache sana. Lakini nitahadharishe tu kwamba kuwa na hati safi haimaanishi kwamba halmashauri zenye hati safi ndizo zinazofanya kazi nzuri kimaendeleo; hii si kweli.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii inatokana na nini; ni kutokana na mfumo wetu wa ukaguzi wa miradi ya maendeleo kwa sasa. Tunachokagua, unakuta tunakagua *input* na *output,* lakini *performance audit* tumeiacha, *impact* hatuiangalii sana. Kwa hiyo, tunakwenda kwenye *input* ambayo kwa Kiswahili nimetafuta sana Kiswahili chake, tulihangaika sana kwenye Kamati lakini nimepekuapekua nikakuta *input* ni pembejeo, ila sio pembejeo za kilimo. Ukisema *input* ina maana ni pembejeo, na *output* ni pato ila sio mazao ya kilimo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunakwenda kwenye *input-output,* ikiwa na maana kwamba kama unajenga kituo cha afya umeweka *input* pale ambazo ni fedha, na *output* ni kituo cha afya. Sasa tunashindwa bado Ofisi ya Mkaguzi inahitaji kuimarishwa zaidi ili iweze kufanya *performance audit. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niseme tu kwa uchache kutolea mfano mradi mmoja wa maji; unaweza usiamini kwamba tuna *engineer* wa maji ana-*design* mradi lakini ana-*skip* ile hatua ya kufanya *water treatment,* na mradi huu unaripotiwa kwamba umekamilika. Lakini ukishafika kwenye mradi sasa kuangalia *performance* au *impact* ya ule mradi, wananchi hawachoti maji pale badala yake wanaendelea kuchota maji katika visima binafsi, tena kwa kununua. Kwa hiyo, hapa ndipo mahali ambapo naona kuna *gap,* na kwa sababu hiyo niombe sana Ofisi ya Mkaguzi Mkuu iwezeshwe ili iweze kufanya *performance audit.* Ni kengele ya kwanza?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, utakuta pia – pengine itakuwa ni makusudi ana-*skip* hii hatua. Na miradi mingi tumeikuta hivyo, ni Kamati tumekwenda na tumekuta mambo kama hayo. Sasa wana-*skip* baadhi ya hatua, lakini baadaye kuna kichochoro fulani, kichaka tuseme, cha kuibia fedha, wanaweka *variation* kuongeza fedha na zile fedha unakuta ni nyingi sana, na kwa sababu hiyo sasa ndipo ubadhirifu ambapo unatokea.

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa niongee mengi sana lakini pia niombe hata kwenye vituo vya afya tuangalie suala la kuboresha hivi vituo vya afya viendane na kupunguza vifo vya akina mama na watoto. Kwa sababu kituo cha afya ni jambo moja lakini *impact* au ile athari ndiyo tunayoitaka hasa. Sasa tatizo ni ule usimamizi wa wale wahusika katika yale maeneo; waganga wakuu wa wilaya, waganga wakuu wa mikoa, sidhani kama wanafanya usimamizi wa kutosha kwa sababu ukiangalia takwimu utakuta kwamba kazi imefanyika kubwa, fedha zimetumika nyingi lakini vifo vya akina mama na watoto viko palepale katika baadhi ya maeneo.

Mheshimiwa Naibu Spika, naunga mkono hoja. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa, dakika saba, atafuatiwa na Mheshimiwa Selemani Zedi, Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza ajiandae.

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru, binafsi nianze kwa kuipongeza kwa sehemu Kamati kwa kazi nzuri ambayo wameifanya, na kazi kubwa ya Kamati hii, hii ni *oversight committee,* hasa baada ya kupata ripoti ya CAG ambaye ndio jicho letu la Bunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini pamoja na mambo mengi ambayo mmetupa Kamati Mwenyekiti, kuna mambo mengi ya msingi ambayo sisi kama Wabunge na kama wasimamizi wa rasilimali za Taifa hili tunataka tuyapate majibu kama Wabunge. Na wajibu wetu sisi kama Bunge ni kuisimamia Serikali na kwa bahati nzuri sana Serikali hii imejipambanua sana kwamba haitaki fedha zitumiwe hovyo.

Mheshimiwa Mwenyekiti, sasa nina maswali kadhaa ambayo ninamini kwamba Kamati yako haijatutendea haki kama Wabunge. Baada ya Ripoti ya CAG kuna mambo mengi sana ambayo CAG aliyaona. Kwa mfano kwenye ripoti yako sijaona masuala ya *flow meter;* ripoti ya CAG ilionesha kwamba haifanyi kazi, na Mheshimiwa Rais pamoja na Waziri Mkuu wamekwenda mara kwa mara na inaonekana *flow meter* hii kule bandarini haifanyi kazi; kwa nini kwenye Kamati yako hujatupa ripoti hii tukaweza kujua kuna kitu gani kinachoendelea?

Mheshimiwa Naibu Spika, katika Ripoti ya CAG, CAG alihoji masuala ya *uniform* za polisi, na kwenye ripoti yake CAG alisema kukosekana kwa nyaraka za kuthibitisha uletaji wa mzigo, niliomba hati ya kupokelea shehena ya mizigo bandarini ukurasa wa 311, Mheshimiwa Waziri aliyekuwa Waziri wa Mambo ya ndani hapa aliweka rehani mpaka Ubunge wake. Nilitegemea Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati hii, hizo gharama za ripoti na ile sintofahamu…

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mch. Msigwa; Mheshimiwa Waziri, Kanuni iliyovunjwa.

**KUHUSU UTARATIBU**

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA WAZIRI MKUU, SERA, BUNGE, KAZI, AJIRA, VIJANA NA WENYE ULEMAVU:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni ya 68 ambayo inazungumza kuhusu utaratibu, lakini nakwenda Kanuni ya 60(9) na Kanuni hiyo inasisitiza kila Mbunge kuchangia kwenye hoja ambayo ndiyo imewekwa Mezani kwa kuzingatia kile kilichowekwa Mezani.

Mheshimiwa Naibu Spika, tukienda kuitazama hotuba iliyosomwa na Mwenyekiti wa Kamati, yapo maeneo lakini upo ushauri wa kimsingi ambao amekwishakuuchangia, lakini sasa hayo ambayo hayako kwenye hii hotuba ya Mwenyekiti wa Kamati, sasa tukianza kuupanua tu huu mjadala kila mtu akaingiza na kusema na kusema kila anachofikiri anaweza kukisema hapa ndani, nadhani tunaweza sisi kama Serikali kushindwa sasa kupata mwongozo wa Waheshimiwa Wabunge katika kazi nzuri ambayo imekwisha kufanywa na Kamati. Kamati imetushauri kwa kupitia ripoti yake na hivyo tunatakiwa angalau tuweze kujielekeza katika mjadala na kupata yale ambayo kwa kweli ni maudhui.

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi hapa kujua ni kwa nini Kamati haikuleta mambo hayo yote ambayo mtu anaweza akayasema ama mtu mwingine anaweza kwenda mahali popote na kuongeza jambo lingine lolote.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Ester Bulaya, naomba ukae kwa sababu kwa Kanuni zetu ukishasemwa utaratibu inabidi mimi nitoe maamuzi yangu, sasa na wewe unataka kuomba juu ya utaratibu tena wewe utakuwa unamuombea yupi utaratibu. Kwa hiyo, wacha nizungumze nimalize halafu utapewa fursa. Mheshimiwa Ester Bulaya, naomba ukae. Naomba ukae, naomba ukae!

Waheshimiwa Wabunge, alikuwa akichangia Mheshimiwa Mch. Peter Msigwa na Mheshimiwa Jenista Mhagama amesimama kwa mujibu wa Kanuni ya 68 akionesha kwamba kuna kanuni inavunjwa katika uchangiaji wa Mheshimiwa Mch. Msigwa na ametupeleka kwenye Kanuni ya 60(9) inayomtaka Mbunge kulisema jambo ambalo liko katika mjadala na kutokurudiarudia maneno yale, na katika maelezo ya Mheshimiwa Jenista yanayoelekeza kwamba Mheshimiwa Mch. Msigwa amevunja Kanuni, Mheshimiwa Mch. Msigwa alikuwa anataja mambo ambayo yeye ameyaona kwenye taarifa ya Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali anajaribu kuonesha kwamba taarifa ya Kamati haioneshi mambo hayo ambayo yeye ameyaona.

Sasa mjadala uliopo mbele yetu, Kamati imeleta taarifa yake, pamoja na hiyo taarifa wameeleza maazimio ambayo wanatuongoza Bunge kuelekea huko na wakati wakihitimisha hoja zao wametamani kwamba yale mapendekezo yaliyoletwa na Kamati na yale maazimio ambayo wameyaleta wanatarajia kwamba Bunge tutakuwa tumewasikia ama tumesoma taarifa yao na tumewaelewa na yale maazimio wanayoyaleta tunajaribu kuchangia hapa na kwa kanuni zetu yule ambaye atapata fursa atakuwa pengine ama ameshafanya ama bado hajafanya kuleta marekebisho.

Sasa Waheshimiwa Wabunge, haya mambo aliyokuwa anayasema Mheshimiwa Mch. Msigwa anasoma kile kitabu cha *CAG* na hii taarifa ya *CAG* inaletwa hapa Bungeni halafu

inakwenda kwenye Kamati. Na pengine Mwenyekiti wa *LAAC*, lakini pia Mwenyekiti wa *PAC* watapata fursa ya kutoa ufafanuzi kwenye mambo kadhaa ambayo pengine Wabunge wangependa kuyazungumzia.

Hata hivyo, Mheshimiwa Mch. Msigwa ilikuwa nikupe maelezo kwa sababu unamuelekezea Mwenyekiti, hiyo nayo ni shida, unatakiwa uniambie, yaani usizumgumze na Mwenyekiti, unazungumza na Kiti ili Kiti ndiyo kiamue namna ya kwenda nalo jambo. *(Makofi)*

Kwa hiyo, usimpe Mwenyekiti, ukimpa Mwenyekiti ni kama unataka kuirudisha Kamati ikafanye kazi, sio? Kwa hiyo wewe zungumza na Kiti halafu Kiti kitajua namna ya kumpelekea Mwenyekiti. Na yeye anakusikia ndiyo maana atapewa fursa ya kujibu baadaye ama kujibu hoja za Waheshimiwa Wabunge kwenye hayo mambo ambayo pengine Wabunge wangependa kupata ufafanuzi kutoka kwa Mwenyekiti.

Mheshimiwa Mch. Msigwa!

**MHE. MCH. PETER S. MSIGWA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana. Ninashangaa kwa kweli kuona Serikali inashindwa kujibu hoja, hizi hoja ni kitabu cha Serikali, tunafanya kazi ya Umma, nikushukuru kwa kutoa uamuzi ambao ni sahihi kabisa.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja yangu niliyokuwa naizungumza ni kwamba haya ni mambo ya msingi, nimezungumza hii *flow meter* ilionekana kuna wizi mkubwa, na Rais alizungumza. Kwa nini Kamati haijatuambia Wabunge tuone huo wizi umedhibitiwa vipi?

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini nilienda kwenye hoja nyingine kuhusiana na *CAG* alidai *documents* zinazohoji nani aliagiza sare za polisi. Hizo bilioni 16 zinalipwaje, mlipwaji ni nani, tenda ilikuaje? Ninahoji ni kwa nini Kamati – bilioni 16 siyo hela ndogo – kwa nini Kamati haijaleta hapa tuone huyo mtu alilipwajelipwaje kwa sababu *CAG* alionesha haya mambo. Haya mambo ni kama yanapotea gizani, ni mambo ya msingi ambayo Serikali inataka tutunze hela na ni kweli ni haki yetu kusimamia hela, haya ni mambo ya msingi hayahitaji kufichwa. Watanzania wanapaswa wajue, Bunge hili linapaswa lijue.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Lugola alisema ataweka rehani Ubunge wake hapa. Mwenyekiti naomba atuambie hivyo vitu vyote *CAG* alivyovidai vimepatikana? Na juzi hapa tumesikia Rais anasema amelipwa sijui bilioni 10; amelipwalipwaje? *The Government moves on paper,* amelipwaje huyu mtu, kwa namna gani? Kamati haijatuletea.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, kwenye masuala ya *TPA* kule bandarini; *TPA* inataka kuvunja mkataba wakati mkandarasi yule ameshalipwa zaidi ya asilimia 70 na walimleta mtaalam kutoka nje asimamie, ni kwa nini wanataka kuvunja mkataba? Tunataka tujue haya mambo ili Bunge tusimamie vizuri Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine, watu wa *NIDA; CAG* alishasema vile vifaa vya *BVR* havifanyi kazi, vilikuwa sio *compatible* na *windows* ili vitoe vitambulisho vya uraia pamoja na vya kupigia kura lakini inasemekana sasa hivi vile vitu havifanyi kazi na wameagiza vitu vingine tena vipya hivi vingine vyote vinatupwa nje. Hizi ni hela za Watanzania tunataka tujue haya mambo yanakwendaje, yanafanyikaje haya mambo kienyejikienyeji na hili ni Bunge na Mheshimiwa Rais amesema watu wanafanya mikataba bila Bunge kujua. Haya masuala sisi hatujui yanafanyikaje? Masuala ya *e-passport* tulizungumza sana hapa Bungeni mauzo ya *passport* wakati mwingine yanaonekana kwamba kuna faida inaonekana. Hii *passport* chanzo chake kilikuwaje, tuliingia mkataba na nani? Tulitumia kiasi gani? Tunalipaje, *tender* ilikuwaje? *Passport* moja gharama yake ikoje? Sasa litakuwa Bunge la aina gani ambalo haliwezi kuhoji mambo kama haya.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Kamati ni *oversight committee* ambayo inapaswa isimamie pesa za walipa kodi, wana wajibu wa kutuambia mambo makubwa kama haya ndani ya Bunge lazima tuyajadili, hatuwezi tukawa tunashughulika na mambo ya Simba na Yanga hapa tunaacha mambo ya msingi haya ya hela ya wananchi. Hatukuja kwenye Simba na Yanga pamoja na kwamba mimi mpenzi wa Simba. Tumekuja hapa kuhakikisha tunasimamia kodi za wananchi, hela ya wananchi, si ndiyo mtazamo wa Mheshimiwa Rais kwamba hela ya nchi isiibiwe, haya mambo makubwa Kamati inaweza kuachaje ili yasijadiliwe kwa upana wake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba Mwenyekiti anapokuja kuhitimisha hapa, kuna mambo ya msingi ambayo ni lazima Bunge lijue, hizi ni hela nyingi, mabilioni ya Watanzania ambayo yanapaswa tuyajadili kwa kina ili Bunge lichukue nafasi yake. Hii mikataba mingi imeenda kimyakimya, kiholela holela Wabunge tunapita tu tunaondoka na sasa hivi tunamaliza muda wetu, tukienda kuulizwa kwa wananchi tutaenda kusema nini. Naomba Mheshimiwa Mwenyekiti atakaposimama hapa atuambie kwa nini kwenye ripoti yao hawajatuambia masuala ya *e-passport*, masuala ya *NIDA*, masuala ya nguo za Polisi; na nasikia kuna baadhi walienda wakachungulia tu watuambie walipata hizo *documents,* walienda kuchungulia tu makontena, kama walioneshwa mlangoni tu kule ndani labda kulikuwa na baiskeli tutajuaje sisi, kama walidanganywa zimetoka China inasemekana zimetengenezwa hapa hapa Tanzania, tunataka hayo mambo tujue, ndiyo wajibu wa *oversight committee. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo ningeomba Mheshimiwa hoja yangu ni kwamba pamoja na kazi nzuri waliyoifanya na mambo mengine, lakini kuna mambo ya msingi ambayo Taifa la Watanzania wanataka wayajue na yapatiwe majibu.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikushukuru sana kwa kunipa nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Selemani Zedi, atafuatiwa na Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza na Mheshimiwa Ritta Kabati ajiandae.

**MHE. SELEMANI J. ZEDI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi hii ili na mimi niweze kuchangia taarifa hizi mbili ambazo zimewasilishwa leo hapa Bungeni. Kwa kuanzia naunga mkono taarifa ya Kamati ya Hesabu za Serikali za Mitaa *(LAAC)* ambayo mimi pia ni Mjumbe kama ambavyo imewasilishwa na Mwenyekiti wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, mojawapo ya kazi za Kamati ya *LAAC* kikanuni ni kushughulikia maeneo yenye matatizo sugu katika matumizi ya fedha za umma zinazopelekwa kwenye Serikali za Mitaa. Sasa mimi nilipata bahati ya kuwa pia kwenye Kamati hii ya *LAAC* kwenye Bunge la Kumi na sasa hivi pia niko kwenye Kamati hii ya *LAAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninachoweza kusema katika eneo hili la maeneo yenye matatizo sugu ya matumizi ya fedha za umma zinazopelekwa kwenye Serikali za Mitaa ni kwamba, pamoja na kwamba maeneo haya yenye matatizo sugu hajashughulikiwa kikamilifu yote, lakini kuna *improvement* kubwa sana ukilinganisha hali ilivyokuwa miaka mitatu, minne nyuma kwenye maeneo haya haya na hali ilivyo sasa pamoja na kwamba hayajakwisha kabisa lakini *improvement* kubwa sana ambayo inatia moyo.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitazungumzia eneo moja la mapato ya ndani, kama ambavyo tunafahamu vyanzo vikubwa viwili vya fedha kwenye Serikali za Mitaa ni fedha zinazotoka Serikali Kuu na fedha ambazo ni makusanyo ya ndani ya halmashauri yenyewe.

Sasa Kamati yetu baada ya kupitia halmashauri kadhaa na kufanya mahojiano jambo ambalo limebainika wazi ni kwamba halmashauri zilizo nyingi karibu zote zina tatizo kubwa sana la kushindwa kukusanya mapato yao ya ndani kwa mujibu wa bajei zao ambazo zilikuwa zimepangwa. Ukisikia tunasema halmashauri haikuweza kukusannya mapato ya ndani maana yake ni kwamba kuna kazi ambazo zilipaswa zifanywe hazikufanywa, ndiyo maana yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano, huu mwaka wa fedha ambao tunauhoji ambao taarifa yake imewasilishwa ni mwaka wa fedha wa 2017/2018 ambako miongozo ya kibajeti ilikuwa inazitaka halmashauri zichangie kutoka mapato yake ya ndani, zichangie asilimia 60 kwenda kwenye miradi ya maendeleo. Kwa hiyo ukisikia tunasema halmashauri haikukusanya mapato yake ya ndani kwa mujibu wa bajeti maana yake ni kwamba hizi fedha zitakazopelekwa kwenye maendeleo hazikupelekwa na kama hazikupelekwa maana yake kuna kazi za maendeleo zilizokuwa zinapaswa zifanywe hazikufanyika, kuna madarasa yalikuwa yajengwe hayakujengwa, kuna zahanati zilizokuwa zijengwe hazikujengwa na shughuli nyingine mbalimbali za kimaendeleo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo *impact* ni hiyo, tunaposema halmashauri zinashindwa kukusanya mapato yake ya ndani haiishi hapo maana yake tunasema kuna shughuli za kimaendeleo zilizotakiwa zifanywe hazikufanyika na hii ndiyo inafika wakati wanafunzi wanamaliza darasa la saba wamefaulu kwenda kidato cha kwanza, tunajikuta madawati hakuna, vyumba vya madarasa hakuna, ni kwamba hayo yote yaliyokuwa yafanywe hayakufanywa kwa sababu halmashauri hazikukusanya mapato ya ndani na ile asilimia iliyopaswa kwenda kwenye miradi ya maendeleo haikuweza kwenda na hili haliathiri tu miradi ya maendeleo, lakini hata matumizi ya kawaida.

Mheshimiwa Naibu Spika, kutokana na halmashauri kushindwa kukusanya ndiyo maana karibu halmashauri zote sasa hivi zina tatizo kubwa, Madiwani hawalipwi kwenye vikao vyao vya Kisheria na unakuta kwa mfano pale Nzega halmashauri ya Nzega *DC* sasa hivi hata Madiwani wanashindwa hata kupita hesabu wanadai halmashauri kiasi gani kwa sababu wakati mwingine wakienda kwenye kikao wanalipwa posho ya kikao *night* hawalipwi, wakati mwingi wanalipwa *night* posho ya kikao hawalipwi, wakati mwingine hawalipwi posho ya kikao wala hawalipwi *night* na wakati mwingine unakuta halmashauri ya Nzega *DC* ina Madiwani 52 wamefanya kikao wamemaliza wanakwenda kwenye foleni ya kulipwa posho wanalipwa mpaka Diwani wa 23 hela zinakwisha, waliobaki wengine hawalipwi, kwa hiyo ni vurugu tupu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo tunaposema kwamba halmashauri inashindwa kukusanya maana yake ni kwamba kuna madhara makubwa sana na hili kwa kweli ushauri wangu ni kwamba; TAMISEMI itoe maagizo mahususi kwa Wakurugenzi wa halmashauri ili kabla mabaraza hayavunjwa mwezi wa Sita hawa Madiwani wawe wamepata stahiki zao zote wanazodai ili mabaraza yanapovunjwa wawe hawadai, hata ikiwezekana kwa halmashauri kukopeshwa na TAMISEMI na watajua namna ambavyo watafidiana wao wenyewe. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo Kamati imebaini baada ya kuhoji halmashauri ni eneo la miradi inayotekelezwa kwa *force account*. Kwa ujumla wake imethibitika bila shaka yoyote kwamba miradi inayotekelezwa kwa *force account* inashia kuwa ni miradi yenye gharama nafuu ukilinganisha na ile miradi ambayo ilikuwa inatekelezwa na ma-*Contractor*. Hata hivyo, *issue* iko kwenye *quality* (ubora) na hii inatokana na halmashauri nyingi kutokuwa na Wahandisi wa kutosha wa kwenda kuzikagua kazi kadri zinavyojengwa kwa sababu *force account* huko vijijini kwenye kata wanaajiri ma-*local* Fundi, Mafundi wanaopatikana kulekule. Kwa mfano wanajenga darasa, wakijenga msingi ni lazima Mhandisi wa Wilaya aende akaukague aone uko sawa atoe *go ahead,* ndiyo waendelee. Sasa unakuta Wilaya kama ya Nzega vijiji 167Mhandisi mmoja vijiji vyote vinamuhitaji unakuta kijiji kinahitaji

Mhandisi aje aangalie kazi atoe *go ahead* kina msubiri miezi mitatu, minne wamekaa hawaendelei.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, mwisho wa siku unakuta kazi iliyokuwa ifanywe kwa miezi mitatu inafanywa kwa mwaka. Kwa hiyo maana yake ni kwamba gharama inakuwa kubwa na ubora unakuwa ni *compromise*. Kwa hiyo eneo hili ushauri wangu ni kwamba pamoja na kwamba Mainjinia wengi walikwenda *TARURA*, lakini halmashauri kwa maana ya majengo na usimamizi wa hii miradi ya *force account* ni lazime iwezeshwe kwa kuwa na Wahandisi wa kutosha ili waweze kuzikagua kazi na kutoa *go ahead* na kuhakikisha miradi ya *force account* siyo tu kwamba inapunguza gharama, lakini inahakikisha ubora wa miradi unakuwepo kadri ambavyo tunatarajia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo tumebaini baada ya kuhoji halmashauri ni kwamba, halmashauri zina tatizo la kutowasilisha michango ya akiba ya uzeeni ya wafanyakazi wake kwenye mifuko husika. Hili ni hatari, sasa hivi unaweza usilione kama hatari, lakini baadaye mfanyakazi anapostaafu, akifika kule fedha zake hazipo hapati, anateseka na inakuwa kero kubwa. Kwa hiyo ushauri wangu hapa ni kwamba iwe ni kipaumbele kwa Wakurugenzi kuhakikisha kwamba makato ya akiba za uzeeni kwa wafanyakazi yanawasilishwa kwenye mifuko husika kuliko ilivyo sasa ambavyo yanakatwa lakini hayapelekwi yanatumika pale halmashauri na baadae inakuwa kero kubwa kwa wahusika.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimalizie…

*(Hapa kengele ililia kuashiria kwisha kwa muda wa Mzungumzaji)*

**NAIBU SPIKA:** Muda wako umekwisha Mheshimiwa, ahsante sana. Mheshimiwa Conchesta Rwamlaza, atafuatiwa na Mheshimiwa Ritta Kabati na Mheshimiwa Mriam Kisangi ajiandae.

**MHE. CONCHESTA L. RWAMLAZA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru kwa kunipa nafasi nafasi niweze kuongea kidogo kuhusu hoja ya Kamati yetu ya *LAAC* ambayo na mimi ni Mjumbe. Kwa sababu nina muda mfupi naomba niende moja kwa moja.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda niongelee kuhusu asilimia kumi ya wanawake na vijana pamoja na wanawake na watu wenye ulemavu ambayo inapaswa itolewe na halmashauri kutoka na *own source* yake. Tumegundua na kwa muda mrefu katika ukaguzi wetu tuliona kwamba kuna madeni mengi ambayo halmashauri haiwezi kulipa kutokana na uwezo mdogo wa kuweza kulipwa madeni ya asilimia kumi, tumeishauri Serikali kuhusu kufuta madeni na Serikali imekubali kwa hili imefuta madeni yete ya nyuma lakini mwaka 2018/2019 michango hii inapaswa kuendelea kulipwa. Ukitazama kwamba Serikali imekubali kufuta hayo madeni, sasa napenda kujua Waziri atueleze kama amefuta madeni ya halmashauri kuna pesa ambazo tayari zilikuwa zimekuwa kwenye vikundi, je na zenyewe zimefutwa? Ina maana halmashauri inakwenda kupata hasara kwa kwa sababu hizi ni pesa ni za *own source*. Kwa hiyo tunapenda kupata majibu kuhusu hilo.

Mheshimiwa Naibu Spika, halmashauri zinapeleka pesa katika Bohari ya Dawa, lakini wakati mwingine wanachewa kuleta dawa na wakati mwingine wanaleta dawa ambazo zinakaribia kuisha muda wake. Kwa hiyo na hilo tumeliona kwamba si kitu sahihi kuhakikisha kwamba *MSD* inatoa dawa ikizingatia kwamba halmashauri kazi yake ni kutoa huduma kwa wananchi ni pamoja na afya, elimu na mambo mengine.

Mheshimiwa Naibu Spika, iko miradi ya kimkakati, kwa mfano iko miradi ya hapa Dodoma ya stendi kuu ya mabasi na soko, lakini kule Morogoro kuna soko kuu, masoko haya

yanachukua gharama kubwa, pia tunapenda kujiuliza pamoja na gharama kubwa zilizowekwa katika miradi hii na hasa masoko, je, watu wa chini wataweza kufaidika na masoko haya? Kwa sababu kwa mfano lile soko la Morogoro tumekuta kwamba katika ziara hilo soko halina mkopo hata kidogo ni pesa zimetoka Serikali Kuu pamoja na ule mradi wa kuboresha Miji. Tunachoishauri Serikali ili miradi hii iweze kutumika vizuri, basi halmashauri hizo zisiweke gharama kubwa katika kupangisha, waweke gharama ambazo zitasaidia watu wengi kuweza kuingia ndani ya soko mle na kuweza kufanya kazi na hatimaye halmashauri kupata mapato.

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda *particularly* kuongelea kuhusu Dodoma; ninayo hoja ya msingi na watu wa Dodoma watanisamehe na hasa Mbunge na Madiwani. Dodoma ina mapato mengi sasa hivi, wanapata mapato zaidi ya bilioni 60, wanayo miradi mikubwa ambayo wanatekeleza ni sawa, lakini Jiji la Dodoma limeshindwa kutengeneza barabara za mitaani, huko mitaani kumeoza. Napenda kusema kwamba, je, hizi barabara ni za nani, ni za Halmashauri ya Jiji, au ni za *TARURA*, na kama ni *TARURA* ina maana hawana sensa, hawajui idadi ya barabara zao walizonazo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa Sheria tuliyopitisha ni kwamba halmashauri ikiwa na pesa inapaswa kuichangia *TARURA* ili kuhakikisha kwamba inatengeneza barabara za mitaa. Hatukatai kwamba tuna miradi ya *Word Bank*, inatengeneza lami katika maeneo mbalimbali katika jiji, lakini kule kwenye mitaa hakuko vizuri. Kwa wale wanaokaa mitaani nafikiri mmeshaona kinachoendelea hapa, mimi mpaka nimejiuliza maswali mengi, hivi hawa Madiwani wa hapa huwa wanasema nini ndani ya Baraza lao la Madiwani, sielewi hata wachokisema, kwa sababu kama Jiji linaweza kuwa na pesa za namna hii, inawezekanaje wasitenge pesa za kuweza kutengeneza barabara hata zile za vumbi, kurekebisha kwa sababu Dodoma ni mahali ambapo ardhi mvua inaponyesha hali inakuwa mbaya.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema neno hili kwa sababu tumekagua juzi Halmashauri ya Jiji la Dodoma wanayo mapato makubwa na wanajivuna kwa kweli, wamekusanya, wana hela nyingi. Kwa hiyo tunaomba Waziri na yeye anaishi hapa na wengine wote mnaishi hapa. Tunaomba Dodoma watutengenezee barabara za mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Ritta Kabati atafuatiwa na Mheshimiwa Joyce Sokombi, Mheshimiwa Omar Kigua ajiandae.

**MHE. RITTA E. KABATI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa kunipa nafasi ili na mimi niweze kuchangia Kamati ya *PAC* na *LAAC*. Nianze kwanza kuipongeza Serikali yetu ya Chama cha Mapinduzi ambayo kwa kweli imefanya kazi kubwa sana. Vilevile nizipongeze Kamati ya *PAC* na *LAAC* kwa ripoti zao ambazo wameziwasilisha hapa. Tulipokuwa tunachangia zamani tulikuwa tunasema halmashauri zetu zilikuwa kama vichaka vile vya pesa nyingi tulikuwa tunazipeleka kwenye halmashauri, lakini tunaona miradi haikamiliki, lakini sasa hivi Serikali imefanya kazi kubwa sana ya kusimamia mapato katika halmashauri zetu na tunaona sasa miradi mingi sana inakamilika kwa wakati na mambo yanakwenda sawa.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna machache ambayo nataka kuchangia; jambo la kwanza ni kuhusiana na mkopo, ile asilimia kumi, yaani asilimia nne akinamama, asilimia nne ya vijana na asilimia mbili ya watu wenye ulemavu. Kwanza niipongeze sana Serikali nimeona hata katika ripoti Kamati imesema kwamba ni kitu ambacho ilifanya kazi ikahakikisha kwamba inakuwa Sheria. Kwa hiyo hii ni pongezi pia kwa Serikali yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa mchango wangu ni kwamba, nikitoa mfano kwenye halmashauri yangu, imefanya vizuri sana. Kwa mfano halmashauri yetu ina vikundi karibu 1200

na utaona kwa mwaka tukichukua 2018/2019, vikundi 98 viliweza kupatiwqa mikopo karibu milioni 400. Sasa ushauri wangu halmshauri nyingi sana hazina uwezo wa kukopesha, yaani hii pesa tulikuwa tuna imani kwamba akinamama, vijana na watu wenye ulemavu iweze kuwasaidia katika miradi ili waweze pia hata kuchangia kodi Serikalini.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ushauri wangu ni kwamba, kuwepo na vikundi kwa mfano kuna makundi mengine yanafanya kazi nzuri sana, mtaji wao ni mkubwa wanapewa pesa kidogo inakuwa haiwasaidii, lakini kingekuwepo kiwango ambacho vile vikundi vikubwa viki-*graduate* wasikopeshwe na halmashauri, pengine kungekuwepo na Mfuko wa Vijana au Mfuko wa Rais, wale sasa wafanyabiashara wakubwa wakubwa wakopeshwe huko ili hawa wadogo waweze kukopeshwa na halmashauri ili na wenyewe waweze kupata ile pesa, vikundi vyao viweze kupata na kuendelea kuliko ilivyo sasa hivi ambapo pesa inakuwa haitoshi wanapewa kidogo kidogo kiasi kwamba inakuwa haiwasaidii wale vijana na akinamama.*(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nilikuwa nataka kuchangia ni kuhusu madai ya wastaafu; kwa kweli wastaafu maana yake ni wafanyakazi ambao wameitumikia hii Serikali yetu kwa muda mrefu. Kuna walimu, kuna wauguzi, kuna wafanyakazi wengi ambao wamefanya lakini wanapostaafu wanacheleweshewa sana malipo yao. Wanakuwa na madeni makubwa sana. Mstaafu anastaafu anaanza kufuatilia *lile* fao mpaka anaweza akafa, anaweza akaugua. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikitoa tu mfano kwenye Halmashauri yetu, unakuta Mwaka 2018/2019 na 2019/2020 wastaafu wanadai fedha kama milioni 81 sasa ukija Mwaka 2020/2021 wale ambao wanastaafu wanahitaji malipo ya karibu milioni 45. Sasa Serikali imeweka mpango mzuri sana, wafanyakazi wote wapo kwenye *data* wanajua kwamba Mwaka kesho watastaafu. Ni kwanini wasingekuwa wanawaandalia kabisa hawa ambao watategemea kustaafu kipindi kingine ili baadaye kusiwepo na usumbufu ambao wanaupata.

Mheshimiwa Naibu Spika, ningeomba kwa kweli Serikali ingefanya kitu kama hicho ili wastaafu wetu wengine wanakuwa wakishastaafu wanataka kwenda kwao lakini naona hizi pesa wanazodai ni kusafirisha mizigo kurudi kwao. Wastaafu wengine walikuwa ndiyo wanataka wakimaliza anagalau sasa waweze kusihi maisha mazuri lakini matokeo yake sasa wanaugua, wanakuwa wanapata mateso makubwa. Naomba Serikali, wanaostaafu mwakani leo hii iwawekee kabisa unapondoka wapewe cheque zao waweze kuondoka bila ya kuwa na madai mengine yoyote. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ambalo nilikuw anataka kuchangia bado ni kuhusiana na madeni ya Madiwani; wenzangu wamezungumzia sana na mimi ni kwamna jamani Madiwani wetu waweze kulipwa yale madeni yao ya posho na stahiki zao nyingine pamoja na Watumishi hii inawapa motisha ya kufanyakazi vizuri sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kuna madeni pia ya wazabuni; wazabuni wameweza kzilisha Halmashauri zetu, wamefanya zabuni mbalimbali lakini wanakuwa wanadai muda mrefu na tunajua kwamba hawa wazabuni ndiyo wafanya biashara ndiyo tunawategemea tupate kodi zao sasa kama tukiwa-*paralysis* wakapoteza biashara zao bado tutakuwa hatujawasaidia. Mheshimiwa Rais amekuwa akisema hawa watu ndiyo wa kuwasaidia maana yake ni watu ambao tunatakiwa na wenyewe tunategemea tuwakamue yaani tuwape maziwa na tukamua, tupate kodi nyingi za kutosha. Kwa hiyo, ningeomba hili pia Serikali ingeliweka vizuri ili kusiwepo na madeni makubwa sana ya Wazabuni.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine ni uhaba wa Watumishi katika halmashauri zetu; wahasibu, walkaguzi, wakuu wa idara lakini ni muhimu sasa Halmashauri au Serikali kuna mamlaka mpya kwa mfano; *RUWASA, TARURA* wanatoa wale watalam kwenye halmashauri

zetu wanapelekwa kwenye hizo Taasisi, kwenye mamlaka lakini kwenye halmashauri sasa tunakuwa hatuna wale wataalam. Kwa hiyo, utakuta halmashauri nyingi hazifanyi vizuri hata kwenye miradi, hakuna wale wataalam. Kwa hiyo, ningeomba pengine hili lingewekwa voizuri kwamba wanapotolewa tu wataalam wowote basi mara moja Halmashauri wanaziba yale mapengo ili ziendelee kufanya vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo jingine nizungumzie kuhusu Serikali kupeleka pesa katika miradi ya kimkakati katika Halmashauri zetu; kumekuwa na tatizo kubwa la kuchelewesha hizi pesa za miradi ya kimkakati pamoja na kuwa na nia nzuri sana ya halmashauri kwamba miradi ya kimkakati isaidiwe ili iweze kusaidia mapato katika halmashauri lakini utakuta miradi imekuwa ya muda mrefu sana kwa hiyo sasa inatia tu hasara lakini tulikuwa tunategemea kwamba kama huu mradi ungepewa pesa kwa wakati ule pengine ungefanyika upembuzi yakinifu, kuna miradi mingine inahitajika pesa kidogo sana ingekuwa imeshakamilika. Kwa mfano; tuna mradi wa machinjio pale kwetu ni wamuda mrefu, mashine zimefungwa muda mrefu mpaka zinaweza zikapata kutu laklini kwa mfano mkitoa pesa tu kidogo ule mradi utaleta mapato makubwa kwenye halmashauri kwa hiyo utasaidia mapato na mambo mengi yatakwenda vizuri zaidi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kuzungumza hayo niendelee kuwapongeza Mawaziri wote waliopo TAMISEMI na wafanyakazi wote na Kamati zote ambazo zimewasilisha report zao hapa lakini na ambayo tumeyatolea ushauri basi yafanyiwekazi ili tuendelee na maboresho lakini nampongeza pia Mheshimiwa Rais kwa akzi kubwa amabyo amekuwa akiifanya katika nchi yetu na Chama cha Mapinduzi kwa utekelezaji wake wa ilani. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Joyce Sokombi atachangia dakika tano atafuatiwa na Mheshimiwa Omary Kigua, Mheshimiwa Hassan Elias Masala ajiandae.

**MHE. JOYCE B. SOKOMBI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante nami kwa kupata nafasi hii niweze kuchangia.

Mheshimiwa Naibu Spika, nipende tu kuipongeza Kamati na Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* ni Mujumbe wa *PAC*. Nitaongelea suala la *TBA* (Wakala wa Majengo Tanzania).

Mheshimiwa Naibu Spika, TBA ilipewa jukumu la ujenzi wa majengo kujenga Taasisi mbalimbali za Serikali nchini Tanzania na mkataba wenye gharama ya shilingi bilioni 24,068,482,278. Pesa hii ni ndogo sana ukilinganisha na mradi wenyewe jinsi ulivyo na kutokana na uhaba wa pesa iliyotolewa wkamba ni ndogo tunaona miradi mingi ya TBA inasuasua. Mapungufu yamekuwa mengi sana. Kutokana na hilo pia hata *bill of quantity* haikufuatwa. Kwa hiyo, kama haikufuatwa *BOQ* kumefanya gharama za mradi kutojulikana hadi sasa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya serikali kutoa bilioni 24 tunaona kabisa ni jinsi gani miradi hii inayosimamiwa na *TBA* haifanyikazi kwa ukamilifu kwa sababu unakuta msimamizi mmoja wa mradi ana miradi miwili. Aende huku akasimamie mradi, atoke huku aende akasimamie mradi huu kwa hiyo unakuta mradi huu mwingine ambao anakuwa ameuacha unakua umesimama anaporudi kwenye huu mradi mwingine na huu nao unasimama. Na pia inabidi achukue vifaa hivi anavyotumia kujengea kwenye mradi huu mwingine, mradi (a) aende akachukue tena akajengee kwenye mradi (b) kwahiyo tunakuta kuna upungugfu mkubwa sana wa ufanisi wa kumaliza miradi kwa ufasaha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa mfano; jengo la Makao Makuu ya Tume hapa Dodoma, *TBA* ilikuwa inafanyakazi pale kujenga lile jengo matokeo yake wameshindwa na baada ya kuona kwamba lile jengo halitaisha kwa wakati ikabidi sasa wachukuliwe SUMA JKT kwenda

kumalizia ule mradi pale na hadi sasa SUMA JKT ndiyo bado inaendelea kujenga ule mradi ambao ulikuwa unasimamiwa na *TBA.(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nitaenda pia upande wa *NHC;* upande wa *NHC* miradi mingi nayo imetelekezwa yaani haieleweki kwamba hii miradi itakwisha au laa! Mfano; mradi ule wa Kawe 711; ule mradi una thamani ya shilingi bilioni 142. Bilioni 142 ni pesa nyingi sana lakini cha ajabu mradi unatelekezwa. Pesa ambayo imetolewa haijafanyakazi yoyote. Kwa kweli inakuwa ni kitu ambacho kinailetea hasara Serikali yetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ukaguzi wa *CAG* ulibaini pia ongezeko la gharama la shilingi bilioni 6.86 pesa ambayo haikutolewa maelezo yoyote hadi leo hii. Tunaomba tuelezwe kinagaubaga pia tuelewe kama Kamati hii bilioni 6.86 imetoka wapi na kwa sababu haikutolewa maelezo yoyote kwa hiyo hatujui mpaka sasa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauri wangu kwa Serikali ni kwamba; iwe inatoa pesa kwa wakati. Itakapokuwa inatoa pesa kwa wakati, majengo yale yatakamilika kwa wakati na *value for money* itaonekana.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante na nashukuru kwa kupata nafasi hii. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Nilikuwa nimeshamuita Mheshimiwa Omary Kigua, Mheshimiwa Omary Kigua atachangia kwa dakika 15 atafuatiwa na Mheshimiwa Hassan Elias Masala, Mheshimiwa Mary Chatanda ajiandae.

**MHE. OMARY M. KIGUA:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante kwa kunipa nafasi ili niweze kuchangia taarifa ya Kamati ya *PAC*.

Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote kama Mjumbe wa Kamati ya *PAC* ambayo kwa takribani kwa miaka minne nimekuwa kwenye Kamati hii. ni lazima niseme wazi kabisa kwamba mabadiliko makubwa yapo katika uandaaji wa hesabu na hoja nyingi zimepungua.

Mheshimiwa Naibu Spika, na yasema hayo kwa sababu ukipitia hesabu za Serikali Kuu, Mashirika ya umma. Pale mwanzoni kulikuwa na hoja za ukaguzi nyingi sana. Sasa ukiangalia kwa taarifa hii tunayopitia hapa tunazungumzia taarifa ya Mwaka 2017/2018 na msingi wa taarifa hii ni taarifa ambayo inaandaliwa na Kamati ikishirikisha wataalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nilikuwa namsikia mzungumzaji mmoja hapa anaanza kuhoji kwamba jambo fulani halipo, jambo fulani halipo. Msingi wa Kamati ni kwamba ni maoni ya washiriki wote na ukitaka kuona hilo limefanyika ni kwamba hata Mwenyekiti ambaye anatoka upande mwingine ndiye ambaye ameongoza vikao hivyo. Kwa hiyo, nataka kutoa wasiwasi kwamba haya ambayo yameingia kwenye taarifa hii ya Kamati ya *PAC* ni maoni ya Kamati ya *PAC* na wala siyo maoni ya mtu mmoja kwa sababu msingi wa hoja za Kamati ni hoja za *CAG* na kama *CAG* ameleta hoja anaitwa *accounting officer* au Katibu Mkuu, anapoleta majibu lazima yapelekwe kwa *CAG* ayaptie apate majibu sasa inawezekana haya unayoyauliza sasa hivi ni miongoni mwa mambo ambayo yanafanyiwa kazi na *CAG* ili yarudi tena katika Kamati. Hilo nilitaka kuliweka sawa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo lingependa kulzingumzia ni juu ya mambo mbalimbali ambayo Kamati yetu imeiona na ambayo kwa kiasi kikubwa Kamati ya *PAC* imetoa maoni yake.

Mheshimiwa Naibu Spika, nataka nijikite eneo ambalo ni eneo muhimu sana kwenye Ofisi za Mamlaka ya Mapato *(TRA);* tumegundua changamoto nyingi sana, Kamati imegundua

changamoto nyingi sana sasa hizi kwa kiasi fulani zinaonekana ni changamoto ambazo inaonekana kwamba Serikali haijakusanya mapato kwa kiasi kikubwa sana lakini ukitazama hoja za *CAG* utaona kwamba kile kinachoonekana katika hesabu za Mamlaka ya Mapato *(TRA)* ni mambo ambayo yemafanyika kitaalam ambayo pengine yamefanyika kwa makusudi au yemefanywa na watu ambao hawana utaalam.

Mheshimiwa Naibu Spika, nitoe mfano mmoja, ni juu ya kodi la zuio *(withholding tax);* utaona kwamba maeneo mengi inaonekana mapato hayajakusanywa kwenye eneo hilo. Lakini pia yapo maeneo mbalimbali ambayo mamlaka ya mapato yanaonekana hayajafanya vizuri. Mfano, kuna kesi takribani 417 ambazo zilipaswa ziwe tayari zimetolewa maamuzi hazijafanyika mpaka sasa hivi.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa nini ushauri wangu? Najua Ofisi ya Mamlaka ya Mapato *(TRA)* wanafanyakazi nzuri sana kupitia kwa Kamishina wa *TRA* na watu lakini naona sasa umefika umuhimu sasa wa kuhakikisha kwamba hoja hizi ambazo zinaonekana Serikali haijakusanya mapato wakati hakuna uhalisia wa mapato basi ziweze kutafutiwa majibu na namna gani wanaweza wakafika hapo ni kuhakikisha kwamba wanakuwa na wataalam wa kutosha ambao wanafanya *assessment* ya kodi.

Mheshimiwa Naibu Spika, leo hii unaweza ukamkadiria mtu kwamba kwa mwaka anaweza kukusanya milioni 800 kumbe pato lake ni milioni 200. Hesabu zile zitaingia kwenye Ofisi ya Mamlaka ya Mapato *CAG* akipitia ataona kwamba *TRA* hawajakusanya mapato kumbe ni makadirio mabaya ambayo yamefanyika. Mimi nimuombe Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha yuko hapa alione hilo wakae na watu wa *TRA* waone namna ambavyo ukadiriaji ufanywe na watu sahihi kwa wakati sahihi na watu ambao wana taaluma ya kutosha vinginevyo itaoneonekana siku zote kwamba hesabu hizi haziko sawa, Serikali haijakusanya mapato kumbe siyo mapato sahihi hata kidogo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningepanda kulitolea maelezo au kulichangia ni hija ambayo imeonekana kwamba watu wa mfuko wa Bima walitoa pesa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali ya Benjamin. Sasa ukiangalia hapa utaona kwamba hapa hakuna hoja ya matumizi mabaya ila no hoja ya kuweka hesabu vizuri kwa maana kwamba hesabu za watu wa *National health Insurance* hazionyeshi kwamba wamewekeza kiasi hicho kwa ajili ya ujenzi wa hospitali.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni jukumu la Serikali sasa hivi kuangalia watu wa *National Health Insurance* wakae na watu wa Wizara ya Elimu kupitia Benjamin pale kuona kwamba hesabu hizi, uwekezaji huu wa *National health Insurance* utaweza kuwekwa kwenyte vitabu kiasi gani. hilo ndilo ambalo linesemekana ndiyo maana hoja ya *CAG* imeonyesha kwamba uwekezaji ule hauonekani kwenye vitabu vya wenzetu wa *National Insurance* kwa sababu wanaonekana mfuko wa Bima ya afya wao mfuko ule hauendi vizuri lakini kama hesabu hizi, kama uwekezaji huu wa ujenzi wa hospitali ya Benjamin ungeweza kuonekana katika hesabu zao pengine wangeonekana wanafanya vizuri sana. Naomba wahusika walisikie hili na waweze kulifanyia kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kuchangia ni juu ya Shirika letu ya Nyumba; sisi Wajumbe wa Kamati ya *PAC* tulifanya ziara kutembelea miradi mbalimbali. Tulipata fursa ya kwenda pale Morocco kuangalia ujenzi wa majengo makubwa lakini tulienda Kawe. Sasa kinachoonekana pale ni kwamba watu wa *National Housing* miradi ile imesimama. Mkandarasi yupo pale *site* na kila siku analipwa takribani milioni 20, uwekezaji ule umesimama lakini unajiuliza kwanini umesimama? Ndiyo tunaamini na Kamati inaamini kabisa kwamba uwekezaji ule haukuwa mzuri, sasa nii kifanyike?

Mheshimiwa Naibu Spika, ushauari wangu kama Mbunge; kwa sababu ukiangalia kama Serikali itasitisha miradi ile maana yake yule Mkandarasi tutamlipa bilioni 99.99 ni takribani bilioni 100 lakini tayari watu wa Shirika na Nyumba wameshapokea kodi ya bilioni 2.6 sasa nini kifanyike hapa? Waziri wa Ardhi yupo hapa ambae Shirika la Nyumba liko chini yake; hebu wakae chini waangalie namna gani wanaweza kutoka kwa sababu kuendelea kutokuendeleza ile miradi maana yake ni kuipelekea Serikali kupata hasara. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nashauri sana tuangalie waliofanya makosa hawapo sasa hivi, menejimenti iliyopo ni mpya sasa tuangalie kwamba Serikali isiendelee kupata hasara. Miradi ile iko pazuri ukichukulia mfano mradi wa Kawe uko karibia na bahari pale kwa maana tukimalizia majengo pale Serikali inaweza ikapata kiasi kikubwa sana cha pesa na ukianglia unapofanya *investment* lazima *return* yake ile ionekane. Sasa pesa ile tumeiweka chini tunatarajia nini maana Mkandarasi yule hawezi kuondoka, ukiondoka maana yake utalipa bilioni 100. Hebu tuangalie namba ya kutafuta pesa miradi ile tuyikwamue itoke hapo ilipo iende mbele zaidi.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini lingine ambalo ningependa kulizungumzia ni juu ya Bodi hizi za kusuluhisha kwa sbabau mwaka jana hapa tulipitisha Sheria kwamba tunaanzisha kitengo pale Wizara ya Fedha kwamba kama umekadiriwa vibaya basi unahakikisha unapeleka malalamiko yako Wizara ya Fedha pale. Ninaushauri mmoja; kuna Bodi hizi ambazo ndizo zinazotatua kesi, naona Bodi hizi hazifanyikazi sawasawa na ndiyo maana bado kuna kesi nyingi sana zinazohusu ukadiriwaji wa mapato. Namuomba Waziri wa Fedha aliangalie hili pengine kama hawana wataalam wa kutosha ili kesi ziendelee na hoja hizi ambazo zimekwama ziweze kuondoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, lingine ambalo ningependa kuchangia ni juu ya Kamati ya *LAAC;* yupo Mheshimiwa mmoja amezungumza hapa kwamba mfumo wa *Force account* ni mfumo ambao una tija. Ni kweli una tija kwa sababu kwa kiasi kikubwa umeweza kuokoa fedha lakini kitu ambacho nimekiona na ambacho hata halmashauri yangu ya Wilaya ya Kilindi inacho ni kwamba hatuna wataalam, hatuna Mainjinia wa *Civil engineering* ambao ndiyo wasimamizi wakuu wa miradi hii. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ni kwamba kama hatuna wataalam, imefika wakati Waziri wa TAMISEMI yupo hapa naomba anisikilize; hakikisha unapeleka wataalam, fundisha wataalam, wapeleke katika halmashauri. Miradi hii lazima iwe na wataalam wa kusimamia vinginevyo thamani ya pesa haitapatikana hata kidogo. Tutasimama hapa, tutasema *Force account* ni nzuri lakini bila wasimamizi wenye taaluma ya kutosha hatuwezi kufika mbele na wala hatuwezi kufanikiwa. Naomba Serikali ione kwamba ni eneo lenye changamoto kubwa sana ambalo lazima lifanyiwe kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, eneo lingine ambalo ningependa kulizungumzia, Waheshimiwa Wabunge wamezungumzia juu ya *TBA*, mimi ushauri wangu kama Mbunge, naamini kabisa *TBA* wamefanya kazi nzuri lakini walikuwa wameelemewa na mzigo, nadhani kama Serikali inaweza ikachukua njia iliyo sahihi, wachukue miradi hii ya ujenzi wawapelekee watu wa *National Housing* waweze kufanya kazi hizo kwa sababu wao wameonekana baadhi ya miradi wanafanya kazi vizuri sana, vinginevyo tutapelekea kuwalaumu, tutawalaumu lakini kumbe wamezidiwa. *TBA* wamezidiwa kwa sababu walipewa kazi nyingi sana na hili linaonesha wazi kwamba wakiendelea kutopewa kazi hizi basi watafeli hawataweza kufanikiwa kwa sababu Kamati yetu sisi imepitia miradi mingi ikaona kwamba *TBA* wameshindwa kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, mwisho, naomba kurudia kusema tena kwamba tulipoanza na tulipo ndio ni vitu viwili tofauti, Serikali inakusanya mapato ya kutosha, *TRA* wanafanya kazi vizuri,

lakini waangalie mapengo, waangalie namna ya kuimarisha utendaji wa *TRA* hususani kwa wataalam wanaofanya makadirio kwa sababu malalamiko ni mengi sana ili tuweze kutengeneza hesabu ambazo ni hesabu sahihi.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema hayo, naunga mkono hoja. Ahsante. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Hassan Elias Masala, atafuatiwa na Mheshimiwa Mary Chatanda na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo ajiandae.

Haya Mheshimiwa Mary Chatanda, atafuatiwa na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo na Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI ajiandae.

**MHE. MARY P. CHATANDA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru kwa kunipa nafasi ya kuweza kuchangia katika taarifa iliyowasilishwa ya *LAAC* pamoja na *PAC* kwanza naziunga mkono. Nampongeza Mheshimiwa Waziri wa TAMISEMI kwa namna alivyofanya kazi ya kuboresha na kuzisambaza *PoS* za kukusanyia mapato ambayo *PoS* hizi zinaweza kuzisaidia sana Halmashauri zetu kudhibiti wizi wa mapato katika halmashauri zetu, amefanya kazi kubwa tunamshukuru sana na tunakusudia sasa kuona kwamba kwenye halmashauri zetu mapato yataongezeka kutokana na vitendea kazi ambavyo vimepatikana. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yapo mambo mengi ambayo tumeyazungumza na wenzangu wameshayazungumza katika Kamati yetu ni pamoja na suala zima la ajira za watumishi. Tumejenga vituo vya afya, tunajenga zahanati, lakini kumekuwa na upungufu mkubwa wa watumishi katika vituo hivyo vya afya na zahanati. Jambo ni jema sana na tunaishukuru sana Serikali kwa kazi kubwa ambayo imeifanya kwa ajili ya kujenga hizo hospitali tunazojenga, tunajenga hivi vituo vya afya, tunajenga hizi zahanati lakini sasa tuna uhitaji mkubwa watumishi katika maeneo hayo. Kwa hiyo tuiombe sana Serikali angalau basi waweze sasa kutoa ajira ili kusudi hospitali hizi na zahanati hizi ziweze kufanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, yako mambo mengi ambayo yamezungumzwa ni pamoja na suala zima la kutumia hii *force account,* ni jambo jema sana na linaisaidia sana Serikali katika kubana matumizi ya ujenzi wa vyumba vya madarasa, vituo vya afya na hospitali zetu na mambo mengi ya maendeleo. Hata hivyo, kama walivyosema wenzangu kwamba tunahitaji sasa Wahandisi katika halmashauri zetu maana Wahandisi waliokuwepo wakati huo wote wamechukuliwa, wako asilimia kubwa wamekwenda sasa *TANROADS,* wamekwenda *TARURA.* Sasa mara nyingine wanaenda kuwachukua *TARURA* au kuwaomba waje kuwasaidia kazi, inakuwa ni kazi kubwa sana katika kusimamia hii miradi ambayo tunatumia *force account.* Mradi wenyewe wa *force account* ni mzuri lakini tunahitaji watendaji angalau wale watakaokuwa wapo muda wote kuhakikisha kwamba wanasimamia hii miradi katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo nataka nilizungumzie ni suala la watumishi. Tumegundua kwamba watumishi wanapandishwa madaraja lakini wanapopandishwa madaraja hawaendi sambamba na maslahi yao. Wakishapandishwa tu basi mtu anaweza akakaa mwaka mzima, miaka miwili haongezewi yale maslahi ambayo yanahusiana na kule kupandishwa kwake daraja. Kwa hiyo, naiomba sana Serikali, ili kuwapa motisha wafanyakazi hawa anapopandishwa basi aende sasa na maslahi yake kwa nafasi ile ambayo amepandishwa nayo daraja. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu mengi yamezungumzwa nilikuwa nafikiri ni vizuri nikasema haya machache kwa sababu wenzangu wengi waliotangulia ambao tuko kwenye Kamati hii ya *LAAC* wamekwishayasema, hivyo nishukuru na niendelee kuipongeza sana Serikali

kwa juhudi kubwa ambazo wameendelea kuzifanya katika kuyaletea maendeleo nchi yetu. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Sikudhani Chikambo, atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Nchi Ofisi ya Rais, TAMISEMI na Mheshimiwa Waziri wa Madini ajiandae.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana. Awali ya yote napenda nimshukuru Mwenyezi Mungu aliyenijalia tena kusimama tena katika Bunge lako hili Tukufu, naamini hili ni Bunge la pili kutoka mwisho, lakini namwomba Mwenyezi Mungu anijalie ili nirudi tena katika Bunge lijalo. Pia nawaombea na Waheshimiwa Wabunge wenzangu warudi tena maana si vizuri kujiombea mwenyewe peke yangu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nipongeze taarifa ambazo zimewasilishwa siku ya leo, lakini naomba pia nipongeze michango mizuri ambayo imezungumzwa na Waheshimiwa Wabunge wenzangu na hasa Wajumbe wa Kamati ambao wamekuwa wakifanya kazi kwa karibu na hizi Wizara ambazo zimewasilisha leo taarifa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ninayo mambo machache ambayo naomba pia niseme, niweke nyongeza katika maeneo ambayo wenzangu wameyazungumza. Naomba nizungumzie suala la utekelezaji wa miradi ya maendeleo katika halmashauri zetu. Nafahamu kwamba Serikali inapeleka pesa katika halmashauri zetu kwa ajili ya kutekeleza miradi mbalimbali kupitia *force account,* hiyo ni hatua nzuri na kwa kweli naomba niipongeze Serikali kwamba ilikuwa na lengo zuri sana kupitia *force account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nisisitize suala la uhakiki wa miradi, tunaenda tunatekeleza hii miradi, lakini wakati mwingine pengine miradi inatekeleza kwa haraka sana inakuwa inakosa ubora. Unaweza ukakuta jengo limekabidhiwa kwamba limekamilika, lakini baada ya mwezi mmoja ukienda kuhakiki unakuta tayari lina ufa. Sasa kwa namna nyingine inaonekana kama pesa yetu imekwenda lakini haijafanya kazi kadri inavyokusudiwa. Kwa hiyo naomba sana nisisitize uhakiki wa miradi ambayo inatekelezwa katika halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, naendelea kusisitiza kwamba mfumo huu ni mfumo mzuri kupitia *force account* lakini tuwe imara katika kuhakikisha miradi hii inayojengwa, basi hiyo ni miradi yenye ubora. Kama jengo linajengwa basi liwe jengo bora, kama ni kituo cha afya, kama ni madaraja na miradi mingine yote ambayo inatekelezwa katika halmashauri zetu iwe na ubora unaohitajika.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine naomba nizungumze suala la vyanzo vya mapato. Katika halmashauri zetu sasa ni kama vyanzo vinaenda kwa kusuasua, naomba niseme kwamba Serikali ilikuwa na dhamira nzuri sana ya kufuta vyanzo vya mapato ambavyo vilikuwa vinakusanywa na halmashauri na kuleta kwenye Serikali Kuu, lakini kwa lengo la kurudisha pesa kwenye halmashauri ili ziendelee kufanya kazi ilivyokusudiwa. Naomba niseme na jambo hili nimekuwa nikisema lakini hata Waheshimiwa Wabunge wenzangu wamelisema, kwamba pesa haziendi kwa wakati. Kutopeleka pesa kwa wakati ni kuifanya ile miradi isikamilike na tunapochelewa kupeleka pesa miradi ile inaongezeka gharama za uendeshaji. Kwa hiyo, naomba sana kupitia Bunge lako hili, ni vizuri tupeleke pesa kwa wakati ili halmashauri ifanye kazi iliyokusudiwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sambamba na hilo kuna suala la miradi viporo, kwenye halmashauri zetu tuna majengo mengi, majengo mengine nguvu za wananchi wanakuwa wamefyatua tofali kwa lengo la kuanzisha miradi na wakati mwingine ni maagizo ya Serikali kwamba lazima mradi unapokwenda kuwepo na nguvu za wananchi. Hivyo wananchi wanafyatua tofali kwa maana ya nguvu zao, maeneo mengine wanakusanya mawe,

wanapeleka mchanga, lakini kukiwa kuna jengo limejengwa jengo halikamiliki kwa ajili ya kukosa pesa ambapo ndio mchango wa Serikali kwenye lile jengo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niombe sana kupitia Serikali tuhakiki miradi yetu viporo, vinginevyo unaweza ukakuta majengo mengi saa hizi badala ya kufanya kazi iliyokusudiwa wanakaa popo au mengine wanalala mbuzi na mengine yanafanyika mambo ambayo hayakukusudiwa. Kwa hiyo naomba sana niisisitize Serikali yangu na sina shaka kwa kweli na Serikali yangu naamini ni Serikali sikivu, isikie iufanye uhakiki, vile ambavyo tunahakiki watumishi hewa, turudi sasa tuhakiki hata miradi viporo ili tupeleke pesa ile miradi ikamilike. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo naomba nilizungumze, ni suala la posho za Madiwani, wenzangu wamesema na mimi nafahamu ukiachia kwamba ukiwa Mbunge pia ni Diwani, lakini mimi pia nimekuwa Diwani toka huko nyuma, sasa nafahamu mazingira ambayo wanaishi Madiwani wetu kwenye halmashauri. Hili jambo limesemwa sana na linaposemwa sana na Waheshimiwa Wabunge wengi inaonesha kwamba jambo hili ni la halmashauri zote, Madiwani wetu hali zao sio nzuri, posho zenyewe hawapati kwa wakati, lakini mwingine amesema, Diwani anaweza akaenda amefanya kikao anapomaliza kikao hakuna anachosaini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, wakati naanza kujiombea hapa ili nishinde tena niliwaombea na wenzangu, lakini hata wale Madiwani kule pia tunawaombea, sisi hapa tumejaza, tukishajaza *per diem,* ukijaza Jumatatu *per diem* mpaka siku ya pili ya tatu hujaona mnaanza kuulizana, hapa nilikuwa nateta na jirani yangu vipi kuhusu utaratibu na naamini jambo hili ni kwa wote tunaulizana. Sasa vile tuone nafsi, lile ambalo sisi tunaliona sio jambo jema hata wenzetu kule haliwapendezi. Kwa hiyo, tuhakikishe Madiwani wetu wanapata pesa zao kwa wakati, wanadai na inaonekana wengine mpaka tutamaliza Mabaraza hata haki yao hawataipata. Sasa jukumu la kuhakikisha wanapata haki zao ni sisi tuliomo humu ndani, tuhakikishe wale wanapata haki zao kama vile ambavyo sisi leo tunaanza kuuliza utaratibu utakuwaje na ndio maana nimesema hili ni Bunge la pili kutoka mwisho, kwa hiyo…

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani Chikambo kuna taarifa Mheshimiwa John Heche.

**T A A R I F A**

**MHE. JOHN W. HECHE:** Mheshimiwa Naibu Spika, nampa taarifa kwamba ni kweli kwamba Madiwani hawana pesa na hawalipwi, lakini kuna baadhi ya Ma-*DC* wanaona kwamba Madiwani wakilipwa ni *fever* na sio haki yao, mfano mzuri ni *DC* wa Gairo anaona kwamba Madiwani wakilipwa sio haki yao na wanafanya kazi. Kwa hiyo anachozungumza ni sahihi Madiwani wanahitaji kulipwa pesa zao.*(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Sikudhani unapokea taarifa hiyo.

**MHE. SIKUDHANI Y. CHIKAMBO:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba niendelee kuchangia. Kama nilivyosisitiza upande wa Madiwani, lakini pia tunapozungumza halmashauri tunaanzia ngazi ya kijiji hata Wenyeviti wetu wa Vitongoji, Wenyeviti wa Vijiji tumekuwa tukiyazungumza sana. Hii miradi tunayoizungumza hapa inaenda kutekelezwa kwenye vijiji, lakini unamkuta Mwenyekiti wa Kijiji, Mwenyekiti wa Kitongoji hapati chochote, hawezi kufanya kazi kwa sababu hakuna motisha yoyote. Kwa hiyo, niombe sana tunapowafikiria Madiwani lakini pia hata viongozi wetu wa ngazi zile ambazo ndiko tunakoenda kufanya kazi ni lazima tuwafikirie.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimeona niyaseme hayo, lakini kwenye suala hili la posho nimalizie kwenye matatizo ambayo yanajitokeza kwenye halmashauri. Tunafahamu kwamba miradi yote ambayo tunapeleka kwenye halmashauri wahakiki wa miradi ni Kamati ya Fedha, ndio inatakiwa ikahakiki miradi kwa niaba ya Baraza zima, lakini inasikitisha Kamati ya Fedha mnaweza mkakaa hata miezi mitatu haijaenda kwenda kuhakiki miradi, sasa nani atajua ubora, nani ataleta changamoto kwenye halmashauri, hiyo inaleta tabu. Wakati mwingine inaonekana halmashauri zingine wanapeleka Madiwani au Kamati ya Fedha kwenda kuhakiki ni kama funika kombe mwanaharamu apite, kuna utaratibu wa kutaka ile Kamati ikahakiki, lakini unaiambia Kamati ya Fedha iende ikahakiki siku moja, hivi kweli itapitia miradi yote ikamaliza. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niiombe Wizara itoe tamko kwa ngazi ya halmashauri, ni vizuri kama haya mambo yako kwa mujibu wa Katiba au kwa mujibu wa sharia, basi tuagize halmashauri wahakikishe wanatekeleza kwa mujibu wa utaratibu kwa sababu kupeleka pesa ni hatua nyingine, lakini pia hata kuhakiki ubora wa miradi yetu ni jambo lingine. Nimeona niliseme sana kwa sababu mimi ni sehemu ya Madiwani, naona madhara yanayojitokeza kwenye halmashauri zetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, jambo lingine ambalo hata wenzangu wamelizungumza ni suala la *TARURA*. Naomba niipongeze Serikali wazo lilikuwa zuri la kuweka *TARURA*, inawezekana kukawa na wazo zuri lakini katika utekelezaji tukabaini changamoto. Mimi binafsi changamoto mojawapo ambayo naiona ni watu wa *TARURA* kutokuwa sehemu ya halmashauri, wanaenda kwenye halmashauri pale wanapoalikwa, si kama vile ilivyokuwa nyuma, kwa sababu mimi kama Diwani kuna shida mradi unategemea ninavyokwenda kwenye Baraza la Madiwani ndipo ambapo nitaenda kusema kulingana na barabara yangu, kulingana na zahanati yangu lakini ukija kwenye masuala ya barabara wale watu wa *TARURA* sio sehemu ya halmashauri.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa naomba sana Serikali yangu narudia kusema ni Serikali tukufu na Serikali sikivu ni vizuri sasa ione uwezekano watu wa *TARURA* wawe sehemu ya Wakuu wa Idara katika halmashauri zetu ili wa-*report* taarifa zao.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa kunipa nafasi. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI atafuatiwa na Mheshimiwa Waziri wa Madini na Mheshimiwa Waziri wa Fedha ajiandae.

**WAZIRI WA NCHI, OFISI YA RAIS, TAWALA ZA MIKOA NA SERIKALI ZA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, awali ya yote naomba niwapongeze Wenyeviti wa Kamati zote mbili pamoja na Wajumbe wa Kamati, hakika wamefanya kazi kubwa. Mimi nikiwa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, TAMISEMI, kwa hakika naomba niipongeze Kamati ya *LAAC* ambayo binafsi nasema Wajumbe wa Kamati ya *LAAC* wamesaidia sana ofisi yangu kufanya kazi vizuri. Ushauri wote uliotolewa kwa kipindi chote umeendelea kuimarisha utendaji wa ofisi yangu lakini na Mamlaka za Serikali za Mitaa. Tunajua kwamba hatuwezi kuwa *correct a hundred percent* katika muda mfupi, lakini tumejitahidi kwa kadri iwezekanavyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna hoja mbalimbali zilijitokeza hasa katika upande wa suala zima la ukusanyaji wa mapato. Tukumbuke kwamba ukichukua historia tulikotoka nyuma hali ilikuwa mbaya sana na Kamati ya *LAAC* na Wajumbe huko tulikotoka hali yetu ya mwanzo ilikuwaje. Hata ukifanya *reflection* ya muda mfupi uliopita wa miaka michache *collection* yetu ilikuwa haifiki hata 80% kwa mwaka. Katika bajeti ya mwaka wa fedha wa 2017/2018, tulifikia 81%. Katika mwaka wa fedha wa 2018/2019, tumefikia 90% na haya yote ni mafanikio makubwa katika ukusanyaji wa mapato. Hata hivyo, ushauri wa Kamati ya *LAAC* na Wajumbe kwa ujumla

wake umesaidia, ndio maana katika utekelezaji huo ofisi yangu mwaka huu iliamua kununua *PoS* takribani 7,227 ambazo tumezigawa katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa.

Mheshimiwa Naibu Spika, tumefanya hivi kwa sababu halmashauri zingine uwezo wake ni mdogo wa kuweza kununua hizi *PoS,* kwa hiyo nishukuru sisi kama TAMISEMI tutaendelea kutekeleza maagizo yote yanayotolewa kwa lengo kubwa la kuboresha utendaji wa kazi wa Serikali na nia yetu ni kuhakikisha kwamba kazi zinafanyika vizuri katika Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Hakika sasa hivi ukiipima Mamlaka ya Serikali za Mitaa ukusanyaji wa mapato umeongezeka na tutaendelea kuhakikisha kwamba ule upungufu wote uliojitokeza kama tulivyonunua *PoS* na kuweza kuzigawanya katika halmashauri. Pia tunaenda kuzisimamia kwa kuwa hali ya ukusanyaji wa mapato ilikuwa inasuasua, ili sasa tuweze kuliondoa tatizo hilo kwa kiwango kikubwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, katika eneo lingine ni suala zima la matumizi ya *force account*. Niseme kwamba tulikotoka huko na sasa ni vitu viwili kidogo tofauti, japokuwa inawezekana kuna upungufu wa hapa na pale, lakini matumizi ya *force account* yamesaidia sana. Majengo yale tuliyokuwa tunajenga kwa wastani wa shilingi bilioni mbili leo hii kujenga kati ya shilingi milioni 400 mpaka milioni 500, ni mafanikio makubwa na katika hili niwapongeze Waheshimiwa Wabunge wote kwa sababu miradi hii haikujengwa hewani imejengwa katika halmashauri zetu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikiwa na timu yangu ya akina Mheshimiwa Waitara tulivyotembelea maeneo mbalimbali, miradi mingi kwa kweli kwa sababu kulikuwa na *specification* hata za ununuaji wa *materials,* bati iwe ya *gauge* namba ngapi, tofali, mfuko mmoja utoe tofali ngapi, kwa kweli kwa kiwango kikubwa pale wananchi na viongozi nyie mmefanya kazi kubwa ya utekelezaji wa hii miradi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hatuwezi kubeza hata kidogo mafanikio yaliyopatikana katika matumizi ya *force account*, kwa mfano unaenda mpaka kule ndani kabisa Nyasa utakuta hospitali ya Wilaya imejengwa nzuri kwa *quality,* lazima tuone kwamba tuna kila sababu ya kujisifu kwa matumizi ya *force account*. Hata hivyo, niishukuru sana Kamati ya *PAC* pamoja na Kamati ya *LAAC,* wote walipata fursa ya kutembelea miradi ya afya katika maeneo mbalimbali. Walijionea hali nzuri, japokuwa kunaonekana kuna upungufu wa hapa na pale na kazi ya Serikali yetu ni kuhakikisha kwamba pale kwenye upungufu tunaenda kuuboresha lakini kwa kiwango kikubwa matumizi ya *force account* yamesaidia sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, niwaombe sana Waheshimiwa Wabunge na Kamati za Fedha, tuhakikishe kwa pamoja licha ya kuwepo wataalam watakuwepo kule lakini sisi tuna jukumu kubwa sana kuhakikisha hii miradi tunaisimamia kwa karibu kwa kupitia Madiwani wetu kwa lengo kwamba tupate miradi iliyokuwa mizuri na naamini miradi mingi tumepata mafanikio makubwa sana kwa kutumia *force account*.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja kwamba Jiji la Dodoma halina barabara kabisa. Mimi nilikuwepo katika Bunge la Kumi na sasa hivi ni Bunge la Kumi na Moja. Nishukuru kwa hoja ya mama yangu inatusaidia kuhakikisha kwamba tuweze kuongeza juhudi ya ujenzi wa miundombinu ya barabara. Naomba niwahakikishie kwamba Dodoma katika Miji ukifanya ulinganifu miaka mitano iliyopita na hali ya sasa ni tofauti sana, tunajitahidi kujenga miundombinu katika Jiji la Dodoma na hivi sasa tumekamilisha zaidi ya kilometa 168 ndani ya mtandao wa barabara za lami katika Jiji la Dodoma. Haya ni mafanikio makubwa sana ukilinganisha na maeneo mengine. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hata hivyo, sasa hivi tumeweka vifaa, tumeshasaini kandarasi ya ujenzi wa kilometa takribani 51 kwa ajili ya kujenga miundombinu ya lami. Leo hii watu wa

llazo, watu wa Kikuyu na watu wa maeneo mbalimbali mnafahamu maeneo mliyokuwa mnaishi mwanzo hali ilikuwa mbaya, hali ya mwanzo sio hali ya sasa lakini ushauri unachukuliwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, lengo letu kubwa yale mapungufu mengine lazima tutayafanyia kazi kwa sababu, hapa ndio makao makuu ya nchi yetu, lazima tuhakikishe tuna *speed,* tunaongeza juhudi kuhakikisha Jiji la Dodoma linakuwa vizuri. Lakini hata hivyo niwahakikishie Jiji la Dodoma litakuwa ni jiji la pekee lenye miundombinu ya barabara za lami ukilinganisha na maeneo mengine hivi sasa kwa kadiri tunavyokwenda. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, *agenda* nyingine, kulikuwa na hoja, vituo vya afya vipo, lakini vifo vimeongezeka. Wajumbe naomba niwahakikishie, kwa sasa kwa takwimu zetu na wenzetu, Dada yangu hapa Mheshimiwa Ummy Mwalimu, Wizara ya Afya. Kwa kweli vituo hivi vimesaidia sana kwa kiwango kikubwa, isipokuwa tutaendelea kufanya juhudi kubwa kuviboresha vituo hivi kwa juhudi ya Serikali tuliyofanya kwa ujenzi wa vituo vya afya.

Mheshimiwa Naibu Spika, hali kadhalika kuhakikisha vyote vyenye mapungufu hasa ya vifaa tiba na kupeleka wataalam ndio maana hata sasa hivi ninapozungumza kuna watu wengine tayari tunawaajiri kipindi hiki kuhakikisha tunaongeza *human resource* kule katika maeneo yetu vituo hivi viweze kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, ushauri wa wajumbe niseme tunaupokea, lakini hata hivyo Serikali imeshafanya juhudi kubwa na inaendelea kufanya. Lengo letu ni wananchi waendelee kupata huduma nzuri katika maeneo mbalimbali.

Mheshimiwa Naibu Spika, kulikuwa na hoja suala zima la mfuko ule wa asilimia 10 ya vijana, akinamama pamoja na walemavu, huko tulikotoka hali ilikuwa mbaya na niishukuru sana Kamati ya *LAAC* ilipendekeza tufute yale madeni ya nyuma na kweli tulifuta. Na hata hivyo, naomba niwahakikishie kwamba sasa hivi kwa mujibu wa kanuni fedha hizi zinatoka vizuri sana. Kwa mara ya kwanza niliposoma ripoti yangu mwezi Septemba, 2019 zaidi ya shilingi bilioni 47 zilipekekwa katika vikundi hivi ambayo haijawahi kutokea ukilinganisha na miaka yote. Imani yetu ni kwamba, zile halmashauri zenye kulegalega na baadhi ya mapungufu mengine tutaenda kuyafanyia kazi kwa makundi haya yaweze kupata fursa vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini hata hivyo, tunashukuru kwa maoni mazuri ya wadau na Wabunge pale wanapotoa maoni, inawezekana kwa mujibu wa kanuni zetu uboreshaje utakuwaje. Tutaendelea kuboresha kanuni ili mradi mifuko hii iweze kufanya vizuri.

Mheshimiwa Naibu Spika, agenda ya madai ya Madiwani, wajumbe wa Kamati ya *LAAC* na Kamati ya TAMISEMI ni mashahidi, juzi nilivyokuwa natoa zile mashine za *electronic* nilitoa maagizo kwa halmashauri zote zenye madeni wakurugenzi walipe hayo madeni kabla ya Baraza la Madiwani halijavunjwa. Na hata jana nilipokuwa nikizindua Jengo la *ALAT* nikatoa agizo tena halmashauri zote, wakurugenzi wote wahakikishe madeni ya madiwani wanayodaiwa katika mabenki mbalimbali yaweze kulipwa. Na nimemuagiza Katibu Mkuu wangu TAMISEMI afanye mawasiliano kuona ni akina nani ambao ni changamoto kubwa na jana nilitoa mfano mmojawapo, halmashauri hiyo ni Halmashauri ya Gairo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, niwaambie jukumu letu kubwa TAMISEMI tutaendelea kusimamia maeneo haya yote kuhakikisha Wananchi, hasa Madiwani wetu ambao wamefanya kazi kubwa na nzuri zaidi hakikisha siku ile ya kupata kiinua mgongo chao wasipate mashaka kwamba, fedha zao zinakatwa kwa ajili ya kupelekwa katika maeneo ya mabenki.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini agenda ya ujenzi wa masoko, tumelipokea hili, lakini hata hivyo masoko yote tunayojenga hivi sasa tumetoa maelekezo wale wafanyabiashara wa mwanzo wote, hivi sasa nina orodha katika ofisi yangu kuanzia Soko lile la Kisutu, Soko la magomeni, Soko la Morogoro na masoko yote.

Mheshimiwa Naibu Spika, nimesema wafanyabiashara walikuwepo mwanzo wote nipate orodha yao na hivi sasa orodha nimehifadhi pale TAMISEM. Kwamba, wale wafanyabiashara asilia lazima kila aliyetolewa pale soko linapokamilika aweze kupata nafasi ya kufanya biashara. Kwa hiyo, niwahakikishie kwamba, tume-*consider* mambo haya yote kwa maslahi mapana ya Wananchi wetu wa kawaida. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini kulikuwa na suala zima la ujenzi wa miundombinu ya barabara, hili naomba nimelichukua katika upande wa *TARURA* kwa ujumla wake, ushauri umetolewa.

Mheshimiwa Naibu Spika, suala zima la michango kwamba, watumishi michango inaonekana deni limeongezeka, tumelichukua kwamba, kila linalotolewa kwa wajumbe hapa twende tukalifanyie kazi kwa maslahi mapana ya kuboresha Serikali yetu kwa maslahi mapana ya kuboresha suala zima la wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo, binafsi nikiwa kama Waziri wa Nchi, Ofisi ya TAMISEMI niseme nimechukua maoni yote ya wajumbe na Wabunge wote kwenda kuboresha pale maeneo ambayo yanaonekana yana changamoto kubwa tuyafanye yaende vizuri kwa maslahi mapana ya nchi yetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana, naunga mkono hoja zote kwa jumla. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Madini, tutamalizia na Waziri wa Fedha.

**WAZIRI WA MADINI:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nichukue nafasi hii nikushukuru sana kwa kunipa fursa hii ya kuchangia hoja ya kamati. Na ninaomba vilevile nimpongeze sana Mwenyekiti wa Kamati, Mheshimiwa Mama yangu Mama Kaboyoka, kwa kazi kubwa yeye pamoja na kamati yake akisaidiana na Mheshimiwa Aeshi Hilal kwa kuendesha kamati ile vizuri na kuja na taarifa nzuri ambayo kwa kweli, imesheheni mambo mengi ya kufanyia kazi, nawapongeza sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, kumetokea hoja tatu zinazohusu Shirika la madini Nchini *(STAMICO)*. Na hoja hizo zote kwa ujumla wake kama Wizara tunazipokea na ni hoja za msingi sana ambazo zinahitaji kufanyiwa kazi. naomba tu nitoe taarifa kwa kamati kwamba, yako mambo ambayo tayari tumeshaanza kuyafanyia kazi. ni kweli kwamba, shirika hili lilikuwa linakumbwa na tatizo kubwa sana la utendaji na hivyo kulifanya kutokufanya kazi nzuri zaidi ya kuzalisha kama ambavyo lilikusudiwa toka kuanzishwa kwake mwaka 1970.

Mheshimiwa Naibu Spika, *STAMICO* toka wakati ule haijawahi kufanya kazi yoyote ya kuipatia faida isipokuwa siku za hivi karibuni baada ya mabadiliko ambayo nitayaeleza hapa:-

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza utendaji uliotajwa kwenye kamati ni utendaji ambao tumeshaanza kuufanyia kazi. Shirika kwa muda mrefu halikuwa na Mwenyekiti wa Bodi. Nafurahi kusema kwamba, Mwenyekiti wa Bodi amekwishakuteuliwa na alivyoteuliwa na sisi tukaangalia menejimenti nzima ya shirika, tumeifanyia maboresho mengi sana na kumpata mtendaji ambaye kwa sasa kwa kweli, mabadiliko yanaonekana sana.

Mheshimiwa Naibu Spika, shirika lilikuwa linazalisha hasara na madeni mengi sana. Wakati tunaingiza bodi mpya na kubadilisha uongozi shirika lilikuwa limekwishakuzalisha madeni yanayozidi bilioni 35; ninafurahi kuripoti mbele ya Bunge lako Tukufu kwamba, sasa shirika linafanya biashara bila kuzalisha hata deni la shilingi moja. Na mwezi uliopita shirika limefanya biashara ya bilioni 24 na ndio maana umeona hata mwaka huu ulioisha tumeweza kutoa mchango kwa Serikali, jambo ambalo halikuwahi kufanyika toka shirika kuanzishwa miaka ya 70.

Mheshimiwa Naibu Spika, limeelezwa jambo hapa la mikataba ambayo shirika linaingia na ubia na mikataba miwili ambayo imeelezwa hapa, Mkataba wa kwanza ni wa *Tanzanite One* pamoja na Mkataba wa *Bacliff*:-

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa taarifa kuwa mikataba hii yote imekwishakupitiwa na ule mkataba ambao ulikuwa unatusumbua wa *Bacliff* tayari tumekwishakutoa *notice* ya kimakosa ya kileseni, ili tuweze kufuta leseni hiyo baadaye irudi Serikalini, ili Serikali iweze kujua namna gani itaifanyia kazi leseni hiyo. Kwa kweli, ubia ule ulikuwa sio ubia wa kutupatia faida maana ilikuwa ni leseni ile inatumika na mbia mwenzetu kukopa fedha nje ya nchi na anakwenda kuwekeza mahali pengine ambapo sisi hatujui. Sasa tumeshachukua hatua na tayari tumeshatoa *default notice* kwa ajili ya kufuta hiyo leseni, ili Serikali iweze kuifanyia kazi.

Mheshimiwa Naibu Spika, ama kuhusu Mkataba wa *TML* tarehe 23 Disemba, mwaka wa jana:-

Mheshimiwa Naibu Spika, tayari tumeshatoa *Surrender Certificate* ya leseni ile na sasa ninavyozungumza hapa ni mali ya Serikali. Serikali itaangalia utaratibu mzuri wa namna ya kuisimamia leseni hiyo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, na hapa kwenye mkataba wa *TML* ndio pametuopatia matatizo mengi sana. Hata hiyo *disclaimer opinion* ambayo *CAG* ameipata ni kutokana na mbia huyo kutokuandaa vitabu vyake vya kihasibu na kutokuweka rekodi zake vizuri na kwa hiyo, *CAG* akienda wakati wote anakuta hakuna taarifa yoyote; kwa kweli, ulikuwa ubia ambao tusingeweza kupata faida hata tungekaanao kwa muda wa miaka 1,000. Serikali imechukua hatua baada ya maoni mbalimbali ya Serikali yakiwemo ya Wabunge wa Kamati ya Kudumu ya Nishati na Madini tumefanyia kazi na tayari leseni hiyo imerudi mikononi mwa Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, la tatu ambalo Kamati imeeleeza ni kufanya tathmini ya kujua mali za shirika:-

Mheshimiwa Naibu Spika, nafurahi kuieleza kamati na Bunge lako tukufu kwamba, kazi hiyo tayari imekwishakufanyika na hata muundo wenyewe wa shirika tumeanza kuupitia upya. Tulikuwa na kurugenzi nyingi ambazo hazina kazi, tumezi-*consolidate* ili zibaki chache ziweze kuongeza tija kwa shirika na hatimaye tuweze kupata faida.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba nitoe tu taarifa kuwa, shirika hili tukilipa nafasi kwa kipindi hiki na *turn arround* tuliyoifanya kwa kweli, imani yetu ni kwamba, tutaanza kupata faida muda si mrefu. Hata yale madeni ambayo yalikuwepo miaka mingi tuliyoyarithi na yenyewe tumeanza kuyalipa kidogokidogo kadiri ya faida tunayoifanya. *Asset* tuliyonayo ni kubwa na utajiri tulionao ni mkubwa, kazi iliyopo ni kuweka akili kidogo ya kuweza kugeuza hizo *assets* kuwa mali na baadaye kuweza kulipa faida shirika letu. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nisingependa kuzungumza mengi, Kamati naipongeza tena kwa michango yake na kwa yale waliyotuelekeza. Wizara yetu kwa kweli, iko tayari kuyafanyia kazi na tunawatakia kila la heri baada ya kusema hayo. Nakushukuru sana. *(Makofi)*

**SPIKA:** Ahsante sana. Mheshimiwa Waziri wa Fedha, Mheshimiwa Naibu Waziri wa Fedha na Mipango, Dkt. Ashatu Kijaji.

**NAIBU WAZIRI WA FEDHA NA MIPANGO:** Mheshimiwa Naibu Spika, ahsante sana kwa fursa hii adhimu kwa Wizara yetu na sisi kuweza kuchangia kuhusu hoja iliyowasilishwa Mezani na Waheshimiwa Wenyeviti. Na nitajikita zaidi kwenye hoja zilizowasilishwa na Mwenyekiti wa *PAC,* Mheshimiwa Kaboyoka.

Mheshimiwa Naibu Spika, nianze kwa kumshukuru sana Mwenyekiti yeye pamoja Kamati yake kwa kazi kubwa waliyoifanya na kuleta taarifa hii muhimu sana ndani ya Bunge letu Tukufu. Niseme tu kama ambavyo wamekiri ndani ya taarifa yao hoja zote ambazo ziliwasilishwa mwezi Februari mwaka 2019 tunazifanyia kazi kama ambavyo wamekiri, zimebaki chache sana ambazo tunaendelea kuzishughulikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa niende kwenye hoja ambayo imeonekana imevuta hisia kubwa ya Waheshimiwa Wabunge, nayo ni kuhusu Uchambuzi wa Taarifa ya *CAG* kwa Hesabu za Serikali kwa Mafungu ya Serikali Kuu na Mashirika ya Umma, hasa hali halisi ya ufanisi katika utendaji wa Mamlaka ya Mapato Tanzania *(TRA).* Kamati ilipendekeza, kama tulivyosikia na kuona wote kwa pamoja kwamba, Serikali iziboreshe na kuziongezea uwezo Bodi za Rufaa za Kodi na Baraza za Rufaa za Kodi kwa kuteuwa Wenyeviti, Makamu Wenyeviti na wajumbe wa kutosha, ili kuziwezesha taasisi hizi kufanya vikao vyake vya kusikiliza na kuhitimisha kesi za kodi kwa wakati, lakini pia kamati ikapendekeza Serikali iweze kutoa bajeti ya kutosha kwa ajili ya taasisi hizi, ili zifanye kazi zake kwa wakati na kwa ufanisi:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako Tukufu kwamba, kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa Bodi hizi za Rufaa za Kodi Mheshimiwa Rais ameweza kuteuwa Mwenyekiti na Makamu Wenyeviti pamoja na wajumbe wote wa bodi hizi mbili. Kwa hiyo, hilo ni jambo la kwanza kabisa ambalo kama Wizara tulikuwa tunaliomba na ambalo lilikuwa linachelewesha utendaji kazi wa taasisi hizi mbili muhimu sana katika ukusanyaji wa mapato. Kwa hiyo, sasahivi bodi hizi zina wajumbe wake wote pamoja na Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kama ambavyo sheria ilivyopitishwa na Bunge letu Tukufu.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kupata wajumbe hawa bodi hizi zimeanza kufanya kazi vizuri kabisa na tumeweza kwa mwaka 2019 bodi imeweza kushughulikia jumla ya kesi 652 zenye thamani ya shilingi trilioni 2.073 na Dola za Kimarekani 81,644,013. Tuishukuru pia Ofisi ya *CAG* kwa kuweza kuyasema haya kwenye taarifa yake ya mwaka 2017/2018; imetusaidia na tumeanza kufanyia kazi yote haya na sasa tunaendelea kumalizia machache yaliyobaki.

Mheshimiwa Naibu Spika, niliambie pia Bunge lako Tukufu kwa kesi za mwaka 2017 zote zimeshashughulikiwa na taasisi zetu hizi mbili, hatuna kesi hata moja ambayo imebaki ya mwaka 2017. Kesi za mwaka 2018 zimebaki kesi 13 tu na sasa hivi bodi hizi zinashughulikia kesi zilizofunguliwa mwaka 2019. Kwa hiyo, tumefuta kabisa *baklog* ambayo taasisi hizi mbili ziliikuta na sasa tunafanya kazi vizuri. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, niweze kulitaarifu Bunge lako Tukufu kwamba, bajeti pia, taasisi hizi zinapatiwa bajeti ya kutosha na kwa kesho tu, kesho siku ya Alhamisi zitatolewa hukumu kwa kesi zaidi ya 10. Kuna Makamu Wenyeviti wako Arusha na baadhi ya wajumbe wanaendelea kuendesha kesi hizi. Mwenyekiti yuko Dar es Salaam anaendelea na kesi na baadhi ya wajumbe na Makamu Mwenyekiti wa pili yuko Mwanza na baadhi ya wajumbe wote wanaendelea

kuzishughulikia kesi hizi. Ni dhamira ya Serikali yetu kwamba, mpaka kufikia mwezi Juni, 2020 kesi zote za mwaka 2019 ziwe zimekwisha, ili tuanze kushughulika na kesi za mwaka 2020. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo ningependa kuitolea ufafanuzi nayo ilikuwa ni mapendekezo ya Kamati kwamba, Serikali iongeze wataalamu, lakini pia wataalamu waongezewe uwezo wa kufanya kazi katika maeneo yao husika:-

Mheshimiwa Naibu Spika, napenda kuliarifu Bunge lako tukufu kwamba, Serikali yetu kupitia Mamlaka ya Mapato Tanzania imeendelea kuwajengea uwezo watumishi wetu wa Mamlaka ya Mapato katika masuala mbalimbali ya usimamizi wa kodi ikiwa ni pamoja na weledi katika sheria za kodi, ukaguzi na ukadiriaji kupitia mafunzo ya ndani na mafunzo ya muda mfupi na muda mrefu pia. Mafunzo haya hutolewa na chuo chetu cha kodi *(Institute of Tax Administration)* ambacho kinafanya kazi kubwa sana katika eneo hili kutuandalia wataalam wetu, ili waweze kufanya kazi hizi kwa ufanisi wa hali ya juu.

Mheshimiwa Naibu Spika, na hii tunaiona kwa pamoja kama Taifa. Ni kwa mara ya kwanza tangu kuanzishwa kwa Mamlaka ya Mapato Tanzania kwa mwezi Juni, kuanzia mwezi Julai, 2019 hadi mwezi Disemba, 2019 Mamlaka ya Mapato walitarajiwa kukusanya shilingi trilioni 9.45 na kwa sababu sasa tunawawezesha wataalam wetu kufanya kazi hii kwa weledi mkubwa Mamlaka ya Mapato kwa miezi hii sita imeweza kukusanya zaidi ya shilingi trilioni 9.1 ambayo ni sawasawa na 96.3%. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ni ufanisi wa hali ya juu, tuendelee kuwapa moyo wataalam wetu, lakini pia Watanzania kwa ujumla tuendelee kulipa kodi kwa hiyari tusisubiri kulazimishwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni muhimu sana tukafahamu mengi makubwa yanayotendwa na Serikali yetu ya Awamu ya Tano inayoongozwa na Rais wetu Dkt. John Pombe Magufuli yanatendwa kwa sababu ya makusanyo mazuri ya mapato. Kwa hiyo, niwaombe Watanzania kwa pamoja tujitolee kwa hiyari yetu kila mmoja kulipa kodi yake ile anayostahili. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nilishukuru pia Bunge lako Tukufu walipotupitishia sheria yetu ya fedha ya mwaka jana na mwaka huu tunayoitekeleza pale tulipoleta hoja ya *Tax Amnest,* imetusaidia sana pia kuweza kukusanya kodi. Hii yote ni mikakati mbalimbali ambayo Serikali inakaa na kutafakari na kuona ni jinsi gani ya kupeleka unafuu kwa walipa kodi, lakini pia Serikali yetu iweze kupata kodi yake inavyotakiwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya kusema maneno haya naomba niwapongeze tena Wenyeviti na wajumbe wa kamati zote mbili ambazo zimewasilisha taarifa zao mbele ya Bunge lako Tukufu. Kama Wizara tunasema kwa niaba ya Serikali tutaendelea kuyafanyia kazi yote yaliyopendekezwa na Kamati kwa sababu, tayari tumeshayaanza na ufanisi wake tunauona.

Mheshimiwa Naibu Spika, nashukuru sana kwa fursa hii ya kutoa mchango wangu kwenye hoja hizi. Ahsante sana. *(Makofi)*

**NAIBU SPIKA:** Ahsante sana. Sasa nimuite Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali aje ahitimishe hoja yake; Mheshimiwa Naghenjwa Kaboyoka.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru tena kwa mara nyingine kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja hii muhimu ya Kamati. Naomba kuwashukuru Waheshimiwa Wabunge wote waliochangia hoja ya Kamati na pia naomba kutoa ufafanuzi na maelezo ya msisitizo kwa baadhi ya hoja zilizotolewa na Waheshimiwa Wabunge.

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza ni kuhusu utaratibu wa utekelezaji wa kazi *za PAC,* Kamati ya *PAC* inafanya kazi kwa mujibu wa Kanuni za Bunge. Hoja zilizowasilishwa na Kamati katika taarifa hii ni zile tu ambazo Maafisa Masuuli husika walihojiwa na Kamati na majibu ya hoja zao kufanyiwa uhakiki yaani *verification* na Mdhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali *(CAG)*.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo hoja ambazo hazikufanyiwa uhakiki na *CAG* na Maafisa Masuuli husika kutohojiwa hazikujumuishwa katika Taarifa hii. Kwa muhtasari hoja zote za Waheshimiwa Wabunge zimesisitiza utekelezaji wa mapendekezo ya Kamati katika maeneo mahsusi ili kuboresha usimamizi wa fedha za umma katika Serikali Kuu na Mashirika ya Umma.

Mheshimiwa Naibu Spika, mapitio ya baadhi ya hoja hizo ni kama ifuatavyo:-

Mheshimiwa Allan Kiula amechangia kuhusu hoja ya ukusanyaji wa mapato inayotekelezwa na *TRA*. Amesisitiza kuwa *TRA* ni roho ya Taifa, hivyo, lazima *TRA* ifanyie kazi changamoto kadhaa ili kodi zote ziweze kukusanywa kwa wakati. Ni vyema hoja na pendekezo la Kamati linalohusu weledi na ufanisi likazingatiwa. Aidha, kesi za kodi ni muhimu zikamalizika kwa wakati na zile kodi ambazo hazikusanyiki ni vema zifutwe ili vitabu vya hesabu za *TRA* ziwe sahihi. Aidha, Mheshimiwa Kiula amesisitiza pia kuhusu kukwama kwa Miradi ya *TBA* na *NHC* na hivyo mapendekezo ya Kamati kuhusu kukamilisha Miradi ya Taasisi hizi ni vyema yakazingatiwa ili kuokoa fedha za Serikali;

Mheshimiwa Ali Salim khamis ameongelea suala la kutokamilika kwa usimikaji wa mifumo ya usimamizi na udhibiti wa shughuli za Mamlaka ya Usimamizi wa Bandari *(TPA)*. Amebainisha namna ambayo Viongozi wetu Wakuu wa Nchi wamekuwa wakisisitiza kuhusu suala la mapato ya Bandari, hivyo anasisitiza *TPA* ikamilishe Usimikaji huo mapema ili kudhibiti mapato ya Serikali;

Mheshimiwa Felister Bura amebainisha kuhusu gharama zinazoongezeka kwa Miradi ya *NHC* iliyosimama kwa muda mrefu kutokana na Wakandarasi kuendelea kuwepo eneo la Mradi. Kama Waheshimiwa Wabunge walivyochangia mawazo, naye pia anasisitiza kutekelezwa kwa mapendekezo ya Kamati ya kuangalia namna bora ya kukamilisha Miradi hiyo ili kuokoa fedha za Serikali.

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimimiwa Anatropia Theonest, mchangiaji wa nne pamoja na mambo mengine amesisitiza kuhusu umuhimu wa *TRA* kuendelea kuongeza ufanisi ili kufikia lengo la ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kamati inaamini mapendekezo ya Bunge yatazingatiwa na mwaka ujao wa fedha *TRA* itavuka malengo ya ukusanyaji kodi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Joyce Sokombi amechangia kuhusu ucheleweshaji wa Miradi ya *TBA* kwa sababu mbalimbali kama usimamizi mbovu wa Miradi na uhamishaji wa vifaa katika miradi. Ametoa mfano wa Jengo la Tume ya Uchaguzi Dodoma, hivyo ni muhimu mapendekezo ya Kamati kuhua *TBA* yakafanyiwa kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Kigua amelifahamisha Bunge kuhusu kupungua kwa hoja za Ukaguzi ikilinganishwa na miaka ya nyuma. Namshukuru pia Mheshimiwa Kigua kwa kutoa ufafanuzi kuhusu namna Kamati inavyoshughulikia hoja za Ukaguzi baada ya uhakiki wa *CAG*. Aidha, amesisitiza kuhusu umuhimu wa ukadiriaji sahihi wa kodi na kumalizika kwa kesi zaidi ya mia nane za kodi, amesisitiza kuhusu pia *NHIF* na *NHC*. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna mambo mawili ambayo yamejitokeza ambayo nafikiri Kamati ni vyema tukayazungumzia, pamoja na kwamba tunasema kwamba mambo haya hayako kwenye, maeneo haya hayako kwenye Kamati yetu katika Taarifa hii, ni vyema mimi nikiwa Mwenyekiti wa *PAC* kwa vile yametajwa na kwa vile Rais wetu wa Nchi, Mheshimiwa Dkt.

John Pombe Joseph Magufuli ametajwa kuhusiana na kumwajibisha Mheshimiwa Kangi Lugola ni vizuri pia nikataja mambo ambayo nafikiri kwamba yataweza kumfanya Rais Dkt. John Pombe Magufuli asionekane ni mtu wa *double standard (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, Mheshimiwa Anatropia alisema kwamba kama Mheshimiwa Kangi Lugola alitolewa katika nafasi yake kutokana na kutoleta Mikataba ya Zimamoto hapa Bungeni, yeye alitoa wasiwasi kwamba kuna Mikataba ambayo imeonekana haikuletwa hapa na ikafanya Kamati ishindwe kufanya kazi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa ninachosema kama Mwenyekiti wa *PAC* ni kwamba, kwanza kuna Mkataba huu wa *E-Migration*, huu Mkataba Kamati ilikaa na ikaomba Serikali ilete ule Mkataba ili uweze kuufanyia kazi. Badala ya Afisa Masuuli kujibu au kuleta tukapata maelezo ambayo barua ninayo sina haja ya kusema *details* kwamba Kamati tulimalize tu maana lina mambo nyeti, kitu kilichonishangaza uandishi wa maelekezo haya hauonyeshi kwamba una weledi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza mwandishi huyu hakuweza kuelewa kwamba Kamati ya *PAC* inafanya kazi kutokana na taratibu zilizowekwa na Bunge hili Tukufu, Kamati haina Mamlaka kufuta hoja yoyote ya *CAG* kama hoja ile haikuletewa vielelezo au kama *CAG* hakuelewa au hakukubaliana na yale maelezo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa maana hiyo nilichukua hatua ya kuongea na Spika na kumwambia Mheshimiwa Spika, kazi uliyotupa *PAC* ni kufuata taratibu za Bunge, taratibu zilizowekwa na Bunge kwamba hela yoyote ya Serikali ambayo imetolewa lazima itolewe maelezo kwamba imetumikaje. Kutokana na huu mfumo wa *E-Migration,* kilichotakiwa siyo kuangalia kama kuna *coding* au kuna nini nyeti za ule mfumo, kilichotakiwa ni jinsi manunuzi yalivyofanyika kama Sheria ya Manunuzi imefuatwa, pesa zimelipwa ilivyotakiwa na ni kiasi gani ili kusudi hata mapato yanayotokana na hizi *passports* ionyeshe kwamba inawiana na *investment* iliyofanyika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, nikasema kama Mwenyekiti kwamba, inaelekea Rais hakushauriwa vizuri maana Rais angeshauriwa vizuri ingekuwa ifuatwe taratibu iliyowekwa na Bunge na ndiyo maana Rais alivyogundua yaliyotokea kwa Mheshimiwa Kangi Lugola alimsimamisha akamwajibisha. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kama hivyo ndivyo tunategemea hata hili la *E-Migration* halijakwisha, bado tutalifanyia kazi pamoja na *CAG* na kuona kwamba utaratibu unafuatwa na kama kuna jambo lolote tunategemea Rais akae na Spika, ili amweleze tatizo ni nini, Spika aweze kumshauri kutokana na Sheria za Kibunge ili kuanzia hapo sisi na *CAG* Kamati ya *PAC* ndiyo tunaweza kukaa na kusema hili jambo limefungwa au bado. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambalo mimi nilihusishwa na Kamati yangu, wachache wetu kuhusu *uniform* za Polisi, kuhusu *uniform* za Polisi maana tunataka kumtoa Rais wetu asionekane ana *double standard*, mimi nilikuwa nimesafiri, nilikuwa *South Africa* nikapata barua kwamba wenzangu wameteuliwa Kamati ya Mambo ya Nje, Ulinzi na Usalama na wachache wa Kamati yangu kwenda kuangalia zile *uniform* za Polisi, wakati huo alikuwa Mheshimiwa Zungu ndiyo Mwenyekiti wa Kamati hiyo.

Mheshimiwa Naibu Spika, nikamwambia Mheshimiwa Zungu naenda kama nani kwa vile, mimi kama naenda kukagua na Kamati yangu, ina maana tumekaa na *CAG* tumepitia zile nyaraka zote zilizotakiwa maana suala la *CAG* halikuwa kwamba *uniform* tukazione kwa macho.

Suala la *CAG* ilikuwa tuangalie namna *uniform* zile zilivyonunuliwa; je, huyo aliyepewa tender alipatikanaje? Uniform zililetwa kutoka wapi? Ziliingia *bills of laiding* ziliingia vipi, zikoje, kiasi cha fedha iliyotumika ni ngapi, *from there* ndiyo *CAG* aweze kwenda *store* kuangalia kuna nini? Kutokana na zile ripoti aone kwamba hizi *uniform* ziliagizwa 100, zimekuja 100, viatu viliagizwa 10 vimekuja 10? Kinyume cha hapo *CAG* hawezi kutoka akaenda kwenye *store* akaangalia kitu ambacho hana *documentation* kwamba anaangalia nini. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo kulikuwa na mis-conception ambayo Mheshimiwa Kangi Lugola ali *miss-lead* Bunge kwa kuapa na kusema atavua nguo kama *uniform* hazipo. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ina maana hasomi hata taratibu za kwamba...

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Mwenyekiti, ngoja tuongozane vizuri.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Wewe hapo sasa hivi unavyozungumza ni kana kwamba nawe ni mchangiaji wewe ni mtu ambaye ni Mwenyekiti wa Kamati ambaye umekasimiwa madaraka ili uje ujibu hoja za Wabunge na humpi mtu mwingine hoja na baada ya kuzungumza wewe, maazimio uliyotuletea Bunge litahojiwa.

Sasa kama unatupeleka kwenye hoja tena nyingine na wewe ndiye uliyeleta taarifa hapa ndani Mwenyekiti utakuwa unaliongoza Bunge sehemu siyo. Kwa sababu wewe unapaswa kuzijibu hoja za Wabunge na siyo kuuliza kwa sababu hakuna mtu wa kukujibu, Serikali kwenye hoja hii wao ni wachangiaji kama mchangiaji mwingine, sasa ukija na wewe unauliza maswali, sasa nani atakayekujibu hayo maswali na wewe hii ndiyo hoja yako wewe. Hii ni hoja Mwenyekiti, kwa hiyo hoja zote zilizoletwa na Wabunge wewe ndiyo unazijibu hapo siyo mtu mwingine.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa. Nakushukuru.

**NAIBU SPIKA:** Ngoja tuongozane vizuri, kama kuna hoja ambazo kwenye Kamati hamkuzimaliza hilo ni la kwako Mwenyekiti, Serikali haiwezi kujibu hapa.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawasawa.

**NAIBU SPIKA:** Wewe ndiyo unayejibu hoja zote zilizotolewa na hata hayo maswali unayouliza nilikuwa nataka tu nione unaelekea wapi.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa.

**NAIBU SPIKA:** Hata maswali unayouliza yote ni ya kwako wewe utujibu hapa kama Bunge ili tuweze kuamua kwenye Maazimio uliyoyaleta wewe na Kamati yako.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru sana kwa muongozo wako na hapo ndiyo nilikuwa nafikia. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, ili nitalitaja huko kwamba bado hili tutalifanyia kazi, kwa hiyo, umenieleza vizuri sana na nimekuelewa. Nataka nisahihishe kwamba…

**NAIBU SPIKA:** Mwenyekiti samahani, nisikilize kidogo.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, ndiyo naendelea na hoja.

**NAIBU SPIKA:** Kwenye maazimio ya kwenye kitabu chako hiki hayo unayotaka kuyaleta, sina hapa mezani mabadiliko yoyote kwenye taarifa hii.

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge tufuate Kanuni zetu, kama unataka kuleta mabadiliko kwenye Maazimio lazima mimi niwe nayo hapa mezani ni wapi unabadilisha na hayo mimi sina, kwa hivyo Mwenyekiti huwezi kutoa ahadi hapo ukataraji tutalihoji Bunge kwenye hizo ahadi, hapana, siyo utaratibu kikanuni.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, nimekuelewa. Ni kwa vile…

**NAIBU SPIKA:** Kwa hiyo wewe jibu hoja za Wabunge walizokuletea, huwezi kuanzisha hoja mpya ili Bunge lihojiwe, Bunge litahojiwa kwenye taarifa uliyoleta na Maazimio uliyoyaleta.

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, sawa nakuelewa sana na nakushukuru, nilitaka nitoe tu ile kwamba Rais asionekane ana *double standard.*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naomba Mwongozo wako…

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, maana kuna mambo ambayo inawezekana hakupelekewa ndiyo nilitaka tu kueleza hivyo.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Mwongozo tu kidogo.

**MBUNGE FULANI:** …asituletee mambo yenu hapa…

**NAIBU SPIKA:** Hamna Mwongozo akiwa mtu anazungumza, wewe unajua Kanuni na nitakuruhusu uisome hapo umesema mwongozo hakuna mwongozo mtu akiwa anazungumza, naomba ukae.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu…

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae, naomba ukae…

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, kuhusu utaratibu…

**NAIBU SPIKA:** Naomba ukae Mheshimiwa Halima. Naomba ukae. Mheshimiwa Kaboyoka.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kuhusu Utaratibu…

**MBUNGE FULANI:** Nyamaza…

*(Hapa baadhi Wabunge walizungumza bila kufuata utaratibu)*

**MHE. NAGHENJWA L. KABOYOKA - MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI:** Mheshimiwa Naibu Spika, kwanza nipende kumpongeza Mheshimiwa Waziri Biteko kwa jinsi alivyoeleza kuhusu *STAMICO* na hatua ambazo amezichukua pamoja na Waziri wa Fedha. Kwa hiyo, nasema kwamba pamoja na maelezo yao ambayo ni mazuri na nawashukuru kwamba wameonyesha picha halisi hasa Mheshimiwa Biteko ambaye ameonesha jinsi ambavyo *STAMICO* imeshughulikiwa bado tutahitaji kupata *verification* kutoka kwa *CAG. (Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa hiyo nahitimisha kwa kumshukuru Mheshimiwa Spika kwa uongozi wake thabiti, nakushukuru pia wewe binafsi kwa uongozi wa Bunge letu, nawashukuru Wajumbe wenzangu wa Kamati kwa ushirikiano wao mkubwa hadi kukamilika kwa taarifa hii.

Mheshimiwa Naibu Spika, ni matumaini yetu kuwa Serikali itazingatia kwa ukamilifu uchambuzi wa Kamati na kutekeleza mapendekezo ya Kamati.

Mheshimiwa Naibu Spika, nakushukuru na nawashukuru pia Wabunge wote kwa kunisikiliza.

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo, naomba kutoka hoja kwamba Bunge lako sasa lipokee na kukubali taarifa ya Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali *PAC* kuhusu shughuli za Kamati hiyo kwa mwaka 2019.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. DAVID E. SILINDE:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono Waheshimiwa Wabunge tutaendelea na utaratibu wetu wa kawaida. *(Makofi)*

Waheshimiwa Wabunge, Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali ameleta maazimio ambayo yako kwenye taarifa ya Kamati na sote tumeyapitia hayo na michango tumeisikia sasa kwa utaratibu wetu, hoja imeungwa mkono, sasa nitawahoji kuhusu mapendekezo na yale maazimio ambayo Kamati imeyaleta kwa Bunge ili Bunge liweze kuhojiwa na kuamua kwenye hayo mapendekezo.

Waheshimiwa Wabunge tulishakataa watu wachache kuwasha *microphones*.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya kuunda Kamati Teule.

**NAIBU SPIKA:** Mheshimiwa Halima, naomba ukae, naomba ukae.

Waheshimiwa Wabunge nilishasema, narudia tena, ukiwasha *microphone* wakati wa kuhojiwa inaonekana kana kwamba ni mtu mmoja anasema na bahati mbaya sana huyo aliyewasha *microphone* ndiyo hao hao wanaoanzisha hoja huko nje kwamba ni mtu mmoja alisema ndiyo. Huo utaratibu si mzuri, sisi wote ni watu wazima tufuate utaratibu, usiwashe *microphone* saa ya kuhojiwa kwa sababu ninyi wenyewe ndiyo wapotoshaji huko nje. Sasa nitawahoji kuhusu hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na kuafikiwa)*

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Hoja ya Kuunda Kamati Teule mwisho…

**NAIBU SPIKA:** Kanuni.

**MHE. HALIMA J. MDEE:** Mheshimiwa Naibu Spika, Kanuni 120(1) na (2) sasa nitaenda 120(2)(a) inasema:

*"Baada ya hoja iliyokuwa ikijadiliwa kuamuliwa, Mbunge yoyote mwenye nia ya kutoa hoja chini ya Kanuni hii anaweza kusimama mahali pake na kutoa taarifa ya mdomo kwamba anakusudia kutoa Hoja ya Kuunda Kamati Teule."*

Mheshimiwa Naibu Spika, katika ukurasa wa 13 na 14 wa Taarifa ya *PAC* umeonyesha kwa namna gani Kamati ya *PAC* inatoa malalamiko kwamba kwenye hoja zinazohusiana na masuala ya kifisadi na ikatoa mfano Jeshi la Polisi pale ambapo Kamati zinatoa taarifa uchunguzi ufanyike Serikali imekuwa ni wazito sana kufanya uchunguzi. *(Makofi)*

Mheshimia Naibu Spika, hili limethibitishwa wakati Mheshimiwa Mwenyekiti wa Kamati ya *PAC* anaelezea mosi kunyimwa Mkataba wa *E-Passport;* pili, ufisadi mkubwa wa *uniform* za Jeshi la Polisi na usanii uliofanywa na Wizara, lakini katika muktadha ule ule ameonekana anazuiwa kuendelea kueleza wakati hoja ilizungumzwa kwa mapana na Mheshimiwa Msigwa.

Mheshimiwa Naibu Spika, sasa kwa kuwa hili Bunge lina mamlaka ya kuunda Kamati teule pale ambapo kunakuwa kuna utata, na kwa kuwa Kamati ya Bunge, imeonyesha kwamba kuna shida kubwa ambayo ni sugu. Ninaomba nitoe taarifa hili ili nifanye utaratibu sasa rasmi kuleta ombi hili rasmi kimaandishi ili Bunge lako liunde kamati teule kisha tuweze kufukunyua huu uvisadi unao fichwa fichwa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, naamini umenielewa naomba kuwasilisha.

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali imeamriwa kwa kupita na Wabunge kusema ndio. Kwa hivyo kwa utaratibu wetu tutendelea na Mwenyekiti mwingine lakini ngoja nimalize hili lililojitokeza hapa.

Mheshimiwa Mdee amesimama kwa mujibu wa kanuni 120 akitupeleka kwenye fasili ya kwanza na fasili ya pili. Ukizisoma hizi zote kwa pamoja yeye ameenda kwenye fasili ya pili (a) ambayo inazungumza kuhusu kusimama mahali pake na kusema hicho ambacho amekieleza. Wakati mwingine kuna (b) lakini kuna yale ambayo yamekwisha kuletewa kwenye moja na mbili na kabla hujasoma fasili ya pili inakutaka usome fasili ya kwanza kwa sababu fasili ya pili inasema bila kuathiri masharti yaliyowekwa kwenye fasili ya kwanza.

Sikusudii kurudia yale aliyoyasema na wala sikusudii kuzisoma hizi kanuni sote tunazo kwenye hizi nimeambiwa kishkwambi sijui tumeambiwa haya tutajifunza taratibu. Kwenye hizi *tablet* sote tunazo hizi kanuni tunaweza kupitia taratibu. Lakini kwa maelezo aliyokuwa akiyatoa hapa, ameyatoa kana kwamba kuna hoja ambayo kamati imeleta, ambayo yeye ndipo aliposimamia kwa maelezo yake kwanini anataka hiyo kamati teule iundwe. Anaeleza kwamba kwa namna moja ama nyingine kamati kuna jambo ambalo imeleta ambalo halijakaa sawa.

Waheshimiwa Wabunge, taarifa ya kamati sote tunayo na ndiyo maana wakati wa kuhitimisha hoja Mwenyekiti tukaongozana vizuri hapa ili afahamu yeye kama Mwenyekiti wa Kamati ya Hesabu za Serikali anapaswa kufanya nini hapa. Yeye kama Mwenyekiti hapa ndani

chochote ambacho amekileta kwenye taarifa ndicho ambacho kinajadiliwa. Na wengine pengine mmekuja baadaye hamkuwepo mwanzo, wakati tukianza uchangiaji na Mheshimiwa Msigwa alikuwa akichangia. Hoja za Kamati za *PAC* na *LAAC* zinatokana na taarifa ya Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali. Kwa sababu hiyo taarifa tunayoletwa na hizi kamati mbili ni kwamba wao wamepata fursa ya kuchambua mambo mazito waliyoyaona huko halafu wanakuja hapa kulishauri Bunge lije na maazimio gani.

Pamoja na hayo ndio maana hao wenyeviti kama ambvyo serikali huojiwa yale mambao amabyo wameleta hoja zao hapa kwa namna hiyo hiyo wenyeviti hao huhojiwa kwenye yale mambo ambayo wameyafanyia kazi. Mwenyekiti anapokuja kujibu hapa hawezi kuanzisha hoja yeye, anapaswa kujibu hoja za Wabunge ili kuwaongoza Wabunge wakafanye maamuzi kwenye maazimio aliyoyaleta kwenye taarifa yake. Sasa leo kilichotokea pengine ndio cha ajabu kidogo mwenyekiti anaanzisha hoja wakati wa kuhitimisha hoja yake.

Ambayo hoja yake ameisoma tangu asubuhi na hayo maelezo ya ziada yaliyoletwa na Wabunge ni kazi yake kujibu hizo hoja kwa mujibu wa walivyoyafanyia kazi. Sio kazi yake yeye kuja kutuanzishia hoja hapa Bungeni kwamba wameshindwa kufanya kazi kwenye ngazi ya kamati kwa hivyo anakuja hapa wakati wa kuhitimisha hoja kana kwamba anashtaki yale yaliyotokea kwenye kamati.

Sio utaratibu kikanuni, Mwenyekiti humu ndani hawezikuanzisha hoja na kwa namna hiyo hiyo kanuni ya 120 inayozungumzia Mbunge kusimama kutaka kusema jambo ambalo anataka kamati teule iundwe, lazima hilo jambo liwe limefika hapa kwa utaatibu unaotakiwa.

Kwa hiyo, maelezo ya Mheshimiwa Halima yametoka kwenye yale ambayo nilikuwa nikimrekebisha hapa Mwenyekiti wa kamati ambaye amepelea kwenye kazi yake kwa sababu alipaswa kujibu hoja za Wabunge na sio kuanzisha hoja mpya. (*Makofi*)

Nadhani tumeelewana vizuri hapo, kwa namna hiyo hii hoja tuelewane vizuri, tuelewane vizuri, tuelewane vizuri. Kwa maana hiyo kwa kuwa hoja anayoisimamia hapo ili iundwe kamati teule haijaja hapa kwa utaratibu ambao unatakiwa, hiyo taarifa haipo na hata hiyo kanuni 120 haiwezi kutumika katika hayo mazingira. *(Makofi)*

Tutaendelea na Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Mitaa aje ahitimishe hoja yake.

**MHE. ABDALLAH D. CHIKOTA - MAKAMU MWENYEKITI WA KAMATI YA KUDUMU YA BUNGE YA HESABU ZA SERIKALI YA MITAA:** Mheshimiwa Naibu Spika, nikushuru kwa kunipa nafasi ya kuhitimisha hoja yangu. Wabunge waliochangia hoja yetu ni Wabunge 14, na kiujumla hoja zao zilikuwa zinalenga katika kutoa msisitizo wa yale ambayo kamati iliwasilisha kama mapendekezo ili baadaye yalidhiwe kuwa maazimio ya Bunge. Kwa muhtasari nitapita hiyo michango yao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya kwanza ilikuwa malipo kwa Waheshimiwa Madiwani. Na hii imechwangiwa na Mheshimiwa Lubeleje, Mheshimiwa Msuha na Mheshimiwa Sikudhani Chikambo.

Mheshimiwa Naibu Spika, vile vile Mheshimiwa Jafo Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais TAMISEMI ametoa ufafanuzi jinsi gani ametoa maagizo kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa. Lakini Kamati inaendelea kusisitiza kwamba pamoja na maagizo hayo TAMISEMI iendelee kufuatilia ili Waheshimiwa Madiwani walipe kabla ya mabaraza ya kuvunja hayo mabaraza yao. Kwa hiyo, naomba sana TAMISEMI mfuatilie ili ifikapo Juni Waheshimiwa Madiwani hawa wawe wameshalipwa stahili zao zote, posho za mwezi na posho za vikao vyao.

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya pili ambayo wachangiaji wengi wamechangia na imechangiwa vizuri na Mheshimiwa Msuha ni hoja ya dosari katika kanuni ambayo imetolewa na hivi karibu na Ofisi ya Rais TAMISEMI ambayo inasimamia uendeshaji wa mfuko wa wanawake, vijana na walemavu. Hapa kuna changamoto zimeshaanza kujitokeza kwanza kipindi cha kuanza malipo uundaji wa vikundi. Lakini je, mamlaka ya serikali za mitaa zitachangia fedha hizi 10% kwa muda gani?

Mheshimiwa Naibu Spika, kwa sababu kuna mamlaka za Serikali za Mitaa zina uwezo mkubwa, kwa mfano juzi tulikuwa Jiji la Dodoma wao wanatenga takribani bilioni 6 kila mwaka. Je watachangia bilioni 6 kila mwaka kwa muda gani? Kwa hiyo, nafikiri Wizara yenye zamana itafanya marekebisha kuhusu kanuni hii kwa sababu ya hii sio Quran au *Bible* wanaweza kurekebisha kulinga na mapato ya halmashauri husika. Kuna halmashauri zina kipato kikubwa na kuna halmashauri ambazo uwezo wao ni mdogo.

Mheshimiwa Naibu Spika, Waheshimiwa Wabunge wengi wamechangia kuhusu mashine hizi ya kieletroniki kwa ajili ya kuchangia mapato *POS* Mheshimiwa Chatanda, Mheshimiwa Msuha, Mheshimiwa Komanya na Mheshimiwa Wambura wamechangia kuhusu hili. Na wameelezea changamoto ambazo zimejitokeza kuhusu *PoS* ambazo zimenunuliwa huko nyuma kwanza zilikuwa zinachezewa lakini zimenunuliwa kwa bei ya juu. Nichukue nafasi hii kuipongeza Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa tendo la hivi karibu la kutoa bure mashine hizi 7,200 kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, tunawaomba sasa TAMISEMI wafuatilie matumizi ya *POS* hizi na kutatua changamoto ambazo zitajitokeza. Naomba Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi iimarishe mitandao katika mamlaka ya Serikali za Mitaa zilizopo pembezoni ili basi mashine hizi ziweze kutumika kwa ufanisi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, kuna suala lingine ambao Wabunge wengi wamelichangia suala la *Forces Account.* Wachangiaji wote wamekubaiana na maoni ya kamati kwamba *Force Account* imeonyesha mafanikio makubwa sana tunajenga vituo vya afya, hospitali za wilaya kwa gharama nafuu na kwa ubora ambao ukubalika. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, changamoto ambayo hata sisi kwenye kamati yetu tumeisisiza kwamba kuna upungufu wa wataalam wa ujenzi (waandisi). Kwa hiyo, kama huko nyuma ilivyofanya ajira maalum kwa wahasibu basi kwa kuwa ma-*engineer* wengi wamehamia TARURA naomba Ofisi ya Rais TAMISEMI kwa kushirikiana na Ofisi ya Rais Utumishi watoe kibali cha ajira maalum kwa ajili ya watumishi hawa wa kitengo cha ujenzi ili miradi hii isimamiwe ipasavyo. Lakini kwa ujumla *force account* ni mkombozi kwa fedha za umma. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, hoja ya tano ambayo Wabunge wengi wamechangia ni kuhusu miradi ya kimkakati, na kipekee nichukue nafasi hii kumpongeza Mheshimiwa Rais na Wizara wa Fedha na Mipango kwa ubunifu huu mkubwa kwa kuzianzishia mamlaka ya Serikali za Mitaa miradi ya kimkakati. Miradi hii ikikamilika itapunguza utegemezi wa halmashauri kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, hivyo, ushauri wa kamati kama tulivyotoa kwenye Kamati yetu, kwanza Ofisi ya Rais, TAMISEMI miradi hii inakaribia kukamika sasa hivi, tumetembelea Soko la Job Ndugai hapa Dodoma, tumetembelea *Dodoma Bus Terminal*. Lakini kuna soko kubwa linajengwa pale Morogoro, miradi hii sasa naomba Ofisi ya Rais, TAMISEMI iweke utaratibu maalum wa kuikabidhi kwenye Serikali za Mitaa na namna yakuziendesha ili ilete tija. Tumeambiwa hapa soko la Ndugai na ile *Dodoma Bus Terminal* miradi hii ikikamilika itakusanya bilioni 18 kwa mwaka. Huu ni ukombozi mkubwa kwa mamlaka ya Serikali za Mitaa na itapunguza utegemezi kwa Serikali Kuu.

Mheshimiwa Naibu Spika, lakini ombi letu la pili kwenye kamati tumezungumzia suala la viwango kwa sababu suala hili la kimkakati fedha zimetoka hazina kama ruzuku. Basi tuhakikishe viwango tutakavyoviweka vya tozo viwe rafiki kwa wananchi wetu tusiweke viwango vikubwa na miradi hii ikakimbiwa na wafanyabiashara. Tujifunze lile funzo ambalo limetokea soko la Mwanjelwa kule Mbeya wameweka viwango vikubwa na wafanyabisha wadogo wamekimbilia lile soko. Ni matarajio yetu Ofisi ya Rais, TAMISEMI itasimamia vizuri na miradi hii ya kimkakati ikawa na manufaa kwa wananchi wetu.

Mheshimiwa Naibu Spika, kama nilivyosema wachagiaji wote hakuna aliyepinga hoja ya kamati, walikuwa walikuwa-*qualify* au wanasisitiza kile ambacho kamati imekifanya. Kwa hiyo, nichukue fursa hii kumpongeza Mheshimiwa Rais kwa jinsi anavyosimamia Mamlaka ya Serikali za Mitaa na jinsi alivyoongeza usimamizi wa fedha za umma na jinsi anavyoelekeza matumizi ya fedha za Umma kwa Mamlaka ya Serikali za Mitaa. Ni matarajio yetu kwamba *speed* hii itaendelea na mwenye macho haambiwi tazama kuna mabadiliko makubwa sana kwenye mamlaka ya Serikali za Mitaa sasa hivi. *(Makofi)*

Mheshimiwa Naibu Spika, baada ya maelezo hayo sasa nikushukuru wewe kwa jinsi ulivyoendesha mjadala wa Kamati yetu. Niombe sasa maapendekezo yetu tisa ya kamati ambayo tumewasilisha naomba sasa yawe maazimio ya Bunge lako tukufu yote tisa tuliyowasilisha yapitishwe.

Mheshimiwa Naibu Spika, naomba kutoa hoja. *(Makofi)*

**MHE. PAULINE P. GEKUL:** Mheshimiwa Naibu Spika, naafiki.

**NAIBU SPIKA:** Hoja imeungwa mkono sasa nitawahoji kwa utaratibu wetu. Wabunge wanaoafiki hoja ya Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu ya Bunge ya Hesabu za Serikali za Mitaa waseme ndio.

*(Hoja ilitolewa iamuliwe)*
*(Hoja iliamuliwa na Kuafikiwa)*

**NAIBU SPIKA:** Waheshimiwa Wabunge, kwa niaba yenu nyote nichukue fursa hii kuwashukuru sana Kamati hizi mbili wajumbe wao lakini pia na viongozi wao kwa maana ya Wenyeviti na Makamu Wenyeviti kwa namna wametusaidia kuleta hizi taarifa ambazo zimelimeisaidia Bunge kufikia mahali pazuri pa kuazimia haya ambayo tumeazimia kwa Kamati zote mbili na kwa hivyo maazimio hayo yanakuwa ni ya Bunge uzuri Serikali hasa kwenye yale maazimio yanahusika wao wameyapokea na wameahidi kuyafanyia kazi na kama ambavyo wote ni mashahidi kuanzia michango ya asubuhi Wabunge wengi mmeungana na hizi Kamati lakini mmeunga mkono haya maazimio yao na mapendekezo yao.

Lakini pia wote mmekiri kwamba Serikali imefanya kazi nzuri yakurekibiesha hapa na pale na mmeonyesha kwamba mengi mnayoyapendekeza na yale ambayo Bunge lilishaazimia huko nyuma Serikali imeyatilia mkazo na imefanya mabadiliko ndio maana Kamati zimeleta taarifa ambazo zimeboreshwa zaidi. Kwa hiyo, tunawashukuru sana kamati kwa kazi nzuri yakufuatilia, kwa kufanya kazi pamoja na Makaguzi na Mdhibiti Mkuu wa Serikali.

Kwa hiyo, mmelisaidia Bunge kuweza kuadhimia hivyo na tuwatakie kila kheri upande wa Serikali kwenye haya maazimio ambayo Bunge leo kwenye kuyafanyia kazi ili utendaji kazi wenu uweze kuwa bora zaidi na zile changamoto ambazo Wabunge wamezitaja kwenye maeneo mbalimbali basi ziweze kufanyiwa kazi.

Baada yakusema hayo Waheshimiwa Wabunge naahirisha shughuli za Bunge mpaka kesho saa tatu asubuhi.

*(Saa 07.17 Usiku Bunge liliarishwa mpaka Sikuya Alhamisi, Tarehe 30 Januari, 2020 Saa Tatu Asubuhi)*